# UCHANGANUZI WA VITENDO NENI KATIKA KHUTUBA ZA IJUMAA NA ATHARI ZAKE KWA WAUMINI WA BUGISU, MASHARIKI MWA UGANDA

**MATASI BADRU HAROON**

**Tasnifu hii imewasilishwa katika Shule ya Waliohitimu, kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamifu (Ph.D Kiswahili) ya Chuo Kikuu cha Egerton**

**CHUO KIKUU CHA EGERTON**

**JANUARI, 2014**

## UNGAMO NA IDHINI

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

**Matasi Badru Haroon**

**AD12/0203/07**

Sahihi……………………………………… Tarehe…………………………

**IDHINI**

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa katika Shule ya Waliohitimu kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Egerton.

Sahihi……………………………………… Tarehe…………………………

Dkt. Furaha Chai

Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu, Chuo Kikuu cha Egerton.

Sahihi……………………………………… Tarehe…………………………

Prof. Catherine Kitetu

Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu, Chuo Kikuu cha Egerton.

**HATILINZI**

© 2013

Matasi Badru Haroon

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuigwa, kutafsiri, kunakili, au kuhifadhi tasnifu hii kwa njia yoyote bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Egerton.

## TABARUKU

Kwa wazazi wangu marehemu Haji Harun Makhuwa na Bi. Sabia Nakirya kwa malezi yao bora na dua zao walizokuwa wakiniombea kila uchao. Mwenyezi Mungu awarehemu na awaweke mahali pema peponi.

**SHUKRANI**

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake nyingi na kumsalia mja wake Muhammad (SAW), ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt Furaha Chai na Prof. Catherine Kitetu kwa kukubali kusimamia kazi hii yenye kuchosha na kuchusha hasa nikitambua kwamba walikuwa na majukumu mengi ya kutekeleza. Ingawa niliwasumbua mara kwa mara, walikubali kupokea rasimu za tasnifu yangu kwa moyo mkunjufu. Maoni yao kuhusiana na pendekezo na sura mbalimbali za tasnifu nzima yalinifaa sana

Dkt. Beja S.Karisa amekuwa mwalimu wangu tangu kiwango cha shahada ya uzamili kama Dkt Mukuthuria na amekuwa akinihimiza mara kwa mara kusomea shahada ya uzamifu. Alinishawishi sana kuja Egerton. Pamoja na kwamba hakusimamia kazi yangu, alikubali kuipitia na kunipa ushauri wa mara kwa mara juu ya jinsi ya kuiboresha.

Ningependa pia kutoa shukurani zangu kwa utawala wa Chuo Kikuu cha Egerton kwa kuweka mazingira mwafaka yaliyoniwezesha kukamilisha masomo yangu. Walimu wangu Prof. T.S.Y.Sengo, Prof.Mohamed A. Mohamed, Prof.Aswan Buliba, Prof. James Onyango Ogola, Prof. Ilieva, Dkt. Mukuthuria, Dkt. Mayaka, Dkt. Issa Mwamzandi, Prof. Mutiti, Dkt. Wako, Dkt. Kwea, na Dkt. Kibet Ngetich Dean wa Ndaki ya Sanaa na Sayansi za kijamii nawashukuru sana kwa kupalilia masomo yangu. Prof. Onyango na Dkt Mayaka walinisaidia pia katika kunipatia marejeleo yanayohusiana na utafiti wangu.

Nawashukuru wanafunzi na walimu wenzangu Bw. A.H.Taib, Bw. Yasin Salum Musa, Bw. Ally Nkonge na Dkt. Hasan Kiyingi kwa mahusiano mazuri tuliyokuwa nayo. Wakati fulani nilipata shida ya pesa mwalimu Taib akanitumia pesa nikaweza kumaliza masomo. Mwalimu Yasin alinivumilia sana kwa sababu nilikuwa nikimsumbua kila uchao na msaada wake ulichangia sana kukamilika kwa kazi hii. Nawatakia ufanisi mwema katika utetezi na kazi zao.

Shukrani zangu pia ni kwa Rekta wa Chuo Kikuu cha Kiislamu cha IUIU Dkt Ahmad Kawesi Sengendo ambaye alinipatia fursa hii ya kuendelea na masomo. Chini ya uongozi wake wa busara, Chuo Kikuu cha IUIU kilinipatia mkopo, nikaendelea kulipwa mshahara muda wote wa

likizo ya kimasomo. Namshukuru pia Kaimu Rekta anayeshughulikia mambo ya kiusomi Dkt Muhammad Mpezamihigo kwa kufuatilia masomo yangu ya Egerton na ndugu Bumali Woira Kaimu Bursar IUIU kwa ushauri alionipa kuhusu kuomba chuo mkopo ili nilipe ada.

Walimu wangu katika shule ya upili, Shekhe Umar Juma Nsereko, Shekhe Issa Yiga, Dkt Sulait Kabali, Shekhe Ishaq, Shekhe Abtwahi Kinobe, Bw.Abbas Samaali na marehemu Shekhe Sulaiman Jagwe walichangia pakubwa masomo yangu kwani ndio walionilipia ada ya shule kuanzia kidato cha 3 hadi kidato cha 6, kaka yangu alipolemewa na mzigo. Tafadhalini! Pokeeni shukrani zangu za dhati.

Namshukuru sana Mufti wa Uganda Mheshimiwa Shekhe Shaban Ramadhan Mubaje na rafiki yake wa siku nyingi Mzee Muhammad Abdul Aziz Al Habib wa Saud Arabia kwa msaada wao usio kifani. Kaka yangu Bw. Muhammad Haruna Buyera namshukuru sana kwa ihsani, ukarimu na kugarimia mahitaji na masomo yangu. Kaka yangu Bw. Idrisa Wazemba na wadogo zangu mabwana Ramadhan Harun Natiko na Shekhe Muzammil Harun Mataya, na dada zangu Bi. Hawa Harun Wanyenze, Bi. Zowena Namarome na Bi. Jaria Nambuya nawashukuru sana kwa msaada wao kwangu binafsi na kwa familia yangu kwa ujumla wakati nilipokuwa masomoni. Msaada wao pia kwa mama yangu Bi. Sabia Nakirya ulinituliza mtima nikapata wepesi wa kupambana na masomo bila tashwishi. Ingawa badaye mama yetu alifariki dunia kutokana na saratani ya ini, walifanya bidii kumhudumia kadri ya uwezo wao.

Shukrani zangu pia zimwendee Kadhi wa mkoa wa Bugisu Shekhe Issa Ahmad Masaba kwa kuniwezesha kufanikisha kazi hii. Nilipokuwa katika hatua za mwanzo, nilitafuta ushahidi wa kuonyesha kwamba kweli kuna malalamishi dhidi ya Maimamu kuhusiana na khutuba za Ijumaa. Nilimwendea Kadhi katika ofisi yake na kumwomba msaada na baada ya kupekua mafaili yake, ushahidi huo ulipatikana. Aidha namshukuru Shekhe Murshid Saad Luwemba, Katibu wa mambo ya kidini katika Baraza Kuu la Waislamu wa Uganda kwa kunitambulisha kwa Kadhi na Waislamu wa eneo la utafiti wangu. Kadhi wa jiji la Kampala Shekhe Abdulkadir Mbogo, Waislamu wa miskiti ya wilaya za Sironko, Mbale, Bududa na Manafa pamoja na Maimamu wao, nawashukuru sana kwa kunipatia data ya utafiti wangu.

Vivyo hivyo, wasaidizi wangu katika utafiti nakushukuruni sana kwa mchango wenu. Shekhe Shaaban Muyeye, Shekhe Ali Juma Shiuyo, Bi.Mariam Nambuya na Bi.Khadija Wagogo walifanya kazi kubwa sana. Shekhe Mudathir Uthuman Gibedya na Bw. Muzammil Mafabi waliniwezesha kupiga hatua kubwa sana katika utafiti waliponipunguzia gharama kwa kuniazima laptop zao. Mungu awatilie wepesi na baraka katika kazi zao.

Rafiki yangu Shekhe Ali Nsimba, Imam wa msikiti wa Njoro, namshukuru sana kwa mchango wake mkubwa katika kufanikisha malengo yangu. Familia ya Shekhe Nsimba kwa muda wa miaka minne, ilinihudumia vizuri sana katika malazi, maakulati na kwa ujumla kuniandalia mazingira mwafaka kwa masomo yangu ya shahada ya uzamifu. Naomba Mwenyezi Mungu aibariki familia hiyo na amjazie Shekhe Ali majaza mema.

Wake zangu Mama Ramla, Mama Hassan, Mama Husnu na Bi.Asia Nambozo nawashukuru sana kwa subira, kunipa matumaini, kunituliza mtima na kuwalea watoto. Mama Ramla alipiga hatua zaidi na kunitumia pesa kila nilipoishiwa. Siwezi kuwasahau watoto wangu Ramla na wenzake. Tangu nianze kusomea shahada hii, hali ya maisha ilikuwa ngumu na muda wangu wa kuwatumikia ulikuwa mchache sana.

Na hatimaye, ningependa kuwashukuru wale wote walionisaidia kwa namna moja au nyingine na ambao sikuweza kutaja majina yao. Mola atusitiri sote, atuafu, atubariki na atukidhie haja zetu na atulipe mema duniani na Akhera. Amina.

## ABSTRACT

Language is a very important tool that is used by man to communicate messages, ideas and societal values. It had been claimed, however, that language used in Islamic religious sermons had negative effects on the audience. However, no research had been conducted to confirm the claim and establish the extent of the effects of the language used in those sermons. This study, therefore, investigated the effects of the language of *khutuba* on the faithfuls who listen to these Friday sermons. The objectives of the study were to establish speech acts in Friday sermons and their effects on believers who profess Islam. The study was intended to answer specific research questions namely; do Friday sermons have specific speech acts, do those speech acts affect listeners in certain ways and what recommendendations could be suggested to ensure that speech acts with positive effects, preferred by the listenership are used in the sermons?. The study was guided by the Speech Acts Theory and supplemented by the Implicature Theory. Speech acts and opinions of listeners as regards the Friday sermons formed data for the research. The data was collected from *Khutubas* delivered in mosques in Eastern Uganda i.e. Mbale, Sironko, Manafa and Bududa districts. Participant observation method was used in data collection. This entailed tape recording 30 sermons from 30 Mosques and taking notes regarding paralinguistic features in the sermons. In addition, 30 Imams who represent 10% of the total number of Imams in mosques found in the area under study and 108 faithfuls were purposively selected. The taped sermons were transcribed and speech acts identified. Thereafter, respondents were contacted and interviewed regarding the intention and effects of the speech acts identified from the sermons. The data was analyzed using simple descriptive statistics to show the frequency distribution of speech acts emerging from the sermons and the findings were described and interpreted using the qualitative method. The study is a contribution to the area of discourse analysis. Speech acts in Friday sermons were identified. The study revealed that the speech acts had negative effects on the believers who listened to the sermons and recommended the use of speech acts that believers seemed to prefer as a measure of preventing inflammatory utterances that might cause conflicts in society.

# IKISIRI

Lugha ni chombo muhimu ambacho hutumika kuwasilishia ujumbe, fikra na maadili ya kijamii. Hata hivyo kumekuweko madai kwamba matumizi ya lugha katika khutuba za Kiislamu za Ijumaa yana athari hasi kwa hadhira. Pamoja na hayo hapakuwa na utafiti uliofanyika ili kuthibitisha madai hayo na kiasi cha athari za lugha iliyokuwa ikitumika katika khutuba hizo. Kwa hivyo, utafiti huu ulidhamiria kuchunguza athari za matumizi ya lugha kwa waumini waliokuwa wakisikiliza khutuba za Ijumaa. Madhumuni ya utafiti yalikuwa kubainisha vitendo neni katika khutuba za Ijumaa na athari zake kwa waumini wa Kiislamu. Maswali ya utafiti yalikuwa, Je, khutuba za misikitini hubeba vitendo neni ? Je, vitendo neni vinavyokitwa katika khutuba za msikitini vina athari hasi kwa Waislamu wanaosikiliza khutuba hizo? na Je, pana uwezekano wa kutumia vitendo neni vinavyopendelewa zaidi na Maamuma ili kuleta athari chanya kwa waumini? Utafiti huu umebainisha athari za matumizi ya lugha katika khutuba za Ijumaa, umeweka msingi imara kwa tafiti za baadaye na kupendekeza njia bora za kuwasilisha ujumbe. Uliongozwa na nadharia ya vitendo neni ikisaidiwa na Nadharia ya Udokezi. Khutuba na maoni ya wasikilizaji juu ya khutuba za Ijumaa viliunda data ya utafiti huu. Data ilikusanywa kutoka kwenye misikiti iliyoko mashariki mwa Uganda - yaani wilaya za Mbale, Sironko, Manafa na Bududa. Mbinu ya uchunguzi shirikishi ilitumika katika kukusanya data. Mtafiti alinasa khutuba hizo kwa kinasa sauti na kuandika maalumati juu ya yale aliyoona. Khutuba 30 zilinaswa kutoka misikiti 30 na maalumati kuhusu viziada vya lugha ambavyo mtafiti aliviona katika misikiti hiyo yaliandikwa. Zaidi ya hayo Maimamu 30 wanaowakilisha aslimia 10% ya Maimamu walioko katika eneo la utafiti na waumini 108 walihojiwa kimakusudi. Baadaye mtafiti aliwaendea wasailiwa wengine ambao ni Maamuma na kuwahoji juu ya nia yao na athari za vitendo neni vilivyoainishwa katika khutuba. Baada ya kupata data, mtafiti aliichanganua kwa kutumia mbinu ya wingi idadi ili kuonyesha umaratokezi wa vitendo neni na mbinu ya kimaelezeo kueleza matokeo ya utafiti. Kazi hii ni mchango kwa taaluma ya uchanganuzi usemi. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa khutba za Ijumaa zina vitendo neni maalum ambavyo vilikuwa na athari hasi kwa waumini waliosikiliza khutuba. Aidha, utafiti ulionyesha kuwepo kwa upendeleo wa matumizi ya vitendo neni maalum ili kuzuia athari na migogoro Kadhaa wa Kadhaa katika jamii.

**YALIYOMO**


**UNGAMO NA IDHINI** ..... ii

**HATILINZI** ..... iii

**TABARUKU** ..... iv

**SHUKRANI** ..... v

**ABSTRACT** ..... viii

**YALIYOMO** ..... x

**SHERIA ZA UNUKUZI** ..... xiv

**VIFUPISHO** ..... xv

**ORODHA YA MAJEDWALI** ..... xiii

**MAELEZO YA ISTILAHI ZA KIGISU NA KIARABU** ..... xvi

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ..... 1

1.1 Usuli wa Mada ..... 1

1.2.1 Masharti ya Kusihi kwa Ijumaa ..... 4

1.2.1 Uislamu Nchini Uganda ..... 7

1.2.2. Historia ya Khutuba Nchini Uganda ..... 8

1.2.3 Idadi ya Waislamu ..... 13

1.2.4 Jamii ya Wagisu ..... 14

1.2.5 Utamaduni wa Wagisu ..... 15

1.2.7 Malalamishi Dhidi ya Maimamu ..... 24

1.3 Mada ya Utafiti ..... 26

1.4 Madhumuni ya Utafiti ..... 26

1.5 Maswali ya Utafiti ..... 27

1.6 Sababu na Umuhimu wa Utafiti ..... 27

1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti ..... 28

1.8 Ufafanuzi wa Istilahi ..... 29

**SURA YAPILI : MAPITIO YA MAANDIKO** ..... 30

2.1 Utangulizi ..... 30

2.4 Misingi ya Nadharia ..... 49

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI** ..... 61

3.1 Utangulizi ..... 61

3.2 Mahali pa Kufanyiwa Utafiti....62
3.2.1Ukusanyaji Data....65
3.2.3 Unasaji Sauti....66
3.2.4 Mahojiano na Wahusika....66
3.2.5. Watafiti Wasaidizi....68
3.2.6 Maadili katika Utafiti....68
3.3 Uchanganuzi wa Data....68
3.3.1 Unukuzi....68
3.3.2 Jinsi ya Kuchanganua Vitendo Veni na Athari zake....69
3.3.2.1 Utaratibu Uliofuatwa katika Uchanganuzi wa Vitendo Neni na Athari zake....69
3.3.3. Jinsi ya Kuchanganua Viziada vya Lugha....72

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA....74**
4.1 Utangulizi....74
4.2 Vitendo Neni katika Khutuba za Ijumaa....74
4.2.1 Vitendo Neni Vielekezi (VE)....78
4.2.2 Vitendo Veni Viwakilishi (VW)....101
4.2.3 Vitendo Neni Vitathminishi (VT)....105
4.2.5. Maana ya Matamko ya Khutuba Kulingana na Nadharia ya Udokezi (NU)....119
4.3 Athari za Vitendo neni vya Khutuba Kulingana na Wasailiwa....127
4.6. Hitimisho....149

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO....150**
5.1 Utangulizi....150
5.2 Muhtasari....150
5.3 Hitimisho....153
5.3.1 Vitendo Neni vya Lugha ya Khutuba za Ijuma....154
5.3.2 Athari za Vitendo Neni Vilivyojitokeza katika Lugha ya Khutuba....154
5.4 Mapendekezo....155
5.4.1 Matumizi ya Sifa za Lugha Zinazopendelewa Zaidi....155
5.4.2 Mapendekezo Juu ya Tafiti za Baadaye....160

**MAREJELEO ........................................................................................................................161**
**KIAMBATISHO A: MWONGOZO WA MASWALI ........................................................168**
**KIAMBATISHO B: VITENDO NENI KATIKA KHUTUBA ZA IJUMAA NA ATHARI ZAKE KWA WAUMINI...........................................................................................169**
**KIAMBATISHO C: MAONI YA MAAMUMA KUHUSU VITENDO NENI VILIVYOJITOKEZA KATIKA KHUTUBA........................................................................198**
**KIAMBATISHO D: MAONI YA MAIMAMU JUU YA KHUTUBA ZA IJUMAA.......207**
**KIAMBATISHO E: BARUA YA RUHUSA WA KUFANYA UTAFITI .........................209**

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Mfano wa Jinsi Vitendo Neni, Nia, Athari na Hisia za Kijumla Zilivyotambuliwa 72

Jedwali 2: Mfano wa Jinsi Viziada Vilivyochanganuliwa........................................................ 73

Jedwali 3: Mfano wa Jinsi Vitendo Neni Vilivyoainishwa ...................................................... 75

Jedwali 4: Viwango vya Vitendo Neni katika Khutuba mbalimbali. ........................................ 76

Jedwali 5: Viwango vya Athari ya Vitendo Neni vya Khutuba kwa Waumini....................... 131

Jedwali 6: Vitendo Neni vya Khutuba za Ijumaa na Athari zake kwa Waumini .................... 145

## SHERIA ZA UNUKUZI

1. Herufi kubwa: Zimetumika katika mada, vichwa vikuu na vifupisho.
2. Wino mzito: Umetumika katika vichwa vikuu na vidogo sawia.
3. Herufi za mlazo: Zimetumika katika tasnifu kutofautisha kati ya matamko ambamo vitendo neni vimekitwa na maandishi mengine. Zimetumika pia katika maneno yasokuwa ya Kiswahili.
4. Alama “ ”: Zimetumika katika unukuzi wa kauli mbalimbali.
5. Alama [[ ]]: Zimetumika kubania matamko yanayobeba viteno neni.
6. Alama [ ] : Zimetumika kuonyesha hali ya ukimya inayobainika wakati khutuba inapowasilishwa.
7. Alama ( ): Imetumika kubania miaka ya uandishi, mahali kauli fulani zilipo, na vifupisho kama vile SW na SAW.

## VIFUPISHO

**AS:** Alaihis salaam; yaani amani iwe juu yake. Hutumika kila anapotajwa mtume yeyote miongoni mwa mitume ya Mungu na pia malaika yeyote.

**BK:** Baada ya Kristo.

**KE :** Kielekezi. Ni moja wapo ya aina za vitendo neni.

**KN:** Kitendo neni.

**KT :** Kitathminishi. Ni aina ya vitendo neni.

**KU:** Kaida ya ushirikiano.

**KUN:** Kanuni ya Unyenyekevu.

**KW :** Kiwakilishi. Ni aina nyingine kati ya aina tano za vitendo neni.

**MI:** Maoni ya Maimamu.

**MM:** Maoni ya Maamuma.

**NKN:** Nadharia ya Kitendo Neni.

**NU:** Nadharia ya Udokezii.

**RA :** Radhia Allahu anhu. Tamko lenye maana ya Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na hutumika kumrejelea sahaba yeyote kati ya sahaba za mtume Muhammad (SAW).

**SAW:** Swala Allahu Alaihi Wasallam ; tamko lenye maana ya rehema na amani zimshukie na ambalo hutumika kumrejelea Mtume Muhammad.

**SW :** Subhaanahu wa Ta-aala ; yaani ametakata na kutukuka kutokana na yale anayoshirikishwa nayo.

**TUC:** The University of Chicago.

**UMSC:** Uganda Muslim Supreme Council.

## MAELEZO YA ISTILAHI ZA KIGISU NA KIARABU

***Baasambwa*:** Ni mizimu ambayo watu huamini kuwa ikiridhishwa mambo yao yatatengenea. Hurejelewa pia kama baakuuka.

***Bitsenze*:** Hivi ni vifaa vinavyovaliwa mapajani na kijana anayejitayarisha kwa tohara. Vimetengezwa kutokana na bati gumu na ndani yake kuna vyuma vidogo ambavyo vikigusana na bati hilo hutoa mlio ama sauti kama ya Kengele.

***Buuse*:** Ni kinyesi cha mbuzi ambacho hutolewa kwenye utumbo wa mnyama huyo.

***Dhulhijja*:** Huu ni mwezi wa kumi na mbili kulingana na kalenda ya Kiislamu. Katika mwezi huu kuna matukio mawili muhimu ambayo ni kwenda Makka kuhiji na kusherehekea Idi kuu- Idul Haji.

***Iddah* :** Huu ni muda mwanamke aliyepewa talaka au yule aliyefiwa na mumewe anaokaa nyumbani kwa mume wake akisubiri uishe ndiyo aende kwao au aolewe. Aliyetalakiwa hukaa huko kwa kipindi cha miezi mitatu au kipindi cha kupitikiwa na hedhi tatu, mama mja mzito akitalakiwa iddah yake pindi anapojifungua ilhali yule aliyefiwa na mume itamchukulia miezi minne na siku kumi.

***Imamu*:** Kiongozi wa dini ya Kiislamu ambaye ana jukumu la kuongoza Waislamu katika sala tano za kila siku, sala ya Ijumaa na kutoa khutuba siku hiyo.

***Imbalu*:** Hili ni neno la Kigisu linalorejelea tohara na miviga inayoambatanishwa nayo**.**

***Imono*:** Ni aina ya mbegu ambayo mti wake huirusha mbali na kumelea huko. Mti huo hujulikana kama *liibono* na hutumika kuzuia upepo kuiangusha migomba.

***Isumbati*:** Hili ni vazi linalovaliwa na mzee anayepewa mamlaka ya kubeba kibuyu cha pombe na usimamizi juu ya familia maalum katika miviga ya tohara.

***Iyabwaana*:** Ni mbuzi au ng'ombe atolewaye kwa mamaake mwari kama ishara ya kuonyesha shukrani kwa kumlea vizuri.

***Kimisaambwa*:**Hii ni mizimu ambayo huabudiwa na watu kutokana na imani kwamba ina nguvu za kuwadhuru au kuwafaa.

***Khatibu* :** Mtu anayetoa khutuba; mhubiri.

***Khuuselela*:** Ni hali ya kupeleka posa kwa babaake msichana.

***Khutuba*:** Mahubiri ya kidini yanayotolewa na Imamu wa msikiti ama mwakilishi wake siku ya Ijumaa kabla ya sala au siku kuu za Idi baada ya sala.

***Khubiita*:** Ni kuwarushia vijana wanaoandaliwa kwa tohara pombe iliyowekwa kwenye kibuyu.

***Kumwendo*:** Hiki ni kibuyu kilichowekewa pombe ya kurushiwa vijana watakaotahiriwa.

***Luusoola*:** Hii ni aina ya mti ambao mbegu zake huanguka na kumelea karibu.

***Maamuma*:** Waislamu wanaosali nyuma ya Imamu na kusikiliza khutuba yake.

***Mimbari*:** Kijukwaa chenye ngazi za kupandia kinachowekwa mbele ya msikiti ili Imamu asimame juu yake anapowahutubia waumini.

***Nikahi* :** Kitendo cha kufunga ndoa kulingana na sheria za Kiislamu.

***Ramadhani*:** Mwezi wa tisa kulingana na kalenda ya Kiislamu. Waislamu wanatakikana kufunga katika mwezi huu.

***Shiilindwa*:** Sehemu ilioko vichakani ambako kijana hupelekwa kwa matambiko siku ya tohara. Wagisu wengine hurejelea sehemu hiyo kama *mwiikoya* au *mwiigoya*.

***Shirk*:** Kitendo cha kuabudu au kuonyesha utiifu kwa miungu wengine badala ya Mwenyezi Mungu.

***Showal*:** Mwezi wa kumi katika kalenda ya Kiislamu.

***Sunna*:** Matendo na matamko ya mtume Muhammad (SAW).

***Thalitha thanawi:*** Ni kidato cha sita kwa upande wa elimu ya dini. Kulingana na mfumo huo, shule ya upili ina viwango viwili. Kila mojawapo ya viwango hivyo humchukulia mwanafunzi miaka mitatu kuhitimu.

***Wudhu*:** Hali ya kujitia tohara wakati Waislamu wanapojiandaa kusali.

# SURA YA KWANZA
# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Khutuba ni mahubiri yanayotolewa msikitini siku ya Ijumaa wakati wa adhuhuri. Khutuba pia husomwa katika siku za Idi mbili-yaani Idul-Fitri na Idul–Adhuha (Glasse, 1993 na Huches, 1982). Khutuba za misikitini zilianzishwa na Mtume Muhammad (SAW) mwaka wa 622 BK, baada ya kuhama kutoka Makka kwenda Madina. Mtume huyu ndiye alikuwa wa kwanza kusoma khutuba akiwa amesimama kwenye mimbari (Annadwy, 1993 na Glasse, 1991).

Neno khutuba hutokana na kitenzi cha Kiarabu *khataba* chenye maana ya "alikhutubia". Khutuba huchukuliwa kama fani na *khatibu* ama mhubiri anatakikana awe na weledi katika *fannil khitaba*. Fani hiyo ilikuwa mashuhuri miongoni mwa Waarabu kabla ya majilio ya Uislamu. Inaaminika kuwa kila kabila lilikuwa na mzungumzaji wake ambaye jukumu lake lilikuwa kujieleza kinathari kwa lugha yenye mvuto`akisifu kabila na watu wake kwa upande mmoja huku akitaja udhaifu wa makabila hasimu.

Mtume Muhammad ( SAW) alikuwa akiwasilisha khutuba yake katika minasaba mbalimbali kama vile baada ya kuuteka mji wa Makka mnamo mwaka wa 630BK na katika hadhira ya Waislamu huko Arafa Saudi Arabia alipokuwa katika hija yake ya mwisho almaaruf kama *Hijjatul Widaa* (hija ya kuaga). Baada ya enzi ya mtume (SAW), makhalifa wake wanne (Abubakar, Umar, Uthman na Ali), makhalifa wa ukoo wa Bani Umayya na magavana wao wa mikoa mbalimbali walikuwa wakiwasilisha khutuba wenyewe katika maeneo yaliyokuwa chini ya utawala wao. Khutuba zao zilishughulikia maswala ya kiserikali, matatizo ya kisiasa na hata maamrisho ya moja kwa moja ambayo yalitakikana yatekelezwe.

Katika utawala wa makhalifa wa Bani Abbas, makhalifa wenyewe hawakuwasilisha khutuba. Badala yake makadhi wa kidini ndio waliopewa jukumu hilo. Shabaha ya kuwatumia makadhi ilikuwa kuutakasa Uislamu kutokana na fikra za kutenganisha mambo ya dini na dunia ambazo zilishikiliwa na watawala wa ukoo wa Bani Umayya. Kitendo hiki kilichangia sana katika kuipa

khutuba nguvu na hadhi inayostahiki. Zaidi ya hayo, kilipelekea vyuo mbalimbali vya mitazamo ya Kiislamu kuweka sheria madhubuti zinazohusu uwasilishaji wa khutuba (TUC,1983).

Kwa mujibu wa Shauqi (1963) majilio ya Uislamu yalitangaza maendeleo na maenezi ya khutuba. Hii ni kwa sababu mtume Muhammad (SAW) alitumia khutuba kama nyenzo ya kulingania dini kwa miaka 13 ambapo alikuwa akiwahutubia jamaa zake Makuraishi na wale wote aliokutana nao huku akiwasomea aya za Kur'ani tukufu. Fani ya khutuba ilikita mizizi mtume huyo alipohamia Madina kwani aliwawekea Waislamu sheria, akawachorea mipaka ya dola lao, akawapangilia maisha yao kwenye misingi ya undugu, usawa na ushikamano kwa ajili ya ya haki na heri. Kwa kutumia khutuba pia mtume aliwabainishia Waislamu maana ya kiroho ya Uislamu ambayo misingi yake ni kumtambua Mungu mmoja na kudumisha uhusiano naye, kutambua amali njema na kwamba nyuma ya maisha haya ya dunia, kuna maisha ya Akhera ambapo atakuja kuhesabiwa mwanadamu kwa yale aliyotanguliza.

Vivyo hivyo, mtume huyo aliongoza umma wa Kiislamu kwa maamrisho ya kidini na makatazo yake huku akitoa utatuzi kwa matatizo yanayomkumba mwanadamu hapa duniani kama vile tatizo la utumwa, ugavi wa miirathi, uhusiano baina ya mwanamume na mwanamke na matatizo mengine ambayo utatuzi wake humhakikishia mwanadamu maisha ya raha na furaha. Kwa njia hiyo khutuba za mtume (SAW) zilikuwa kijalizo cha Kur'ani na kutokana na hilo khutuba ilifaradhishwa katika sala za Ijumaa, Idi na misimu ya Hija.

Katika Kur'ani tukufu, khutuba imerejelewa kama *dhikr ullah* yaani kitendo cha kumdhukuru, kumkumbuka au kumtaja Mwenyezi Mungu. Hivyo ni kwa sababu sifa zake hutajwa na waumini huhimizwa kumjali sana Muumba wao, kwa kutekeleza sheria zake na kuzichukulia kuwa dira inayowaongoza katika maisha yao. Mtazamo huo humtaka muumini awe mwenye kukumbuka kwamba Mwenyezi Mungu humsikia na kumwona kila anapofanya jambo lolote liwe zuri au baya na kwamba atamlipa kwalo. Waumini hutakiwa kuisikiliza khutuba kutokana na matumaini kwamba wanaweza kubadili mienendo yao na kutengeneza maisha yao kulingana na mawaidha motomoto yanayotolewa katika khutuba. Mtazamo wa Kur'ani pia huichukulia khutuba kuwa bora kuliko amali nyingine zinazowashughulisha wanadamu kama vile michezo na biashara na waumini wanaruhusiwa kutawanyika katika sehemu mbalimbali ili kujishughulisha na mambo

mengine baada ya sala. Aya za Kur'ani zinazozungumzia khutuba na sala ya Ijumaa ziliteremshwa baada ya tukio la waumini wa zama za mtume Muhammad (SAW) kutoka msikitini huku mtume akihutubu na kukimbilia biashara baada ya kubaini kuwa kafila ya kibiashara ya kutoka Shami (Syria) imewasili.

Waislamu wanaamrishwa kwenda msikitini mapema katika siku ya Ijumaa ili wawahi khutuba na sala ya Ijumaa (Al-Farsy, 1984). Wakishafika msikitini, wanatakiwa kusali rakaa mbili zinazojulikana kama *tahiyyat ulmasjid*; yaani maamkuzi kwa msikiti. Baadaye wanatarajiwa wakae wakielekeza nyuso zao upande wa kaskazini mashariki unaojulikana kama kibla kwenye Kaaba ilioko Saudia. Wakiwa katika hali hiyo, wanaweza kusoma Kur'ani na kuonyesha unyenyekevu wao kwa Mwenyezi Mungu kwa kumhimidi, kutaja sifa zake, na kusoma dua mbalimbali, mpaka atakapokuja Imamu.

Wakati wowote, kuanzia saa saba kasorobo, Imamu huingia msikitini na baada ya kusali rakaa mbili, hupanda mimbari na kuwatolea waumini salamu. Papo hapo, mwadhini hunyanyuka na kuanza kuadhini. Baada ya adhana, Imamu huanza kuwasilisha khutuba yake ya kwanza kwa kumhimidi Mwenyezi Mungu (SW), Kumsalia Mtume (SAW), kuwatakia radhi sahaba na aila ya mtume, kusoma aya ya Kur'ani, kutoa ujumbe wa wiki na hatimaye kuwaombea dua waumini walio hai na waliokufa na kiongozi wa nchi. Muda huo wote, wanatakiwa kusikiliza kwa makini na wazingatie mahubiri ya Imamu. Mtume Muhammad (SAW) alinukuliwa akisema:

"Ukimwambia mwenzako: 'Nyamaza', siku ya Ijumaa, hali ya kuwa Imamu anawasilisha khutuba, basi utakuwa umetamka yasiyofaa (mambo ya upuuzi)" (Muslim, 2008).

Kwa mujibu wa Maimamu wanne, ambao ndio waasisi wa madhehebu manne ya Kiislamu, ni sharti kuwasilishwa khutuba ili sala ya Ijumaa ikubalike. Hivyo ni kwa sababu Mtume Muhammad hakuacha khutuba kwa vyovyote vile, na kutokana na amri ya Mwenyezi Mungu inayowalazimu Waislamu kwenda haraka msikitini ili wahudhurie ibada ya kumtaja na kumkumbuka Allah. Sharti hilo lilisisitizwa na khalifa wa pili wa Waislamu, Umar bin Al-Khattaab (RA) aliposema kwamba sala ya Ijumaa ilifupishwa tu kwa sababu ya khutuba. Alichokusudia ni kwamba sala ya Ijumaa husaliwa wakati wa  na badala ya sala ya Dhuhuri

ambayo ina rakaa nne. Kwa hiyo sala ya Ijumaa ina rakaa mbili na khutuba mbili zilizofaradhishwa badala ya rakaa mbili zilizosalia. Hivyo basi, khutuba ni sehemu ya sala ya Ijumaa na inatakikana ifupishwe ili isiwe mtihani kwa wazee, wagonjwa na waumini wengine ambao wangetaka kutoka mapema kwenda kutekeleza shughuli zao zingine (Abdul Fallah, 2004).

Kwa vile Uislamu unachukuliwa kuwa mwenendo wa maisha, khutuba inaposomwa hugusia maswala ya kidini, kijamii, kiuchumi na kisiasa. Zaidi ya hayo, lugha inayotumika lazima iwe ile inayoeleweka na waliowengi na yenye athari chanya kwa wasikilizaji.

### 1.2.1 Masharti ya Kusihi kwa Ijumaa

Kwa mujibu wa Al-Fauzan (2009) masharti yanayoipelekea khutuba kusihi ni pamoja na kumhimidi Mwenyezi Mungu, kunena shahada mbili, kutoa mawaidha na kusoma chochote katika Kura'ni hata kama ni aya moja. Akimnukuu Ibn Qayyim alisema:

"Yeyote anayeangalia kwa makini khutuba za Nabii (SAW) na sahaba zake atakuta zikiwa zimevyazwa na kuelezea maongozi na kumpwekesha Mwenyezi Mungu, kutaja sifa za Rabbana Mwenye utukufu, misingi ya imani, kuwalingania watu kurejea mbele ya Mwenyezi Mungu, kutaja neema zake…siku zake ambazo zitawatia hofu kutokana na masaibu yake, kuwaamrisha kumkumbuka na kumshukuru…kumtii Mwenyezi Mungu na kumdhukuru…" (Taz. Al-Fauzan, 2009:129).

Alitaja kwamba Ibn Qayyim hakupendezwa na baadhi ya khutuba zilizokuwa zikiwasilishwa baada ya enzi ya Mtume Muhammad na sahaba zake kwa sababu hazikutilia maanani mambo muhimu yanayotakikana. Al-Fauzan alielekea kukubaliana na maoni ya Ibn Qayyim alipobaini kwamba baadhi ya Maimamu hutunga khutuba kiholela bila kuzingatia masharti yake jambo ambalo huchangia kushuka kwa hadhi yake na kutotekeleza malengo zilizowekewa. Alikariri kuwa baadhi ya makhatibu huingiza katika khutuba maudhui ambazo haziendani na mada na ambazo hazieleweki kwa wasikilizaji wengi kwa vile kiwango chake ni cha juu. Alipendekeza kwamba khutuba yafaa zizungumzie maswala yanayowiana na Kura'ni na sunna kutegemea haja iliopo. Baadhi ya maudhui ambazo aliona kwamba lazima zijitokeze katika khutuba ni wosia juu

ya ucha Mungu, mawaidha bora, kutibu magonjwa yaliyokumba jamii zao kwa ihtisari na uwazi na pia kusoma sana Kur'ani. Akimnukuu Ibn Taymia, Al-Fauzan alisema kwamba:

"Haitoshelezi katika khutuba kuishutumu dunia na kutaja mauti, bali hapana budi kuhimiza juu ya ucha Mungu, kuonya dhidi ya maasi, kuwapigia wito warejee kwa Mwenyezi Mungu, na kuwakumbusha neema zake"(Taz. Al-Fauzan, 2009:124).

Khatibu anatakikana asimame kwenye mimbari, aelekeze uso wake kwa wasikilizaji, aegemee mkwaju au kitu kingine chochote na apaze sauti yake ili asikike vyema. Alieleza kwamba Mtume Muhammad (SAW) alikuwa akipaza sauti, ghadhabu yake ikashtadi, macho yake yakawa mekundu, akaonekana kana kwamba anaonya jeshi dhidi ya adui.

**1.2.1.2 Hadhi ya Siku ya Ijumaa na Sala ya Ijumaa**

Muslim alimnukuu Abi Huraira akisema kwamba mtume (SAW) akisema:

"Sisi ndio wa mwisho na sisi ndio watakaotangulia siku ya kiyama. Hakika kila umma ulipewa kitabu kabla yetu, nasi tukapewa kitabu baada yao. Halafu Mwenyezi Mungu alitujalia siku hii (Ijumaa) na watu wakawa wanatufuata. Wayahudi ni kesho na Wanaswara ni kesho kutwa (Taz. Muslim, 2008: 387)".

Wayahudi ndio waliokuwa wa kwanza kupata utume wakateremshiwa Torati. Wanaswara ama Wakristo wakawa wa pili kuteremshiwa kitabu kitakatifu ambacho ni Injili. Waliokuja mwisho ndio Waislamu nao wakateremshiwa Kur'ani takatifu. Katika siku za Ibada, Waislamu walipewa Ijumaa, Wayahudi Jumamosi na Wakristo Jumapili.

Kulingana na hadithi za mtume Muhammad (SAW), Adam (AS) aliumbwa katika siku ya Ijumaa, akaingizwa peponi katika siku hiyo na Kiyama itatokea siku hiyo. Inaaminika pia kuwa katika siku hiyo ya Ijumaa, kuna wakati ambamo maombi ya muumini huzingatiwa na Mwenyezi Mungu.

Kwa mujibu wa Muslim (2008), sala ya Ijumaa imefaradhishwa kwa Waislamu na hairuhusiwi kuiacha ila kama kuna udhuru kulingana na mafundisho ya Kur'ani na hadithi za mtume (SAW).

Waislamu wanashauriwa wakisikia adhana ya sala ya Ijumaa, wafanye hima kwenda msikitini ili kuwahi khutuba ambayo ni sehemu ya sala hiyo. Kulingana na mafundisho hayo, Mwislamu yeyote anayeacha sala ya Ijumaa kwa siku tatu mfululizo, huchukuliwa kuwa mnafiki. Ifahamike kwamba udhuri unaozingatiwa ni ugonjwa, mvua au kuandaa jeneza.

Katika nchi za Kiislamu hususani Uarabuni, Alhamisi na Ijumaa ni likizo ya wiki ambapo wananchi hupumzika kutokana na shughuli za wiki na kujiandaa kwa sala ya Ijumaa na Khutuba. Nchini Uganda katika utawala wa Idi Amin (1971-1979), Ijumaa ilikuwa siku ya kupumzika pia (Tibenderana, 2006). Kimsingi Ijumaa ni siku ya mkutano wa kila wiki. Ni katika siku hiyo ndipo Waislamu huonyesha umoja wao kwa kushiriki katika ibada inayotanguliwa na khutuba. Katika khutuba hiyo, Imamu huangazia maisha ya wanajamii ya wiki na kutoa nasaha na mafunzo juu ya uendeshaji bora wa maisha. Nasaha hiyo husheheni aya nyingi za Kur'ani (Ali, 1973).

Ingawa sala tano za kila siku inatakikana zisaliwe msikitini, lakini hakuna siku ambayo idadi ya wanaosalia msikitini huongezeka maradufu kama siku ya Ijumaa. Wingi wa waumini hutoa, fursa ya kutangamana na jamaa na marafiki, kujuliana hali na kujadiliana juu ya maswala mbalimbali yanayowahusu. Maimamu nao hupata fursa ya kuwahutubia wafuasi wao juu ya maswala ya kuwajenga kiimani, kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Baada ya kusikiliza khutuba na kumaliza kusali, waumini hutawanyika na kwenda katika shughuli zingine wakiwa wamepata somo la wiki la kuwafaa katika maisha yao ya kila siku. Lakini endapo kutakuwa na jambo la kushughulikiwa kutokana na khutuba iliyowasilishwa, waumini hao wataungana bega kwa bega ili kuitikia wito huo. Mifano inayoweza kutolewa hapa ni maandamano ambayo yamekuwa yakifanyika katika ulimwengu wa Kiislamu kupinga ukaliaji wa kimabavu wa ardhi ya Wapalestina, maandamano yaliyofanyika kupinga mashambulizi ya Marekani dhidi ya Iraqi na Afghanstani, maandamano yaliyofanyika dhidi ya kuongezeka kwa bei ya vyakula huko Misri na ya kutaka baadhi ya viongozi wa Kiarabu wang'atuke yaliyoanza Disemba 2010 huko Tunisia na kusambaa nchini Misri, Lybia, Bahrein, Yemen, Syria na yale yaliyofanyika nchini Uganda kupinga uwasilishaji wa hoja juu ya sheria

ya ndoa katika bunge la nchi hiyo ambayo iliwataka wanaume waombe ruhusa kutoka kwa wake zao wakubwa ili wawaruhusu kuoa wake wengine.

Kinachowasukuma Waislamu, kufanya hivyo ni khutuba za Ijumaa zenye matamko ambayo huwachochea, huwahimiza na kuwaamrisha, almuradi waathirike na watende vitendo mbalimbali. Kwa hivyo, lugha ya khutuba ina nguvu si haba, zinazoweza kubadilisha nyoyo za wasikilizaji na ikitumika vizuri, kuna uwezekano wa kuendeleza jamii katika nyanja mbalimbali za kimaisha.

### 1.2.1 Uislamu Nchini Uganda

Kwa mujibu wa Tibenderana (2006), Uislamu uliingia Uganda kwa mara ya kwanza na wafanyabiashara Waarabu na Waswahili kutoka pwani ya Afrika mashariki, katika miaka ya 1840. Lukyamuzi (2005) na Mahadi (2001) wameeleza kwamba Uislamu uliingia nchini Uganda mwaka wa 1844 kutokana na juhudi za Ahmed bin Ibrahim, Mwarabu kutoka Zanzibar, ambaye alikuwa mfanyabiashara aliyetembelea kasri ya mfalme wa Buganda Kabaka Suuna II. Kabaka Mutesa I ambaye alimrithi Suuna II mwaka wa 1856 alisilimu kisha akawaamrisha machifu wake kusilimu pia na kufunga katika mwezi wa Ramadhani. Mfalme huyu aliritadi baada ya kushinikizwa kupashwa tohara na mashekhe kutoka Sudani  na kutokana na kitendo cha waumini kukataa kusalia katika msikiti wake kwa sababu ya kususia ada hiyo. Kitendo hicho kilimkasirisha sana Kabaka kiasi kwamba aliamrisha kuuawa kwa Waislamu wasiopungua 70 na kuamua kumwalika mmishonari Henry Morton Stanley ambaye alikuja Buganda mwaka wa 1875 akaanza kuufundisha Ukristo.

Mnamo mwaka wa 1888, Kalema alichukua hatamu za ufalme wa Buganda baada ya kukubali kutahiriwa na kwa hiyo akapata uungaji mkono wa Waislamu. Vita vikali vilitokea kati ya Waislamu na Wakristo ambao walimuunga mkono mwana wa mfalme Kiweewa. Kapteni Lugard wa IBEA aliwasaidia Wakristo wakawashinda Waislamu na kuwalazimisha kuhamia katika sehemu mbalimbali za Uganda katika mwaka wa 1889 na 1891 (Lukyamuzi, 2005). Kuhama huku kulichangia sana maenezi ya Uislamu nchini Uganda hasa sehemu za mashariki na magharibi. Kufuatia maenezi hayo, kulizuka haja ya watu waliosilimu kusomeshwa Uislamu ili waweze kutekeleza mafundisho yake ipasavyo. Kwa hivyo, mbinu mbili zilitumika kufanikisha

mpango huo. Mbinu ya kwanza ilikuwa kuwapeleka vijana Zanzibar na Mombasa ili wakihitimu warudi makwao waendeleze elimu ya dini. Wakati huo huo, mbinu ya kuwaleta walimu kutoka Zanzibar ilitumika. Mbinu hizo zilichangia sana katika kuwaelimisha watu.

Mwanzoni, wanafunzi walitakiwa kuhamia nyumbani kwa walimu ambako mafunzo yalikuwa yakitolewa mabarazani kwani shule hazikuwepo zama hizo. Wanafunzi walitakiwa kuwasaidia walimu wao kuchapa kazi mbalimbali kama njia pekee ya kuwalipa. Kwa vile wanafunzi walikuwa wakifanya kazi ngumu na mara nyingi walimu walikuwa wakiwapa adhabu kali kama vile kuchapwa viboko kwa kutotamka maneno ya Kur'ani ipasavyo au kutohifadhi sehemu ya Kur'ani waliyotengewa katika kipindi maalum, watu wengi walikimbia visomo hivyo jambo ambalo liliathiri sana ujifunzaji wa dini. Waislamu waliosoma dini wakati huo walikuwa wachache na kutokana na tatizo hilo misikiti mingi ilikosa Maimamu. Ili kutatua tatizo hilo iliamuliwa kwamba wale waliosoma kisomo japo kidogo wawafunze wenzao. Uamzi huo uliipelekea misikiti mingi kuwa na Maimamu ambao walikuwa na uwezo wa kusoma sura chache katika Kur'ani bila ya kujua maana yake. Ruhusa ulipotolewa kusalisha sala ya Ijumaa, Maimamu hao walilazimika kusoma aya za Kur'ani walizokuwa wamehifadhi kama khutuba ya Ijumaa (Mahojiano na Mzee Khamisi tarehe 2, Februari 2010).

### 1.2.2. Historia ya Khutuba Nchini Uganda

Khutuba ya Ijumaa ina historia ndefu. Nchini Uganda khutuba imepitikiwa na miaka 85 tangu ilipoanza kuwasilishwa katika mwaka wa 1928. Hadi mwaka huo na kuanzia mwaka wa 1844 ambapo Uislamu uliingia kwa mara ya kwanza nchini Uganda , miaka 84 ilikuwa imepita huku Waislamu wakisali tu sala tano za kila siku. Hawakuruhusiwa kusali sala ya Ijumaa muda huo wote na kwa hiyo khutuba isingewasilishwa kwa vyoyote vile. Hivyo ni kwa sababu kulingana na madhehebu ya Kisunni ya Imamu Shafi, lazima idadi ya waumini wa Kiislamu itimie wanaume arubaini ndipo khutuba na sala ya Jumaa viwepo (Taz. Al-Jaziry, 2003).

Kwa mujibu wa Mbogo (Mahojiano ya ana kwa ana na Shekhe Mbogo, tarehe 11 Februari, 2012), khutuba ilianza mwaka wa 1928, baada ya Waislamu wa Uganda kutembelea nchi ya Zanzibar. Waislamu wengi wa Uganda walisomea dini huko Zanzibar ambako khutuba zilikuwa

zikiwasilishwa kutoka katika kitabu maalum. Kitabu hicho kilikuwa kikisomwa kwa uangalifu mkubwa na ndani yake kulikuwa na aya za Kurani na hadithi za Mtume Muhammad (SAW). Shekhe Mbogo alibaini kuwa mnamo mwaka huo wa 1928, aliyekuwa kiongozi wa Waislamu Shekhe Nuhu Mbogo ambaye pia alikuwa mwana wa Mfalume wa Buganda, alimtuma Bwana Musa Wesubawa kwenda Mombasa amnunulie vitabu vya khutuba 12. Shekhe Nuhu aliwaita Waalimu wa tarafa mbalimbali akawagawia vitabu hivyo na kuwataka wawahimize Maimamu wa misikiti wavinukuu ili kila msikiti uwe na nakala.

Khutuba hizo zilikuwa zikiwasilishwa kwa Kiarabu pekee na haikuwa ikiruhusiwa kuzifasiri kwa lugha za kienyeji kutokana na madai kwamba kufanya hivyo ni kuongelea katika sala. Kama ilivyoelezewa hapo mwanzo, kulingana na mafundisho ya Uislamu, khutuba huchukuliwa kuwa sehemu ya sala. Kadiri idadi ya Waislamu ilivyozidi kuongezeka, ndivyo misikiti ilivyoongezeka na vitabu vya khutuba kuuzwa kwa wingi na wafanya biashara wa Kiarabu na Waswahili. Khutuba hizo zilikuwa na duwa ya kumwombea Haqan bin Haqan Sultan wa zama hizo almaarufu kama sultani wa mabara mawili na bahari mbili.

Kitabu cha khutuba kilichokuwa kikitumika mwanzo kabisa kilitungwa na kuchapishwa huko Misri kwa hiyo kilirejelewa kama *Khutubat Misri*. Istilahi nyengine iliyotumika kurejelea kitabu hicho ni *Khutbat Haqan bin Haqan*. Hivyo ni kwa sababu Sultan huyo wa enzi za ukhilafa wa Waturuki wa dola la Wauthumani alikuwa akiombewa dua na Maimamu katika khutuba ya pili ili Mwenyezi Mungu aulinde ufalme wake. Ingawa Sultani huyo alifariki dunia kitambo na dola la Wauthumani likasambaratika mwanzoni mwa karne ya ishirini, lakini Haqan aliendelea kuombewa dua na khutuba hiyo ilikuwa ikikaririwa tu kikasuku pasina kutambuwa maana yake. Kilichotakikana ni Maimamu kuwaombea viongozi wa nchi zao (Walwenje, tarehe 15 Oktoba 2012).

Kitabu cha pili kilikuwa kikijulikana kama *Diwaan Khutwabi Ibn Nabaatah* kilichoandikwa na Ibn Nabaatah. Kitabu hicho kilichapishwa New Delhi. Tofauti iliyokuwepo baina ya vitabu hivyo ni kwamba cha kwanza kiliandikwa kwa lugha ngumu ijapokuwa zote kama ushairi, mistari yake huishia kwa kina maalum. Utambuzi wa maana ya khutubat Misri hutegemea mtu aliyebobea katika ushairi wa Kiarabu. Kitabu kingine cha khutuba ambacho kilikuwa kikisomwa

nchini Uganda ni *Al-uquud Aljawhariyyah fi Khutwabil Minbariyyah* cha Muhammad Saad bin Abdillah kilichochapishwa pia New Delhi. Katika karne ya ishirini na moja, vitabu vingine vya khutuba viliandikwa na waandishi wa Kiarabu ili kuwaongoza Maimamu. Vitabu hivyo vinazungumzia maudhui mbalimbali na hutumika sana na wale ambao hawawezi kujitungia khutuba.

Yafaa ieleweke kwamba kitabu cha khutuba kilikuwa na khutuba zilizosomwa katika miezi kumi na miwili. Kwa vile kila mwezi ulikuwa na khutuba nne, jumla ya khutuba katika kitabu hicho ni khutuba arobaini na nane. Khutuba ya ziada ambayo ilikuwa lazima isomwe kama ya pili kila Juma ni ile ya kumsalia Mtume Muhammad (SAW), sahaba zake, waumini na viongozi, miongoni mwa mambo mengine yanayopaswa kujitokeza ndani yake. Kwa vile siku kuu mbili za Waislamu yaani *Idul Fitri na Idul Adhuhaa* huangukia katika miezi kumi na miwili ya mwaka, khutuba za siku hizo ni miongoni mwa khutuba zilizomo katika vitabu hivyo. Kwa hiyo kitabu kizima kiliundwa kwa khutuba arobaini na tisa za Ijumaa na mbili za Idi (Namonye, tarehe 23 Disemba, 2012).

Kila khutuba ilikuwa ikianza kwa kumhimidi Mwenyezi Mungu na kuishia kwa dua na kuwasihi waumini kutubu mbele ya mola wao kutokana na madhambi waliyoyatanguliza. Kwa upande wa maudhui khutuba zilizungukia juu ya mambo yaliyojiri au matendo yanayopaswa kutendeka katika mwezi maalum. Maudhui za khutuba hizo hutegemea matukio ya kila mojawapo ya miezi ya Kiislamu ambayo ni *Muharram, Swafr, Rabi'ul awwal, Rabi'uth thaani, Jumaadal awwal, Jumaadath thaani, Rajab, Sha'ban, Ramadhan, Showwal, Dhul qa'da* na *Dhulhijja*.

Walwenje (2012) alibaini kwamba khutuba za zamani, zilikuwa na mguso mkubwa katika nyoyo za waumini, ijapokuwa zilikuwa zikisomwa kwa Kiarabu na kwa hiyo hakikueleweka kwa wengi wao. Hivyo ni kwa sababu zilichukuliwa kama matamko matakatifu kutokana na utajo wa Allah na Nabii Muhammad (SAW).

Kwa mujibu wa Kitakule (2011) na Kasozi (1996), mwanzoni Waislamu hawakuwa wakisali sala ya Jumaa katika siku ya Ijumaa kwa sababu walikuwa wachache. Lakini baadaye Shekhe Khalfan mzaliwa wa Kilwa nchini Tanzania alitoa ruhusa na Waislamu wakaanza kusali sala ya

Ijumaa. Hata hivyo, aliwaamrisha kusali sala ya Dhuhuri baada ya kusali sala ya Ijumaa. Hivyo ni kwa sababu walikuwa wachache.

Ijapokuwa idadi ya Waislamu iliongezeka, baadhi ya Waumini waliendelea kuunganisha sala hizo. Hata hivyo, misikiti mingine ilisitisha kusali sala ya Dhuhuri kwa madai kwamba kulingana na madhehebu ya Imam Abi Hanifa, Idadi ya waumini wanaoipelekea khutuba kusihi ni wanaume watatu, huku Imam Malik akiona kwamba wanaume kumi na wawili wanatosheleza haja. Alieleza kwamba Waislamu waligawanyika katika makundi mawili, kundi la Waislamu wa Juma na Dhuhuri (*Juma ne zukuli*) na lengine la Jumaa pekee (*Juma Njereere*).

Mbogo (2012) alieleza kwamba Shekhe Abdallah Sekimwanyi alisafiri kwenda Makka huko Saudi Arabia katika mwaka wa 1921 ili kuhiji na pia kutafuta suluhisho kuhusiana na swala la Ijumaa na Dhuhuri. Huko Saudi Arabia alipata fatua kwamba katika siku ya Ijumaa, sala ya Dhuhuri haisaliwi. Badala yake khutuba mbili huwasilishwa na Imamu na rakaa mbili za sala ya Ijumaa husaliwa.

Inasemakana kuwa Bwana Kibali mzaliwa wa Butambala, mojawapo ya tarafa za Mkoa wa Kati, ndiye aliyegharamia safari hiyo na kwa bahati mbaya mdhamini huyo alifariki dunia huko Saudi Arabia. Shekhe Sekimwanyi alirudi Uganda na kuwapa Waisalamu taarifa juu ya fatua iliyohusu kusali Jumaa pekee. Baadhi ya waumini waliitupilia mbali hiyo taarifa kwa madai kwamba Shekhe Sekimwanyi alikwa akijitafutia umaarufu ili achukue uongozi wa Uislamu nchini Uganda.

Inasemekana kwamba Shekhe huyo alipewa ardhi na Bwana Ayub mmojawapo wa matajiri wa Kampala katika tarafa ya Bukoto, Kaskazini mwa mji wa Kampala ambako alijenga msikiti na kuanzisha makao ya chama cha Kiislamu kilichojulikana kama Juma Njereere au Bukoto Natete.

#### 1.2.2.1 Kutafsiriwa kwa Khutuba

Kama ilivyoelezewa hapo awali, khutuba haikuwa ikitafsiriwa kwa sababu ilichukuliwa kama sehemu ya sala ya Ijumaa na Waislamu hawaruhusiwi kuongea wakiwa kwenye sala. Hata hivyo, mitazamo mbalimbali ilizuka kuhusu swala hilo. Baadhi ya wanazuoni walikataa kuruhusu kufasiriwa kwa khutuba na hata Kur'ani na kutishia kwamba 'mbingu ingeripuka'. Kulingana na

Mbogo (2012), kwa vile Waislamu walikuwa hawajasoma sana, ilihofiwa kwamba wangepotosha ujumbe na mafundisho ya Uislamu jambo ambalo lingemkasirisha Mwenyezi Mungu. Miongoni mwa mashekhe walioshikilia msimamo huo ni Shekhe Shuaib Semakula wa Katumu, kitongoji kilioko katika tarafa ya Bulemezi, wilaya ya Luwero, mkoa mdogo wa Buganda; Shekhe Muhammad Luboowa, Shekhe Kasakya na Shekhe Abdul Kadir Sentamu.

Shekhe Abdallah Sekimwanyi ndiye aliyeshikilia msimamo wa pili ambao uliruhusu Maimamu kuifasiri Kur'ani, hadithi za Mtume na khutuba. Alidai kwamba kutowatafsiria watu ujumbe unaowasilishwa hakuwaendelezi kiimani. Alifananisha hali hiyo na hali ya punda anayebebeshwa pipa la maji na yeye mwenyewe asikate kiu kwa maji hayo.

Kwa mujibu wa Nsiimba (2012), baadhi ya mashekhe walipinga kufasiriwa kwa khutuba kwa sababu walihofia kwamba watu wangeelimika na kuchukuwa nafasi zao. Aidha, alieleza kwamba kutokana na ukosefu wa elimu ya dini, mtu aliyesoma kidogo alikuwa akipewa Uimamu na kwa hivyo hawakujifunza Kiarabu ambacho kingewawezesha kufasiri mafundisho ya Kiislamu. Maimamu kama hao walijificha nyuma ya ujinga waliokuwa nao wakadai kwamba mbingu ingeporomoka kama tafsiri ingefanyika.

Kama ilivyoelezewa hapo awali vitabu maalum vilivyosheheni khutuba kadhaa ndivyo vilikuwa vikisomewa Waislamu siku ya Ijumaa. Ingawa Waislamu waliendelea kupata elimu ya dini na lugha ya Kiarabu na kuruhusiwa na mashekhe wao kutafsiri Kur'ani na khutuba, haikuwawia rahisi kutafsiri *khutubat Misri* kutokana na ugumu wake. Badala yake walipendelea *khutubat Ibn Nabaatah* ambayo Kiarabu chake kilikuwa chepesi.

Inasemekana kwamba Shekhe Salim Masolo ndiye aliyekuwa Mgisu wa kwanza kuwasilisha khutuba ya Ijumaa huku akiitafsiri kwa Kigisu akichanganya na Luganda, mnamo mwaka wa 1939 (Masayi, 2012). Kadiri Maimamu walivyojiendeleza katika elimu ya dini na Kiarabu, ndivyo walivyowezeshwa kujitungia khutuba zao wenyewe na kuziwasilisha misikitini kwa lugha za kienyeji. Maimamu hao hutunga khutuba kulingana na kadhia mbalimbali zinazoikumba jamii.

Karne ya 21 ilishuhudia majilio ya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ambayo kazi yake ni kuwasaidia Waislamu katika nyanja mbalimbali. Mashirika hayo yalichangia sana katika uwanja wa elimu ambapo yalisambaza vitabu vya kidini vilivyotafsiriwa kwa lugha mbalimbali kama vile Kiswahili, Kiingereza na Luganda. Vitabu hivyo viliwapa Maimamu wepesi wa kutunga khutuba juu ya maudhui walizodhamiria kuwafunza waumini wao. Shirika la African Muslim Agency lenye makao yake huko Kuwait lilipiga hatua zaidi likatafsiri khutuba za Ijumaa kwa lugha ya Luganda. Kitabu hiki hugawiwa bure na hutumika sana na Maimamu ambao hawakimudu Kiarabu.

Ijapokuwa baadhi ya Maimamu wanajitungia khutuba zao, kuna wengine ambao wanaendelea kusoma vitabu na kutafsiri maana yake. Hata hivyo, Imamu anatakikana atoe ujumbe wa Ijumaa kwa lugha ya kienyeji kabla ya kupanda kwenye mimbari na kusoma khutuba zilizoandikwa ili kutekeleza sharti ya kuwasilisha khutuba kwa Kiarabu. Ifahamike kwamba, lugha ambazo hutumika katika khutuba mashariki mwa Uganda ni Kiganda, Kigisu, Kisoga, Kigwere, Kinyoli, Kisamia, Kiluo, Kiteso, Kisabiny, Kiswahili, Kiarabu na Kiingereza. Hata hivyo, katika mkoa mdogo wa Bugisu, Kiganda na Kigisu ndizo lugha zinazotumika sana sambamba na Kiarabu. Kiswahili hutumika katika baadhi ya misikiti ya mji wa Mbale na miskiti michache sana vijijini katika wilaya za Mbale na Sironko kwa sababu ya kuwepo kwa wazawa wenye lugha hiyo na wageni wasojua lugha za kienyeji wala Kiingereza. Kwa upande mwengine, Kiingereza hutumika katika misikiti ya vyuo vikuu, vyuo vya ualimu na shule za upili.

### 1.2.3 Idadi ya Waislamu

Idadi ya Waislamu imekuwa ikiongezeka taratibu kuanzia mwishoni mwa karne 19. Kwa mujibu wa Tibenderana (2006) akimnukuu Kasozi (1985), Waislamu walikuwa aslimia 5.6 ya jumla ya idadi ya raia wote wa Uganda mwaka wa 1959, aslimia 11 mwaka wa 1991 na aslimia 12 mwaka wa 2002. Takwimu hizo, hata hivyo, zimepingwa vikali na Baraza kuu la Waislamu wa Uganda. Kwa mfano, uchunguzi wa Mahadi (2001), ulidhihirisha kuwa Waislamu wamefikia aslimia 25. Tibenderana(2006) aliendelea kueleza kwamba kufikia mwaka wa 1959, aslimia 41.7 ya Waislamu wa Uganda waliishi katika mkoa wa Buganda, aslimia 38.2 mashariki mwa Uganda, aslimia 14.7 kaskazini mwa Uganda na aslimia 3.4 katika mkoa wa magharibi.

Alidokeza pia kwamba Waislamu wengi hupatikana mijini ikilinganishwa na wanaoishi vijijini. Kulingana na takwimu za serikali za mwaka wa 2002, wakazi wa Bugisu kwa ujumla ni 718,240. Idadi ya Waislamu ni 132,247 ambayo ni asilimia 18.4 (UBOS, 2005).

### 1.2.4 Jamii ya Wagisu

Kwa mujibu  wa serikali ya kimkoa ya Mbale (1997-2001), Jamii ya Wagisu huishi katika mkoa mdogo wa Bugisu. Mkoa huo hupatikana katika eneo lililoko magharibi na kusini magharibi mwa mlima Elgon kwenye digri $34^0$ 15' hadi $34^0$ 30' za long'itudo kusini mwa Ikweta na digri 0.45' hadi $1^0$ 30' za Latitudo kaskazini mwa Ikweta. Mkoa huo umetwaa eneo la kilomita 2504 za mraba mashariki mwa Uganda. Kwa upande wa mashariki hupakana na Jamhuri ya Kenya. Mikoa ya Teso na Pallisa hupatikana upande wa magharibi ilhali Wilaya ya Tororo ikiwa kusini. Mkoa wa Karamoja umekaa upande wa kaskazini huku wilaya ya Kapchorwa ikiwa kaskazini mashariki.

Mubaje (1995) alieleza kuwa Wagisu ni mojawapo ya jamii za Kibantu ambao walihamia Uganda kutoka Abyssinia (Ethiopia) kutokana na mateso ama usumbufu waliokuwa wakipata. Ayot (1975)akizungumza juu ya asili ya jamii hiyo alisema kwamba Wagisu ni mojawapo ya Wabantu waliohama kutoka katika msitu wa Congo kabla ya mwaka wa 1000 BK. Alieleza kwamba walihama kutoka huko wakitafuta ardhi yenye rutuba kwa ajili ya kilimo.

Wagisu hujulikana pia kama *Bamasaba* ikizingatiwa kuwa babu yao ni Masaba. Neno Gisu lilikuja kutumika badala ya Masaba kutokana na kisa cha Mwambu mmojawapo wa wana wa Masaba na Wakalenjin.  Inasemekana kuwa watu kutoka katika jamii ya Wakalenjin walimwibia Masaba mifugo yake, Mwambu akawaandama na kupigana nao. Alipowashinda, walisema: "*Erono gisuno*". Aliporudi na mifugo, aliwaeleza jamaa zake yaliyojiri kati yake na Wakalenjin na kuwambia yale maneno ya Kikalenjin waliyosema. Tangu siku hiyo, Mwambu akabatizwa jina *gisu*. Baadaye, matumizi ya neno hilo yalipanuka kiasi kwamba *Bamasaba* wote hurejelewa siku hizi kama Wagisu (Buyera, 2008).

Kulingana na maelezo yaliyotolewa na Serikali ya kimkoa ya Mbale (1997-2001), mkoa mdogo wa Bugisu umekaliwa na watu wa jamii mbalimbali kama vile, Wanyore, Wasamia,Wagwere,

Waganda, Wasoga na Wateso. Hata hivyo, Wagisu ndio walio wengi zaidi kwa sababu wanawakilishwa na asilimia 92%.

### 1.2.5 Utamaduni wa Wagisu

Uislamu uliingia Uganda mwaka wa 1844 (Taz. Lukyamuzi, 2005) na jamii ya Wagisu inasemekana kuwepo tangu mwaka wa 1000 BK (Ayoy, 1975). Hii ina maana kwamba Uislamu ulipoingia Bugisu, utamaduni wa Kigisu ulikuwa umekita mizizi. Wagisu walikuwa na mwenendo wao wa maisha. Mwenendo huo huakisiwa katika mambo kama vile ukarimu, ujirani mwema, ushujaa, tohara, ndoa, mazishi, mirathi, dini na kadhalika. Baadhi ya mambo yanayojikita katika utamaduni wa Kigisu yalikuwa mazuri na kwa hiyo hayakukinzana na Uislamu. Wagisu waliosilimu walitakiwa kuendesha maisha yao kulingana na mwenendo wa maisha wa dini hiyo. Kwa hivyo, ijapokuwa mambo mengi yanayounda utamaduni wa Kigisu yanaruhusiwa katika Uislamu, namna yanavyofanyika ndiyo swala linalozua ugomvi.

Ifahamike kwamba kutokana na juhudi za viongozi wa kidini za kusambaza elimu ya dini miongoni mwa waumini wa Kiislamu, kumekuweko mabadiliko katika baadhi ya mienendo. Kwa mfano, zamani yeyote aliyetaka kuwakirimu jamaa zake, ilimbidi awaalike kisha amchukue ng'ombe kutoka zizini na kumpiga hadi kifo. Kitendo hicho kilijulikana kama *khukhupa luukhoonyo*. Baada ya kumchuna ng'ombe huyo, kila mtu alipewa nyama yake. Siku hizi mtindo umebadilika na wale wanaotaka kuwakirimu jamaa zao kitamaduni huwaalika na kisha wanaweka ukamba kwenye shingo ya ng'ombe kama ishara ya kumnyonga. Baadaye humchinja ng'ombe huyo kulingana na mafundisho ya Uislamu. Tukichukuwa mfano wa tohara, Uislamu huruhusu kitendo hicho lakini tatizo lililopo ni kwamba huku Uislamu ukishurutisha kuwa kitendo hicho kifanyike katika siku ya saba, utamaduni wa Kigisu hushurutisha kuwa anayetahiriwa lazima awe amebaleghe kwani uvumilivu wa kisu cha ngariba ni kielelezo cha ushujaa na utuuzima.

Wagisu wengi wangali wanashikamana na mambo ya utamaduni wao, wengine wengi wamelegeza ukamba kidogo kwa kuchanganya mambo hayo na ni wachache sana ndio walihitari kuendesha maisha yao kulingana na mwenendo wa Uislamu. Kutokana na hali hiyo, migogoro hujitokeza Maimamu wanapozungumzia maswala yanayohusiana na utamaduni katika

khutuba zinazowasilishwa kila Ijumaa. Ili kupata uelewa bora wa migogoro hiyo na chanzo chake, mtafiti ametoa maelezo kuhusu utamaduni wa Wagisu.

#### 1.2.5.1 Tohara

Miongoni mwa mila za Wagisu kuna kuwatahiri vijana wa kiume katika miaka shufa, sherehe ambayo inajulikna kama *Imbalu.* Kitendo cha kutahiriwa ni cha lazima miongoni mwa Wagisu na ikitokea kwamba kuna aliyekwepa tohara, atatafutwa popote pale alipo mpaka atimize faradhi hiyo kwa kulazimishwa. Mtu huyo akifariki kabla ya kutahiriwa, hatazikwa mpaka maiti yake itakapopashwa tohara. Wagisu wametambulikana sana na ada ya tohara kwa sababu ni sehemu ya utamaduni wao tofauti na jamii zilizotajwa hapo juu. Katika musimu wa tohara, baadhi ya Waislamu hujitosa katika mambo ya utamaduni kikamilifu na kuyapiga kisogo mafundisho ya dini yao.

Inaaminika kuwa mgisu aliyetahiriwa mwanzo ni Bwana Fuuya aliyekuwa akiishi katika kijiji cha Bukhuumwa, tarafa ya Bungokho. Bwana Fuuya alifanya hivyo kutokana na shinikizo la mke wake Nabarwa kutoka katika jamii ya Wakalenjin. Inasemekana kwamba Nabarwa alidai kwamba wazazi wake wasingemruhusu kuolewa na mtu ambaye hajatahiriwa. Kutokana na shinikizo hilo, Fuuya aliandamana na Nabarwa akatambulishwa kwa wazazi wake na kisha akatekeleza mahitaji yao. Inaaminika pia kwamba walipojaaliwa watoto wa kiume, Fuuya aliwaalika wakwe zake kuja Ugisuni ili wasaidie katika kuwatahiri wapwa zao.

Ifahamike kuwa mwanzoni tohara haikuwa na mambo mengi yaliyohusishwa nayo kama ilivyokuwa katika siku za baadaye. Kuimba nyimbo, kucheza ngoma kwenda msituni na mengine mengi hayakuwepo hapo awali. Dhana hiyo ilichukuwa sura mpya na istilahi *imbalu* hueleweka vyema miongoni mwa Wagisu kuliko tohara.

Tohara miongoni mwa Wagisu si kitendo cha kukatwa tu ngozi iliyoko kwenye tupu ya mwanamume bali imeambatanishwa na masharti anuwai. Ndiyo maana mwanamume yeyote anayetahiriwa hospitalini hastahiki kupewa heshima. Kijana anatakikana awe na umri wa zaidi ya miaka 15 na aruhusiwe na baba yake (Mubaje,1995). Hivyo ni kutokana na imani kwamba mtu wa umri huo, anaweza kustahamili maumivu yatokanayo na kisu cha ngariba na pia

kutokana na mazoea, kwani tangu jadi umri huzingatiwa sana. Wakati wa kutahiriwa, haifai kwa mtahiriwa kuvunja mwiko kwa kulia, kutetemeka, kutikisa kiungo chochote cha mwili au kukunja uso. Akilia, itambidi mzazi wake atoe kafara kwa kuchinja mbuzi ili kuwaridhisha mababu (Mubaje,1997).

Tohara lazima ifanyike katika miaka shufa kama vile 2008, 2010, 2012 kwa utaratibu huo. Miaka isiyofuata mpangilio huo huchukuliwa kama ya wanawake. Kijana anayejiandaa kwa tohara ana mavazi rasmi ambayo anatakikana ayavae. Mavazi hayo ni kaptura na mkanda uliotengenezwa kutokana na ngozi na kupambwa kwa simbi, shanga zinazovaliwa badala ya shati, kofia iliyotengenezwa kutokana na ngozi ya tumbili na *bitsenze* ambavyo huvaliwa kwenye mapaja na kuchacharisha kila anapocheza. Katika shughuli hiyo, mvulana anatakikana kuimba au kuimbiwa nyimbo za ushujaa na kucheza ngoma huku akishangiliwa na watu, wanaume kwa wanawake na akiwatembelea jamaa na marafiki kuwaarifu rasmi kwamba ameamua kutahiriwa. Kawaida katika safari hiyo, kijana huzawadiwa pesa, kuku, mbuzi na hata ng'ombe. Wale ambao hawana cha kuwapa wakati huo, hutoa ahadi ya kuwazawadia baada ya sherehe.

Katika misafara hiyo, wasichana na wanawake hucheza ngoma kwa kutingisha viuno huku wanaume wakishangilia na kuruka juu na kumwamrisha kijana kukanyaga ardhi kwa nguvu zake zote. Ngoma ikikolea, wanawake huvua nguo zao zilizofunika sehemu za juu za miili yao na kutikisa viuno, matiti na mabega yao kufuata mdundo wake huku wakizifunga nguo hizo viunoni. Kitendo hicho huwavutia sana baadhi ya wanaume ambao hubabaika na kuanza kuwaandama wanawake hao mpaka wapate kusemezana. Siku tatu kabla ya kufanyika kwa tohara, pombe huandaliwa na kijana hupakwa mwili wote unga wa mtama uliorovywa ambao hutumika katika kuitengeneza hiyo pombe. Ifikapo siku ya tohara, mbuzi huchinjiwa uani, kijiti cha mita mbili unusu husimikwa na kijana husimamishwa kwenye gunia na kupakwa ule unga pamoja na *buuse.* Moyo na mapafu ya mbuzi huyo hubandikwa kwenye kijiti hicho ili kuwaridhisha mababu. Kutoka hapo, atapelekwa kwa wajomba zake ambako pia atachinjiwa mbuzi au ngombe na akirudi, atapelekwa kwenye msitu ulioko kijijini mwake ambako inaaminika kuwa kuna mizimu ya babu zake waliofariki zama za kale. Msitu huo hurejelewa na baadhi ya Wagisu kama *shiilindwa* na baadhi yao kama *mwiigoya* au *mwiikoya*. Huko atapakwa

udongo kisha asindikizwe kuelekea kwenye uwanja mkubwa wenye msongamano wa vijana na washangiliaji wao, wacheze ngoma na huku wakirushiwa pombe hadi alasiri.

Kitendo cha kwenda kwenye msitu huo kinalenga kuwaridhisha mababu ili kijana awezeshwe kustahamili maumivu. Kutoka kwenye uwanja huo, kila kijana atapelekwa nyumbani kwao huku akipigiwa makelele na kuonywa dhidi ya kisu cha ngariba. Baada ya kuwasili kwenye ua la nyumba yao, kijana huyo ataruka juu ya gunia lililowekewa mchanga kisha aweke fimbo katika shingo lake na aishikilie kwa mikono yake. Akisaidiwa na mwenzake, ngariba ataikata ngozi ya juu na ndani ya sehemu ya siri ya kijana huyo. Wakati huo wote, watu watakuwa wamemchungulia kijana huyo na kuutazama uso wake wakimhimiza kustahmili maumivu. Akishamaliza kazi yake, ngariba huyo atapuliza filimbi na watu watatawanyika wakishangilia kwa vifijo na nderemo. Baada ya kufurahikia ushindi wa kijana, jamaa na marafiki watamwendea huko uani alikokalishwa ili wampe zawadi kama ishara ya kumshukuru kwa ushupavu, ujasiri na ukomavu wake.

Tohara huchukuliwa kama asasi ya kuwakomaza vijana wa kiume miongoni mwa Wagisu. Kwa hiyo ikisha fanyika, ngariba humkalisha chini kijana huyo akamnawisha mikono kisha akampa wosia ambao anatakikana autilie maanani. Kwanza, anampongeza kwa ukomavu alioufikia na kumhakikishia kwamba ameshakuwa mtu mzima kwa hiyo hachukuliwi tena kama mtoto. Pili, anamhimiza kuchukuwa jambia na jembe aende akalime ili apate kumudu maisha. Zaidi ya hayo anashauriwa kujenga nyumba, kuoa, kufanya kazi kwa bidii na kutunza familia yake ipasavyo.

Ifahamike kwamba sherehe ya uzinduzi wa musimu wa tohara hufanyika tarehe mosi Agosti kila baada ya miaka miwili katika kitongoji cha Mutoto kilichoko umbali wa maili moja kutoka mjini Mbale. Inaaminika kwamba Mgisu wa kwanza kutahiriwa Bwana Fuuya aliishi mahali hapo alipohama kutoka Bukhumwa kijiji chenye umbali wa maili sita mashariki mwa Mutoto na kilioko karibu na mlima Wanaale. Ni baada ya uzinduzi huo ndipo sherehe za tohara hupamba moto kote Ugisuni.

Kama ilivyoelezewa hapo awali, Waislamu wanaofuata mila ya Kigisu hushiriki kikamilifu katika miviga ya tohara kiasi kwamba wanayapiga kisogo mambo yanayohusu dini katika miaka

shufa. Hivyo ni kusema kwamba wanaihama misikiti na kuiacha sala muda huo wote, wengine wanatengeneza pombe na kuinywa, wanachinja mbuzi ili kuwaridhi babu zao. Vitendo vya zinaa na kuwanajisi wanawake hukithiri muda huo kwa sababu wanaume na wanawake hutangamana na kucheza ngoma pamoja. Ajali za barabarani hukithiri kwa sababu wachezaji ngoma hawataki kupisha magari na zaidi ya hayo watu hao huwa kero kwa jamii kwa sababu vurugu hutanda na kuwakosesha raha wale wasioshangilia sherehe hiyo (Mahojiano na Imamu Abubakar, tarehe 20 Mei, 2012).

#### 1.2.5.2 Ndoa

Ndoa ni asasi nyingine inayounda utamaduni wa Wagisu. Mwanamume huoa kulingana na uwezo wake na utamaduni unamruhusu kujipatia zaidi ya mchumba mmoja. Hivyo ni kwa sababu anatakikana kuzaa watoto wengi wa kike na wa kiume ili kupanua ukoo wake. Aidha, watoto wa kiume huchukuliwa kama *luusoola* kwa vile hawaendi mbali na nyumbani kwao ilhali wasichana wakirejelewa kama *imono* kwa sababu huolewa mbali na nyumbani kwao na kuendeleza koo na jamii tofauti. Jambo la uwezo katika ndoa huzingatiwa hasa kutokana na imani kwamba babake mvulana huchangia tu katika kutoa mahari ya mke wa kwanza lakini akioa mke mwengine yeye mwenyewe ndiye anayegharamia mahitaji hayo.

Zamani wazazi ndio waliokuwa na jukumu la kuwatafutia vijana wao wake wazuri. Kulikuwepo mpango maalum uliojulikana kama *khuuselela.* Kulingana na mpango huo, wazazi walikuwa wakipeleka posa nyumbani kwa msichana ambaye alipendeza kwa sura na maadili na endapo msichana huyo atakuwa mdogo kwa umri kiasi kwamba hawawezi kujua tabia yake, basi watazingatia tabia ya wazazi wake. Kutokana na kubadilika kwa mienendo ya maisha, siku hizi vijana ndio wanaojitafutia wachumba.

Kuna wanaopata wachumba kutoka ngomani kama ile inayorejelewa kama *inemba* inayochezwa mwanzoni mwa mwaka unaofuata mwaka wa tohara na kuna wengine hukutana nao tu njiani na kuwapeleka nyumbani kwao. Katika hali hizo mbili, wasichana hukamatwa kwa nguvu na kulazimishwa kuingia katika maisha ya ndoa.

Baada ya kuishi na mwanamke kwa miezi kadhaa, kijana huandika barua ya kujitambulisha kwa wakwe zake na kuwaarifu kwamba yeye ndiye aliyewaibia binti yao. Barua hiyo huambatanishwa na pesa za kuwapoza wazee na hupelekewa baba au kaka au baba yake mdogo. Iwapo msichana atapatikana kama hajavunja ungo au bado mdogo, mama mkwe atatangulia kwenda kuchukua *iyabwana* kabla ya wazazi wa kiume kwenda kudai mahari. Akishapata ng'ombe au mbuzi huyo, atachukuwa sehemu na kuwagawia jamaa zake wa kike sehemu iliyobaki.

Baada ya miezi kadhaa, baba mkwe humwaandikia barua akimwarifu kwamba watakuja kumtembelea kwa minajili ya kuchukua mahari. Siku hiyo ikifika, wazee kutoka upande wa msichana watakuja kwa babaake mvulana wajadiliane na wazee kutoka upande wa kijana juu ya mahari. Wakishakubaliana, wazee hao watapewa mahari hayo na baada ya karamu waliyoandaliwa kumalizika, wataaga na kurudi nyumbani.

Katika jamii ya Wagisu, mtu akijaliwa watoto wa kike, huchukuliwa kuwa tajiri. Hivyo ni kwa sababu wakiolewa, babaake atapata mahari ambayo ni ng'ombe watatu au wanne, mbuzi watatu na jogoo mmoja kutokana na ndoa ya kila binti. Lita ishirini za mafuta ya taa huwa miongoni mwa vitu vitolewavyo kama mahari. Mahari hayo yanaweza kutolewa katika sura hiyo hiyo au kwa pesa taslimu.

Wageni wakirudi nyumbani, baba mkwe huwagawia sehemu ya mali hiyo na kutunza iliyobaki kwa manufaa ya watoto wake wa kiume. Endapo binti yake atajaliwa watoto wa kiume, babu yao au mrithi wake atawazazawadia kutokana na ng'ombe hao wakisha fanya uwamzi wa kutahiriwa. Lakini huyo msichana akishindwa kuolewa na kurudi nyumbani kwao, basi mumewe atarejeshewa ng'ombe na mbuzi wake.

Kwa mujibu wa mila na desturi za Wagisu, wachumba wakijaaliwa mtoto ni lazima apewe jina la mmojawapo ya jamaa zake kutegemea uana wake. Endapo mtoto huyo atalia kwa siku kadhaa na igunduliwe kwamba hakuugua, basi itasemekana kwamba kuna marehemu miongoni mwa jamaa zake aliyesahaulika na kwa hiyo anamliza mtoto. Wakati mwingine jamaa huyo anaweza kuwajia wazazi wa mtoto au babu au bibi yake katika ndoto. Akisha fanya hivyo, basi mtoto

huyo itabidi apewe jina la mtu huyo ili anyamaze na apate siha nzuri. Itokeapo kwamba msichana hakujaliwa mtoto, wazazi wake watapata wasiwasi na kuenda kwa waganga au kuangalia ni nani miongoni mwa jamaa zake ambaye hayuko radhi na binti yao.Wakisha mgundua mtu huyo basi watamshauri binti yao aende kwake na zawadi ili amwombe radhi. Lakini wakishindwa kumpata mtu wa kumshutumu, watampeleka kwa waganga.

#### 1.2.5.3 Kifo na Mazishi

Kifo ni tukio la huzuni miongoni mwa Wagisu kama ilivyo katika makabila mengine. Kwa hiyo kikitokea, jamaa na marafiki hujumwika na kukaa matangani kwa siku kadhaa kuwahani wafiwa na kushiriki katika majonzi. Watu hulia vilio vya kwi kwi na maiti huwekwa sebuleni ili kila anayetaka kumwona apate wepesi wa kufanya hivyo. Baadhi ya jamii za wagisu, hususani zile zilizoko sehemu za kaskazini mwa mkoa huo, humtoa maiti ndani ya nyumba punde tu baada ya kufariki na kumweka huko barazani. Maiti hazikwi ila baada ya kuhakikisha kwamba jamaa zake walioko mbali wamekuja. Ni muhali mazishi kufanyika katika siku ambamo kifo kilitokea. Aghalabu mazishi hufanyika baada ya siku moja, mbili au tatu. Mtu akifariki, shughuli ya kilimo husitishwa na ni baada ya siku tatu za maombolezi ndipo sherehe ya kushika mipini na kuchoma majani ya ndizi waliyokuwa wakilalia hufanyika.Tukio hilo, huchukuliwa kuwa tukio la kutoa kisirani cha ugonjwa katika nyumba ya marehemu. Siku hiyo, chakula huandaliwa na wale wanaotoka mbali wanaweza kurudi nyumbani kwao baada ya kula chakula hicho. Ikiwa marehemu alikuwa mfugaji, au tajiri, basi ng’ombe atachinjwa siku hiyo.

Baada ya siku arobaini tokea siku ya mazishi, jamaa watakusanyika tena na karamu itaandaliwa. Katika siku hiyo, mrithi hutambulishwa na watoto wa marehemu wanashauriwa kumtii mrithi huyo kama walivyokuwa wakimtii baba au mama yao. Aidha, mali ya marehemu hugawiwa watoto wa marehemu wa kiume na ndugu zake.Wanawake hawapewi chochote. Baada ya karamu hiyo, jamaa wote waliokuwa wamebaki matangani hurudi kwao na wafiwa huanza kuchapa kazi zao kama kawaida.

#### 1.2.5.4 Mirathi

Miongoni mwa Wagisu, mirathi ni haki ya watoto wa marehemu wa kiume na jamaa zake wa kiume tu**.** Wake zake na binti zake hawastahiki kuchukuwa sehemu yoyote ya mali aliyoiacha.

Wakati mwingine ndugu zake wa kiume ndio huirithi mali ikiwa marehemu hakuacha watoto waliokomaa kiakili. Lakini katika hali kama hiyo, wao huirithi kama wakuza watoto walio mayatima hivi kwamba wakikomaa, watawakabidhi mali yao. Pale ambapo hakuna mrithi, ndipo watakaporuhusiwa kuirithi wao wenyewe. Mke wa marehemu hana haki katika mirathi bali naye hurithiwa na mmoja wapo wa ndugu za marehemu kwa sababu ya mahari yaliyotolewa na mumewe. Akikataa, atalazimishwa kwenda nyumbani kwa wazazi wake (Buyera, 2008).

**1.2.5.5 Dini**

Majilio ya Uislamu na Ukristo nchini Uganda katika robo ya mwisho wa karne ya kumi na tisa, yaliwakuta waafrika na imani zao za kijadi. Wagisu walikuwa wakiabudu mizimu ambayo ilikuwa ikirejelewa kama *kimisaambwa* au *baakuuka*. Ufanisi katika shughuli mbalimbali ulikuwa ukihusishwa na miungu hao. Kwa hiyo, kabla ya kutenda jambo lolote, walikuwa wakimchinja mbuzi na kuangalia utumbo ili kuhakikisha iwapo miungu wako radhi au la. Wakati wa mavuno walikuwa hawali ila baada ya kutoa sadaka kwa miungu kutokana na nafaka mpya. Ingawa hali ya kuabudu mizimu imepungua, lakini baadhi ya watu wangali wanaizingatia sana katika maisha yao ya kila siku. Hivyo ni kwa sababu kuna watu ambao, pamoja na kuwa Waislamu au Wakristo, huwajengea miungu vijumba nyumbani kwao. Katika vijumba hivyo, sadaka za kila aina hupelekwa (Abubakar, 2012).

Ulinganifu kati ya utamaduni wa Wagisu na Uislamu katika ada ya tohara hudhihirisha kuwa kuna mgogoro unaojitokeza kulingana na nguzo ya kwanza ya Uislamu. Kwa mujibu wa nguzo hiyo, kila muumini anapaswa kutilia maanani kwamba hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad ni mtume wake. Kwa hiyo, kitendo chochote cha ibada kama vile kusali, kutoa sadaka, kuchinja, kutoa nadhiri, kutafuta kinga na kadhalika yapaswa kielelekezwe kwa Mwenyezi Mungu pekee. Utamaduni wa kigisu kwa upande mwingine hulenga kuiridhi mizimu ya mababu kwa vitendo kama hivyo ili kijana anayeandaliwa kwa tohara apate kubarikiwa. Aidha, Uislamu huwataka waumini kuwatahiri wana wao katika siku ya saba au wakiwa na umri mdogo lakini utamaduni wa kigisu hukinzana sana na mafundisho hayo. Kwa mujibu wa utamaduni huo, kijana huruhusiwa kutahiriwa akiwa amebaleghe. Aghalabu vijana wanaotahiriwa huwa na umri wa zaidi ya miaka kumi na nane.

Isitoshe, vijana hao hutahiriwa mbele ya watu huku wakiangalia sehemu zao za siri jambo ambalo ni marufuku katika Uislamu.

Ndoa ya Kigisu ni miongoni mwa mambo ambayo pia hupishana sana na mafundisho ya Uislamu na kwa hiyo baadhi ya migogoro inayotokana na matamko ya Maimamu chanzo chake ni mpishano huo. Kwa mujibu wa Uislamu, mwanamke haolewi isipokuwa kutokana na idhini ya mzazi wake na mahari ni mali ya binti yake na ndio ufunguo wa maisha ya ndoa.

Kipengee cha mazishi pia mara nyingi huzua migogoro kwa sababu kinapishana na Uislamu katika mambo kadhaa. Kulingana na mafundisho ya Uislamu, mtu anapofariki hairuhusiwi kutoa vilio vya kwi kwi, kumtoa ndani ya chumba chake wala kuchelewesha mazishi bali kila anayepatwa na msiba lazima avumilie akijua kwamba ni mtihani kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Uislamu huchukuliwa kama mwenendo wa maisha na kwa hiyo humtaka muumini atangulize sheria za dini na siyo utamaduni wake. Katika kufanya hivyo, itamlazimu kila tendo atendalo liwe kulingana na mafundisho ya Uislamu. Pale ambapo matakwa ya utamaduni wake hayakinzani na Uislamu basi anaruhusiwa kuendelea na kitendo chake. Lakini panapotokea ukinzani anatakikana kuyatupilia mbali na kuufwata Uislamu. Ifahamie kwamba mafudisho ya Uislamu hupatikana katika Kur’ani Tukufu na hadithi za Mtume Muhammad (SAW).

Khutuba zinazotolewa msikitini zinatakikana zisheheni mafundisho hayo ili waumini wapate kunufaika na ujumbe wa kila wiki. Khutuba hizo hazitolewi katika ombwe tupu bali hutolewa kulingana na muktadha wa maisha halisi yanayorejelewa. Maswala ya kiuchumi yanayozungumziwa sana katika khutuba ni kuwa mwaminifu, kutokuwa mdanganyifu unapowauzia watu bidhaa anuwai, kuepukana na mikopo yenye riba na kutowanyang’anya watu mali yao kwa kupandisha bei au kwa namna nyengine yoyote. Maswala ya kijamii yanayogusiwa sana ni malezi ya watoto, ndoa ya Kiislamu, mahusiano na jirani na binadamu wenzako, ukarimu, uungwana na kadhalika.

Khutuba zikigusia maswala kama yale yanayoenziwa na baadhi ya Wagisu na Waislamu kwa ujumla, wataathirika kwa namna mbalimbali. Athari hizo mara nyingi hutegemea mazingira

ambamo khutuba zinawasilishwa. Katika mazingira ya mijini, mafunzo ya dini hutolewa kila siku misikitini na kwa hiyo watu wengi wameweza kubaini umuhimu wa mafunzo ya dini katika maisha yao. Zaidi ya hayo watu hao hutangamana na wenzao kutoka makabila mbalimbali ambao huathiri mitazamo yao. Kwa upande mwingine, utamaduni umekita mizizi vijijini kwa hiyo, Imamu yeyote ambaye anatoa mafundisho yanayokinzana na mazoea yao, nia yake itatiliwa shaka na anaweza kuchukuliwa kama adui wa mila zao.

Ifahamike kwamba Maimamu ambao wanazungumzia sana maswala ya utamaduni wa Kigisu na jinsi unavyokinzana na Uislamu ni Wagisu wenyewe. Kinachowapelekea kufanya hivyo ni imani kwamba Uislamu ni mwenendo wa maisha na kwa hiyo ni vyema Waislamu Wagisu wajitambulishe kama Waislamu na wafuate utamaduni wa dini yao. Pili, wao ndio wanaouelewa utamaduni wa jamii yao na vipengee vinavyokinzana na Uislamu kuliko Maimamu wa kutoka katika jamii nyingine. Tatu, ingawa hujuma wanazofanya dhidi ya utamaduni wa jamii zao huwakera baadhi ya Waislamu wenye mielekeo ya kijadi, lakini wana kinga kutokana na jamaa zao. Kwa hiyo, si rahisi kwa mtu yeyote kuwashambulia kwa namna inayoweza kuwadhuru.

### 1.2.7 Malalamishi Dhidi ya Maimamu

Mahubiri yanayotolewa misikitini na Maimamu siku ya Ijumaa wanapowasilisha khutuba, inasemekana yana athari hasi kwa wasikilizaji. Kwa mujibu wa Tegle (2008), baadhi ya wahubiri huonyesha uhasama dhidi ya Israel na Wayahudi ambao wanawalaumu kwa kupanga mashambulizi ya tarehe 11 Septemba 2001 huko Marekani na vita dhidi ya Iraq. Tegle alidai kwamba lawama dhidi ya Marekani na vyombo vya habari vya kimagharibi zimekuwa zikitolewa katika khutuba za Ijumaa, katika nchi mbalimbali za Kiislamu. Ameeleza kwamba khutuba hizo vilevile zinawakaripia viongozi wa Kiislamu na wanavyuoni.

Crow (2000), akimnukuu Dale (1997) alisema kwamba kuongezeka kwa juhudi za kupigania haki za kidini na pia kuongezeka kwa makundi yanayopigania mageuzi tangu mwaka ya 1980, kulisababishwa na ugunduzi wa dhana anuwai na kujitokeza kwa mitandao ya kimawasiliano na vitendo ambavyo vinaelekea kuwaathiri Waislamu wote na kuchonga mwelekeo wa tafakuri za kisasa za Mwislamu. Alibaini kwamba mapinduzi ya Iran ya 1978-1979, yalizindua matumizi ya

istilahi za Kiislamu ili kuelezea hisia za wengi juu ya siasa. Akielezea athari za usemi wa Kiislamu, Crow alisema kwamba mbali na matini takatifu, kuna usemi chipukizi ambao ni muhimu kwa fikra za wataalamu wapya wa kidini na hadhira yao, kidini na kisiasa. Alitaja vitabu vya Kiislamu ambavyo vyauzwa kwa bei rahisi, kanda za redio na video ambazo zina hotuba mbalimbali, usemi wa kuwashawishi wasikilizaji na mijadala juu ya mada mbalimbali, kama aina mbalimbali za usemi wenye uwezo mkubwa wa kuchochea na kutoa motisha kwa hadhira inayoongezeka.

Mubaje (1995) alishughulikia swala la tohara ya kijadi *Imbalu* akiilinganisha na tohara ya Kiislamu. Alitaja kwamba kulingana na utamaduni wa Kigisu, tohara ya Kiislamu imepungukiwa na mambo Kadhaa ya kijadi hususani miviga inayoambatanishwa nayo na kwamba baadhi ya Wagisu Waislamu wanashindwa kutimiza matakwa ya mihimili ya desturi za tohara ya kijadi na Kiislamu katika jitihada yao ya kupatanisha kati yake. Alikariri kwamba kuna mfarakano, hali ya kutoaminiana na wasiwasi miongoni mwa Wagisu Waislamu na wasiokuwa Waislamu jambo ambalo mara nyingi husababisha chuki, mapigano na kuvunjika kwa familia.

Ifahamike kwamba baadhi ya Wagisu huchukizwa na matamko ambayo yanapinga ada ya kuwatahiri vijana kwa kufuata desturi za kijadi. Matamko kama hayo hujitokeza mara nyingi katika khutuba za Ijumaa sana sana katika msimu wa tohara inayokuwepo katika mwaka shufa miongoni mwa Wagisu.

Tibenderana (2006) alibaini kwamba ni jambo la kawaida kuwasikia Maimamu wakiwasilisha khutuba za uchochezi wakilaani serikali ya NRM kwa kuweka sheria na sera zinazopingana na Uislamu. Alidai kuwa Maimamu hao huchochea hadhira kupigania alichokiita haki zao.

Uchunguzi awali umeonyesha kwamba nchini Uganda kumekuweko malalamishi dhidi ya Maimamu ambayo pia chanzo chake ni matamshi wanayotoa katika khutuba za Ijumaa. Malalamishi hayo yalionyesha kwamba baadhi ya Maimamu huwasilisha khutuba zinazowakashifu waumini wa Kiislamu hadharani. Walidai kuwa baadhi ya Maimamu wamekuwa wakiwavunjia heshima kwa kuwatusi. Malalamishi mengine yalihusu kutotafsiri khutuba hizo katika lugha wanazozielewa waumini jambo ambalo limewapelekea kupoteza

wakati wao kwa vile hawanufaiki na mafunzo ya kila wiki. Khutuba hizo hufuata mtindo na mbinu za kijadi ambazo haziendani na usasa hivi kwamba mara nyingi huwachukiza wasikilizaji na kuwachosha.

Waumini hao wamekuwa wakiwasilisha manung'uniko yao kwa mashekhe wa Tarafa na pia kwa Kadhi wa Wilaya, wakitaka Maimamu hao wahamishwe au wafutwe kazi au wapelekwe vyuoni ili wapate mafunzo juu ya mbinu mwafaka za kuwasilishia khutuba za Ijumaa. Viongozi hao wamekuwa wakiitikia malalamishi hayo kwa kuwahamisha Maimamu na kuwafuta kazi wengine pindi wanapopata ushahidi juu ya madai hayo.

Malalamishi hayo dhidi ya Maimamu yalithibitisha kuwa kulikuwa na tatizo la khutuba na kwamba baadhi ya khutuba hizo hazikuafiki matakwa ya waumini. Utafiti huu, kwa hiyo, ulishughulikia suala hilo ili kuona namna Maimamu walivyotumia lugha walipotoa mahubiri yao siku ya Ijumaa na jinsi Maamuma walivyoathirika nayo.

## 1.3 Mada ya Utafiti

Khutuba za Ijumaa zina maadili ya kijamii ambayo kimsingi jamii ya waumini wa Kiislamu wanaozisikiliza hufaidika nayo sana. Hata hivyo, kumekuweko madai miongoni mwa Waislamu kwamba maadili hupitishwa kwa lugha inayowakashifu Waislamu na pia yenye athari hasi kwa waumini wa Kiislamu ingawaje inawasilisha ujumbe wa Mungu. Hata hivyo sifa mahsusi za lugha hii zilizokuwa zikizua malalamishi kama hayo hazikuwa zikijulikana na athari zake kwa waumini zilikuwa hazijawekwa bayana. Kwa hiyo, kazi hii ilikuwa na azma ya kubainisha vitendo neni vilivyojitokeza katika lugha hiyo na athari mbalimbali zilizotokana na lugha ya khutuba kwa waumini hao.

## 1.4 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa:

i. Kubainisha vitendo neni katika lugha ya khutuba za Ijumaa zinazotolewa misikitini.
ii. Kudhihirisha athari za vitendo neni hivyo kwa Waislamu wanaosikiliza khutuba hizo.
iii. Kupendekeza matumizi ya vitendo neni vilivyodhihirika kupendelewa zaidi na waumini katika khutuba.

### 1.5 Maswali ya Utafiti

i. Je, lugha ya khutuba zinazotolewa misikitini imesheheni vitendo neni maalum?
ii. Je, vitendo neni vinavyojikita katika lugha ya khutuba za misikitini vina athari hasi kwa Waislamu wanaosikiliza khutuba hizo?
iii. Je, pana uwezekano wa kutumia vitendo neni vinavyopendelewa zaidi na Maamuma na ili kuleta athari chanya kwa waumini wanaosikiliza khutuba?

### 1.6 Sababu na Umuhimu wa Utafiti

Mada hii ilichaguliwa kwa sababu ya manung'uniko kutoka kwa Maamuma kuhusu namna ambavyo khutuba za Ijumaa zilivyokuwa zikiwasilishwa. Kutokana na manung'uniko hayo, ilibainika kwamba kulikuwako vitendo neni katika khutuba za Ijumaa ambavyo havikushughulikiwa kadri tujuavyo. Vitendo neni navyo vilikuwa na athari zake ambazo hudhihirika wasikilizaji wanapotoa hisia na maoni yao kuhusu usemi. Hata hivyo, athari za vitendo neni katika khutuba hizo zilikuwa hazijachunguzwa. Utafiti huu utakuwa nyongeza kwa tafiti za hapo awali zilizofanywa juu ya vitendo neni endapo vitendo neni katika khutuba za Ijumaa na athari zake kwa waumini zitabainishwa. Utawafaidi wachanganuzi usemi kwa vile unatarajiwa kuweka msingi thabiti ambao wanaweza kuutumia kuchanganua vitendo neni vya usemi wowote ule na kudhihirisha athari zake kwa wasikilizaji. Aidha, utawafaa Maamuma ambao wanasikiliza khutuba za Ijumaa kila Juma endapo tatizo la utafiti huu litatatuliwa na kupelekea athari za khutuba kuwa chanya. Vivyo hivyo, Maimamu watanufaika kwa vile utafiti huu utaonyesha hisia za Maamuma zinazotokana na nguvu za matamko yao. Kwa kutumia hisia hizo wanaweza kutathmini uwasilishaji wao wa khutuba na kuuboresha ili kufanikisha shughuli nzima ya kuwasilisha ujumbe kwa waumini ipasavyo.

Kwa kuzingatia kwamba khutuba za Ijumaa zina jukumu la kusambaza maadili yenye athari chanya kwa jamii, utafiti kama huu unaoshughulikia matumizi ya lugha ni muhimu. Hii ni kwa sababu lugha, kama chombo cha kuwasilishia maadili, inatakikana itumike kuwavutia wanajamii ili waendelee kupata mafunzo yatakayowafaa katika maisha yao ya kila siku.

## 1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulishughulikia tu khutuba za Ijumaa wala sio khutuba za siku nyingine kama vile khutuba za Idi na ndoa kwa vile malalamishi ambayo yalipelekea utafiti huu kufanyika hayakujihusisha nazo bali yalifungamana na khutuba za Ijumaa pekee. Maimamu thelathini wa misikiti ya sala ya Ijumaa katika wilaya nne za mkoa mdogo wa Bugisu Mashariki mwa Uganda na Maamuma mia moja na wanane kutoka katika misikiti hiyo walihojiwa. Sababu ya kufanya hivyo ni kwamba misikiti isiyosaliwa sala ya Ijumaa haina khutuba za namna hiyo. Aidha, kwa kuzingatia kigezo cha wakati na ubora wa kazi ya utafiti, sehemu zilizochaguliwa zitakuwa mfano kwa khutuba za nchi nzima. Zaidi ya hayo vitendo neni vya kutosha, nia yake na athari zake zilitarajiwa kutoka kwa watu hao.

### 1.8 Ufafanuzi wa Istilahi

**Athari :** Ni mabadiliko yanayojitokeza katika hisia za wasikilizaji kutokana na matamko ya wazungumzaji. Mabadiliko hayo yanaweza kuwa chanya au hasi kutegemea nguvu za tamko au nia ya mzungumzaji.

**Jinsi:** Ni istilahi iliyotumika pia katika muktadha wa uneni na hurejelea ufupi, ushahidi na upangiliaji sawa wa maneno ambao mzungumzaji anapaswa kuzingatia ili kuzuia utata unaoweza kujitokeza.

**Kiasi :** Ni kiwango toshelezi cha matamko kinachohitajika katika mawasiliano baina ya watu.

**Kihesabu**

**Kusihi:** Ni istilahi iliyotoholewa kutokana na neon la Kiarabu *swaha* lenye maana ya kuwa sahihi na kukubalika.

**Masharti ya**

**Sampuli:** Ni kundi dogo la watu au vitu linalotumika katika uchunguzi ili kutoa taarifa inayohusu kundi kubwa.

**Tamko:** Sauti au maneno yenye maana fulani.

**tepu:** Hii ni sehemu ya kinasa sauti yenye nambari za kile kilichorikodiwa.

**Uafiki au umwafaka:** Ni hali ya kuoanisha kati ya matamko ayatoayo mzungumzaji na mazungumzo yanayoendelea au hali halisi ya mambo.

**Ubora:** Hii ni hali ya ya kutoa matamko sahihi yaliyopambwa na ushahidi toshelezi.

**Udokezi:** Hurejelea maana anayokusudia mzungumzaji kutokana na tamko lake.

**Ufelisiti:** Haya ni masharti ambayo kulingana na mwanafalsafa na mwendelezaji wa NKN Searle tamko la mzungumzaji halina budi kuyatimiza ili kitendo kifanikiwe au la. Hurejelewa pia kama masharti ya ufaafu.

**Vitendoneni:** Matamko yanayotendesha ama kuashiria vitendo Fulani Kama vile Kuuliza, kuomba, kuamrisha, kuonya, na kadhalika.

# SURA YA PILI
# MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.1 Utangulizi

Sura hii ilimulika tafiti zilizo na uhusiano wa namna moja au nyingine na utafiti huu. Ilionyesha kufanana au kutofautiana kuliopo kati ya kazi hii na zile za wataalamu wengine na pengo la kielimu lililotakikana kujazwa. Mambo yaliyoangaziwa ni pamoja na mahubiri ya dini ya Kikristo, matumizi ya lugha katika uhamasishaji wa wanawake kuhusu haki zao, athari ya lugha ya matangazo kwa vijana wa kike wa shule za upili, rejista ya kidini na mtindo wautumiao katika sala na mambo mengine, umilisi wa kimawasiliano, mikakati ya kiusemi katika usemi wa benki, matumizi ya lugha katika utangazaji, mbinu za kiisimu katika matangazo, uwasilishaji bora wa khutuba, toni na malalamishi katika khutuba za Ijumaa, utata wa lugha, ufungamano wa kileksia katika khutuba za Ijumaa, matumizi ya usemi wenye amani, matumizi ya lugha inayoeleweka kwa watu wa kawaida, mtindo katika hotuba mbalimbali, kaida za uzungumzi wa hadharani, fani ya khutuba na maendeleo yake miongoni mwa Waarabu na sheria za kimtindo kwa mwandishi wa kibiashara. Fauka ya hayo, imeangazia Nadharia ya Kitendo neni (NKN) na Nadharia ya Udokezi (NU) kwa kuelezea waasisi wa nadharia hizo, mihimili yake na jinsi zilivyotumika kuongoza utafiti huu.

## 2.2 Maandishi Kuhusu Vitendo Neni

Ogolla (2007), alichunguza namna lugha inavyotumika kuhamasisha wanawake kuhusu haki zao. Alibainisha vitendo neni vinavyojitokeza katika matamko ya kuwahamasisha wanawake na jinsi wanavyoweza kuathirika nayo. Aliongozwa katika utafiti wake na NKN iliyoasisiwa na Austin (1962) akapata data yake na kuichanganua kwa kutumia mbinu ya wingi-idadi na kiuthamano. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kwamba lugha inayotumika wakati wa uhamasishaji wa wanawake ina vitendo neni na athari chanya kwa wasikilizaji. Matokeo hayo yalionyesha kuwa madai kwamba lugha inayotumika kuwahamasisha wanawake kuhusu haki zao ilikuwa na athari hasi hayakuwa na mashiko kwa sababu kilichogunduliwa kutokana na utafiti ilikuwa ni kinyume chake. Pamoja na hayo, kazi ya Ogolla ilihusiana na utafiti huu kwa vile ilidhihirisha vitendo neni vya lugha  ya uhamasishaji wa wanawake na athari zake.

Kwa upande mwingine kazi hiyo inatofautiana na utafiti huu kwa sababu ilishughulikia matumizi ya lugha katika uhamasishaji wa wanawake juu ya haki zao ilhali mtafiti huyu

aliazimia kuchunguza matumizi ya lugha katika khutuba za misikitini akitumia Nadharia ya Udokezi sambamba na Nadharia ya Kitendo Neni ili kudhihirisha vitendo neni na maana yake. Zaidi ya hayo, mtafiti alihusisha hadhira tofauti na ile ya Ogolla ambayo ilikuwa waumini wa Kiislamu, wanaume kwa wanawake, ambao ndio Maamuma wanaosikiliza khutuba za Ijumaa. Isitoshe, kazi hiyo ilishughulikia hoja kwamba wahamasishaji wa wanawake hutoa matamko fulani. Matamko hayo huwahamasisha wanawake na kuwafanya watende matendo fulani yanayowapelekea kupata haki zao. Hii ina maana kwamba waathirika hawalalamiki juu ya matamko ya wahamasishaji kama inavyobainika katika swala la utafiti huu ambapo matamko ya wawasilishaji wa khutuba ndiyo yanayozua malalamishi. Fauka ya hayo wanaolalamika ni wasikilizaji wa khutuba ilhali katika kazi ya Ogolla wanawake wanaohamasishwa hawalalamiki. Kama kuna wanaowanyima wanawake haki zao basi tunaweza kusema kuwa pengine hao ndio wameathirika na taathira hasi kutokana na kuzindukana kwa wanawake na kuwafanya wadai yale yote waliyonyimwa. Lakini kwa upande wa khutuba msisitizo ni kuwa kuna athari hasi ambazo zinapelekea ujumbe wa Ijumaa usipokelewe vyema miongoni mwa waumini wanaozisikiliza.

Hata hivyo kazi yake ilikuwa na faida kubwa katika utafiti huu kwa sababu ilimsaidia mtafiti katika kuainisha vitendo neni vilivyojitokeza katika khutuba za misikitini na athari zake kwa hadhira pamoja na nia ya Maimamu katika kutoa matamko yao. Aidha, mtafiti alitumia nadharia na mbinu alizotumia Ogolla katika kukusanya na kuchanganua data yake. Isitoshe, kazi hiyo ilisaidia pia katika kudhihirisha iwapo athari za vitendo neni vinavyojitokeza katika khutuba ni hasi au chanya.

Walya (1995) alichunguza mikakati ya kiusemi katika usemi utumikao kwenye benki wanapowasiliana wafanyakazi wa benki na wateja wao, akitumia NKN. Alichunguza pia athari za usemi huo katika mawasiliano baina ya wadau hao. Uchunguzi wake ulionyesha kuwa wafanyakazi wa benki hutumia lugha kwa nia ya kupata wateja na kuwashawishi waweze kufurahia huduma zao. Kazi ya Walya inahusina na utafiti huu kwa kiwango fulani kwa sababu ilichunguza usemi na jinsi mawasiliano yanavyoendeshwa na kutimia baina ya wadau wawili ambao wanashiriki katika uzungumzi. Vivyo hivyo, ilichunguza athari za usemi kwa wateja zinazotokana na lugha ya wafanya kazi wa benki.

Tofauti iliopo kati ya kazi hizo mbili ni kwamba utafiti wa Walya haukujihusisha na khutuba na jinsi ambavyo zinaathiri wasikilizaji. Aidha yeye alidhihirisha kuwa lugha ya wafanyakazi wa benki ililenga kutoa athari chanya wakati utafiti huu ulidhamiria kudhihirisha vitendo neni vya khutuba na athari zake kwa wasikilizaji pasina kujali iwapo ni chanya au hasi. Aidha, kazi hii ilijikita katika muktadha wa msikitini na imetumia Nadharia ya Udokezi (NU) kama nadharia saidizi kutambulisha maana ya vitendo neni ili kupata athari zake kwa hadhira. Utafiti wa Walya uliifaa sana kazi hii kwa sababu ulitumia NKN ijapokuwa katika muktadha tofauti. Mtafiti alifaidika nayo katika kudhihirisha vitendo neni vyenye athari hasi katika khutuba. Aidha aliweza kupendekeza matumizi ya vitendo neni vinavyoelekea kufurahiwa na wasikilizaji wa khutuba za Ijumaa ili kuondoa athari hasi.

Wardhaugh (1992) alishughulikia utendaji na uzungumzaji na kuelezea kwamba matamko yanaweza kutazamwa kama vitendo vya aina mbalimbali, huku kubadilishana kwa matamko yanayorejelewa kama mazungumzo yakitazamwa kama vitendo na siyo tu kubadilishana kwa maneno. Akimnukuu Grice (1975), alisema kwamba mazungumzo yanaweza kuendelea kati ya mtu mmoja na mwengine kwa sababu tunatambua malengo ya kawaida katika mazungumzo na njia mahsusi za kutekeleza malengo hayo. Alieleza kwamba katika mazungumzo yoyote, kuna mambo maalum yanayowezekana katika wakati maalum. Hivyo ni kwa sababu kuna vizuizi vinavyodhibiti uzungumzaji ambavyo humwekea mzungamzaji mipaka kuhusu nini anatakikana atambue. Akifafanua kanuni shirikishi ya Grice, Wardhaugh alisema kwamba katika mazungumzo, mtu anatakikana kutilia maanani sheria ya kijumla kwamba anashiriki na msikilizaji au wasikilizaji wake katika shughuli ambayo ni yenye manufaa kwa wote, manufaa ambayo ni kuelewana.

Kazi ya Wardhaugh inahusiana na utafiti huu kwa sababu iligusia utendaji unaohusisha matamko na kuelezea sheria zinazoweza kutumika ili kutambua maana ya mzungumzaji. Ingawa haikujihusisha na khutuba, ilitufaa sana kwa upande wa nadharia. Hivyo ni kwa sababu ilituwezesha kuchanganua vitendo neni ambapo athari zake kwa wasikilizaji zilibainishwa kutegemea maana waliyoitambua kutokana na matamko ya khutuba. Kanuni shirikishi ya Grice iliyotumika katika utafiti huu, ilifafanuliwa vizuri na Wardhaugh na hivyo kutoa mwelekeo

mzuri. Kazi ya Wardhaugh ilimwezesha mtafiti kubaini iwapo wasikilizaji wa khutuba humwelewa mzungumzaji kulingana na nia yake.

Steven (2009) alichunguza hali ya utendaji wa maneno katika usimulizi wa Biblia. Alitumia NKN kuchanganua usimulizi wa Sam2, 15.23-16.14; akizingatia kategoria za vitendo neni za Searle. Alisema kwamba uamilifu wa lugha kiutendaji hujitokeza katika usimulizi pale ambapo wahusika wanapoitikia uzungumzi wa kila mmoja wao kana kwamba wanaitikia vitendo. Alieleza kuwa vitendo kadhaa huelezewa kuwa yale yasemwayo na wahusika kama vile Daudi anapozungumza juu ya Yhwh katika 15.16, mafunzo yake kwa Hushai katika 15.34 na mashtaka ya Ziba dhidi ya Mephibosheth katika 16.3.

Utafiti wa Steven ulidhihirisha kuwa NKN ni kifaa faafu kwa uelewa wa usimulizi wa Biblia hususani usimulizi kama ule uliopo katika Sam2, 15.23-16.14 ambao hutilia mkazo nguvu za uzungumzi. Utafiti huo unahusiana na kazi hii kwa sababu ulichunguza utendaji kazi wa matamko. Fauka ya hayo uliongozwa na NKN katika kuelezea vitendo neni katika usimulizi wa Sam2 moja wapo ya vitabu vya Biblia. Kwa kufanya hivyo ulijihusisha na usemi wa kidini ambao kazi hii ilishughulikia ili kuonyesha athari zake kwa hadhira.

Hata hivyo, utafiti wa Steven hupishana na utafiti huu kwa sababu umeangazia matini andishi na hali kazi hii imemulika khutuba za ijumaa zinazowasilishwa msikitini. Pamoja na hayo utafiti wa Steven uliifaa sana kazi hii kutokana na jinsi ambavyo NKN na kategoria za vitendo neni zilivyotumika kuchanganua data na kujadili matokeo ya utafiti. Mtafiti alitumia NKN kutokana na ugunduzi kwamba ni kifaa faafu kwa uelewa wa usemi ili kubaini nia, nguvu na athari za vitendo neni vinavyojitokeza katika khutuba za Juma.

## 2.3 Maandishi Kuhusu Ufasiri wa Lugha ili Kupata Maana Zinazokusudiwa

Yule (1985) akizungumzia swala la usemi, alieleza kwamba maswali yanayojitokeza sana katika uchunguzi wa lugha ni yale yanayohusiana na jinsi lugha inavyotumika na siyo ni mambo yepi yanayojenga lugha. Alisema kwamba, ingawa katika kufasiri ujumbe maumbo na muundo wa kiisimu hutegemewa, lakini watumiaji wa lugha wana elimu iliyo zaidi ya hayo. Alibaini kwamba mwambatano wa matini, kueleweka kwake, matendo ya kawaida yatendwayo na

wazungumzaji na kanuni shirikishi ambayo huonyesha jinsi tunavyotumia maarifa aslia, huchangia sana ufafanuzi wa usemi.

Ingawa kazi ya Yule ilijikita katika eneo sawa la uchanganuzi wa usemi, haikugusia swala la vitendo neni katika khutuba za Ijumaa na jinsi vinavyoathiri wasikilizaji. Hata hivyo, ilitufaa sana kwa upande wa nadharia na mikabala kwa sababu ilituongoza katika kubaini athari za vitendo neni vya khutuba za Ijumaa kwa waumini. Kauli yake kwamba katika kufasiri ujumbe , watumiaji lugha wanategemea elimu ambayo ni zaidi ya ujuzi wa maumbo na muundo wa kiisimu ilichochea sana uchunguzi huu katika kugundua jinsi wasikilizaji wa khutuba wanavyofasiri matamko ya maimamu na hivyo kuathirika nayo.

Geis (1982) alichunguza lugha ya matangazo hasa yale ya televisheni huko Marekani. Alimulika mbinu za kiisimu zinazojitokeza waziwazi katika matangazo kama vile matumizi ya neno “saidia” katika vishazi. Alikariri kwamba kwa ujumla watangazaji hupendelea matumizi ya lugha isiyodhahiri na madai yenye upendeleo kuliko lugha iliyodhahiri na madai yasiyokuwa na upendeleo. Utafiti wa Geis ulikuwa muhimu kwa kazi hii pamoja na kwamba haukugusia lugha ya khutuba za Ijumaa. Hivyo ni kwa sababu ulimulika matumizi ya lugha isiyodhahiri ambayo hupatikana pia katika usemi wa khutuba na huweza kufasiriwa na NKN na NU ambazo zimeongoza utafiti huu. Aidha ulimwezesha mtafiti kubaini iwapo athari za vitendo neni vilivyojitokeza katika khutuba za Ijumaa zilitokana na matumizi ya maneno maalum kama mbinu inayolenga kuibua athari mahsusi. Tofauti na kazi hii, utafiti wa Geis ulishughulikia matumizi ya mbinu za kiisimu zinazojitokeza katika matangazo ya huko Marekani ilhali kilichoangaziwa na utafiti huu ni vitendo neni na jinsi vinavyowaathiri waumini wa Kiislamu nchini Uganda.

Goldingay (1995) alishughulikia mifano ya ufasiri wa maandiko matakatifu na kubaini kuwa wahubiri hamsini wanaweza kuzua mitazamo tofauti kuhusu matini moja. Aidha alieleza kuwa maana ya matini ya Biblia hupatikana kutoka kwa hadhira na kwamba matini moja inaweza kueleweka kwa njia mbalimbali na wasomaji mbalimbali.

Kazi ya Goldingay ni muhimu sana kwa utafiti huu kwa sababu imeonyesha kwamba mitazamo kadhaa inaweza kuzuliwa na wahubiri anuwai. Ijapokuwa imeshughulikia matini ya Biblia, ilitumika kama msingi wa kueleza iwapo maana ya matini ya Kur'ani na hadithi za mtume Muhammad (SAW) zinazotumika na wahubiri wa Kiislamu katika khutuba za Ijumaa inaweza kupatikana kutoka kwa Maamuma wanaozisikiliza na pia kueleweka kwa namna mbalimbali na Maamuma hao. Kazi hiyo inaelekea kurandana na NKN nadharia iliyoongoza utafiti huu ambayo kwa muujibu wa waasisi wake msikilizaji au hadhira huathirika na usemi au matini kulingana na jinsi alivyoitambua nia ya mzungumzaji. Aidha, inarandana na Nadharia ya udokezi inayoangazia sheria zinazotawala uzungumzi ambazo kufuatwa kwake na kukiukwa pia huashiria maana Kadhaa wa Kadhaa.

**2.3 Maandishi Kuhusu Matumizi ya Lugha Inayozuia Athari Hasi**

Crystal na Davy (1973) walichunguza mtindo wa Kiingereza ambapo walishughulikia rejista mbalimbali ikiwemo ya dini. Walieleza kwamba dini ya Ukristo hutumia mpangilio maalum katika mtindo, sala, na kadhalika. Wametoa mifano ya mtindo huo ambayo inadhihirisha Kiingereza cha kale kimaandishi na kimuundo. Wamedhirisha kuwa unukuzi wa Bibilia hutokea katika miktadha ya kidini na kwamba mahubiri huakisi lugha ya ibada za kanisani (*liturgical language*). Walieleza kuwa kumekuwako shinikizo kubwa litokanalo na mielekeo ya matumizi ya lugha faafu na ambayo inaeleweka kwa urahisi. Walipendekeza kwamba inapasa kuchagua lugha ambayo haipingwi na watu hasa katika muktadha wa kidini na pia kuepukana na lugha inayoweza kuwakanganya watu.

Kazi ya Crystal na Davy inahusiana na utafiti huu kwa vile inajihusisha na lugha ya dini. Mtafiti aliitumia kuangalia iwapo matamko kutokana na Kur'ani au duru nyingine zinazoaminika hunukuliwa na Maimamu wanapowasilisha khutuba na iwapo wanajiepusha na matamko yanayoweza kuwakanganya waumini. Vilevile, ilimwezesha mtafiti kuonyesha iwapo kutofanya hivyo huweza kuzua athari hasi miongoni mwa wasikilizaji. Halikadhalika, ilimwezesha kuainisha lugha ya mahubiri ya Kiislamu ya siku ya Ijumaa. Vile vile ilisaidia katika kutoa mapendekezo juu ya lugha inayopendelewa zaidi kutumika katika khutuba jambo ambalo lilichangia katika utatuzi wa tatizo la utafiti huu.

Pamoja na hayo kazi ya Crystal na Davy inatofautiana kwa kiasi fulani na kazi ya mtafiti huyu kwa sababu ilishughulikia mtindo wa Kiingereza na pia rejista ya dini ya Kikristo. Mtafiti alijikita zaidi katika muktadha wa msikitini ambapo alichunguza vitendo neni katika khutuba za Ijumaa na athari zake kwa Waumini.

Leech na Svartvik (2002) walishungulikia sarufi ya kimawasiliano ama umilisi wa kisarufi wa lugha ya Kiingereza. Kazi yao iliangazia umilisi wa kisarufi, umilisi wa kiisimu-jamii, na umilisi wa stadi za kimawasiliano. Walieleza kwamba kuwasiliana, kwa maoni yao, hugubiza kuwasiliana katika uzungumzi na uandishi. Walisisitiza kuwa kuna uhitaji wa aina hiyo ya sarufi ili kuelezea na kutoa mifano ya aina mbili hizo za matumizi ya lugha. Wataalamu hao walibainisha kwamba lugha ya Kiingereza sio tu njia ya kutoa na kupokea taarifa, bali pia ni njia ya kuwasiliana kati ya watu. Kwa mtazamo huo, lugha mara nyingi huelezea hisia na mielekeo ya mzungumzaji, na mzungumzaji huyo aghalabu hutumia lugha kuathiri mielekeo na tabia za wasikilizaji.

Kazi ya wataalamu hao ilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa sababu imemulika umilisi wa lugha katika vipengee vyake vyenye kulenga uendelezaji wa mawasiliano. Isitoshe, imegusia swala la matumizi ya lugha kwa madhumuni ya kuathiri wasikilizaji. Mtafiti aliitumia kazi yao kama msingi wa kuonyesha namna lugha inavyotumika katika khutuba za Ijumaa na kudhihirisha jinsi lugha hiyo inavyowaathiri wasikilizaji. Leech na Svartvik (2002) walimulika matumizi ya lugha kiujumla na kwa hiyo hawakuangazia muktadha wa msikitini, kazi ambayo mtafiti huyu aliishughulikia.

Ogilvy (1963) alifanya utafiti wake juu ya lugha inayotumika katika utangazaji na kutaja maneno ambayo aliyachukulia kuwa ni yenye ufanisi katika matangazo. Maneno hayo ni pamoja na: *mpya, huru, ajabu, zuri, bora, bora zaidi*. Alieleza kwamba lugha ya matangazo hukusudiwa kutoa ushawishi unaolenga kuuza na kutumia maneno kutenda kazi kwa weledi na uangalifu ili kufanikisha madhumuni mahasusi. Kazi hii ilikuwa na manufaa kwa utafiti huu kwa sababu ilitumika kama kielelezo cha matumizi ya lugha kwa namna ambayo itafanikisha uwasilishaji wa ujumbe wa khutuba za Ijumaa kwa wasikilizaji wake. Mtafiti aliitumia kupendekeza matumizi ya lugha inayoelekea kupendelewa zaidi na wasikilizaji wa khutuba za Ijumaa. Hivyo ni kwa

sababu kulingana na utafiti wa Ogilvy, ikiwa matumizi ya maneno fulani yanaweza kufanikisha madhumuni ya mzungumzaji, ina maana kwamba baadhi ya maneno yakitumika huenda yakazua athari zisizopendelewa na wasikilizaji. Ijapokuwa kazi hiyo kwa kuangazia lugha ya matangazo inatofautiana na utafiti huu, ni wazi kwamba inafanana nao katika kadhia nzima ya kutendesha maneno ili kufanikisha yale anayodhamiria mwasilishaji wa ujumbe.

Alkhairo (1998) alizungumzia uwasilishaji bora wa khutuba ya Ijumaa. Alibaini kwamba ijapokuwa khutuba na sala ya Ijumaa ni asasi zenye nguvu zilizoanzishwa ili kujenga jamii mbalimbali, lakini hazina athari kubwa kwa waumini wa Kiislamu. Hivyo ni kwa sababu katika nchi nyingi zisizozungumza Kiarabu, khutuba huwasilishwa kwa Kiarabu hali ya kuwa idadi kubwa ya wasikilizaji hawakielewi. Alilalamika kwamba katika baadhi ya jamii za Kiislamu, matendo yao ya kila siku yanakosa maadili na mafunzo ya Uislamu. Alieleza kwamba kiini cha tatizo hilo ni mbinu zisizofaa za kufundishia Uislamu. Alikariri kwamba khutuba inaweza kutumika kama chombo cha kuleta mabadiliko iwapo mbinu za kisayansi na nadharia ya kimawasiliano vitatumika kuiwasilisha. Aidha alipendekeza mada za khutuba ziteuliwe kulingana na kadhia zinazowafaa watu katika maisha yao ya kila siku kama nyongeza juu ya mada za kiimani. Vilevile alipendekeza kwa Maimamu jinsi ya kupangilia, kuandika na kuwasilisha khutuba.

Kazi ya Alkhairo ilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa sababu imeshughulikia uwasilishaji bora wa khutuba na mambo ambayo inafaa yatiliwe maanani katika uwashilishaji huo. Mtafiti aliitumia kutoa mapendekezo juu ya matumizi ya vitendo neni vinavyopendelewa zaidi na wasikilizaji wa khutuba za Ijumaa.  Zaidi ya hayo, kazi hiyo ilimwezesha mtafiti kufikia mapendekezo juu ya mada ambayo watafiti wanaweza kuishughulikia. Hata hivyo, kazi ya Alkhairo inatofautiana na kazi hii kwa sababu haikuangazia vitendo neni vinavyotokana na khutuba na athari zinazoakisiwa na malalamishi ya wasikilizaji kuhusu khutuba.

Maoni ya Alkheiro ni kwamba khutuba hazina athari kwa wasikilizaji kwa maana kwamba matendo ya Waislamu ya kila siku hayaakisi mafundisho ya Kiislamu kutokana na kuwasilishwa kwake kwa lugha wasiyoielewa. Mtafiti katika kazi hii hakuchunguza athari za namna hiyo. Hivyo ni kwa sababu malalamishi yaliyopelekea utafiti huu kufanyika yalitokana na maoni

kwamba maamuma waliwaelewa vyema maimamu wao ila tu walikerwa na sifa fulani za lugha iliyotumika. Zaidi ya hayo haikuchunguza khutuba kwa mkabala wa NKN na NU, kazi ambayo utafiti huu uliifanya.

Tegle (2008) mchambuzi wa maswala ya Mashariki ya kati, aliandika makala yake juu ya khutuba za Ijumaa. Alieleza kwamba khutuba zinazowasilishwa misikitini katika ulimwengu wa Kiislamu, hulenga wasikilizaji na jamii ya Waislamu duniani kwa ujumla. Alitaja kwamba ijapokuwa baadhi ya serikali zinasimamia wahubiri ili kuzuia athari za wale wenye msimamo mkali, na ijapokuwa baadhi ya khutuba za Ijumaa zina msimamo wa wastani, kwa mara chache khutuba hizo zina toni na matamshi yenye chuki dhidi ya ulimwengu wa kimagharibi na Mayahudi. Alipendekeza kwamba ili kuelewa vyema ulimwengu wa Kiislamu, ulimwengu wa kimagharibi inafaa utilie maanani ujumbe unaowasilishwa katika khutuba za Ijumaa.

Makala ya Tegle ilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa sababu imegusia swala la khutuba za Ijumaa na walengwa wake. Ijapokuwa imetaja athari za khutuba hizo, haikuzielekeza kwa wasikilizaji wake ambao ni waumini wa Kiislamu jambo ambalo lilishughulikiwa na utafiti huu. Pamoja na hayo, makala yake ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu imegusia suala la uzuaji wa athari hasi ambazo yumkini zikawapata wasikilizaji wa khutuba na suala la kuelewa ujumbe ili kuuelewa ulimwengu wa Kiislamu. Makala hayo yalimpa mtafiti msukumo wa kutaka kugundua ni nini kilichomo kwenye ujumbe wa khutuba na ni athari gani ambazo zinataka kuzuia ambazo yawezekana waumini wa Kiislamu nchini Uganda wanaweza kuwa wanaathirika nazo.

Anderson na Trudgill (1990) wakielezea utata wa istilahi “lugha mbaya” walisema kwamba ni vigumu kujua namna watu wanavyojenga fikra zao juu ya lugha na kwamba fikra hizo yumkini zina uhusiano na fikra za kimsingi katika utamaduni kuhusu usafi kwa ujumla. Walitoa mfano wa lugha ya Kiarabu cha Kurani na lugha ya kikale ya Biblia ambazo huchukuliwa na waumini wa Kiislamu na Kiprotestanti kuwa lugha safi kwa kuwasilishia mahubiri na sala.

Kazi ya Anderson na Trudgill ilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa sababu imegusia swala la lugha na mahubiri ama khutuba. Kazi hiyo ilimsaidia mtafiti kutambua iwapo matumizi ya

Kiarabu au lugha nyingineyo huathiri wasikilizaji wa khutuba za Ijumaa. Zaidi ya hayo, ilimshawishi mtafiti kuchunguza ni nini hasa wanachokusudia maamuma wanapodai kuwa maimamu hutumia lugha mbaya wanapowasilisha khutuba za Ijumaa.

Adelakun (1997) alichunguza ufungamano wa kileksia katika khutuba za Ijumaa akitumia mkabala wa uchanganuzi wa kiusemi. Alichunguza khutuba za Ijumaa katika msikiti wa Ibadan huko Nigeria kwa lengo la kutaka kugundua iwapo kuna ufaafu katika nyenzo za kuwasilishia ujumbe kwa hadhira. Aligundua kwamba Maimamu walitumia mbinu ya uradidi, maneno ya kijumla yanayorejelea lekzimu maalum na pia mbinu ya kusisitiza. Alitoa mfano wa maneno yaliyorudiwarudiwa kama vile *Allah, He, the Vanguard of Islam, We, Holy Quran, praise, favours, muslim students, some money, the boy, discovered, claimed himself*. Alieleza kwamba mfuatano wa lekzemi hufanikisha lengo hili kwa kuonyesha matini hiyo kama mojawapo ya matini zilizokitwa katika utanzu wa khutuba za Waislamu. Ingawa utafiti wa Adelakun ulishughulikia uchanganuzi wa khutuba za Ijumaa na kudhihirisha vipashio vya kileksia vinavyochangia ufanikishaji na uwasilishaji wa ujumbe, haukuangalia namna ambavyo matamko ya khutuba yanavyoweza kuwaathiri wasikilizaji. Kwa sababu hiyo, utafiti wetu uliazimia kuziba mwanya huo.

Hata hivyo, utafiti wa Adelakun ulikuwa muhimu kwa kazi hii kwa sababu ulisaidia kubaini mbinu zinazotumika katika kuwasilisha khutuba na kuwafanya wasikilizaji watambue maana ya mzungumzaji. Utambuzi wa namna hiyo ndio unaozua taathira ambazo mtafiti alilenga kuzidhihirisha. Aidha, kazi ya Adelakun ilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa sababu ilitumika kuchunguza iwapo vitendo neni vinavyojitokeza katika khutuba na athari zinazozuliwa hutokana na suala zima la kuwepo au kutokuwepo kwa ufaafu katika nyenzo za kiusemi za kuwasilishia ujumbe.

Crow (2000) alishughulikia swala la matumizi ya usemi wa Kiislamu wenye amani. Alieleza kwamba kwa vile harakati za Waislamu zimepamba moto katika ulimwengu wa Kiislamu, kuna haja ya kuwa na usemi ambao unaweza kuyafanya mafundisho ya kidini yawe yenye kuendana na hali na changamoto za kisasa. Alishikilia kwamba kufanya hivyo, ndiyo njia pekee ya kufanikiwa kwao katika juhudi za kujikomboa kutokana na wale wanaowanyanyasa.

Alipendekeza kwamba Waislamu wenye uwezo wa kuangalia hali ya nyakati zao kihakiki wanawajibika kuzalisha usemi aliouelezea kuwa mpya. Alitoa hoja kwamba ikiwa watu binafsi kama vile Bin Laden wanaweza kusajili watu kutoka Afrika, Ulaya mashiriki, ulimwengu wa Kiarabu na Asia, na wakafanikiwa kuratibu shughuli zao kupitia mitandao ya kimawasiliano ya kimataifa, basi kuna uwezekano wa kutumia mitandao hiyo hiyo kusambaza usemi mbadala ambao umekitwa katika maadili ya kimsingi ya Uislamu yanayoendeleza ushirikiano katika utengano, haki, huruma na heshima kwa wanadamu.

Ijapokuwa makala ya Crow imeshughulikia swala nyeti la matumizi ya usemi wa Kiislamu kama ule tunaoangazia, haikugusia athari za usemi wa khutuba kwa waumini wa Kiislamu, kazi ambayo tuliishughulikia katika utafiti huu. Pamoja na hayo, kazi hiyo inastahiki sifa kwa sababu, kwa vile ilipendekeza aina ya usemi ambao unaweza kutumika ili kuendeleza utangamano wa wanadamu bila kujali madhehebu yao, dini zao, tamaduni zao au mbari zao, iliufaa sana utafiti huu.

Aidha, kazi hiyo ilichangia pakubwa katika utambuzi wa nyenzo mojawapo ya kuwasilisha ujumbe wa kidini ambayo ni khutuba ziwasilishwazo kwenye mimbari misikitini. Vilevile, kazi ya Crow ilipiga hatua zaidi ikapendekeza kutazamwa kwa usemi wa Kiislamu kwa jicho la kihakiki kwa minajili ya kusambaza maadili yanayoweza kuwa na athari chanya kwa jamii yoyote ile. Isitoshe, malalamishi ya Maamuma dhidi ya matamko ya Maimamu yumkini yametolewa kutokana na matumizi ya usemi usiokuwa wa amani na urafiki. Ikiwa hivyo ndivyo ilivyo, basi kazi ya Crow ni muhimu kwa vile inapendekeza suluhisho kwa mgogoro unaoweza kuwepo katika ulimwengu halisi.

Maher (1998) anashikilia kwamba fikra na maadili ya Kiislamu yapaswa kuelezewa katika lugha ambayo inaeleweka kwa watu wa kawaida na kutekelezwa na taasisi ambazo zinaweza kushughulikia maswala ambayo ni muhimu kwa watu. Kazi ya Maher inahusiana na utafiti huu kwa sababu ilimulika maadili ya Kiislamu ingawa haikugusia khutuba na athari zake.

Hata hivyo mawazo yake yanaweza kuchangia katika kuondoa tatizo la  wenye taathira hasi kwa hadhira. Hivyo ni kwa sababu, inachangia katika kumwongoza mtafiti kubaini mapendekezo

yanayoweza kuibua hisia zinazopendelewa zaidi na wasikilizaji katika khutuba. Yumkini kutoelezewa kwa fikra na maadili ya Kiislamu katika lugha inayoeleweka huzua athari hasi miongoni mwa hadhira ya maamuma inayosikiliza khutuba.

Bloommaert (1990) alichunguza baadhi ya vipengee vya mtindo katika hotuba za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kilichomsukuma kufanya hivyo ni madai kwamba balagha ya Kiswahili huakisi umbo mwambatano lenye maana changamani zilizofungamanishwa katika dhana za kijadi za Kitanzania na mpangilio wa kijamii na maumbo ya kisasa ya mitazamo ya kisiasa yanayokubalika kimataifa. Alieleza kuwa ingawa uchanganuzi wa kimtindo kwa kawaida huchukuliwa kuwa unaakisi sifa maalum za lugha inayochanganuliwa, lakini uchanganuzi wake ambao ilikuwa uonyeshe sifa maalum za Uafrika katika usemi wa kisiasa ulidhihirisha mchakato wa umataifishaji wa usemi wa kisiasa kisemantiki na kipragmatiki. Alibaini kuwa mtindo wa Kiswahili wa kisiasa umejitokeza kama aina ya usemi uliokitwa baina ya Uafrika na usasa. Alitoa hoja kwamba ikiwa siasa barani Afrika huakisi umbo mseto la uambatani katika maadili na desturi za kijadi na kimataifa, basi usemi wa kisiasa wa Kiafrika lazima uonyeshe dalili za mwambatano huo wa kiusemi kimseto. Alitumia mkabala wa Lakoff na Chafe kuibuka na sifa zinazoonyesha jinsi ya kudhibiti taarifa. Kwa kutumia sifa hizo alichanganua matini nne za hotuba za Mwalimu Nyerere zilizowasilishwa kwa Kiswahili ambazo vichwa vyake ni Nguzo Tano za Ujamaa, Moyo Kabla ya Silaha, Uhuru na Maendeleo na Elimu ya Kujitegemea. Alichanganua hotuba hizo na kudhihirisha kuwa Nyerere alitumia mitindo tofauti tofauti kutegemea vibadiliki viwili. Kibadiliki cha kwanza ni mada. Pale ambapo Mwalimu alikuwa akitoa taarifa mpya iliyohitaji ufafanuzi na uthibitifu wa hoja zilizojitokeza katika usemi wake, alitumia utanzu wa uandishi.

Kwa upande mwingine utanzu wa uwasilishaji kwa mdomo ulitumika wakati ambapo hotuba hazikutoa taarifa mpya bali zililenga tu kuimarisha na kutilia nguvu matamko yaliyotolewa hapo awali na pia kutafuta uungaji mkono sera za kisiasa na kuisihi hadhira. Kibadiliki cha pili ni hadhira lengwa. Alidhihirisha kuwa Nyerere alitumia utanzu wa kuwasilisha hotuba kutegemea hadhira yake. Pale ambapo aliongea kwa wanajeshi hakuthubutu kutumia ujanja kama ambavyo angeongea mbele ya hadhira nyengine siku ya kusherehekea uhuru. Kwa hiyo alitumia utanzu wa

*usalama* kwa kupangilia yaliyomo na kutumia mtindo tofauti. Alieleza kuwa matini andishi zilionyesha sura tata kutokana na matumizi ya vishazi tegemezi.

Matokeo ya uchanganuzi wa Bloommaert yalionyesha kwamba mtindo alioutumia Mwalimu Nyerere ulitofautiana na ule wa kimagharibi kutokana na matumizi yake ya Kiswahili na kuhamishia msingi wa harakati za kisaiasa huko vijijini. Vinginevyo kazi hiyo ilibainisha kuwa sifa za kimtindo za hotuba za Nyerere zilitokana na misingi ya kimawazo na balagha ya kimagharibi aliyoitegemea kuelezea fikra hizo.

Kazi ya Bloommaert ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu ilishughulikia aina ya usemi ambayo utafiti huu uliangazia. Mtafiti aliongozwa na kazi hiyo kubaini iwapo vitendo neni vinavyojitokeza katika khutuba za Ijumaa hutegemea mada zinazozungumziwa na pia hadhira lengwa. Ingawa utafiti huu haukuangazia siasa, kazi hiyo ilikuwa kielelezo cha sifa za lugha zinazojitokeza katika khutuba zikiwemo sifa za kimtindo ambazo huathiri wasikilizaji kwa namna mbalimbali.

Kathleen, Bruce, Dauglas na Alan (2001) walishughulikia kaida za uzungumzi wa hadharani na kubainisha kuwa kuna elementi nne za uzungumzi za kimsingi ambazo hushirikiana ili kuzalisha mchakato wa uzungumzi ambao ni mzungumzaji, ujumbe, wasikilizaji na muktadha. Walieleza kuwa mzungumzaji ndiye chanzo cha ujumbe na huleta mtazamo wake binafsi na mazoea yake katika shughuli ya kuwasiliana. Walieleza pia kuwa ujumbe huundwa kwa ukweli wa yaliomo, mitazamo ya mzungumzaji na thamani ama faida za mada na kwamba ujumbe huo huwasilishwa kwa kuteua maneno na fikra ambazo hupangiliwa katika ruwaza maalum. Walibaini kuwa msikilizaji hutoa maarifa ya awali, mitazamo na hamu kwa hali ya uneni na pia mwitiko wa kiuneni na usio wa kiuneni kama vile mikunjo ya nyuso, kucheka, kupiga miayo au kuuliza maswali. Walisema kwamba mwitiko hurejelea ujumbe ambao wasikilizaji huutumia kabla, wakati wa au baada ya kutoa hotuba na kwamba muktadha unaweza kuwa mandhari halisi ambamo uzungumzi hutokea au matarajio ya jamii na sheria za kitamaduni ambazo huwepo wazungumzaji na wasikilizaji wanapoingiliana.

Kathleen na wenzie waliendelea kueleza kwamba kwa vile kuhutubia hadhira ni mchakato wa kimaingiliano, kuna majukumu fulani ambayo yapaswa yatekelezwe kwa wasikilizaji. Hivyo ni kwa sababu kila mzungumzaji anapohutubia hadhira huwa anachangia mchakato wa kuijenga jamii na kuathiri maisha ya wengine. Kwa hiyo uzungumzi unahusu kuzingatia kipengee cha maadili ambayo humlazimu kuangalia masuala ya haki na dhuluma, uzuri na ubaya, usahihi na usosahihi. Walidai kuwa maswali Kadhaa yanayohusiana na maadili yatajitokeza wakati wa kuandaa na kuwasilisha hotuba. Walishikilia kuwa kuaminika ni nyenzo muhimu ya kuwaathiri watu wengine. Hivyo ni kwa sababu uaminifu hupewa mtu na ni muhimu hususani katika enzi ambamo makundi mbalimbali ya watu inawezekana yasielewe nia za wenzao.

Vivyo hivyo walishikilia kuwa kuonyesha ubingwa ni muhimu kwani huchangia hali ya kuaminika. Kwa hiyo, ingawa mzungumzaji anaweza kujua mengi kuhusu mada kupitia uzoefu, anashauriwa kuchukua muda asome zaidi, apate ushauri wa mabingwa na aone ni vipengee gani katika mada vinavyoweza kuwafanya wasikilizaji wake washiriki katika uzungumzi. Walidai pia kwamba ufasaha, kujiamini na udhibiti wa sauti navyo huchangia uaminifu kwa sababu huonyesha kuwa mzungumzaji ni mwenye ujuzi. Walishikilia kuwa stadi za kimaongezi hupatikana kupitia mazoezi na kwamba wazungumzaji wengi waliofaulu ni wale wanaowajali wengine hivi kwamba hujihusisha na kukidhi mahitaji ya wasikilizaji wao na kuwatatulia matatizo yao. Aidha walidai kuwa wazungumzaji wazuri hutambua na kuheshimu wasikilizaji na mahitaji yao kwa hiyo, huwa na "hisia za kibalagha". Walieleza kuwa hisia za kibalagha ni kiasi ambacho wazungumzaji:

1. Hutambua kuwa wasikilizaji wao ni tofauti na ni wenye tabia changamani. Ingawa mzungumzaji huyo hawezi kuongea kwa kila mmoja katika hadhira lakini anaweza kuheshimu maoni yao.
2. Huufanya ujumbe wao urandane na hadhira maalum. Wazungumzaji wenye makini huwasilisha maoni yao kwa kila kundi la wasikilizaji wakitumia vithibitisho kutokana na mazoea ya wasikilizaji wao na kutumia lugha faafu kwa kundi linalozungumziwa. Walitoa mfano wa wanasiasa ambao huzungumza juu ya masuala na matatizo ya kawaida.
3. Hutafuta kimaksudi na kuitikia miitiko ya hadhira. Kwa kuitikia mitazamo inayoonyesha kutatizika au kucheka na kupiga makofi, wazungumzaji hutambua hali ya kimaingiliano

katika mawasiliano. Utambuzi wa wasikilizaji, kwa hiyo, ni kiungo muhimu katika mchakato wa uzungumzi.

4. Hutambua kuwa maneno huenda yasiondoe tofauti zilizopo kati ya watu.

Kazi ya Katheleen na wenzie inahusiana na utafiti huu kwa sababu ilishughulikia uzungumzi mbele ya hadhira ambao ndiyo nyenzo ya kuwasilishia ujumbe. Ingawa hawakujihusisha na khutuba za Ijumaa, lakini kazi yao ni kielelezo muhimu kwa jinsi ambavyo khutuba zaweza kuwasilishwa ili kutoa athari chanya kwa hadhira. Mtafiti aliitumia kubainisha iwapo Maimamu huteua matamko na fikra zinazojenga ujumbe wao na kisha kuzipangilia katika mpangilio maalum na iwapo huitikia mitazamo na miitiko ya wasikilizaji ya kiuneni na isiyokuwa ya kiuneni wakati na baada ya kuwasilisha khutuba. Hivyo ni kwa sababu uchanya na uhasi wa khutuba hutegemea mambo hayo. Halikadhalika, kaida za uzungumzi walizozipendekeza zilichangia sana katika kukidhi madhumuni ya utafiti huu ambayo ni kupendekeza matumizi ya vitendo neni vilivyodhihirika kupendelewa zaidi na waumini katika khutuba.

Elia (1989) alishughulikia fani ya khutuba na maendeleo yake miongoni mwa Waarabu. Alionyesha msimamo wake kuwa khutuba ni utanzu ambao daima hulenga kuathiri na kuridhisha, kuelezea imani za khatibu na mtazamo wake juu ya matatizo yanayomkumba mwanadamu. Alieleza kuwa khutuba humtoa msikilizaji katika hali moja na kumpeleka katika hali nyingine na katika itikadi moja hadi nyingine huku ikimpa msukumo wa kutenda tendo zuri ambalo hapo mwanzoni alikuwa na mtazamo hasi juu yake. Alifafanua kuwa lengo la khutuba ni kubadilisha fikra kavu zilizoko kwenye ubongo ili ziwe hisia zenye kumwathiri msikilizaji na kumfanya atende kitendo ambacho mwanzoni hakuweza kukitenda. Alieleza kuwa pamoja na kuwa na ujuzi kwamba heri ni bora kuliko shari, heshima ni bora kuliko unyonge na haki ni bora kuliko batili, lakini ujuzi huo hauwezi kuathiri matendo ya mwanadamu mpaka uwashwe kwa kuibuliwa kwa hisia na hamasa.

Aidha, alibaini kuwa shahidi hawezi kufia dini kwa vile anajua ukweli bali hufanya hivyo kutokana na kuhamasishwa na kujitoa mhanga. Alieleza kuwa matumizi ya picha za kibunifu ni kiungo muhimu katika khutuba kwa sababu huibua taathira Kadhaa na kwamba mwanadamu huathirika na kile akionacho mbele yake kuliko anavyoathirika na fikra zilizoko ubongoni.

Kuhusu misingi ya khutuba alieleza kuwa ubunifu na ujenzi wa khutuba au mtindo wake una hatua mbalimbali zinazopaswa kuzingatiwa. Alitaja kuwa ubunifu huhusiana na mtindo na maudhui ambazo huenda zikamfaidi khatibu wakati anapotunga khutuba yake na kuwa una vipengee viwili- cha ndani na cha nje. Alifafanua kuwa vipengee vya ndani ni pamoja na vithibitisho ambavyo hudhihirisha ukweli wa jambo kwa namna hasi au chanya na kwamba si kitu kingine isipokuwa hoja zilizovishwa picha nyingi za ubunifu na hisia na ambazo hubadilika kutoka katika udhanifu na ubahatishaji hadi uyakinifu wa kisaikolojia na kihisia. Alieleza kuwa kipengee kingine kinachoweza kumfaidi khatibu kwa upande wa kuwaathiri wasikilizaji ni utambulishaji ambapo anatakikana kuchukuwa wazo akalielezea kwa kubainisha sifa zake bainifu zilizodhahiri, au kulielezea kwa kutumia tashbiha na stiara na kuonyesha aina zake ili asiache sura yoyote ya kauli bila kuigusia. Alibaini kuwa kipengee cha nje huwakilisha mada ambayo khatibu anapaswa azigusie ambazo ni pamoja na dini, itikadi na desturi huku akifuata nyayo za watangulizi, akitaja kauli za Maimamu yaani Imam Abu Hanifa, Imam Shafi, Imam Malik na Imam Ahmad, na watu wenye hekima na pia ushahidi kutoka kwenye maandiko na kanuni zilizoandikwa na zisizoandikwa.

Akiizungumzia muundo wa khutuba, Elia (1989) alisema kwamba mhutubu katika enzi ya Jahiliyya alikuwa akiingia moja kwa moja katika mada yake pasina utangulizi kwa sababu ya tabia yake ya uwazi, matumizi ya nguvu katika kudhihirisha hisia na kutokana na ukweli kwamba alisukumwa kutoa khutuba na hisia za kuhamasisha au kuzingatia maumbile. Alieleza kuwa pamoja na hayo, mhutubu alikuwa akiendea na kuiwasilisha khutuba yake kwa namna nzuri. Alibainisha kuwa miongoni mwa mada zilizoshughulikiwa ni mawaidha, wosia na ndoa. Alibaini kuwa kila kabila lilikuwa na mhutubu ingawa makabilia mawili ya Iyad na Tamim ndiyo yaliyokuwa mashuhuri katika fani ya kutoa khutuba. Aidha alieleza kuwa mhutubu wa enzi ya kijahiliyya alikuwa akitegemea sana matumizi ya maneno yenye hekima, methali na ushairi ili matamko yake yapate kumakinika katika nyoyo za wasikilizaji. Akizungumzia khutuba katika enzi ya Uislamu, Elia alisema kwamba mabadiliko ya kisiasa, kidini na kijamii yalipelekea khutuba kuendelea kwa sababu mito mipya ilikuwa ikiwahitaji wahutubu daima ili waupashe umma mafundisho yake. Alisema kuwa mtume (SAW) alikuwa akihutubia hadhira katika Ijumaa, vikao na mikusanyiko mbalimbali kwa lengo la kuridhisha, kufundisha na kutoa mawaidha. Alibaini kuwa mtindo wa khutuba za enzi hiyo ulitofautiana na ule wa enzi ya

kijahiliyya kwa sababu khutuba za Kiislamu zilikuwa na utangulizi, zilibainisha sheria zilizotakikana na aya za Kur'ani, zilisheheni maudhui za mawaidha na mafundisho yaliyolenga kuamrisha mema na kukataza mabaya, kukanya na kuonya dhidi ya kutotimiza faradhi.

Kazi ya Elia ina mchango mkubwa sana kwa utafiti huu kwa sababu ilizungumzia fani ya khutuba na maendeleo yake na jinsi ambavyo fani hiyo inaweza kumwathiri msikilizaji na kumfanya atende kitendo ambacho asingeweza kukitenda kabla ya kusikiliza khutuba. Aidha ilipendekeza mbinu ambazo khatibu anaweza kuzitumia ili kuibua hisia Kadhaa wa Kadhaa. Kazi hiyo ilitumika na mtafiti kuangazia iwapo Maimamu wa miskiti mbalimbali hutumia mbinu alizozipendekeza mtaalamu huyo kuibua taathira hasi.

Pamoja na kuwa kazi ya Elia ilihusiana na khutuba, lakini ilitofautiana na utafiti huu kwa kiwango fulani. Hivyo ni kwa sababu ilishughulikia fani ya khutuba na maendeleo yake miongoni mwa Waarabu  ilhali utafiti huu ulihusu vitendo neni katika khutuba za Ijumaa na athari zake kwa waumini. Yeye aliangazia khutuba kwa ujumla wake ilihali utafiti huu ulijihusisha tu na khutuba za Ijumaa. Vivyohivyo, alishughulikia eneo tofauti ambalo ni Uarabuni na watu tofauti ambao ni Waarabu. Zaidi ya hayo kazi hiyo haikuangazia vitendo neni katika khutuba za Ijumaa na athari zake kwa waumini wa Kiislamu nchini Uganda kazi ambayo ilishughulikiwa na utafiti huu.

Paxon (1985) alizungumzia sheria za mtindo kwa mwandishi wa kibiashara. Alisema kuwa maneno na maana yapaswa vipewe heshima inayostahili. Hivyo ni kwa sababu mzungumzaji au mwandishi asipotumia maneno kwa uangalifu, anaweza kusababisha maafa kama yale yaliyowakumba Wajapani. Alieleza kuwa aliyekuwa waziri mkuu wa Japani kuanzia tarehe 6 Aprili hadi 16 Agosti mwaka wa 1945 hakukuwa mwenye kuimudu lugha yake na kutokana na kukosea katika neno moja, dunia ilibadilika kiasi kisichowezekana kukadiriwa. Alifafanua kuwa nchi ya Japani ilikuwa imepokea andiko lililoitaka kusalimu amri mara moja katika siku za mwisho za vita vya pili vya dunia. Lakini Suzuki alitumia tamko *mokusatu* katika majibu yake lililotafsiriwa kuwa alikuwa amepuuza tangazo la Postdam ilhali alikusudia kumaanisha kwamba hakukuwa na la kusema wakati huo. Alieleza kuwa kwa vile wafasiri wa Kijapani hawakutambua maana aliyokusudia waziri mkuu, tafsiri waliyoifanya ilipelekea Marekani

kutupa mabomu ya atomiki huko Hiroshima na Nagasaki yaliyokomesha vita, yakaua Wajapani zaidi ya 120,000 na kuiingiza dunia katika enzi ya atomiki.

Kazi ya Paxson inahusiana na utafiti huu kwa vile imegusia matumizi ya matamko na jinsi ambavyo yanaweza kuathiri hadhira. Ingawa ilishughulikia matini andishi, lakini kwa kubainisha jinsi tamko lilivyopokelewa na Wamarekani na kuzua athari hasi iliyosababisha madhara makubwa, kazi hiyo ilifaa sana utafiti huu. Mtafiti aliitumia kama kiilelezo ili kuonyesha iwapo kutotambuliwa kwa maana inayokusudiwa kuwasilishwa na Maimamu ndicho chanzo cha athari hasi zinazosemekana kuzuliwa kutokana na matamko yanayojitokeza katika khutuba za Ijumaa.

Wataalamu mbalimbali wamezungumzia swala la dini kama sehemu ya maisha ya mwanadamu. Mbiti (1969) alisema:

‘Dini ni kipashio chenye nguvu zaidi katika msingi wa kijadi na huathiri sana fikra na maisha ya watu’(Taz. Mbiti, 1969 : uk1).

Hivyo ni kusema kwamba hata miongoni mwa watu wanaofuata imani za kijadi, fikra zao na maisha yao huathiriwa na dini.

Mtalamu mwengine aliyeakisi maoni ya Mbiti ni Idowu (1973):

‘Dini iko nasi daima.  Iko nasi kila muda wa maisha- katika nafsi na kuhusiana na matukio ya maisha yawe makubwa au madogo; hujadiliwa kila siku magazetini, kupitia radio na televisheni, na katika mazungumzo yetu. Iko nasi kwa namna isiyoepukika…’(Taz. Idowu, 1973 : uk1).

Maoni hayo yanaonyesha kwamba dini imetuzunguka na kwa hiyo huathiri matendo yetu tuyatendayo kila uchao. Ikiwa dini inasi na tu nayo na kwa hiyo haiepukiki, basi mtaalamu huyo anatushauri tufanye jambo moja la maana ambalo ni kuhakikisha kuwa Ukristo au Uislamu unamtwaa mtu kikamilifu jinsi anavyotwaliwa na dini za kijadi, kama si kuzishinda, ili watu waliobadili dini wakatanasari au kusilimu, wasiendelee kurudi katika imani na vitendo  vya kijadi.

Hii ina maana kwamba kuna haja ya kutumia kila mbinu kuhakikisha kwamba waumini wanajifunza dini yao jinsi inavyotakikana na kutekwa fikra zao kikamilifu ili waridhike na maadili ya Ukristo na Uislamu. Kwa hiyo, waumini wa Kiislamu wanatakikana kujisalimisha mbele ya Mwenyezi Mungu kwa kufuata maamrisho yake. Hata hivyo itakuwa muhali kwa kufanya hivyo iwapo Maimamu hawatojitolea ipasavyo na kutumia lugha mwafaka hususani katika khutuba za Ijumaa, ili kufanikisha juhudi za kuwaelimisha waumini juu ya jinsi wanavyopasa kuendesha maisha yao na kuyaendeleza.

Kwa mujibu wa Mahdi (2001) hali ya umma wa Kiislamu nchini Uganda imezorota kwa sababu mambo muhimu ya utamaduni wa Kiislamu yamepuuzwa na Waislamu. Mifano aliyoitoa kuthibitisha madai yake ni pamoja na maisha ya kifamilia, utamaduni wa miskiti na mfumo wa kisheria. Uchunguzi wake ulionyesha kuwa Waislamu wengi hawafungi ndoa kulingana na mafundisho ya Kiislamu. Alieleza kwamba nikahi hufanyika baada ya mwanamume kuishi na mwanamke kwa muda mrefu bila ruhusa kutoka kwa wazazi. Aidha alieleza kuwa wanawake wa Kiislamu waliotalakiwa na waume zao huolewa na wanaume wengine bila kuzingatia *idda*. Zaidi ya hayo alibaini kuwa kinyume na mafundisho ya Kiislamu, wanaume hutangamana na wanawake katika mikutano na kusalimiana nao kwa mikono. Kuhusu mfumo wa kisheria alisema kwamba Waislamu wa Uganda hawajawahi kuonja mfumo wa sheria za Kiislamu. Alielezea matumaini yake kuwa kufuatia mabadiliko katika vipengee vya katiba kulikuwa na uwezekano wa mahkama za sharia (yaani mahkama za makadhi) kuanzishwa kwa manufaa ya Waislamu. Akizungumzia utamaduni wa miskiti, Mahdi alisema kuwa ingawa Waislamu wanakisiwa kuwa aslimia 25% ya idadi ya wakazi wa Uganda, idadi ya wanaosali sala tano huko miskitini ni ndogo. Alieleza kwamba miskiti hujaa tu siku ya Ijumaa.

Maoni ya Mbiti, Idowu na Mahdi ni muhimu sana kwa utafiti huu kwa sababu yamegusia swala la kuathirika kwa waumini kutokana na mafundisho ya kidini. Pengine athari zinazotokana na matamko ya khutuba chanzo chake ni hali ya waumini ya kutouchukulia Uislamu kama mwenendo kamili wa maisha.

## 2.4 Misingi ya Nadharia

Nadharia ni mawazo , maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani (TUKI,2004).

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Kitendo Neni (NKN) iliyoasisiwa na Austin (1962) na kuendelezwa na Searle (1969) na pia Nadharia ya Umaanishaji ilyoasisiwa ya Grice (1975).


### 2.4.1 Nadharia ya Kitendo Neni

Kwa mujibu wa nadharia hii, tamko hugubiza kitendo. Hivyo ni kusema kwamba mtu anapotoa tamko fulani, huwa pia ametenda kitendo kama vile kuuliza, kuahidi, kuonya, kutaja na kadhalika.

Schiffrin (1995) alieleza kuwa nadharia ya kitendo neni hujishughulisha na maana, matumizi na vitendo ambavyo kwavyo msingi wa kuchanganua usemi waweza kufikiwa. Vitendo neni huchukuliwa kuwa sehemu ya umilisi na NKN huchanganua namna maana na vitendo vinavyowasilishwa.

Austin (1962) alishikilia kwamba katika kutamka sentensi yoyote, mzungumzaji anasemekana kuwa ametenda kitendo ambacho huweza kurejelewa kama nia ya mzungumzaji huyo. Nia hiyo huwa na nguvu fulani zinazomwathiri msikilizaji. Nguvu hizo ndizo hasa maana ya tamko. Kitendo neni kwa hiyo huhusisha mambo matatu:-

1. Tamko la mzungumzaji: Hili lazima liwe na umaanisho na urejeleo, yaani kutumia sauti au maneno yenye maana.
2. Nia na nguvu za tamko: Hili ni tendo linalodhamiriwa.
3. Athari ya tamko hili kwa msikilizaji: Hii hurejelea kile kilichofanikishwa kwa tamko fulani. Kwa mujibu wa Akmajan na Wenzie (1995), Austin (1962) na Searle (1969) vitendo neni vina migawanyiko minne inayoonekana katika kielezo kifuatacho:




Wasomi hawa wameeleza kuwa vitendo vya kimatamko ni vya kutamka tu sauti, silabi, Maneno, virai na sentensi, kutoka kwa lugha fulani na kwamba kilicho muhimu sana katika uzungumzi ni vitendo dhamiriwa (*illocutionary acts*). Vitendo vya aina ya pili, hutendwa katika kutamka tamko na ndivyo huibua vitendo athari (*Perlocutionary acts*) ambavyo huzalisha athari kwa msikilizaji. Mfano wa vitendo dhamiriwa ni kuahidi, kushauri, kuamrisha, kutaja, kuuliza, kupendekeza, kuomba, na kadhalika (Akmajan na wenzie, 1995). Vitendo vya aina ya tatu (vitendo athari) ni jumla ya vitendo dhamiriwa na athari zake kwa msikilizaji. Aina ya nne kulingana na kielelezo hicho ni vitendo rejelea. Aina hii hubeba taarifa iliyomo katika vitendo dhamiriwa. Navyo huelezwa kwa kurejelea (*referring*) mtu au kitu na kukitolea sifa au maelezo kitu au mtu huyo (*predicating*). Kwa mfano, katika tamko: *Baker is tired*. “Baker” ni mrejelewa na *is tired* ni sifa au maelezo juu ya Baker. Katika kudai kwamba Baker amechoka, mzumgumzaji huwa anatenda kitendo cha urejeleo (*propositional act*) (Akmajan na wenzie, 1995).

Katika uchanganuzi wa vitendo neni, athari ya matamko kwa tabia ya mzungumzaji huchunguzwa kwa namna tatu. Kwanza kabisa, mchunguzi anapaswa kutambua ukweli kwamba tendo la kimawasiliano limekuwepo. Tendo hilo ndilo linalorejelewa katika nadharia ya vitendo neni kama tamko la mzungumzaji (*locutionary act*). Pili,ni kutazama kitendo kilichotendeka kama tija ya tamko la mzungumzaji ambapo kutamka huchukuliwa kama kutenda. Vitendo vya namna hiyo hurejelewa kama nia na nguvu za tamko ama vitendo dhamiriwa (*illocutionary acts*)

na ndivyo uti wa mgongo wa nadharia ya vitendo neni. Tatu, ni kutazama athari maalum ya tamko la mzungumzaji. Athari hiyo inaweza kujitokeza katika sura mbalimbali kama vile kushangazwa, kubembelezwa, kuonywa na kadhalika (Crystal,1997).

Kwa mujibu wa Searle (1990) vitendo dhamiriwa ni kipashio kidogo zaidi cha mawasiliano ya kiisimu na utendaji wa kitendo hulenga maana fulani ambayo hudhihirika msikilizaji anapotambua nia ya mzungumzaji. Alibaini kuwa katika utendaji wa kitendo dhamiriwa mzungumzaji hukusudia kuibua athari fulani kwa kumfanya msikilizaji atambue nia yake ya kuibua athari hiyo.Akielezea hali ya kitendo hicho, Crystal alisema kwamba kitendo dhamiriwa na kitendo athari yawezekana visipatane. Hivyo ni kwa sababu onyo la mzungumzaji yumkini lisizingatiwe na msikilizaji. Alibaini kuwa vitendo hivyo ni vingi na vimeainishwa katika makundi madogomadogo kama vile uainishaji wa Searle. Hata hivyo alionya kuwa mara nyingi nia za wazungumzaji haziwekwi wazi kwa sababu ya kile alichokielezea kama utata wa vitenzi.

Ili vitendo neni vifanikiwe katika utendaji kazi wake hapana budi vitimize masharti kadhaa yanayorejelewa kama masharti ya ufaafu ama masharti ya ufelisiti. Masharti andalizi (*preparatory conditions*) kwa mfano yafaa yawe sahihi ambapo mtendaji wa kitendo anapaswa kuwa mwenye mamlaka ya kufanya hivyo. Kutoza faini na kutangaza vita ni vitendo ambavyo vyaweza tu kufanyika na watu ambao wamepewa mamlaka ya kufanya hivyo na jamii au taasisi maalum. Kiongozi wa nchi ambaye ni kamanda wa jeshi ndiye aliyepewa mamlaka ya kutangaza vita dhidi ya nchi ya maadui; mahakama ndiyo yenye mamlaka ya kutoza faini; polisi ndio waliopewa jukumu la kuwatia wahalifu mbaroni na kufungisha ndoa hufanywa na viongozi wa dini au mahkama. Swala la mamlaka ni muhimu endapo mzungumzaji atatumia mamlaka yake katika mahali mwafaka. Hakimu kwa mfano anaweza kumhukumu mhalifu katika muktadha wa mahkamani na sio njiani. Hata hivyo si lazima vitendo neni vyote vitimize sharti hilo. Kuomba msamaha, kuahidi na kushukuru ni mifano ya vitendo neni visivyohitaji mtendaji wake kupewa mamlaka maalum.

Yapaswa pia kutenda kitendo kikamilifu na kwa usahihi. Kukaribishwa huwa sawa ikiwa mwenye kufanya hivyo ana uso wenye tabasamu. Vinginevyo hakufanikishwi kwa sababu kukunja uso ni kiziada cha lugha ambacho huonyesha hali ya kutokaribishwa. Kuomba msamaha

hutimia kwa kuonyesha majuto na wala sio kuendelea kumuudhi mtendwa kwa kumdanganya. Aidha haiwezekani kumwamrisha mtu kufunga mlango iwapo hauko wazi au mwamrishwa hana uwezo wa kuufunga. Ikiwa umefungwa au mwamrishwa hawezi kutekeleza amri hiyo kulingana na hali yake, basi tamko hilo litatafsiriwa kama mzaha, utani au kijembe. Maana nyingine inayoweza kupewa amri hiyo ni kusema kwamba mzungumzaji haoni vizuri au hana akili timamu (Crystal,1997; Cook,1989 na Hogan, 2000).

Kwa mujibu wa Fraser (1996) kila sentensi inahusu jambo fulani; yaani ina urejeleo wa yaliyomo (*propositional content*) na mara nyingi mzungumzaji husema yale yanayokiuka urejeleo huo. Kwa mfano, tamko "nitakuwa nyumbani adhuhuri" kulingana na Fraser linaweza kukusudiwa kuahidi, kutisha, kuonya, au kutoa maelezo fulani (*predication*). Fraser amebaini kwamba kuna mielekeo minne ambayo inaweza kuelezewa na mzungumzaji na ambayo inaweza kuchukulia vitendo neni kugawika katika mapote kadhaa:-

A- Imani (*belief*): Mzungumzaji anaelezea imani yake kwamba ule urejeleo ni sahihi.

B - Hamu (*Desire*): Mzungumzaji anaelezea hamu yake kuhusu kitendo mahsusi kilicho ndani ya urejeleo.

C - Kujitolea (*Commitment*): Mzungumzaji anaelezea nia ya kujitolea kunakoambatana na kitendo mahsusi kilicho ndani ya urejeleo.

D - Tathmini (*Evaluation*): Mzungumzaji anatoa tathmini yake binafsi juu ya kitendo kilichopita.

IIi kufanikisha kuwasiliana kiisimu, inabidi msikilizaji atambue kilichosemwa na mwelekeo alionao mzumgumzaji katika urejeleo wa yaliyomo ya tamko lake. Kwa kuzingatia mielekeo hiyo minne, tunaweza kupata mapote yafuatayo ya vitendo neni:

i) Viwakilishi (*Representatives*):

Hivi ni vitendo neni ambavyo kwavyo mzungumzaji anaelezea imani kwamba urejeleo wa yaliyomo ni sahihi. Vitendo neni vya kiwango hiki hutumika kuwambia watu mambo yalivyo. Aina hii pia hujulikana pia kama vitendo vya kudai (*Assertives*). Kwa mfano: kuthibitisha, kudai, kushikilia, kusema, kutaja, kuamini, kufikia uamzi, kukanusha, kutoa taarifa na kadhalika.

ii) Vielekezi (*Directives*):

Hivi ni vitendo neni ambavyo kwavyo mzungumzaji anaelezea hamu yake kuhusu kitendo mahsusi kilicho ndani mwa urejeleo wa yaliyomo. Vitendo neni vya kiwango hiki hutumika kujaribu kuwafanya watu watende vitendo fulani. Kwa mf: kuomba kitu, kualika, kuhimiza, kuamrisha, kukataa, kukanya, kuonya,kushikilia, kutoa changamoto, kuuliza, na kadhalika.

iii) Vilazimishi (*Commissives*):

Hivi ni vitendo neni ambavyo kwavyo mzungumzaji anaazimia kuwa tamko lake linamlazimu kutenda kitendo kilichotajwa katika urejeleo wa yaliyomo. Kiwango hiki hutumika kumfanya mzungumzaji binafsi ajitolee kutenda vitendo fulani.Kwa mf: kuahidi, kuapa, kuhakikishia, kujitolea, kudhamini, kuweka nadhiri na kadhalika.

iv) Vitathminishi (*Evaluatives*):

Hivi ni vitendo neni ambavyo kwavyo mzumgumzaji anaelezea mwelekeo wake juu ya kitendo kilichotokea. Kiwango hiki kinajulikana pia kama vielezi (*Expressives*) na hutumika kuelezea hisia na mtazamo wake juu ya kitendo fulani. Kwa m.f: kuomba msamaha, kuliwaza, kulaani, kusalimia, kushukuru,kupongeza, kukaribisha, kulaumu, na kadhalika.

V) Viarifu(*Declaratives*):

Hivi ni vitendo neni ambavyo kwavyo mzungumzaji huleta mabadiliko katika jambo au hali iliopo kwa kutoa tamko. Hutumika kuleta mabadiliko katika ulimwengu halisi kupitia kwenye tamko lenyewe. Kwa mfano: Najiuzulu, nabatiza, vita vimetangazwa, umefutwa kazi, na kadhalika (Fraser, 1996; Leech, 1995 na Crystal,1997).

Searle (1975), Parker (1986) na Crystal (1997) walibaini kwamba vitendo neni ni vya aina mbili:-

i) Kitendo neni cha moja kwa moja.

ii) Kitendo neni kisichokuwa cha moja kwa moja.

Kwa mujibu wa Crystal (1997) baadhi ya vitendo neni hulenga kuwasilisha ujumbe kwa msikilizaji kwa njia ya moja kwa moja, lakini katika mazungumzo ya kawaida vilivyo vingi si dhahiri. Alieleza kuwa mara nyingi katika hali ya kawaida tamko *funga mlango* ni la mkato mno na pengine huonyesha ufidhuli na kwamba matamko mbadala kama yafuatayo ndiyo yanayofaa

katika kumwomba mtu kufunga mlango:

- Unaweza kufunga mlango?
- Unajali kuufunga mlango?
- Kuna baridi humu ndani.
- Tunaweza kuuzuia upepo?
- Sasa Jane, umesahau kufanya nini?Brrr.

Coulthard (1985), akielezea tofauti kuu iliopo kati ya Austin na Searle alisema kwamba tofauti hiyo hujikita katika kazi ya nguvu za tamko. Huku Austin akishikilia kuwa nguvu za tamko zina uamilifu wa kutupatia nia ya mzungumzaji, Searle aliona kwamba nguvu hizo ni zao la mzungumzaji.

Brown na Yule (1993) wanaona kwamba utambuzi wa msikilizaji wa nia ya mzungumzaji ndio unaoonyesha ni aina gani ya kitendo neni inayokusudiwa katika usemi. Tamko linaweza kukaa kimaumbo kama swali hali ya kuwa kinachokusudiwa ni ombi.

Utafiti huu ulitumia nadharia ya NKN kubainisha vitendo neni vilivyojitokeza katika lugha ya khutuba za misikitini, kuonyesha nia na nguvu za matamko na pia athari zake kwa waumini wa Kiislamu ambao walikuwa wakisikiliza khutuba hizo. Nadharia hiyo ilimsaidia mtafiti kubainisha maana ya matamko, uamilifu wake na namna tamko moja linavyoweza kuashiria kitendo zaidi ya kimoja kutegemea muktadha.

Schiffrin (1996) ameeleza kwamba tamko la sentensi ni sehemu ya utendaji wa kitendo. Amesema kwamba hali hii ndiyo inayorejelewa na Austin kama utendaji. Amefafanua kwamba kitenzi kitendaji (*performative verb*) huibua tendo maalum ambalo kinalitaja kwa jina katika muktadha mahsusi. Hivyo ni kusema kwamba vitendo vitendaji huhitaji vitu viwili:

i. Muktadha faafu
ii. Lugha faafu

Katika utafiti huu mtafiti alitumia NKN kuonyesha iwapo lugha ya khutuba inafaa muktadha wa msikitini.

Kwa mujibu wa Fromkin na Rodman (1988), NKN hujikita katika pragmatiki taaluma ambayo huchunguza jinsi muktadha unavyoathiri namna sentensi inavyotoa taarifa. Walielezea kuwa pragmatiki ni sehemu ya utendaji wa kiisimu kwa sababu inaangazia jinsi watu wanavyotumia lugha ndani ya muktadha maalum.

Mwanzoni, Austin (1962) alivutiwa na kile alichokiita matamko tendaji yaliyo dhahiri (explicit performative utterances) kama vile:"Nakutangazeni mume na mke", na: "Naahidi kwamba sitachelewa" ambayo hutumika kutenda vitendo vilivyotajwa na kitenzi kama vile kutangaza na kuahidi. Alishikilia kuwa ili kitenzi kichukuliwe kama kitendaji ni sharti kiwe cha wakati uliopo na kiwakilishi nafsi katika sentensi ambamo kimekitwa kiwe cha nafsi ya kwanza. Baadaye alighairi msimamo wake alipogundua kwamba vitenzi vyote hufanya kazi sawa na si lazima mtu aseme: ''Ninapendekeza'' kupendekeza, "Ninaomba radhi" kuomba radhi, "Ninadai" kudai na kadhalika (Taz. Halion, 2008).

Fromkin na Rodman (1988) walibaini kuwa kila tamko ni aina fulani ya kitendo neni hata kama hakuna kitenzi dhahiri cha utendaji. Wakifafanua kauli hiyo walisema kwamba tamko "mvua inanyesha" ni tamko tendaji la kutaja, tamko "je,mvua inanyesha? Ni tamko tendaji la kuuliza" na "Ondoka" ni tamko tendaji la kuamrisha.

Searle (1969) aliendeleza na kuifanyia upanunzi dhana ya vitendo neni kwa kushikilia kwamba matamko yote, sio tu yale yanayogubiza vitendaji, huashiria vitendo. Kwa mfano: Unaposema "Nasikitika kwa kukukanyaga", na pia kwamba "Bob alisema kuwa alisikitika kwa kukukanyaga" kauli zako mbili zitakuwa zimesheheni vitendo neni sawia.

Kwa mujibu wa Searle (1979) kila mojawapo ya viwango vya vitendo neni kina vibadiliki vitatu vya kimsingi ambavyo huungana na yaliomo katika urejeleo wa kitendo. Vibadiliki hivyo ni nguvu ama nia ya hoja, mwelekeo wa kitendo na sharti la uaminifu. Nia ya hoja hurejelea lengo la kitendo na mwelekeo wa kitendo huelezea kitendo neni kama juhudi za kuyafanya maneno yaafikiane na ulimwengu au kuufanya ulimwengu uafikiane na maneno. Kibadiliki cha tatu ambacho ni sharti la uaminifu, huelezea hali ya kisaikolojia ya mtu anayetoa tamko.

Nadharia hii imejikita katika eneo la uchanganuzi wa usemi ambalo hujishughulisha na lugha katika matumizi. Uchanganuzi Usemi umefasiliwa kama taaluma inayochunguza vipashio vya lugha kwa kuhusisha muundo ambao ni zaidi ya sentensi na ambao umeunganishwa na mfumo wa mada zenye uhusiano. Ni mbinu ya uchanganuzi inayomulika lugha ya washiriki. Uchanganuzi Usemi uliibuka kutokana na taaluma ya elimu jamii na ina sura mbalimbali. Mfano wa sura hizo ni barua, utani, mikasa na visa, mihadhara, hotuba, mahubiri na kadhalika (Yule,1995 na Akmajan, 1995).

Katika uchanganuzi wa lugha kuna masuala yanayoibuliwa kuhusiana na jinsi lugha inavyotumika mbali na jinsi ilivyoundwa. Maswali yanayoulizwa ni je, watumiaji wa lugha wanawezaje kufasiri yale ambayo watumiaji wengine wanakusudia kuwasilisha; tunawezaje kuelewa yale tunayoyasoma katika matini, kufahamu yale yanayokusudiwa na wazungumzaji, kutumia usemi uliofungamana na ulioparaganyika na tukafanikiwa kushiriki katika mazungumzo? Majibu ya maswali hayo yote hupatikana katika uwanja wa Uchanganuzi Usemi (Yule, 1995).

Mtafiti alichunguza mahubiri yanayotolewa katika khutuba za Ijumaa ambayo ni mojawapo ya sura mbalimbali za usemi ili kudhihirisha vitendo neni vilivyomo ndani ya khutuba hizo. Aidha, aliangazia jinsi wasikilizaji wa khutuba za Ijumaa wanavyofasiri matamko ya Maimamu wao, ili kubaini kuathirika kwao.

Kwa mujibu wa Mills (1999), wachanganuzi usemi hamu yao kubwa ni lugha kama inavyojitokeza kihalisia. Hawa wanajishughulisha na uchanganuzi wa semi kama zinavyojitokeza katika matamko yaliyonaswa kwa kinasa-sauti au matini yaliyoandikwa. Kwa hivyo vitendo neni vya khutuba vilinaswa na kuchanganuliwa baadaye kama inavyopendekezwa na mkabala huo.

NKN ilimsaidia mtafiti katika kubainisha vitendo neni ili kukidhi haja ya madhumuni yake ya kwanza.

### 2.4.2 Nadharia ya Udokezi

Mtafiti alitumia Nadharia ya Udokezi (NU) ili kutosheleza mahitaji ya madhumuni ya pili, ambayo ni kubainisha athari za vitendo neni kwa waumini. Hivyo ni kwa sababu ili kupata athari lazima maana itambulikane na NU na kanuni zake ndizo zinayoweza kumwonyesha mchanganuzi usemi waziwazi jinsi vipashio maalum vya Kiisimu vinavyotumika katika muktadha maalum wa kimaongezi vinavyotafsirwa na kupewa maana maalum. Kwa mfano mzungumzaji anaposema “Nitakuja huko” tutajuaje iwapo kilichokusudiwa na tamko hilo ni kutoa tishio, onyo, ahadi, au tu maelezo ama taarifa fulani?

Nadharia ya Kitendo neni, kwa hiyo, ilijalizwa na Nadharia ya Udokezi (NU) ya Grice (1975). Nadharia hiyo inatumika kuelezea yale ambayo mzungumzaji anaweza kumaanisha kiuhusishi. Msikilizaji anaweza kutafsiri maana ya tamko kwa kutumia sheria za udokezi wa uzungumzi (*conversational Implicature*). Miongoni mwa sheria hizo ni kanuni shirikishi (Co-operative principle) ambayo inasisitiza kwamba mzungumzaje aufanye mchango wake kama unavyohitajika, katika awamu ile unamotokea na kwa misingi ya malengo yanayokubalika au katika mwelekeo wa mahusiano ya mazumgumzo ambayo anashiriki.

Mihimili ya NU ni kanuni shirikishi za kiasi, ubora, uafiki, na jinsi.

i) Kiasi (Quantity): Kanuni hii inasisitiza kuwa mchango wa mzungumzaji wapasa uwe wenye kutoa habari kiasi kinachohitajika kwa minajili ya mazumgumzo. Mchango wake usiwe na taarifa zaidi ya ile inayohitajika kwa kusudio lililopo wakati huo.

Grice (1990) alisisitiza umuhimu wa kutoa taarifa inayohitajika kwa kueleza kuwa kanuni ya pili yaweza kuzua mgogoro kwani inaweza kusemekana kwamba kutoa taarifa zaidi ya ile inayohitajika si ukiukaji wa kanuni shirikishi ila tu ni kupoteza wakati. Alibaini kuwa utoaji wa taarifa ya ziada kama hiyo huweza kukanganya kwa vile inawezekana ukazua maswala mengine ya huko kando; na pia athari isiyokusudiwa moja kwa moja yaweza kujitokeza, hivi kwamba wasikilizaji wanaweza kupotoshwa kutokana na fikra kwamba kuna hoja katika kutoa taarifa ambayo ni zaidi ya inayohitajika.

ii) Ubora (Quality): Hapa msikilizaji anashurutishwa kutoa mchango ambao ni sahihi na kuonywa dhidi ya kusema yale ambayo anaamini kuwa ni ya uwongo, ama yale ambayo hana ithibati toshelezi juu yake.

iii) Uafiki (Relevance): Kanuni hii inasisitiza kuwa matamshi anayoyatoa mzumgumzaji yawe mwafaka kwa mazumgumzo yanayoendelea.
iv) Jinsi (Manner): Tofauti na kanuni zilizotangulia, kanuni hii haihusiani na kile kinachosemwa bali huhusiana na jinsi yanayosemwa yanavyopaswa kusemwa. Kanuni hii inamlazimu mzungumzaji azumgumze kwa ufupi na kwa njia sahihi ili matamshi yake yaepukane na utata wa maelezo na yawe yamepangiliwa kisawa sawa (Grice,1990),(Leach,1995) na (Fromkini na Rodman,1988).

Ifahamike kwamba mazungumzo yakikiuka kanuni shirikishi, basi maana itakuwa inawasilishwa kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja. Katika hali kama hii, kanuni za unyenyekevu (KUN) ndizo zinazotumika kuelezea kwa nini mzumgumzaji akwepe kanuni fulani miongoni mwa kanuni shirikishi na badala yake awasiliane kwa njia isiyo ya moja kwa moja (Leech, 1995) na ( Fraser,1983).

Grice (1975) ametoa sababu mbili kuu zinazomfanya mtu akiuke kanuni shirikishi na badala yake atumie kanuni za unyenyekevu kwa kutowasilisha matamko yake kwa njia isiyo ya moja kwa moja, ambazo ni:-

- Kukwepa kusema ukweli kwa kuhofia kwamba unaweza kumdhuru mzungumzaji.
- Kukwepa kusema ukweli kwa kuhofia kwamba unaweza kumdhuru mtu mwingine.

Mfano alioutoa kuhusiana na ukiukaji huo ni barua ya profesa mmoja aliyeombwa aandike barua ya kumpendekeza mtu fulani kwa taasisi ambayo alikuwa amewasilisha maombi yake kwake ili apate kuajiriwa kama mwalimu (Taz. Brown na Yule, 1983).

**Kwako Bwana Colligne**

Bwana John J, Jones ameniomba niandike barua kwa niaba yake. Acha niseme kwamba Bwana Jones ni mpole daima, nadhifu nyakati zote na kawaida hufika darasani mapema.

**Wako mwaninifu**

**H. Homes.**

Ukiitazama barua hiyo kwa makini, utagundua kwamba Profesa huyo ana taarifa aliyoificha katika matamko aliyoyatoa. Hivyo ni kwa sababu, mnasaba wa barua hiyo ulikuwa wa kuomba kazi na sio wa kwenda kwenye sherehe ambako anayetaka kuzihudhuria hulazimika kuwa nadhifu. Aidha, kusema kwamba Bw. Jones ni mpole si utambulisho unaompelekea mtu kupata kazi. Kwa hiyo, ilikuwa ataje sifa ambazo waajiri hutaka wafanyakazi wajipambe nazo kama vile "ni mchapa kazi hodari, hujituma na ni mwaaminifu".

Pamoja na hayo, Profesa Homes, kwa kutotaka kumkasirisha mwanafunzi wake kwa kutaja kwamba hafai (ukizingatia kwamba angeweza kuifungua barua hiyo na kuisoma), alitumia kanuni ya unyenyekevu na kukiuka ile ya kiasi ambayo ilimtaka kutoa habari kiasi kinachohitajika. Hata hivyo mpokeaji wa barua anajua kwamba ukiukaji wa kanuni hiyo ni kidokezo cha maana fulani ambayo mwandishi hakutaka aiwasilishe kinaga ubaga.

Brown na Levinson (1987) walishughulikia usifabia katika matumizi ya lugha. Walionyesha kuwa unyenyekevu chanya kwa mihimili yake ni muhimu kuzingatiwa na mzungumzaji. Mihimili ya unyenyekevu chanya kwa mujibu wa wataalamu hao ni mitatu:

1. Kudai kuwa hoja inayowasilishwa hukubalika na wote. Kulingana na mhimili huo mzungumzaji anatakikana kuonyesha kuwa jambo linalozungumziwa ni zuri, hupendeza na linamhusu pia. Kwa kufanya hivyo mzungumzaji ataongeza hamu ya wasikilizaji wake. Hamu hiyo pia yaweza kuongezeka endapo mzungumzaji atatoa hadithi ya kusisimua kabla ya kuwasilisha hoja au wakati wa kufanya hivyo. Vivyo hivyo mzungumzaji anashauriwa kutumia vitambulishi husishi kama vile *sisi*, *nyinyi*, *wapenzi*, *ndugu*, na kadhalika; atoe matamko yanayoonyesha kukubaliana na wasikilizaji wake; aepukane na yale yanayoelekea kuonyesha hali ya kutokubaliana kwa kujifanya kuwa anakubaliana nao; na awatanie wasikilizaji wake.
2. Kuonyesha kuwa mzungumzaji na msikilizaji ni washiriki. Hivyo ni kusema kwamba mzungumzaji anapaswa kuonyesha kuwa anajua matakwa ya wasikilizaji na anayatilia maanani. Anatakikana atoe ahadi, aonyeshe matumaini mema, ajiweke pia katika utendaji wa tendo, atoe sababu za kutenda jambo hilo na kushikilia msimamo wa kutendana.

3. Kutimiza mahitaji ya msikilizaji. Hili hutimia endapo mzungumzaji atatoa zawadi kwa msikilizaji. Zawadi hiyo huchukuwa sura mbalimbali kama vile bidhaa, kumwonea mtu huruma, kuonyesha kuwa anaelewa hali yake, kuonyesha msimamo wa kushirikiana na msikilizaji katika jambo linalozungumziwa na kadhalika.

Kazi ya Brown na Levinson ilifaidi sana utafiti huu kwa sababu ilishughulikia kwa mapana sheria ya unyenyekevu ambayo imekitwa katika Nadharia ya Udokezi iliyomwoongoza mtafiti kama nadharia saidizi. Mapendekezo ya wataalamu hao yalichangia sana katika kukidhi mahitaji ya madhumuni ya tatu ya utafiti huu.

Kwa kutumia Nadharia ya Udokezi na sheria ya unyenyekevu, mtafiti aliweza kuchanganua maana mbalimbali za matamko kama yalivyojitokeza katika khutuba za ijumaa ili kuonyesha jinsi lugha inavyotumiwa na Maimamu.

Ifahamike kwamba NKN na NU zilitumika katika ukusanyaji  na uchanganuzi wa data. Mhimili wa kwanza wa NKN ulitumika kudhihirisha matamko mbalimbali yaliyojitokeza kama vitendo neni katika khutuba mbalimbali. Mtafiti aliwauliza wasailiwa wake juu ya matamko hayo ili kubaini nia za Maimamu na jinsi walivyoathirika nayo. Kwa hiyo, mhimili wa pili ulimwezesha kukusanya data inayohusiana na nia na nguvu za matamko huku mhimili wa tatu ukimpatia data inayohusiana na athari za matamko hayo. Katika uchanganuzi wa data NKN ilimwongoza mtafiti kukidhi matakwa ya madhumuni yake kwani ilimwezesha kudhihirisha vitendo neni vilivyojitokeza katika khutuba mbalimbali na kubainisha jinsi walivyoathirika navyo. Kwa upande mwingine, mtafiti alitumia NU ili kubaini iwapo wasailiwa walitambua maana mbalimbali zilizokitwa katika matamko ya khutuba za Ijumaa. Utambuzi huo ndio uliompelekea kudhihirisha aina mbalimbali za vitendo neni na athari zake kwa waumini.

## SURA YA TATU


## MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, mbinu za ukusanyaji na uchanganuzi wa data ziliangaziwa. Mtafiti alifuata hatua nne katika shughuli nzima ya utafiti. Katika hatua ya kwanza, data ilikusanywa. Data hiyo ilikuwa vitendo neni vilivyokitwa katika khutuba za Ijumaa. Ili kupata data hiyo, ilimbidi aende katika misikiti mbalimbali. Katika misikiti hiyo alitumia vifaa mbalimbali kama vile kinasa sauti, daftari na kalamu. Kinasa sauti kilitumika katika kunasa khutuba zilizokuwa zikiwasilishwa na ambazo hubeba vitendo neni. Daftari lilitumika katika kuandika matamko ya khutuba na viziada vya lugha.

Katika hatua ya pili, mtafiti alisikiliza khutuba zilizonaswa huku akizifanyia unukuzi. Kutokana na unukuzi huo, aliweza kudondoa matamko yaliyojitokeza kama vitendo neni. Hatua ya tatu ilihusiana na data ya maoni. Mtafiti alitumia mahojiano kama kifaa cha kuwahoji Maimamu na Maamuma kuhusu nia na athari za vitendo neni vya khutuba. Aidha alinasa sauti zao ili kuhifadhi kumbukumbu kwa matumizi ya baadaye katika hatua ya uchanganuzi. Uchanganuzi wa data uliendelezwa katika hatua ya nne baada ya shughuli ya kuikusanya kukamilika. Ikumbukwe kwamba uchanganuzi awali ulianza na unukuzi na kwamba mtafiti aliongozwa na NKN na NU katika hatua zote za kutekeleza shughuli hii ya utafiti. Kielelezo kifuatacho huonyesha bombwe la utafiti lililofuatwa:

**Kielelezo 1: Bombwe la Utafiti linaloonyesha Mfumo Uliofuatwa**



Kielelezo hicho hudhihirisha mfumo alioufuata mtafiti. Kulingana na bomwe hilo, utafiti ulifanyika katika misikiti iliyoko katika Mkoa Mdogo wa Bugisu na ulihusu khutuba za Ijumaa. Khutuba hizo huundwa kwa vitendo neni ambavyo ndio uti wa mgongo wa NKN. Ili kutambulisha vitendo ni muhimu kubaini nia ambazo kwazo vilitolewa. Ni kutokana na nia ndipo athari zinaweza kudhihirika. Swala la nia humhusu Imamu huku athari zikiegemezwa upande wa Maamuma.

### 3.2 Mahali pa Kufanyiwa Utafiti

Nchi ya Uganda ina mikoa mitano ambayo ni Mkoa wa Mashariki, Mkoa wa Magharibi, Mkoa wa Kati, Mkoa wa Kaskazini na Mkoa wa West Nile. Bugisu hupatikana katika Mkoa wa Mashariki na kabla ya kuzinduliwa kwa sera mpya kuhusu mikoa ilikuwa ikichukuliwa kama wilaya moja miongoni mwa wilaya za mkoa huo. Lakini serikali ya NRM iliinua hadhi ya wilaya hiyo na kuijaalia kuwa mkoa mdogo wenye wilaya nne ambazo ni Mbale, Sironko, Manafa na Bududa. Utafiti huu ulifanywa katika misikiti ya wilaya za Sironko, Mbale, Manafa na Bududa, katika mkoa mdogo wa Bugisu. Misikiti ambayo husaliwa sala ya Ijumaa katika wilaya hizo ndiyo iliyotafitiwa.


Kilichompelekea mtafiti kufanya uchunguzi wake katika eneo la Bugisu ni kwamba malalamishi mengi yanayohusu khutuba za Ijumaa hutokana na sherehe ya tohara ambayo hufanyika mahali hapo na ni sehemu ya utamaduni wa Wagisu. Kwa vile waliojifunza Uislamu katika eneo hilo ni wachache, idadi kubwa ya Waislamu wa Bugisu bado wanautukuza utamaduni wao ijapokuwa baadhi ya vipengee vya utamaduni huo hukinzana na mafundisho ya Uislamu. Kwa hiyo, mgogoro unaotokana na mwingiliano kati ya tamaduni mbili, yaani utamaduni wa Kigisu na utamaduni wa Kiislamu umetanda. Wagisu wachache ambao wamejifunza dini yao hulazimika kuzungumzia mambo ya utamaduni wao ambayo hayaafikiani na mwenendo wa Uislamu. Mambo hayo ni kama vile unywaji pombe ambao hukithiri katika miaka ya tohara na kuwatahiri watu waliobaleghe kinyume na mafundisho ya Uislamu. Ni kutokana na sababu hizo ndiyo uchunguzi ukafanyika katika eneo hilo ili kubaini jinsi Maamuma wanavyoathirika na vitendo neni vinavyotokana na khutuba zinazowasilishwa katika misikiti mbalimbali siku ya Ijumaa.

**RAMANI YA UGANDA INAYOONYESHA MKOA MDOGO WA BUGISU**




Asili: Macmillan Primary Social Studies Atlas for Uganda, 2009

## WILAYA MPYA ZA MKOA WA BUGISU




**Asili: Serikali Ndogo ya Wilaya ya Bugisu, Kitengo cha mipango**

### 3.2.1Ukusanyaji Data

Data aliyoikusanya mtafiti ilikuwa khutuba za Ijumaa na maoni ya waumini waliozisikiliza kabla ya sala ya Ijumaa. Mtafiti alitumia mbinu ya uchunguzi shirikishi. Mbinu hii ilimsaidia katika kusikiliza khutuba na kupata viziada vya lugha vilivyomsaidia katika utoaji wa maelezo juu ya matamko ya Imamu (vitendo neni) na athari zake kwa wasikilizaji. Viziada hivyo na mambo mengine kama vile utelezi wa ulimi na sifa za uhusishaji au kutohusisha wasikilizaji katika uzungumzi zilisaidia katika kuonyesha mkutadha halisi wa matumizi ya lugha. Vilevile mbinu hii ilimwezesha kunasa sauti za Maimamu walipowasilisha khutuba na baadaye kuwahoji wao na Maamuma wao juu ya khutuba hizo. Uchunguzi shirikishi pia ulimwezesha kuandika aliyoyaona na kuyasikia ambayo pengine hayakunaswa au kupambanuka kwa kinasa sauti. Data iliyopatikana kwa njia hiyo ilijaliza ile ya kunaswa.

### 3.2.2 Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli katika utafiti huu ulikuwa wa makusudi. Kulingana na takwimu za Baraza kuu la Waislamu wa Uganda za mwaka wa (2002), kuna misikiti 161 katika wilaya ya Mbale, 76 katika wilaya ya Sironko, 26 katika wilaya ya Manafa na 26 katika wilaya ya Bududa. Jumla ya misikiti kwa hiyo katika mkoa huo ni 289. Sampuli ya iliteuliwa kwa kuzingatia aslimia 10% ya jumla ya misikiti ili kupata uwakilishi sawa. Kwa hivyo, kati ya misikiti 289 ya Bugisu, misikiti 30 tu ndiyo iliyoteuliwa. Wilaya ya Mbale ina misikiti 161 ambayo huwakilisha aslimia 56%. Aslimia kumi ya idadi hiyo ni 16. Wilaya ya Sironko ilikuwa na misikiti 76 ambayo ni aslimia 26% ya jumla ya misikiti ya Bugisu. Kwa upande mwingine, wilaya ya Manafa ilikuwa na misikiti 26 ambayo ni aslimia 10% ya misikiti yote huku Wilaya ya Bududa ikiwa na idadi sawa na ile ya Manafa na kuwakilishwa na aslimia 10% pia. Kwa vile manung'uniko yanayohusu khutuba aghalabu hutokana na ukweli kwamba utamaduni hukinzana sana na mwenendo wa maisha ya Uislamu na kwa kuzingatia kwamba utamaduni huo umekita mizizi vijijini kuliko mijini, mtafiti aliteua misikiti 24 ya vijijini ambayo ni aslimia 80% ya jumla ya misikiti iliyoteuliwa. Aslimia 20% tu ya misikiti ya mijini ndiyo iliyohusishwa katika utafiti. Uteuzi wa idadi hiyo ya misikiti humaanisha kuwa Maimamu 30 ndio waliohusishwa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu kila msikiti una Imamu mmoja. Misikiti ya vijijini ilikuwa 24 na wasailiwa kutoka kila msikiti walikua watatu kutokana na ukweli kwamba idadi ya wanaosali sala ya

Ijumaa huko vijijini ni haizidi waumini 30. Kwa hivyo, jumla ya wasailiwa wa kutoka vijijini ni 72. Misikiti mijini kwa wastan ina waumini wasiopungua 60. Hii ni kwa sababu wilaya mpya hazijaimarika kiasi cha kuwavutia idadi kubwa sana ya watu wakiwemo waumini wa Kiislamu. Kwa hivyo, kila msikiti kati ya misikiti 6 iliyosalia ulikuwa na waumini 6 walioteuliwa kwa ajili ya kusailiwa. Jumla ya waumini walioteuliwa ilikuwa 108 yaani 72 wakijumlishwa na 36.

Uteuzi huu wa sampuli ulimwezesha mtafiti kupata vitendo neni vya kutosha kutokana na khutuba mbalimbali, maoni ya wasailiwa kuhusu nia za Maimamu na jinsi Maamuma walivyoathirika. Ifahamike kwamba, kulingana na maoni ya wataalam wa utafiti, uteuzi wa sampuli kimakusudi huchangia uelewa wa jambo ambalo mtafiti ana hamu nalo. Kwa mfano, Denzin na Lincoln walisema:

"*Many qualitative researchers employ… purposive, and not random, sampling methods. They seek out groups, settings and individuals where … the processes being studied are most likely to occur*" (Taz. Denzin na mwenzake 2000, uk: 370 na pia Silverman 2005, uk: 129).

"Watafiti wengi wa kithamano hutumia mbinu za … uteuzi wa kimakusudi na siyo uteuzi wa kishelabela. Hutafuta makundi, mandhari na watu binafsi pale ambapo sana sana … mifanyiko inayochunguzwa huelekea kujitokeza".

### 3.2.3 Unasaji Sauti

Mtafiti alihudhuria sala za Ijumaa na kunasa khutuba 30 kwa kinasa sauti. Matamko ya Maimaamu yalinaswa kwenye kanda na kuchanganuliwa baadaye kwa madhumuni ya kupata vitendo neni. Vile vile, majibu ya wasailiwa yalinaswa. Mtafiti alitumia kinasa sauti ili kuhifadhi kumbukumbu nzuri zaidi. Ingawa khutuba zilizowasilishwa na maoni yaliyotolewa viliandikwa, lakini kwa vile maongezi huenda kwa kasi kubwa zaidi kuliko kuandika, kuna mengi aliyoyakosa ambayo yalifidiwa na unasaji sauti.

### 3.2.4 Mahojiano na Wahusika

Mtafiti alijitambulisha kwa baadhi ya waumini waliohudhuria sala ya Ijumaa na kuwaomba wakubali kusailiwa akiwaendea kwa ajili ya mahojiano. Aidha, alijitambulisha kwa Maimamu na kuomba idhini ya kuendesha mahijiano kuhusu khutuba zao.

#### 3.2.4.1 Utambuzi wa Hisia za Kijumla

Baada ya kurikodi khutuba na kumaliza kusali sala ya Ijumaa, mtafiti alitoka nje pamoja na waumini waliotoka mwanzo ili asikilize hisia za kijumla juu ya khutuba. Watafiti wasaidizi wawili, mmoja wao akiwa mwanamke, walisaidia kupata hisia pia kutoka kwa waumini waliopitia kwenye milango mingine. Tabia ambazo zilidhihirika kutoka kwa maamuma walipotoka nje ya msikiti ni pamoja na kuonyesha hasira, furaha, kulalamika au kujadiliana juu ya jinsi khutuba ilivyokuwa. Umuhimu wa hisia hizo ni kwamba zilisaidia kupata athari za vitendo neni vinavyokitwa katika khutuba. Hivyo ni kwa sababu watu hawawezi kulalamika ikiwa hakuna tatizo. Aidha, hisia kama hizo hutokana na muktadha halisi ambamo waumini hao wamejikuta na pia huibuliwa na vitendo neni walivyovisikia. Fauka ya hayo, hisia za kijumla husaidia kuchuja maoni ya wasailiwa wateule ili kuhakikisha kwamba Maimamu hawasingiziwi na Maamuma ambao pengine wanawachukia.

#### 3.2.4.2. Utambuzi wa Vitendo Neni

Mtafiti alisikiliza kanda mara Kadhaa kusudi aainishe vitendo neni na kwa kutumia kihesabu tepu alitambua mahali penye matamko yaliyo muhimu kwa utafiti wake. Kisha akaandaa fomu ambayo ilikuwa na sehemu tatu kwa upande wa juu na sehemu moja chini yake. Vichwa vya sehemu za juu vilikuwa: Vitendo neni, nia na athari. Vitendo neni vilijazwa na mtafiti mkabala wa tarakimu za vihesabu tepu ambavyo vinaonyesha mahala pa kila kitendo. Kwa kufanya hivyo mtafiti alikuwa ameanza mchakato wa kubainisha vitendo neni vya khutuba kwa mujibu wa madhumuni yake ya kwanza. Vilevile, alijaza katika sehemu ya chini hisia za kijumla alizozipata kutoka kwa maamuma wakati wa kutoka msikitini.

#### 3.2.4.3 Mahojiano na Maamuma

Baada ya kujaza vitendo neni kwenye fomu hiyo, mtafiti alitoa kivuli cha fomu hizo kwa minajili ya kujazwa wakati wa mahojiano na kila msailiwa aliyeteuliwa kuwakilisha Maamuma. Wasailiwa hao waliulizwa kwanza juu ya sababu za kuwepo kwa hisia za kijumla na kisha wakatakiwa waeleze nia aliyokuwa nayo Imamu alipotoa kila tamko la khutuba na namna walivyoathiriwa nalo. Ili kuwakumbusha, wasailiwa walichezewa tepu kabla ya kueleza hisia zao na maoni yao. Majibu ya kila msailiwa yaliandikwa katika sehemu za nia na athari kwenye fomu. Majibu hayo ndiyo yaliyochangia kumpatia mtafiti madhumuni yake ya pili. Mahojiano hayo yalikuwa yakifanyika siku moja baada ya khutuba kuwasilishwa.

#### 3.2.4.4. Mahojiano na Maimamu

Katika siku ya pili, Maimamu nao walichezewa tepu na kuhojiwa juu ya nia yao walipotoa matamko yao na pia athari walizozitarajia. Majibu yao yaliandikwa kwenye fomu kama ile waliyopewa Maamuma. Umuhimu wa fomu hiyo ni kwamba pamoja na kuwa chombo cha kukusanyia data ilikuwa pia ala ya kuchanganua data iliyopatikana.

### 3.2.5. Watafiti Wasaidizi

Watafiti wasaidizi wawili walitumika kufanikisha kazi ya utafiti. Mmoja kati yao alikuwa mwanamke. Hivyo ni kwa sababu, kwa kuzingatia mazingira ya msikitini na sheria za Kiislamu, mwanamume haruhusiwi kutangamana na wanawake. Kwa hiyo mwanamke ndiye aliyefanya uchunguzi upande huo ili asaidie katika kupata hisia za wanawake wenzake. Mtafiti msaidizi wa kiume alisaidia kupata hisia za kijumla kwa sababu baada ya kusali Waislamu hutoka nje kwa kupitia milango mbalimbali.

### 3.2.6 Maadili katika Utafiti

Mtafiti aliomba ruhusa kutoka Baraza Kuu la Waislamu wa Uganda na akatambulishwa kwa Makadhi na Maimamu wa Wilaya alimofanyia utafiti. Aliwaomba Maimamu kumruhusu kunasa khutuba zao na akawahakikishia wasailiwa wake kwamba taarifa atakayoipata kutoka kwao itakuwa kwa ajili ya utafiti tu na kwa hivyo itahifadhiwa kama siri na haitatolewa kwa mtu yeyote yule. Vile vile, aliomba ruhusa kutoka kwa Maamuma ili anase mahojiano nao na akawahakikishia kwamba taarifa yao itachukuliwa kama siri ya kutumika tu kwa ajili ya utafiti.

## 3.3 Uchanganuzi wa Data

### 3.3.1 Unukuzi

Baada ya kukusanya data, mtafiti alifanya unukuzi wa baadhi ya matamko ambayo ni muhimu kwa utafiti wake kwenye daftari kisha akayatafsiri kutoka lugha za Kiarabu, Kigisu, Kiganda na Kiingereza. Baada ya kufanya hayo, mtafiti alidondoa vitendo neni katika usemi wa khutuba hizo na kisha akabainisha athari zake kutokana na majibu ya wasailiwa na viziada vya lugha alivyoainisha.

### 3.3.2 Jinsi ya Kuchanganua Vitendo Veni na Athari zake

Vitendo neni vilivyodondolewa, viliainishwa kwa kufuata nadharia ya kitendo neni, mkabala wa Austin (1962). Hatua zake za tamko, nia ya mzungumzaji na athari ya tamko kwa wasikilizaji zilizingatiwa katika uainishaji wa vitendo neni. Baada ya kuviainisha kwa namna hiyo mtafiti alitumia mkabala wa Searle (1969) kuonyesha viwango mbalimbali vya vitendo neni vilivyojitokeza katika khutuba.

#### 3.3.2.1 Utaratibu Uliofuatwa katika Uchanganuzi wa Vitendo Neni na Athari zake

Utaratibu uliofuatwa ulitilia maanani vipashio vya vitendo neni kama ilivyopendekezwa na Austin na Searle na pia ufasiri wa maana ya tamko kama ilivyopendekezwa katika Nadharia ya Umaanisho.

**a) Vipashio vya Vitendo Neni:**

Mtafiti alielezea vipashio vya vitendo neni katika khutuba kwa hatua zake zifuatazo:

i) Tamko: Hatua hii ilisaidia kutambua vitendo neni vya khutuba. Matamko yenye urejeleo tu ndiyo yaliyoainishwa.

ii) Nguvu na nia: Hatua hii ilisaidia kutambua nguvu na nia za tamko ambavyo kwavyo mzungumzaji hukusudia kuathiri wasikilizaji. Maimamu na Maamuma walimwelekeza mtafiti kutambua nia na nguvu za matamko ya khutuba.

iii) Athari: Hatua hii ilisaidia kutambua athari zilizotokana na nguvu za tamko na nia ya mzungumzaji. Hisia na maoni ya wasikilizaji vilichangia katika utambuzi wa athari za matamko ya khutuba.

**b) Aina za Vitendo Neni**

Kwa mujibu wa Searle (1969), vitendo neni hujitokeza katika aina mbalimbali ambazo zinaweza kurejelewa kama viwango vya vitendo neni. Aina hizo ni viwakilishi, vielekezi, vilazimishi na vitathmishi. Mkabala huu ulisaidia katika ubainishaji wa vitendo neni vya khutuba aina zake na idadi yake. Hivyo ni kwa sababu kila moja wapo ya aina hizi za vitendo neni huwa na vipashio vitatu vya Austin ambavyo ni tamko, nia na athari. Aidha uainishaji wa Searle ndio uliotupatia sifa za vitendo neni vya khutuba za Ijumaa.

i. Viwakilishi: Huonyesha imani juu ya usahihi wa urejeleo wa yaliomo. Kwa mfano: Kuthibitisha, kudai, kushikilia, kusema, kutaja, na kadhalika.
ii. Vielekezi : Huonyesha hamu ya kitendo mahasusi. Kwa mfano: Kuomba kitu, kualika, kuhimiza, kuamrisha, kukataa, kukanya, na kadhalika.
iii. Vilazimishi: Huonyesha azma ya mzungumzaji juu ya kutenda jambo. Kwa mfano: Kuahidi, kuapa, kuhakikisha, kujitolea, na kadhalika.
iv. Vitathminishi: Huonyesha mwelekeo wa mzungumzaji juu ya kitendo kilichotokea. Kwa mfano: Kuomba msamaha, kuliwaza, kuhani, kusalimia, kushukuru, na kadhalika.
v. Viarifu: Huonyesha nia ya mzungumzaji ya kuleta mabadiliko katika jambo au hali. Kwa mfano: Nabatiza, natangaza vita, najiuzulu na kadhalika.

Kwa kutumia mbinu ya wingi idadi mtafiti alibainisha idadi ya vitendo neni vilivyojitokeza katika khutuba na kuonyesha umaratokezi wake katika kila kiwango kati ya viwango vya vitendo neni vya Searle.

**c) Ubainishaji wa Maana ya Matamko kwa Mkabala wa NU:**

Ili kupata nguvu na nia ya tamko ni lazima maana ya tamko ijulikane. Kwa hiyo NU ilisaidia katika utambuzi wa maana ya matamko ya khutuba kupitia kanuni shirikishi na kanuni za unyenyekevu (Grice, 1975; Leech, 1983).

1. Kanuni shirikishi:

- Kanuni ya kiasi: Taarifa isiwe zaidi ya ile inayohitajika.
- Kanuni ya ubora: Lazima pawepo na ithibati juu ya ukweli wa matamko.
- Kanuni ya uafiki: Matamko yawe mwaafaka na mazungumzo yanayoendelea.
- Kanuni ya jinsi: Matamko yawe mafupi, yaepukane na utata na maelezo yapangiliwe kisawasawa.

2. Kanuni za unyenyekevu:

- Kanuni ya busara: Punguza gharama kwa wengine na uwaongezee manufaa.
- Kanuni ya ukarimu: Punguza manufaa ya kibinafsi na ujiongezee gharama.
- Kanuni ya ukubalifu: Punguza hali ya kutowasifu watu na uwaongezee sifa.
- Kanuni ya staha: Jipunguzie majivuno, ujiongezee madharau.

- Kanuni ya makubaliano: Punguza kutokubaliana kati yako na wengine. Uwe ukikubaliana zaidi nao.
- Kanuni ya huruma: Punguza uhasama na uongeze huruma kati yako na wengine.

**d) Ubainishaji wa Athari za Vitendo Neni**

Hisia na maoni ya waumini juu ya matamko yaliyojitokeza katika khutuba za Ijumaa, yalimwelekeza mtafiti katika kubainisha athari za vitendo neni na iwapo athari hizo ni hasi au chanya.

**e) Muundo wa Uchanganuzi**

Kwa ujumla uchanganuzi wa kila kitendo neni ulifuata muundo ufuatao:

1) Kitangulizi.
2) Maelezo juu ya tamko.
3) Maelezo juu ya nia ama nguvu za tamko.
4) Maelezo juu ya athari za tamko.
5) Maelezo juu ya masharti ya ufelisiti.

Katika shughuli nzima ya uchanganuzi wa vitendo neni, mtafiti alidhihirisha matamko yaliyojitokeza katika khutuba za Ijumaa kama vitendo neni, akabainisha viwango vyake na kuelezea athari zake kwa wasikilizaji zikiwemo chanya na hasi. Jedwali lifuatalo limetoa uchanganuzi huo kwa muhtasari kama inavyodhihirika

Mtafiti alikusanya maoni ya wasailiwa ili kuweza kuipata data yake ambayo ni vitendo neni vinavyojitokeza katika khutuba za Ijumaa na athari zake kwa waumini. Kielelezo cha namna ambavyo vitendo neni, nia na athari hutambuliwa ni katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 1: Mfano wa Jinsi Vitendo Neni, Nia, Athari na Hisia za Kijumla Zilivyotambuliwa**

| KIHESABU TEPU | KITENDO NENI | NIA | ATHARI | HISIA ZA KIJUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 005 | Mmekuwa wakaidi juu ya aya za Mwenyezi Mungu na Hadithi za mtume (SAW). | Kulaumu wasikilizaji kwa sababu ya kuchelewa. | Kukasirika. | Imamu hakutumia lugha nzuri.Haifai kuwashambulia waumini jinsi alivyofanya. |
| 010 | Kuna waliorukaruka usiku, wakachinja kuku eti kwa sababu wamemaliza mwaka… ni Waislamu? | Kushikilia kuwa wanaosherehekea mwaka mpya si Waislamu. | Kushangazwa. | |
| 015 | Na nyinyi watu wa Makuduyi mwataka kuwa kama Waizraili? | Kuwalaumu Waislamu kwa kutotilia maanani ujumbe wake. | Kukasirika. | |

### 3.3.3. Jinsi ya Kuchanganua Viziada vya Lugha

Viziada vya lugha kama vile kukunja uso, kutikisa kichwa ili kuonyesha hali ya kutoridhika, kutikisa mkono na kuashiria kwa kidole ili kulititilia nguvu tamko; kurudiarudia matamko ili yaeleweke vyema; na vingi vinginevyo, huandamana na matamko ili kuleta athari fulani kwa hadhira na kuonyesha nia ya mzungumzaji. Viziada hivyo vilichanganuliwa kwa kuviweka

sambamba na matamko ambayo yalitolewa hali ya kuwa vinatendeka kama inavyobainika katika mfano ufuatao:

**Jedwali 2: Mfano wa Jinsi Viziada Vilivyochanganuliwa**

| KIZIADA | TAMKO LA IMAMU | ATHARI |
|---|---|---|
| **i) Viziada vya Imamu**<br>Imamu anainua kiganja chake na kukunja kidole gumba huku akiashiria kwa vidole vilivyobaki. | Yeyote anayemwendea mpiga ramli, sala zake hazitokubaliwa kwa kipindi cha siku arobaini | Kuzinduka |
| Anaashiria nje kwa kidole cha shahada | Mmekataa kuacha maasi lakini kumbukeni kwamba ziraili anakusubirini | Kuonywa |
| **ii) Viziada vya Maamuma**<br>Maamuma wanakunja nyuso zao huku wengine wakitazama chini | Baadhi yenu mnapoambiwa jifunzeni dini yenu hamtaki. Lakini tutaona ni nani atakuosheeni maiti zenu. | Kuaibika |

Katika jedwali hilo, viziada vitatu vya lugha vimetumika kuelezea maana ya matamko. Matumizi yake yalidhihirisha kuwa khatibu alikusudia maana hizo na wala si zingine na wasikilizaji walimwelewa hivyo. Utikisaji wa kiganja ulikusudiwa kusisitiza swala alilokuwa akizungumzia ili kuwashtua wasikilizaji na kuashiria kwa kidole chake kulikusudiwa kutoa onyo kali kwa watenda maasia. Kwa upande mwengine, kitendo cha maamuma kukunja nyuso na kutazama chini huonyesha hali ya kutofurahishwa na tamko hilo au kuaibika.

## SURA YA NNE

## UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

### 4.1 Utangulizi

Sura hii imejihusisha na uwasilishaji pamoja na uchanganuzi wa data ya utafiti huu ambayo ni khutuba za Ijumaa na maoni ya wasikilizaji kuhusu vitendo neni vilivyojitokeza katiko khutuba hizo. Data hiyo imeorodheshwa na kuchanganuliwa kiwingi idadi na kiuthamano ili kukidhi matlaba ya mada ya utafiti ambayo yalikuwa kubainisha sifa za lugha zinazozua malalamishi dhidi ya khutuba za Ijumaa.

Vivyo hivyo, madhumuni ya utafiti yalikuwa kubainisha vitendo neni vinavyojitokeza katika khutuba za Ijumaa na athari zake kwa waumini wanaozisikiliza. Kwa hiyo, data iliyokusanywa imewasilishwa ili kujibu maswali ya utafiti huu, ikachanganuliwa katika majedwali maalumu na kuelezewa kwa upana kutokana na mwongozo wa Nadharia ya Kitendo Neni na Nadharia ya Umaanishaji.

### 4.2 Vitendo Neni katika Khutuba za Ijumaa.

Kwa mujibu wa Austin (1969) vitendo neni ni tamko linalobeba kitendo kinachotimizwa kwa kunena wala siyo kutenda. Khutuba 30 zilizowasilishwa katika misikiti mbalimbali zilinaswa. Mtafiti alidondoa matamko yaliyojitokeza kama vitendo neni kutokana na khutuba hizo na kufanya unukuzi wa madondoo yaliyotokana na khutuba 20 tu. Hii ni kwa sababu khutuba 10 hazikuwa na usikivu mzuri. Jumla ya vitendo neni vilivyodondolewa ni 325.

Matamko yaliyodondolewa yalitambulishwa kama vitendo neni kwa sababu:

Kwanza, kwa kuyatamka, Maimamu walitenda vitendo vinavyohusisha uneni peke yake yake kama alivyoshikilia Austin (1962) na Searle (1969). Kuhimiza, kuelimisha, kulaani na kuonya ni mifano ya vitendo ambavyo hutimia kwa kutumia kipaji cha kuongea na sio viungo vya mwili kama mikono na miguu ambavyo kwa kawaida ndivyo hutumika katika utendaji wa kazi nyingi. Pili, yalikusudiwa na Maimamu kuwafanya wasikilizaji wao watende mambo mbalimbali kama vile kuungama, kuzinduka, kuelimika, na kadhalika kutokana na kuathirika kwao na yaliyonenwa. Mwisho, Maamuma walitambua nia ya Imamu na kutokana na utambuzi huo, mtafiti aliweza kufahamu kilichokusudiwa katika matamko mbalimbali.

Kwa hivyo, uchanganuzi wa vitendo neni ulizingatia Nadharia ya Kitendo Neni ya Austin (1962) kwa vile unukuzi ulihusu matamko ambayo ndiyo msingi wa kupata vitendo neni na ni hatua ya mwanzo kabisa katika mchakato mzima wa uchanganuzi. Mhimili wa kwanza wa NKN ndiyo ulimwongoza mtafiti katika hatua hiyo ya uchanganuzi na mfano wa matamko yaliyodondolewa kama vitendo neni umetolewa (Taz. Kiambatisho B).

Baada ya kupata data ya vitendo neni, mtafiti alipiga hatua nyingine na kuangazia swala la viwango vya vitendo neni akizingatia mkabala wa Searle (1969) aliyeifanyia upanuzi NKN. Hapa alizingatia pia mhimili wa pili wa NKN ambao ni nia na nguvu za tamko. Kulingana na uainishaji wa Searle, vitendo neni vilivyojitokeza katika khutuba viligawanywa katika viwango mbalimbali ambavyo ni viwakilishi, vielekezi, vitathminishi na vilazimishi. Kwa kuzingatia mkabala huo, matamko yaliyoelekea kushikilia jambo au kutoa madai fulani yaliainishwa kama vitendo neni viwakilishi huku yale yaliyoonyesha hali ya kuamrisha, kukanya au kukataza yakiainishwa kama vitendo neni vielekezi. Kwa upande mwingine matamko yaliyoelekea kutoa tathmini juu ya jambo lililozungumziwa yaliainishwa kama vitendo neni vitathminishi ilhali yale ambayo yalidhihirisha kuwa mzungumzaji inamlazimu kutenda tendo fulani yakiainishwa kama vitendo neni vilazimishi. Mfano wa jinsi vitendo neni vilivyoainishwa ni kama ifuatavyo:

**Jedwali 3: Mfano wa Jinsi Vitendo Neni Vilivyoainishwa**

| **Aina za kitendo neni** | **Tamko** | **Nia** |
|---|---|---|
| **KW** | Ingekuwa vyema matamko haya machache uyazingatie | Kuhimiza |
| **KE** | Msiwaogope hao mabwana, msiwaheshimu | Kuchochea |
| **KT** | Wagisu huichukulia kuwa halali | Kuchukia |
| **KL** | Namhimidi Mwenyezi Mungu Muumba wa mbingu na ardhi | Kuhimidi |

Katika jedwali 3 na kwingineko kwenye utafiti huu, KW huwakilisha kitendo neni kiwakilishi, KE ni kitendo neni kielekezi, KT ni kitendo neni kitathminishi na KL ni kitendo neni kilazimishi. Hizo ni aina mbalimbali za vitendo neni kulingana na uainishaji wa Searle. Jedwali hilo huonyesha kuwa mtafiti aliweza kuainisha vitendo neni vya aina nne ambavyo ni kiwakilishi, kielekezi, kitathminishi na kilazimishi, kutokana na matamko yaliyojitokeza katika khutuba mbalimbali. Hivyo ni kwa sababu matamko huonyesha kuwepo kwa uneni na ni kutokana na uneni ndipo kitendo kinachohusisha ulimi tu hutendwa.

Katika khutuba zilizoshughulikiwa, vitendo neni viliangukia katika viwango vine tu kati ya viwango vitano vilivyopendekezwa na Searle (1969). Hali hii hajitokezi tu ghafla bali hutegemea tabia ya usemi na muktadha unamojitokeza usemi wenyewe. Muhtasari wa viwango hivyo umetolewa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4: Viwango vya Vitendo Neni katika Khutuba mbalimbali.**

| **Khutuba** | **Vitendo neni** | **VW** | **VE** | **VT** | **VL** |
|---|---|---|---|---|---|
| 01 | 19 | 07 | 11 | 00 | 01 |
| 02 | 27 | 04 | 11 | 11 | 01 |
| 03 | 22 | 00 | 01 | 20 | 01 |
| 04 | 15 | 00 | 04 | 10 | 01 |
| 05 | 21 | 01 | 03 | 16 | 01 |
| 06 | 08 | 00 | 06 | 01 | 01 |
| 07 | 23 | 03 | 13 | 06 | 01 |
| 08 | 10 | 00 | 06 | 03 | 01 |
| 09 | 22 | 00 | 15 | 06 | 01 |
| 010 | 11 | 02 | 08 | 00 | 01 |
| 011 | 23 | 01 | 14 | 07 | 01 |
| 012 | 17 | 00 | 16 | 00 | 01 |
| 013 | 11 | 01 | 09 | 00 | 01 |
| 014 | 14 | 02 | 07 | 04 | 01 |
| 015 | 12 | 01 | 08 | 02 | 01 |
| 016 | 16 | 00 | 07 | 08 | 01 |
| 017 | 12 | 01 | 10 | 00 | 01 |
| 018 | 09 | 00 | 08 | 00 | 01 |
| 019 | 15 | 03 | 10 | 01 | 01 |
| 020 | 18 | 00 | 06 | 11 | 01 |
| **Jumla** | **325** | **26** | **173** | **106** | **20** |
| **Aslimia** | **100%** | **8%** | **53%%** | **33%** | **6%** |

Jedwali 4 hudhihirisha matumizi ya kijumla ya vitendo neni bila kuangazia athari zake kwa wasikilizaji. Kutokana na jedwali hilo, viwango vinne vya vitendo neni ndivyo vilivyotumika katika khutuba. Viwango hivyo ni viwakilishi (VW), vielekezi (VE), vitathminishi (VT) na vilazimishi (VL). Vitendo neni vielekezi ndivyo vilivyotumika sana katika khutuba za Ijumaa kwani vilijitokeza katika khutuba nyingi zaidi kati ya hizo zilizochanganuliwa. Aina hiyo ya vitendo neni iliwakilishwa na  aslimia 53%. Vitendo neni vilivyochukua nafasi ya pili katika matumizi, ni vitathminishi ambavyo ni aslimia 33% ya vitendo neni vya khutuba zote zilizochanganuliwa. Nafasi ya tatu katika matumizi, ilikuwa ya vitendo neni viwakilishi. Aina hii iliwakilishwa na aslimia 8%. Nafasi ya mwisho ilikuwa ya vilazimishi ambavyo vilikuwa aslimia 6% ya jumla ya vitendo neni vilivyojitokeza katika khutuba za Ijumaa. Jedwali hilo limedhihirisha pia kwamba katika khutuba, vitendo neni viarifu huwa havitumiki. Kwa hiyo, kinachobainika katika jedwali hilo ni kwamba viwango vinne vya vitendo neni ndivyo hutumika katika khutuba za Ijumaa vikipishana katika daraja. Vitendo  neni viarifu havikujitokeza kutokana na muktadha wa khutuba. Hivyo ni kwa sababu khutuba ni sehemu ya sala ya Ijumaa ambapo Imamu hutazamiwa kutoa ujumbe unaojenga waumini kiimani ingawa unaweza kuhusiana na kuwaendeleza katika nyanja nyingine za maisha. Kwa hivyo haitarajiwi kwamba tamko kama la kufutwa kazi au kujiuzulu litatokea katika mazingira kama hayo. Kubatiza kuna wakati wake maalum ambapo anayetaka kusilimu hutozwa shahada mbili na akiwa mtoto mchanga huadhiniwa kwenye sikio kisha akapewa jina. Hata hivyo, kutangaza vita kunaweza kutokea katika khutuba kwa sababu huhudhuriwa na waumini wengi ikilinganishwa na wale wanaohudhuria sala tano za jamaa. Ingawa kitendo hicho cha kutangaza vita chaweza kujitokeza katika muktadha wa khutuba lakini tofauti na enzi za mtume, sahaba zake na makhalifa wa falme mbalimbali za Kiislamu, Imamu wa kawaida ambaye si kiongozi wa nchi ni muhali kufanya hivyo kwa sababu hana mamlaka hayo.

Yafaa isisitizwe kwamba ingawa khutuba thelathini zilinaswa, ni ishirini tu ndizo zilizochanganuliwa. Hivyo ni kwa sababu baadhi ya tepu zilikuwa na mushkili katika usikivu wake na kwa vile idadi kubwa ilikuwa katika hali nzuri ilitoshelezea haja ya utafiti.

### 4.2.1 Vitendo Neni Vielekezi (VE)

Katika khutuba, VE vimejitokeza katika sura ya kukanya, kuamrisha, kuzindua, kuelimisha, kugombanisha, kuonya, kutahadharisha, kuhimiza na kukaripia. Vitendo neni vielekezi kwa sura hizo zote vilimojitokeza, vina uamilifu wa kuelezea hamu ya mzungumzaji kuhusu vitendo vilivyorejelewa na matamko yaliyokitwa katika khutuba (Taz. Fraser, 1996). Mifano ifuatayo huelezea sura hizo waziwazi:

**Kukanya:**

1. *Ukikuta una aibu kama zile za mwenzako [[usizichambue]]*

Tamko hilo likitizamwa kijuu juu huonekana kama limekusudiwa kuwakana watu wasijihusishe na tabia ya kuwasema wenzao kwa kutaja aibu zao. Lakini kwa njia isodhahiri nia yake ilikuwa kuwachochea waumini dhidi ya Mashekhe wanaowakashifu wenzao hali ya kuwa wao wana aibu fulani fulani. Athari ya tamko hilo ilikuwa kukanganyika. Hivyo ni kwa sababu ni Imamu huyo huyo ndiye anayechambua aibu za watu na wakati huo akawakanya Maimamu na Maamuma kutaja aibu za watu wengine. Hapa kibadiliki muhimu ambacho ilipaswa kiungane na nguvu za tamko ama nia na sharti la uaminifu ili kufanikisha lengo la mzungumzaji hakikuzingatiwa. Kibadiliki hicho ni mwelekeo wa kitendo ambao ni hali ya maneno kuafikiana na ulimwengu halisi.

Maimamu wanatakikana kuwa mfano bora na watumie busara katika kuwasilisha ujumbe wa kidini kwa waumini. Kama kuna mtu ambaye ana madhaifu fulani, ni vyema kumweka faraghani na kumpa nasaha ili aachane na mabaya na ashikamane na mema. Lakini kuyatangaza madhaifu hayo hadharani ni kama kuanika nguo za chumbani sebuleni ambapo si mahali pake. Tabia hiyo imekita mizizi miongoni mwa baadhi ya Waislamu ambao huwasemasema wenzao mbele ya watu au kupeleka manung'uniko dhidi yao kwa wakubwa zao kama vile Mashekhe wa tarafa au makadhi wa wilaya. Baadhi ya Waislamu hao ni wasomi na baadhi yao ni wafuasi wao ambao hushangilia tu madhehebu fulani fulani.

Kauli ya Imamu ni ya kujibizana, baada ya kuwasilisha mawazo yake redioni kulikuwa na waliompigia simu akiwa studioni na kuteta kwamba baadhi ya mambo ambayo alikuwa akiwahimiza Waislamu kuyafanya ni bidia ama uzushi. Alipotaka kuwajibu, msimamizi wa kipindi akamkatalia akasema atamjibu yeye. Kwa sababu ya kukerwa na yale ambayo

aliyachukulia kuwa mashambulizi, aliamua kugusia mambo hayo katika khutuba ambamo tamko 1 lilijitokeza.

Tamko hilo ukilichambua kwa mkabala wa masharti ya ufaafu ama ufelisiti, utakuta kwamba masharti mawili yametimizwa na mengine yamekiukwa. Msemaji ni mwafaka kwani ana mamlaka na ndiye khatibu anayepaswa kuhutubia hadhara kama hiyo na pia hadhira ni mwafaka kwa sababu ni ya waumini wa Kiislamu. Lakini mahali alipotolea tamko hilo si mwafaka na wakati wake si mwafaka hata kidogo. Hivyo ni kwa sababu, tamko lake hurejelea mawaidha aliyoyatoa redioni ikatokea kwamba kuna waliompigia simu miongoni mwa Mashekhe wenzake na kumwambia kwamba yale anayoyafundisha yalikuwa na mushkili kidogo kwa sababu hayafuati misingi ya dini ya Uislamu.

Tamko la Imamu lingetolewa wakati ule ambapo kipindi kilikuwa kikiendelea kurushwa hewani ili alenge hadhira mwafaka ambao ni Mashekhe wenzake. Hali yake ni kama ya yule aliyegombana njiani akaambiwa *Bakuseerera mu katale, oyombesa kkubo!*(Unagombanisha njia wakati walikunyang'anyia huko sokoni!). Sharti linalomtaka mzungumzaji atekeleze kitendo kwa ukamilifu nalo limekiukwa. Hivyo ni kwa sababu anawakataza watu kuchambua aibu za wenzao na hali yeye anawachambua Mashekhe wenzake. Kwa kufanya hivyo amekiuka pia sharti la uaminifu kwa kuwa yeye mwenyewe katika nafsi yake anajua kwamba kwa kuchambua aibu za wenzake hakutoa mfano bora wa kuigwa na wafuasi wake. Imamu amekiuka pia mihimili ya unyenyekevu kwa sababu kama angeamini kuwa ni jambo zuri kuwakanya watu kutokana na kuwachambua wenzao ingefaa atambue kwamba jambo hilo linamhusu pia.

2. *Mwajua kumwanda…mwabiita?[[ Acheni hayo]]*.

Swali la Imamu halitarajii jibu kutoka kwa maamuma bali limekusudiwa kuwakumbusha matendo wanayoyafanya katika shughuli ya tohara ambayo hayafai. Ndiyo maana anawakataza kufanya matendo hayo katika sentensi inayofuata. Kwa hivyo, nia ya Imamu ni kuwakanya Waislamu ili wasishiriki katika miviga hiyo. Athari ya tamko hilo ilikuwa kuudhika kwa maamuma kwa sababu ya kusemwa hadharani kitendo ambacho waliona kwamba kilikusudiwa kuwaaibisha.

Kumwanda ni njia maalum ambayo hupitiwa na vijana wanaoenda kutahiriwa. Kulingana na mila na desturi za Kigisu vijana hao hawaruhisiwi kupitia katika njia nyingine wanaporudi nyumbani kupashwa tohara. *Mwabiita*? Maana yake ni je mlirusha pombe? Kawaida vijana hao wa Kigisu wanaotoka janibu mbalimbali wanapokutana, hurushiwa pombe na wazee walioteuliwa kutekeleza jukumu hilo kabla ya kutahiriwa.

Ingawa Imamu alizingatia masharti ya ufelisiti, hakujali kaida za unyenyekevu jambo ambalo huenda lilichangia katika kuzua athari hasi kama ilivyojitokeza.

3. *Ijumaa iloyopita tulikuwa katika mwezi wa Ashuraa…[[ ni nani aliyefunga]]?*

Tamko hilo hurejelea kitendo ambacho waumini wamezoea kukifanya uingiapo mwaka mpya. Kwa hiyo nia yake ilikuwa kuwakataza Waislamu kushiriki katika kitendo ambacho hakina msingi wowote katika dini. Kutokana na nguvu za tamko hilo baadhi ya waumini waliathirika kwa kupokea kitendo neni hicho kwa moyo mkunjufu wakiona kwamba si sawa kupiga makelele kama wahuni kisha uambulie patupu. Lakini baadhi yao walipuuza tamko hilo wakiona kwamba dini haiwakatazi kufurahika na kujivunia kwa kumaliza mwaka na kuukaribisha mwaka mpya.

Ashuraa ni siku ya kumi katika mwezi wa Muharram kulingana na kalenda ya Kiislamu. Ulimi wa Imamu uliteleza tu aliposema "tulikuwa katika mwezi wa Ashuraa". Mwezi huo wa Muharram ndio mwezi wa kwanza na siku ya Ashuraa ilikuwa ikiadhimishwa na Wayahudi kwa kufunga kwa sababu Nabi Musa (AS) alifanikiwa kuwakomboa wana wa Israil kutokana na mateso ya Firauna huko Misri. Mtume Muhammad (SAW) alipobaini sababu ya kuadhimishwa kwa siku hiyo, aliwaamrisha Waislamu nao kuonyesha ushikamano na ndugu yake Musa (AS). Yeye katika uhai wake alikuwa akifunga siku ya Ashuraa na aliwapendekezea Waislamu kufanya hivyo pia. Imamu anaona kwamba tarehe mosi Januari haistahili kuadhimishwa na badala yake anapendelea iadhimishwe siku ya Ashuraa kwa sababu inafungamana na dini na anayefunga siku hiyo hupata thawabu tofauti na yule anayeadhimisha tarehe mosi Januari kwani hupoteza tu muda wake na nguvu zake.

Kitendo neni hicho kimewasilishwa na mtu mwenye mamlaka, kikajitokeza katika muktadha faafu, kikawalenga wasikilizaji mwafaka kwani wana uwezo wa kutenda wanachoambiwa na lau kama hawakuambiwa wasingekuwa tayari kufanya lolote. Lakini kuhusu sharti la uaminifu kuna wasiwasi kidogo kwa sababu Imamu huyo mwenyewe anaamini kwamba waumini hawajafunzwa ipasavyo juu ya siku wanazotakikana kufunga, hususani siku ya Ashuraa na kuhusu sunna na faida zinazotokana na kitendo hicho. Ni jukumu lake pia kuwaelimisha kuhusu namna ambavyo Mwislamu anaonyesha furaha yake uingiapo mwaka mpya kulingana na kalenda zote mbili, ya Kiislamu na Kimasihia.  Kuwalaumu wakiwa bado katika hali ya kutojua ukweli wa mambo, kama si kuwadhulumu  lakini haiwi kuwatendea haki. Kaida za unyenyekevu zilikiukwa pia.

**Kuamrisha:**

4. *[[Kuwa open]].....hutaki kujitokeza mbele kwa sababu unahofia kutajwa.*

Kitendo neni hicho huonekana kama amri  inayoelekezwa kwa maamuma ili wakalie katika safu za mbele wakiwa msikitini. Lakini kwa njia iso dhahiri limetumika makusudi na nia yake ni kuwalaumu wasikilizaji kwa tabia yao ya kujificha nyuma. Athari ya tamko hilo ilikuwa kuudhika jambo ambalo liliwafanya baadhi ya waumini kuamua kuukimbia msikiti huo ili wasalie katika misikiti mingine ambamo hawasumbuliwi.

Tabia iliopo ni kwamba baadhi ya Maimamu wanawalazimisha Maamuma kutoa sadaka hata kama hawana au walitoa katika siku za nyuma. Kuna Maamuma ambao hawana pesa na wanashurutishwa wakae mpaka wenzao watakapomaliza kutoa michango yao na mpaka Imamu ahakikishe kuwa hakuna cha ziada ndio awaruhusu kutoka. Kukawa na wale ambao huwaita Maamuma kwa majina na kuwambia watoe pesa. Kwa vile Maamuma hao hawataki kukosa kutimiza wajibu wao na kutekeleza ibada msikitini, na kwa vile wanataka kuondoka mapema kufanya shughuli zingine, wanalazimika kukaa katika safu za nyuma kabisa ili baada ya sala wachomoke pasina kutambuliwa. Kwa hivyo, Imamu anawataja akigundua kwamba wanajaribu kumkwepa.

Bila shaka kutoa sadaka kuna manufaa mengi sana. Sadaka kwa aina zake zote huchangia katika uendelezaji wa jamii kidini, kisiasa na kiuchumi. Kama Maimamu wangewatayarisha maamuma wao mapema kwa kuwapa mafunzo ya kimsingi juu ya nguzo za Uislamu na umuhimu wa kutoa sadaka, wasingepata tatizo kama hilo la kukimbiwa na wafuasi wao. Zaidi ya hayo, kama wangeonyesha waziwazi jinsi wanavyosarifu pesa zao wanazozikusanya misikitini, Maamuma wangechangamkia kitendo na wito wa kutoa sadaka na bila shaka wangemtii ipasavyo na ugonvi usingekuwepo. Fauka ya hayo, kama Maimamu wangeonyesha shukrani zao kwa wale waliotangulia kutoa sadaka, wito wao ungeitikiwa kwa wepesi sana.

Hata hivyo, kuna waumini ambao hata kama wangefundishwa mwongo mzima, kwa vile hulka ni hiyo hiyo, changu sitoi nikitoa nitafilisika, hawawezi kutoa hata punje ya haradali.

Tamko hilo linapowekwa kwenye mizani ya masharti ya ufaafu, hudhihirisha kuwa baadhi ya masharti hayo yametimizwa. Kwanza mzungumzaji anaamini kuwa wasikilizaji wanaweza kutenda kitendo walichoamrishwa na pili wasikilizaji wanaweza kutenda kitendo walichoambiwa wakitaka kufanya hivyo. Lakini masharti mengine ambayo yanahusiana na uaminifu na umuhimu yamekiukwa. Hivyo ni kwa sababu wasikilizaji hawawajibiki kutenda walichoambiwa kwani wana uhuru wa kukaa mbele au nyuma ya msikiti madamu mahali hapo panawafaa. Zaidi ya hayo, mzungumzaji hana haki ya kuwatoa watu nyuma ili waje mbele kudhalilishwa bure.

Mihimili ya unyenyekevu imekiukwa pia. Imamu alipaswa kuyajua matakwa ya maamuma wake na ayatilie maanani, kutoa sababu za kuwataka watende kitendo alichokusudia na kutimiza mahitaji ya wasikilizaji wake kwa kuwaonea huruma na kuelewa hali zao.

5. *Kwa sababu[[ imekuwa kawaida ya watu kufichamana hawataki kuonekana]].*
*Wanajificha huko nyuma*.

Katika tamko la pili, Imamu alizungumzia swala la maamuma kujificha katika safu za nyuma. Hapa anaendeleza hoja yake na kusisitiza kwa kutumia mbinu ya mwambatano wa kilekisia ambapo leksemi *"Kufichamana", "kujificha"*, na kinyume chake "*Hawataki kuonekana*" zimetumika katika aya moja. Nia yake ni kuwalaumu kwa tabia hiyo akitarajia kwamba maamuma wake watakubali kujaza nafasi za mbele ili waweze kuchangia katika kutoa sadaka.

Hata hivyo maamuma husika waliathirika kwa kuaibika kwa sababu ya kutajwa kwa kitendo chao katika khutuba. Wanaona kuwa Imamu hapaswi kuwalazimisha watu kutoa sadaka bali kinachofaa ni kuwahimiza na kuwakumbusha tu kwa kutaja faida za kutoa sadaka na hasara zinazotokana na ubakhili. Waumini waliweza kutambua kuwa kitendo neni hicho ni cha kuwalazimisha kutokana na jinsi Imamu alivyosisitiza swala la kukaa nyuma kwa kutumia mbinu mbalimbali kama zile zilizobaionishwa mwanzo.

Tamko hilo likitazamwa kwa darubini ya masharti ya ufelisiti hudhihirisha kwamba kuna ukiukaji wa desturi katika utekelezaji wa kitendo, ukiukaji wa umwafaka katika washiriki na muktadha, ukiukaji katika hali ya kutotenda kitendo neni kikamilifu na hali ya uaminifu. Hivyo ni kwa sababu kuwalaumu waumini kwa kukaa nyuma ya msikiti kulifanywa kimakosa. Kukaa mbele haimaanishi kwamba ndiyo sadaka itolewe kwani mtu anaweza kuitoa akiwa huko nyuma. Ilikuwa awahimize tu kwa kuelezea faida zinazotokana na utoaji sadaka. Washiriki hawawezi kutekeleza kitendo hicho kwa kulazimishwa kwani msikitini si mahali pa kuwalazimisha watu kutenda jambo lolote. Anachopasa kufanya ni kuwaelimisha juu ya umuhimu wa kutenda mambo Kadhaa wa Kadhaa yanayopendekezwa na kukaa katika safu za mbele.

Kulingana na tamko hilo, imebainika kuwa Imamu hakujihusisha na swala la kuwaelezea wasikilizaji wake sababu zenye mashiko za kuwataka watende kitendo alichokusudia kama inavyopendezwa katika kaida za unyenyekevu chanya na kama ilivyoelezewa kuhusu tamko la pili, mihimili mingine ya kaida hizo imekiukwa.

**Kuzindua:**

6. *Huu ndio mwezi pekee wa kuomba toba. [[Msigafilike katika mwezi huu]].*

Tamko la Imamu lilikuwa na nia ya kuwazindua wasikilizaji kusudi wajirekebishe na watubu kutokana na madhambi ambayo huenda wameyafanya ingawa kidhahiri lilikuwa na maana ya kuelimisha waumini juu ya hadhi ya mwezi wa Ramadhani na kuwakanya kutokana na kughafilikia msimu huo. Athari yake ilikuwa kuzinduka kwa waumini na kujiweka tayari kwa mabadiliko katika maisha yao katika musimu huo. Hivyo ni kwa sababu mwezi aliourejelea katika tamko hilo ni mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Mwezi huo ndio mwezi wa tisa katika kalenda ya Uislamu na musimu uliotengewa waumini wa Kiislamu ili wapate kufanya ibada ya kufunga siku ishirini na tisa au thelathini. Waumini hawa wanatakikana kuchukua fursa hii kutubia juu ya madhambi yao na wafanye bidii katika kutenda amali nzuri kama vile kuwasaidia maskini, mayatima, na wajane, na pia kulinda ndimi zao wasiropokwe na maneno ambayo huenda yakawaudhi wanadamu wenzao na kumbughudhi Mwenyezi Mungu. Upekee wake hutokana na saumu na ujira mkubwa unaopewa waja wa Mwenyezi Mungu ambao ni zaidi ya ule unaotolewa katika miezi mingine.

Kutokana na mafundisho ya Mtume Muhammad (SAW), kila amali aitendayo mwanadamu hulipwa mara kumi na ujira huo huongezeka hadi kufikia mara mia saba. Lakini saumu ujira wake ni mkubwa zaidi na aujuaye ni Mwenyezi Mungu. Hivyo ni kwa sababu mtu huacha chakula chake, vinywaji vyake na starehe zake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, tofauti na amali nyingine kama vile sala au zaka ambazo huenda zikatekelezwa kwa ajili ya riaa ama majivuno. Hata hivyo, vitendo vya heri inapaswa ving'ang'aniwe muda wote na Ramadhani iwe tu kilele na chuo cha kuwafunza waumini jinsi ya kuendesha maisha yao katika kipindi cha miezi kumi na mmoja iliyosalia.

Mwezi huo una maajabu yake kwani humlainisha hata jabari, humpoza hata asiyeambilika na husafisha na kuzifanya nyoyo za waumini kuwa kunjufu. Katika musimu huo, ndipo miskiti hujaa na waumini hutega masikio tayari kusikiliza ujumbe. Sala hudumishwa, sadaka hutolewa, almuradi matendo ya kheri huzingatiwa. Ni kipindi cha kugutuka na kutambua kwamba kweli kuna haja ya kurudi mbele ya Mungu. Kinachostaajabisha ni kwamba baada ya Ramadhani watu hurejelea mghafala na usahaulivu wao wa hapo kabla ya saumu.

Tamko hilo limetimiza masharti ya ufaafu. Kile maamuma wanachoombwa kutekeleza ni kitendo cha wakati ujao. Kwa hiyo sharti ya urejeleo wa yaliomo imezingatiwa. Sharti andalizi nayo imetekelezwa kwa vile mzungumzaji huamini kwamba msikilizaji wake ana uwezo wa kutenda kitendo alichomwomba kutenda na kawaida baadhi ya waumini wasipokumbushwa hawawezi kujirekebisha hata katika musimu kama huo. Mzungumzaji bila shaka huwataka wasikilizaji kutekeleza kitendo alichowaomba. Hivyo ni kusema kwamba ametilia maanani sharti la uaminifu pia. Halikadhalika, tamko hilo huchukuliwa kuwa ni jaribio la kumfanya

msikilizaji atende kitendo kilichokusudiwa na hivyo limetimiza sharti la umuhimu. Pamoja na hayo, mzungumzaji haonyeshi dalili kwamba kitendo anachorejelea humhusu pia. Kulingana na kaida za unyenyekevu,  ilipaswa aonyeshe ushirikiano na wasikilizaji wake na asijitoe katika swala la kutubu mbele ya mola wake, kwani naye ana madhambi kama wanadamu wenzake.

7. *[[Mwilini mwako huna sala…kuna wale ambao tunawaosha kwa mara ya kwanza na mwisho…tukakuzika katika sanda tatu, tukakuacha peke  yako, ukakuta uliyoyatanguliza]]*.

Kulingana na matumizi ya kawaida ya lugha matamko hayo huelezea hali inayomkumba kila Mwislamu pindi anapokata roho. Lakini  muktadha yanamojitokeza hutudhihirishia matumizi ya lugha kwa njia ambayo si ya moja kwa moja. Nia  yake ni kuwazindua waumini ili watambue kwamba kuna haja ya kujihami kwa sala tano kabla ya kufikiwa mauti. Athari ya tamko hilo ilikuwa kuzinduka kwa waumini na kuchukulia sala kama jambo muhimu ambalo litawahakikishia hatima nzuri.

Sala ni nguzo ya pili miongoni mwa nguzo za Uislamu na aidumishaye huchukuliwa kuwa ameidumisha dini. Sala ni amali itakayoangaliwa mwanzo siku ya Kiyama. Mungu akiridhika nayo siku hiyo, basi atakuwa radhi  na mja wake katika amali nyinginezo. Imamu anawakumbusha Waislamu wasighafilikie sala kwa sababu ndiyo amali itakayowafanya wasalimike na kunusurika kutokana na mateso ya huko kuzimuni ambako wataachwa peke yao bila mtetezi.

Mwislamu anatakikana kutawadha au kuoga inapomlazimu kufanya hivyo kabla ya kusali. Akisha utakasa mwili wake kwa namna hiyo analazimika kusali sala tano kila siku. Kutokuwa na sala mwilini, maana yake ni kutosali kabisa. Kuoshwa kwa mara ya kwanza na mwisho maana yake ni kutojali kutawadha wala kuoga kwa ajili ya sala mpaka pale anapofariki ndio Waislamu wamwoshe ili atayarishwe kwa mazishi ya kidini. Matamko hayo yameenda sambamba na urejeleo wa yaliyomo. Imamu alizingatia masharti ya ufaafu katika kitendo neni chake na kwa hiyo alifanikisha lengo lake.

8. *[[Mwislamu kila asubuhi ... kwa mfano hapa Lwakhakha, hufikiria juu ya kitu kimoja, mahindi]], ndiyo lugha iliyoko sasa. Butiru "mahindi", Nakhupa "mahindi" madereva nao "usukani",wenye maduka, walioko mashambani hivyo hivyo. Kila mtu katika kazi yake inayomdanganya ukawa humwabudu Allah. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu anasema kwamba "Wana nyoyo lakini hawatambui kwazo".*

Kauli hiyo, iliwalenga waumini ambao hujishughulisha na kazi zao wakapuuza kutekeleza ibada ya kudumisha sala. Nia yake ilikuwa kuwazindua juu ya umuhimu wa kutilia maanani amri ya Mwenyezi Mungu inayohusiana na sala tano. Anaona kwamba waumini wasiosali hudanganyika na kazi zao na hali watakuja kuziacha siku moja faradhi ya mauti itakapowajia, waulizwe juu ya maasi yao na waadhibiwe kwayo. Kulingana na majibu ya wasailiwa, athari ya tamko hilo ilikuwa kuzinduka na kujiweka tayari kughairi mienendo yao.

Waumini wa Kiislamu wamefaradhishiwa sala tano kila siku. Sala ya subhi husaliwa alfajiri punde tu baada ya kutoka usingizini. Wakisha maliza sala hiyo, wanaruhusiwa kwenda kufanya kazi za halali ili kujikimu kimaisha. Sala za dhuhuri na aswiri husaliwa katika nyakati za adhuhuri na alasiri. Ufikapo wakati wa kila moja wapo ya sala hizo, wote hutakiwa wasitishe kazi zao waende wakasali msikitini na kama kuna udhuru wasalie kazini au nyumbani kwao kisha waendelee na shughuli zao. Magharibi ni sala isaliwayo wakati wa magharibi punde tu baada ya jua kutua hadi hapo wekundu unapotoweka katika upande wa magharibi. Kutoweka kwa wekundu huo hutangaza kuingia kwa wakati wa sala ya mwisho katika siku ambayo ni Isha. Hairuhusiwi kuacha sala hizo zote au baadhi yake na afanyaye hivyo huchukuliwa kuwa amekufuru.

Kauli hiyo imetimiza masharti yote ya ufelisiti isipokuwa lile linalomtaka mzungumzaji atoe matamko yake kikamilifu. Ikiwa anaamini kuwa wasikilizaji wake wanadanganyika tu lakini wanaujua ukweli, inakuwaje dalili anayoitoa ili kuthibitisha imani yake hiyo iwe inayoonyesha kuwa hawatambui. Isitoshe hali hiyo ya kutotambua ikazidi kuwa mbaya kwa kuwa imefikia kiwango cha mnyama ambaye kama ng'ombe alivyo, pamoja na kuwa na ubongo, gari humkaribia hali ya kuwa anaendelea kwenda mbele, hana habari.

**Kuelimisha:**

9. *[[Dhulkaada ni mwezi wa kutoa sadaka]]*.

Muktadha ambamo kitendo neni hicho kimejitokeza hudhihirisha kuwa nia ya Imamu ni kuwashtua wasikilizaji ili watanabahi watoe sadaka. Wasililizaji waliweza kutambua nia hiyo ingawa udhahiri wa tamko ulionyesha maana ya kuelimishwa kuhusu mwezi huo na mambo ambayo yanapendekezwa kutendeka ndani yake. Athari ya tamko ni kuzinduka kwa waskilizaji na kujiweka tayari kutoa sadaka.

Kawaida miezi ya Kiislamu hufungamanishwa na vitendo maalum vya kheri kama vile kufunga siku kumi katika mwezi wa Muharram, kusherehekea maulidi ama kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (SAW) katika mwezi wa Rabiul Awwal, kusherekea mwezi wa Rajab ambamo sala tano zilifaradhishwa kwa Waislamu, kufunga katika mwezi wa Ramadhani, kufunga siku sita katika mwezi wa Showwal, kufunga siku ya Arafa ambayo ni siku ya tisa katika mwezi wa Dhulhija au siku zote tisa za mwanzo katika mwezi huo, kufunga siku tatu kila mwezi, kuomba sana dua katika mwezi wa Safar ambamo mtume alifariki, na kuhiji katika mwezi wa Dhulhija.

Kwa mujibu wa Imamu huyu Dhulkaada ni mwezi wa kutoa sadaka. Kufungamanisha utoaji sadaka na mwezi huu ambao ni mwezi wa kumi na moja kulingana na kalenda ya Kiislamu, kulikusudiwa kuwazindua wasikilizaji waone umuhimu wa kutenda amali njema ndani yake. Ukweli ni kwamba hakuna mahala katika Kur'ani wala hadithi za Mtume (SAW) ambapo pametajwa kuwa sadaka mwezi wake ni Dhulkaada. Kinachowapelekea kufungamanisha sadaka na mwezi huu, yumkini, ni kuwashawishi wasikilizaji kuchanga pesa nyingi katika kipindi hicho.

Tamko hilo limetimiza masharti kwani mzungumzaji ni mwenye mamlaka kwa hiyo ana haki ya kuwasihi wasikilizaji juu ya utendaji wa jambo alilozungumzia. Aidha, ana imani kwamba kitendo lazima kitendeke. Wasikilizaji kwa upande wao wana uwezo na wanawajibika kufanya waliloambiwa.

**Kugombanisha:**

10. *[[Mmekuwa wakaidi juu ya aya za Mwenyezi Mungu na Hadithi za Mtume (SAW)]]?*

Waislamu wa Msikiti ulimotolewa matamko ya sita, saba na nane, walikuwa na tabia ya kuchelewa kwenda msikitini katika siku ya Ijumaa. Hivyo ni kwa sababu walidai kwamba walichoshwa na khutuba za Imamu wao ambazo zilikuwa na mashambulizi ya mara kwa mara. Kuchelewa kwao kulitafsiriwa na Imamu kama ukaidi kwa sababu Kur'ani na Hadithi huwahimiza waumini kwenda msikitini mapema ili wawahi khutuba.

Nia ya tamko ni kuwalaumu wasikilizaji kwa sababu ya kuchelewa. Hata hivyo waumini waliathirika kwa kuudhika zaidi na mashambulizi yasiyokuwa na kikomo. Ingawa kitendo cha Imamu cha kuwalaumu wasikilizaji kilikusudiwa kuwazindua wapate kuwahi sala ya Juma, maamuma hawakumwelewa hivyo bali waliona kwamba alitaka tu kuwashambulia.

Tabia ya mwanadamu haibadiliki ovyo. Humchukulia mtu muda mrefu wa subira na kutoa motisha ili apate kubadilisha mwenendo wa mlengwa wake. Asipofanya hivyo, juhudi zake zitaambulia patupu, achoke, azue ugomvi na hatima yake aeleweke vibaya na watu wake ambao amepewa jukumu la kuwasimamia. Ni vyema kutambua kuwa safari ya maili elfu moja huanza kwa hatua moja na hadithi ya Kichina ya "mzee mjinga aliyeondoa milima" ni mfano mzuri wa kuigwa.

Tamko hilo huonyesha kuwa Imamu alikiuka sharti la uaminifu kwa sababu kubadilisha tabia si jambo rahisi hivi kwamba matokeo yake yatapatikana katika kipindi kifupi. Isitoshe hata kama tungechukulia kuwa waumini hao wamekuwa wakaidi, bado tungejiuliza je ukaidi huo ni juu ya nini hasa. Si lazima uwe juu ya aya za Mwenyezi Mungu. Kusema hivyo bila ithibati kunaweza kuchukuliwa kama kumsingizia mtu jambo ambalo hakulitenda wala hanuii kulitenda. Kama angalifanya uchunguzi angaligundua kwa nini waumini huchelewa kuja msikitini. Jibu hilo lingalimpatia suluhisho la kudumu na lingemwepushia ugomvi na waumini wake.

Kwa vile, sharti la uaminifu ni kiungo muhimu kati ya viungo ambavyo vibadiliki vitatu vinavyopaswa kuungana ili kufanikisha lengo la mzungumzaji, ni sawa kudai kwamba tamko halikufaulu. Mzungumzaji hakutilia maanani matakwa ya wasikilizaji, hakuonyesha matumaini mazuri wala hakutoa sababu za kutenda tendo aliokusudia katika tamko lake. Kwa hiyo, alikiuka pia kaida za unyenyekevu chanya.

11. *[[Mmechangia kushindwa kwangu kwa ajili ya viburi vyenu]]...lakini nyinyi shingo zenu mmezifanya ngumu...kama Wayahudi.*

Kuchangia kushindwa kwa Imamu huashiria kuwa waumini wamekataa kufanya yale anayowaamrisha na kwa hiyo wameonyesha kuwa hawako tayari kushirikiana naye katika bo lolote. Kuwa na shingo ngumu ni kutokubali kubadilisha msimamo na Imamu alikatiza maneno yake mara kwa mara kuonyesha uchungu aliokuwa nao. Imamu anaona kuwa kinachowafanya kuwa wakaidi ni hisia za kujiona kuwa wao ni bora kuliko yeye kwa hiyo hawaambiliki.

Tamko hilo nia yake ilikuwa kuwalaumu waumini kwa sababu ya kutojali mafundisho ya mhubiri wao. Wasikilizaji walitakikana waache ukaidi wao na washirikiane na Imamu wao ili waonekane wakichangia katika kufanikisha majukumu yake. Athari ya tamko hilo kwa wasikilizaji ilikuwa kuudhika na waliyoyaona kuwa matusi ya Imamu. Hisia za maamuma huonyesha kuwa waliweza kutambua matumizi ya lugha kwa njia iso dhahiri.

Msikiti huimarishwa na waumini wa Kiislamu wakisaidiana na Imamu wao. Ili kutekeleza jukumu hilo kuna haja ya kudumisha uhusiano mwema kati ya watu wa pande hizo mbili. Lakini, endapo uhusiano huo utazoroteka basi mambo yatabadilika na kuwa kama yaliyomkumba Nabii Musa na wana wa Israeli ama Wayahudi. Kwa mujibu wa Kur'ani wana wa Israili walimsumbua sana Nabii Musa (AS). Kwa mfano alipowaamrisha kwenda vitani wakapigane na adui yao walikataa na kusema: "Nenda, wewe na Mola wako mkapigane. Sisi tutakaa hapa"(Al-Farsy,1984).

Mfano mwengine ni wakati walipoamrishwa kumchinja ng'ombe wakakataa na kusema: "Watuchukulia kuwa watu wa kuchezea shere?" (Afarsy,1984).

Msemaji wa tamko ni mwafaka kwa sababu ndiye aliye na mamlaka ya kuwaongoza waumini katika sala. Hadhira pia ni mwafaka kwani ni ya waumini wa Kiislamu. Hata hivyo, masharti ya mahali ama muktadha na wakati wa kutoa matamko yalikiukwa. Khutuba ya Ijumaa huchukuliwa kama sehemu ya sala ya Ijumaa na sala ni ibada. Kwa hiyo, mahali pa kuhutubia si mwafaka kwa kuzua ugomvi na matusi bali panahitaji matumizi ya maneno ya hekima na busara

la sivyo watu wataharibikiwa katika ibada yao. Vivyo hivyo, wakati wa kutoa matamko kama hayo ni kwenye vikao visivyokuwa vya ibada. Aidha kitendo neni hicho hakikutendwa kikamilifu kulingana na matlaba ya masharti ya ufaafu kwani mzungumzaji alikosea alipodai kuwa wasikilizaji wamechangia kushindwa kwake. Hamu ya wasikilizaji si kushindwa kwake bali ni kuona kwamba wanashirikiana na kuheshimiana.

Kwa hiyo, vibadiliki viwili ambavyo ni mwelekeo wa kitendo na sharti la uaminifu havikuungana na nguvu za hoja kama inavyopendekezwa na Searle ili kuzua hisia zilizolengwa na mzungumzaji. Vivyo hivyo, kaida za unyenyekevu chanya zilikiukwa katika tamko hilo. Hivyo ni kwa sababu wasikilizaji hawalichukulii jambo analozungumzia kuwa zuri kwao na mzungumzaji ameonyesha msimamo wa kujitenga na waumini. Aidha Imamu haonyeshi ana matumaini na yale anayoyakusudia kutokana na matamko yake. Halikadhalika, hakutimiza mahitaji ya wasikilizaji wake kwani ilikuwa aelewe hali zao na kuonyesha ushirikiano nao.

**Kuonya:**

12. *[[Unaenda kwa mganga akakwambia akukinge. Akakupa majini, akakuyapandia njiani. Anakukata chale ili kukukinga]]. Mwenyezi Mungu anasema ulikwenda kuabudu mizimu, leo jitegemee*.

Katika tamko la 5 la vitendo neni vitathminishi, Imamu huyu aliwadunisha waganga kwa kuwachukulia kuwa mashetani na wajinga. Katika tamko hili aliwaandama waumini na kutaja yale wanayoyaendea na matokeo yake. Katika Suratul Yasin, Mwenyezi Mungu anasema: "Jipambanueni leo enyi wahalifu. Sikuwaonyeni kuwa msimwabudu shetani hakika yeye kwenu ni adui aliye wazi. Na nikawaamrisheni kuniabudu mimi. Hii ndiyo njia yangu iliyonyoka?"(Al-Farsy, Suratul Yasin, Aya 59-61). Imamu alirejelea aya hiyo katika matamko hayo ili kuwaonya dhidi ya matendo yao.

Kwa hiyo, muktadha wa matamko hayo hudhihirisha kuwa nia ya Imamu ni kuwaonya waumini dhidi ya matendo yao kwa sababu watakuja kuadhibiwa na Mola wao siku ya kiyama. Athari ya kitendo neni hicho ni kwamba baadhi ya waumini walizingatia onyo hilo na kuamua kuacha kwenda kwa wanganga. Waumini wengine walipuuza matamko ya Imamu na kwa hiyo hawakutilia maanani onyo hilo.

Kulingana na mafundisho ya Uislamu, kinga hupatikana kutoka kwa Mwenyezi Mungu na sio kwa wapiga ramli au mganga mwengine yeyote. Kwa hivyo kumwabudu mtu wa aina hiyo ni kitendo cha kumshirikisha Mungu na viumbe ambacho mwenye kukitenda, asipotubu atakuja kuadhibiwa siku ya kiyama.

Matamko hayo huelezea tabia ya kuwaendea waganga mtu anapopata shida au kwa ajili ya kusaidiwa ili asipate madhara yoyote. Waganga wanaoendewa wanaweza kuwa wapiga ramli au wale wanaotuma majini kuwatendea mambo yao. Imamu anaonyesha msimamo wake kwamba kujiingiza katika mambo kama hayo ni sawa na kuabudu mizimu kitendo ambacho hakifai kwa muumini kukikaribia.

Hapa sharti ya urejeleo wa yaliomo (*propositional content condition*) imetimizwa kwa sababu kitendo neni humtaka msikilizaji aache kutenda yale yatakayompelekea kutengwa katika kundi la wahalifu, tukio ambalo ni la wakati ujao. Sharti andalizi (*preparatory condition*) nalo limetimizwa na mzungumzaji kwa sababu yeye huamini kwamba tukio hilo litajitokeza na litakuwa baya kwa wasikilizaji na kwamba bila ya kuwaonya hawawezi kujua kwamba kutatokea tukio kama hilo. Mzungumzaji ametimiza pia sharti la uaminifu (*sincerity condition*) hivyo ni kwa sababu hafanyi masihara kuamini kwamba hatima mbaya kama hiyo itajitokeza siku ya akhera na itawakosesha raha wasikilizaji wake. Isitoshe Imamu ametilia maanani sharti la umuhimu (*essential condition*) linalomtaka atoe tamko lichukuliwalo kama jaribio la kumfanya msikilizaji atambue kuwa kitakachotokea hapo mbeleni kitakuwa na matokeo mabaya.

Kwa upande mwengine, Imamu alikiuka kaida za unyenyekevu chanya jambo ambalo liliwapelekea baadhi ya wasikilizaji wake kutotilia maanani onyo alilolitoa. Alipaswa kuwaelezea waumini kuwa jambo alilozungumzia lingeleta tija nzuri kwake binafsi na kwa jamii ya waumini kwa ujumla kama lingezingatiwa. Halikadhalika angetoa sababu za kuwaonya dhidi ya kitendo cha kuwaendea makuhani na waganga na kuwahakikishia kuwa anajua na kuyajali matakwa yao. Fauka ya hayo angetoa ubashiri wa jinsi maisha yao yatakavyokuwa endapo wataepukana na waganga na hila zao ili kuwapa matumaini kwamba asaa wakapata mustakbala mwema.

13. *Tumebaini shetani aliyelaaniwa- Ibilisi. Lakini[[ waumini wameshindwa kutofautisha kati ya Mwenyezi Mungu na shetani (AKALIA) unamkuta mtu anachanganya na yeyote anayechanganya ameacha Uislamu]]*.

Maimamu huwasihi waumini mara kwa mara wasimwabudu shetani lakini hawazingatii amri za Mwenyezi Mungu kama zilivyobainishwa katika mafundisho ya dini. Wanafanya juu chini kuelezea sifa za shetani na mikondo yake ili wapate kumwepuka, lakini inaelekea kuwa juhudi za Maimamu hao zimeambulia patupu. Ndio maana Imamu huyu analia na kuonyesha uchungu alio nao juu ya tabia na vitendo vya kuchanganya mambo. Mara wanafuata amri ya Mwenyezi Mungu na mara nyingine wanamtii shetani.

Nia ya Imamu ilikuwa kuwaonya waumini dhidi ya kuchanganya utiifu, kitendo ambacho kinaweza kuwatoa katika Uislamu. Maamuma walitambua nia hiyo na baadhi yao wakaathirika kwa kuzingatia onyo hilo. Waliguswa sana na kilio cha Imamu na kubaini kwamba anayoyazungumzia si utani. Hata hivyo, Maamuma wengine walikasirika kutokana na kile walichoona kwamba Imamu anawachukulia kuwa watenda maasi huku akiona kuwa yeye amekamilika katika mambo yanayohusiana na ucha Mungu.

Matamko hayo yametimiza sharti la urejeleo wa yaliomo kwa sababu yanazungumzia tukio la wakati ujao. Yametekeleza vilevile masharti ya uaminifu na umuhimu. Hivyo ni kwa sababu mzungumzaji anaamini kwamba tukio litakuwa la hatari kwa msikilizaji. Halikadhalika, matamko hayo huchukuliwa kama jitihada ya kuwafanya wasikilizaji watambue kwamba tukio la wakati wa hapo mbeleni litakuwa la hatari. Aidha mzungumzaji anaamini kuwa wasikilizaji hawaoni kwamba kutokea kwa tukio analozungumzia ni jambo linaloyumkinika. Hivyo ni kwa sababu baadhi ya waumini huona kwamba dini haiwazuii kufanya mambo yao madhali wamesali na kutimiza baadhi ya nguzo za Uislamu.

Kwa upande wa unyenyekevu, imebainika kuwa mihimili yake haikuzingatiwa na mzungumzaji. Kwanza, yeye mwenyewe alijitenga na wasikilizaji kwa kutojiweka miongoni mwa wale ambao wanahusika na kitendo neni hicho. Pili, hakuonyesha matumaini kuwa wangeweza kutenda jambo alilokusudia. Tatu, Imamu alishindwa kuzingatia matakwa ya maamuma, kuwaahidi kuwa

wakizingatia onyo hilo watachuma matunda mazuri na kutoa sababu za kuwataka watende kitendo kilichotarajiwa.

14. *Ukisema hatacheza lakini ataenda tu kwa wajomba wanirejeshee ng'ombe angalau mmoja,[[ hiyo ni shirki]].*

Kawaida tamasha kubwa la tohara huandaliwa, ngoma zikachezwa, nyimbo anuwai zikaimbwa na vijana watakaotahiriwa wakashangiliwa. Katika siku ya kupashwa tohara, vijana hao hupelekwa kwa wajomba zao ambako huzawadiwa ng'ombe au mbuzi kulingana na mahari aliyoitoa baba yake kwa baba mkwe. Vitendo hivyo ndivyo vinavyorejelewa na Imamu kama vitendo vya kishirikina. Nia ya tamko hilo ni kuwaonya waumini wasishiriki katika sherehe ya tohara. Athari ya kitendo neni hicho ilikuwa kukasirika kwa wale ambao wanaenzi utamanduni wao, ilhali waumini wengine wakizingatia onyo la Imamu na kukubali kuwatahiri watoto wao wakiwa wachanga.

Tamko hilo limejitokeza moja kwa moja kama kitendo neni cha kudai kwamba kuchukua zawadi wakati kijana anajiandaa kwa tohara ni shiriki kulingana na mafundisho ya Uislamu. Nyuma ya madai hayo kuna kitendo neni cha kuwaonya wale wote wanaokubali kuchukua zawadi kama hiyo. Lakini tamko hilo likichunguzwa kwa makini, hudhihirisha kuwa kuna Maamuma wanaokubali kuwa matendo yanayokinzana na mafundisho ya Uislamu kama vile kumruhusu kijana kucheza ngoma, kunywa pombe, kutangamana kwa wana wake na wanaume, matambiko na kadhalika ndiyo yasiyofaa.

Kutokana na imani hiyo Maamuma hao waliamua kuchukua tu zawadi ambayo wanaona kuwa ni halali yao. Pamoja na jitihada yao hiyo inayolenga kuonyesha utiifu wao kwa Muumba wao, wanaonywa dhidi ya kuchukua zawadi. Kwa kweli kulikuwa na haja ya Imamu kutoa maelezo kamili na ushahidi kutoka katika duru zinazoaminika ili kuthibitisha kuwa hata kitendo cha kuchukuwa zawadi hiyo ni shiriki. Kufanya hivyo kungechangia pia kuthibitisha kwamba Imamu amezingatia vibadiliki muhimu ambavyo huungana na urejeleo wa yaliomo ambavyo ni nguvu za hoja inayowasilishwa, mwelekeo wa kitendo (hali ya maneno kuafikiana na ulimwengu) na sharti la uaminifu. Vivyo hivyo, ili kufanikiwa katika malengo yake Imamu alipaswa kuzingatia usifabia katika matumizi ya lugha kwa kuhakikisha kuwa linalozungumziwa ni zuri na humhusu

pia, na kwamba anatilia maanani matakwa ya wasikilizaji wake. Aidha alipaswa kutoa sababu za kuwataka kutenda kitendo kinachozungumziwa.

15. *Isipokuwa tukitubia…tukikataa… tutaonekana kama Waislamu lakini [[Uislamu hakuna.Twafuata Ibilis]]*.

Kutubu hugubiza kuacha matendo mabaya, kujuta juu ya maovu yaliyofanywa hapo awali, kuamua kutorejelea maovu hayo hapo mbeleni na kumwomba Mwenyezi Mungu msamaha. Kukubali kufanya toba ni kitendo kinachomtambulisha Mwislamu na kukataa ni kumfuata shetani, kwa mujibu wa kauli hiyo. Kauli ya Imamu inaonyesha kuwa amekata tamaa kutokana na tabia ya Waislamu.

Nia ya Imamu ni kuwaonya wasikilizaji wake dhidi ya kumtii shetani na kumwasi Mwenyezi Mungu. Athari ya tamko hilo ilikuwa kukasirika kwa baadhi ya waumini kwa hoja kwamba Imamu amewafungamanisha na shetani aliyelaaniwa na Mungu na kwa hivyo hawatambuliwi kuwa Waislamu.

Matamko hayo yametimiza baadhi ya masharti ya ufelisiti na kukiuka baadhi yake. Sharti la urejeleo wa yaliomo limetimizwa kwa sababu kitendo kinachorejelewa ni cha wakati ujao. Masharti andalizi yamezingatiwa pia na tamko kwa vile mzungumzaji huamini kuwa tukio likitokea litakuwa na madhara kwa msikilizaji na kuwa si wazi kwa msikilizaji kwamba tukio linalorejelewa litatokea. Sharti la uaminifu nalo limetimizwa kwani mzungumzaji huamini kuwa tukio analozungumzia likitokea bila shaka litakuwa na madhara kwa msikilizaji. Kwa upande mwengine, tamko lilikiuka sharti la umuhimu. Hivyo ni kwa sababu muktadha lilimojitokeza haumwongozi msikilizaji kutambua kuwa tukio lililotajwa litakuwa baya na lenye madhara. Hivyo ni kwa sababu taarifa iliyotolewa kuhusu mada iliyokuwa ikizungumziwa haikuwa kamili bali iligusiagusia tu mambo kijuujuu.

Tamko hilo pia lilikiuka kaida za unyenyekevu chanya ambazo zingesaidia kufanikisha lengo la mzungumzaji. Kwanza kabisa, mzungumzaji hakuonyesha kuwa na matumaini kwamba wasikilizaji wake wangeweza kutilia onyo lake maanani wakatubia juu ya madhambi yao. Ilikuwa afanye hivyo ili kuwapa motisha. Pili, mzungumzaji haelekei kuyajua matakwa ya

wasikilizaji wake wala kuyazingatia kwani wao huona kuwa ni Waislamu na kwa hiyo hawataki kuhusishwa kwa vyovyote vile na shetani. Wakadhalika, haonyeshi dalili ya kuelewa hali za wasikilizaji wake. Angalizielewa asingerukia mahitimisho kuwa wanaonekana kama Waislamu lakini wanafuata Iblis kama inavyobainika katika matamko ya 13 na 14.

16. *Kama walienda Mutoto na kufuata… shetani kutoka Kenya akajitambulisha na akatambua wafuasi wake. Ni kama yule aliyekuwa katika kikao cha Makuraishi. Mutoto [[hamkwenda kuona kitu isipokuwa Iblis na watoto wake]].*

*Mutoto* ni kitongoji kilioko nje kidogo ya mji wa Mbale, wilayani Mbale mashariki mwa Uganda. Ni masafa ya maili moja kutoka mjini Mbale. Inaaminika kwamba Bwana Fuuya Mgisu wa kwanza kutahiriwa baada ya kupata ushawishi na kuhimizwa na mke wake Nabarwa Mkalenjini, alikuwa akiishi katika kitongoji hicho. Kwa vile sherehe ya kwanza ya tohara ilifanyika hapo, ikaamuliwa kwamba kabla ya kufanyika kwa shughuli hiyo katika sehemu nyinginezo sherehe ya uzinduzi ifanyike. Vijana wanaotakikana kutahiriwa kutoka katika sehemu mbalimbali za Bugisu na wageni kutoka serikalini na katika kabila la Wabukusu ambao ni jamaa za Wagisu kutoka Kenya, hualikwa. Pombe tele huandaliwa na mbuzi Kadhaa kuchinjwa ili kuwaridhisha *baakuuka* ambao ndio wana nguvu za kuwafanya vijana wastahimili maumivu ya kisu pindi wanapotahiriwa.

Aliyerejelewa kama shetani kutoka Kenya ni kiongozi wa kundi la wageni wanaokuja kushuhudia uzinduzi wa sherehe za tohara inaofanyika Mutoto kila baada ya miaka miwili. Kiongozi huyo amesawiriwa kama Chifu wa kutoka sehemu za Najdi huko Saudi Arabia, aliyehudhuria kikao cha Makuraishi ambacho kilifanya njama ya kumuua mtume Muhammad. Waliorejelewa kama walienda Mutoto na kofia ni Waislamu. Tashibihi na kinaya hiyo hudhihirisha hisia za Imamu juu ya tamasha hilo kwamba ni shughuli mbaya na ni ya kishetani.

Nia ya tamko hilo ni kuwaonya Waislamu dhidi ya kushiriki katika hafla hiyo ya uzinduzi wa musimu wa tohara. Baadhi ya waumini walitambua nia hiyo na kuathirika kwa kuamua kutohudhuria sherehe hiyo. Hata hivyo kuna waumini wengine walioona kwamba Imamu alitumia lugha ya matusi, kwa hiyo wakaathirika kwa kuudhika.

**Kutahadharisha:**

17. *Wanamanjia [[mmekataa kuwatahiri wana wenu]] mnasubiri wakue mfuate shetani?*

Wanamanjia ni wenyeji wa wilaya ya Bududa moja wapo ya wilaya za Bugisu. Kuna ada ya kuwatahiri wavulana wanapobaleghe miongoni mwa Wagisu, kinyume na inavyotakikana katika Uislamu ambapo mtoto hutahiriwa katika siku ya saba baada ya kuzaliwa. Sababu ya kufanya hivyo ni kutaka washerehekee kwa kucheza ngoma na kushiriki katika miviga inayoambatanishwa na tohara. Sababu nyingine ni kushikilia imani kwamba mtoto akitahiriwa akiwa mchanga, maisha yake ya kindoa hayatakuwa mazuri kwani hatabarikiwa kupata watoto. Aidha, kumtahiri akiwa kijana kutamwezesha babaake kurejesha sehemu ya mali aliyoitoa kama mahari kutoka kwa wakwe zake. Washangiliaji wa tohara ya utuzima nao hushikilia kuwa ni njia pekee ya kuwakomaza vijana kwani wakivumilia makali ya kisu cha ngariba, huwa wameonyesha kuwa wamekomaa kiakili na kimwili na kwa hiyo wanaweza kupambana na maisha.

Nia ya tamko hilo ni kuwakemea wasikilizaji ili wajikosoe na wawatahiri watoto wao kulingana na mafundisho ya dini ya Kiislamu. Wasikilizaji walitambua nia hiyo na baadhi yao wakaathirika na kitendo neni hicho kwa kukasirika wakiona kwamba Imamu anawashambulia na kuwaaibisha hadharani.

Tamko limetimiza baadhi ya masharti ya ufelisiti na kukiuka mengine. Imamu ni mwenye mamlaka lakini mahali alimotolea tamko si mwafaka ikizingatiwa kuwa mambo yanayohusiana na utamaduni hayawezi kujadiliwa kwa kina katika muda mfupi kama huo wa khutuba. Mambo hayo yamekita mizizi kiasi kuwa watu wengi wa jamii ya Wagisu huyachukulia kuwa ni ibada ambayo wanajamii hawana budi kuitekeleza. Kwa hiyo, kutarajia kwamba yataachwa kwa urahisi hakuendani na uhalisi wa mambo na ni kukiuka sharti la uaminifu. Kaida za unyenyekevu chanya zimekiukwa pia kwa vile mzungumzaji hakuonyesha kuyajali maslahi ya wasikilizaji, kuelewa hali yao wala kutoa sababu za kuwataka watende kitendo kilichokitwa katika tamko lake. Vivyo hivyo, Imamu hakuwapa matumaini ili kuondoa hofu waliyonayo kuhusu kuwatahiri watoto wao wakiwa wachanga.

18. *Na nyinyi watu wa kisiwa hiki cha Makuduyi, [[mwataka kuwa kama Waizraili]]? Sisi ni wana wa Israili au watu wa lailaha ill'Allah? Kwa nini tunakuwa na roho ngumu?*

Tamko hilo linawasawiri maamuma wa msikiti huo kama Waisraili ambao hawapatani na Waarabu, bali hulumbana mara kwa mara. Kwa hiyo uhusiano wa Imamu huyo na Maamuma wake ni wa vuta nikuvute.

Nia ya Imamu ni kuwalaumu Waislamu wa mtaa wake kutokana na uhusiano mbaya uliopo kati yao. Hata hivyo Waislamu hao waliathirika kwa kuudhika wakidai kwamba Imamu aliwatukana.

Kuwarejelea watu wa mtaa wake ambao hauko karibu na bahari kama "*watu wa kisiwa hiki*" kuna maana ya watu waliojitenga na wenzao kitabia kama walivyojitenga Waisraili na Waarabu. Imamu anawataka wasikilizaji wake wajitambulishe na Uislamu na wasiwe wenye kuvutana na viongozi wao mara kwa mara kama Waisraili walivyofanya. Maelezo yaliyotolewa katika tamko la 7 kuhusu masharti ya ufelisiti husadifu hapa pia.

19. *Lakini mwakazania nyumba* zenu. *Kila mmoja wenu alioko hapa hulala katika nyumba nzuri kwenye godoro la inchi sita kwa sita, blanketi maridadi… kama mngekuwa mkinunua hayo tukayatandika msikitini, tukasalia juu yake! [[Mwakazania dunia lakini kwa Mwenyezi Mungu mtampekeleka nini]]?*

Imamu anazungumzia hali iliyotanda miongoni mwa Waislamu walio chini ya uongozi wake. Kwa hiyo, ametenda kitendo neni cha kutaja yale wayatendao dhahiri shahiri. Kwa kufanya hivyo, ametenda kitendo kingine cha kutahadharisha ambacho ni muhimu zaidi ijapokuwa kwa njia iso dhahiri. Matamko hayo yametolewa kwa nia ya kuwatahadharisha wasikilizaji dhidi ya kuambulia patupu mbele ya Mwenyezi Mungu ikiwa hawatakuwa na amali nzuri ya kuorodhesha kwake siku ya kiyama. Athari ya tamko hilo ilikuwa kuzinduka na kuahidi kuwa wataitumia mali yao katika kutenda amali nzuri itakayowafaa duniani na akhera.

Kukazana katika utendaji wa kazi yoyote ni jukumu la kila mwanadamu. Hivyo ni kwa sababu uvivu husababisha hali ya ufukara na unyonge ambao unampelekea mtu kuombaomba. Hata

hivyo, ukibarikiwa katika kazi yako ukachuma pesa, yafaa uwasaidie binadamu wenzako na utoe pia sadaka kwa ajili ya kudumisha uhusiano mwema kati yako na mola wako. Si vizuri kujali maslahi yako tu bila kuyajali maslahi ya jamii unamoishi. Miskiti yafaa ifanyiwe ukarabati na iwekewe mazulia maridadi ili waumini wakae mahali kuzuri na sio kwenye vumbi. Nyumbani kwa waumini kumetandikwa mazulia mazuri na kupambwa kwa mapambo aina aina. Hakuna anayeweza kughafilikia suala la usafi nyumbani kwake. Lakini mambo ya kuipamba misikiti, baadhi ya Waislamu huona kuwa hayawahusu ndewe wala sikio. Anayehusika ni Imamu.

Tamko hilo limetimiza masharti ya ufelisiti kwa sababu aliyelitoa ni mwenye mamlaka, walioambiwa ni hadhira mwafaka ya waumini wa Kiislamu ambao wanaweza kutenda kile wanachoambiwa na limetolewa kikamilifu. Imamu ametekeleza pia shurutu za uaminifu na umuhimu kwani hakuna utani katika ayasemayo na kuwasaidia watu na kuchunga usafi wa msikiti ni kwa manufaa yao.

**Kuhimiza:**

20. *Waja wa Mungu. Baada ya hayo mliyosikia na ambayo hamkuyaelewa….sisi waja wa Allah twafanya mambo yetu tunavyotaka. Twatembea tutakavyo na ibada twaifanya tutakavyo*. *Wenye ndevu, mikono yao iko kwenye ndevu zao na walionyolewa kishaurini mikono yao iko kwenye vichwa vyao. [[Baadhi yetu, jambo ambalo limetufanya tuzubae ni kupenda utukufu*.*Wengine mnajifanya watukufu…wengine ni kwa sababu ya mali, wengine mavazi, wengine maumbo]]*. *Lakini tumeelimishwa kuwa utukufu ni wa Mwenyezi Mungu na mtume wake.*

Kawaida mtu akitoa ushauri anatarajia msikilizaji auzingatie. Lakini chambilecho wavyele, mwenye akili ishara humtoshelezea. Ilivyombainikia Imamu huyu ni kwamba baada ya kutoa matamko kadhaa, nyuso za maamuma wake hazikuonyesha ishara ya kuyatilia maanani. Ndiyo maana akachukulia kwamba kusikia wamesikia lakini hawakuelewa. Pamoja na hayo, hatumwoni Imamu wetu akikata tamaa, bali anaendelea kuwaandama walengwa wake, lakini mara hii anabadilisha mbinu na kutumia lekizemi husishi “sisi” badala ya “nyinyi” ili kupunguza makali, akitaraji kuwa huenda wakazinduka. Pengine wakitambua kwamba wao ni waja tu wa Mwenjezi Mungu na kwa hiyo wanapaswa kumtii Muumba wao popote walipo na katika mambo yao yote wayatendayo, wanaweza wakabadilika. Anawahimiza kusikiliza mahubiri

yanapowasilishwa kwao kwa makini na kuwaonya dhidi ya kupenda utukufu kwa sababu ndio chanzo cha kuzubaa na kutoyajali majukumu wanayopewa kama waumini.

Kwa hiyo nia ya tamko ni kuhimiza na kuonya kwa wakati mmoja; kuwahimiza waaumini wajali mafundisho ya dini na kuwaonya dhidi ya kushiriki katika vitendo vinavyoweza kuwaweka mbali na Mungu wao. Athari ya kitendo neni hicho ilikuwa kuzinduka.

Kitendo neni hicho kimetimiza masharti ya ufelisiti kama ilivyokuwa katika baadhi ya matamko yaliyotangulia. Imamu ni mwenye mamlaka na amekitumia katika mahali mwafaka kwa hadhira mwafaka. Kitendo kimetolewa kikamilifu na kwa usahihi kwani uso wake na hali yake ya kisaikoljia ilionyesha kuwa hakudhamiria jambo lingine tofauti.

**Kukaripia:**

21. *Msiseme sala ndiyo ibada… na dua ni nini? Ilijibiwa dua ya Nabi Musa na wewe ukimaliza kuswali unawatupa watu wanagongana na milango kwa nini ?[[ Wacha kwenda kufanya da'wa na kuwapoteza watu]]*.

Katika sura Al-Imran Mwenyezi Mungu amesema: "Sema: Ikiwa nyinyi mnapenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni. Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakughufurieni madhambi yenu" (Al-Farsy 3:31).

Sala ni tendo la ibada kama dua ilivyo na hufasiliwa kama dua hivi kwamba huwezi kuvitenganisha. Kwa vile mtume (SAW) alisali na kuomba dua basi lazima wafuasi wake wamfuate kwa kufanya hivyo. Ulazima huo haubagui kati ya Maimamu na Maamuma. Ilivyo ni kwamba hakuna Imamu anayepuuza dua. Tatizo ni kutoiomba waziwazi kama ilivyoelezewa katika mfano nambari 14 wa vitendo neni vitathminishi.

Nia ya tamko hilo ni kuwakejeli mashekhe ambao hawafanyi mambo yaliyotajwa katika khutuba. Athari yake ni kupuuzwa kwa mashekhe hao, kwa wale ambao wanaona kwamba Imamu ana haki kuwasema. Lakini kwa maamuma wengine, tamko hilo liliwaathiri kwa kuudhika.

Tamko hilo halirejelei utendaji wa kitendo katika wakati ujao. Kwa hiyo limekiuka sharti la urejeleo wa yaliyomo. Aidha, halikuelekezwa kwa hadhira wala muktadha mwafaka. Kwa hiyo limekiuka sharti andalizi. Vilevile, halikuzingatia sharti la uaminifu.

22. *[[Wewe unakuja msikitini saa ngapi]]? Wewe saa ngapi? Na wewe saa ngapi?*

Baada ya kuwahutubia waumini kwa ujumla, Imamu alibadilisha mbinu na kuanza kuwarushia maswali baadhi ya watu binafsi. Ijapokuwa maswali hayo yalikuwa ya kibalagha na kwa hiyo hayakuhitaji majibu, yalizua hali ya taharuki miongoni mwa waumini. Maswali hayo yaliashiria kwamba kitendo mojawapo kinachoonyesha ukaidi wa waumini ni kuchelewa kwenda msikitini siku ya Ijumaa. Nia ya Imamu, kutokana na tamko hilo, ilikuwa kuwaaibisha waendao msikitini wakiwa wamechelewa. Hivyo basi, Maamuma waliathirika kwa kuaibika.

Kitendo neni hicho hakiendani na sharti la umwafaka kwa sababu Imamu hana haki ya kumnyooshea mtu kidole mbele ya hadhira kama hiyo ya waumini waliokuja kwa ajili ya ibada. Kufanya hivyo ni kumwaibisha jambo ambalo haliwezi kumpatia matokeo mazuri. Waumini wana habari juu ya muda ambao wanapaswa kuja msikitini kwa hiyo kuwakaripia kwa jambo walijualo hukiuka sharti andalizi. Laiti angalichunguza ili kupata sababu zinazowafanya wachelewe ili tatizo litatuliwe kwa njia mwafaka. Katika matamko ya 16 na 17, Imamu hakutumia kanuni za unyenyekevu chanya. Ingemtoshelezea haja kama angedhihirisha kuwa jambo analozungumzia ni zuri na humhusu pia. Aidha, angefanya bidii kuelewa hali za wasikilizaji na kwamba anashirikiana nao. Kwa vile matamko hayo yamedhihirisha hali ya kutowajali wasikilizaji, athari zake zimekuwaa hasi tofauti na ilivyokusudiwa.

Aina hiyo ya vitendo neni imeongoza kwa wingi katika kujitokeza kwenye khutuba kwa sababu, kwa kawaida maswala yanayojenga jamii ya waumini wa Kiislamu katika nyanja mbalimbali ndiyo hushughulikiwa. Khutuba nyingi zimeshehenezwa maswala ya kiimani na vielekezi hutumika kuwaelekeza waumini kumwamini Mwenyezi Mungu na kumcha vilivyo, kwa kutekeleza aliyoyaamrisha na kuacha aliyoyakataza. Maswala ya kijamii na kisiasa huhitaji vielekezi pia ili yapate kushughulikiwa na waumini. Maamuma huamrishwa, huhimizwa, huzinduliwa, huonywa, hukanywa na kadhalika, kupitia matamko ya pote hili kwa maslahi yao binafsi na maslahi ya jamii kwa ujumla. Kutokana na uamilifu nafasi kubwa ambayo aina hiyo

ya vitendo neni hutekeleza, ilitokea kwamba viliwakilishwa kwa aslimia 53% katika khutuba zilizochanganuliwa.

### 4.2.2 Vitendo Veni Viwakilishi (VW)

Vitendo neni viwakilishi ni matamko yanayokusudiwa kuelezea imani ya mzungumzaji kwamba urejeleo wa yaliyomo ni sahihi. VW huchukua sura mbalimbali pia katika khutuba. Sura zilizojitokeza ni kudai ama kushikilia, kuhakikishia na kutaja. Mifano kadhaa imetolewa ili kuthibitisha madai hayo. Mifano hiyo ni:

**Kudai:**

1. [[*Watu humpenda sana shetani kuliko Mwenyezi Mungu aliyewaumba]]*.

Kawaida mwanadamu hapendi mambo ambayo yatampa ugumu bali hupenda yale ambayo yatampa urahisi. Waumini wa Kiislamu wanaamrishwa kushikamana na mafundisho ya dini yao na kuacha yaliyokatazwa. Hata hivyo utakuta baadhi yao hawayajali mafundisho hayo na badala yake wanafuata mila na desturi zao hata kama zinakinzana na Uislamu. Ndio maana Imamu huyu akawarejelea kuwa wanampenda shetani kuliko Mwenyezi Mungu. Tamko hilo limeakisi Kur'ani ambayo husema: "Na wanapoambiwa fuateni aliyoyateremsha MwenyeziMungu husema bali tutafuata yale tuliyowakuta nayo baba zetu. Je, hata kama baba zao walikuwa hawafahamu cho chote wala hawakuongoka watawafuata tu (Al-Farsy, Sura 2 aya 170). Na katika Surat 2 aya 165, twaambiwa: "Na katika watu kuna wanaofanya waungu wasiokuwa Mwenyezi Mungu. Wanawapenda kama kumpenda Mwenyezi Mungu. Lakini walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana. Na laiti waliodhulumu nafsi zao wanaijua (balaa itakayowapata) watakapoiona adhabu (siku hiyo ya kiyama, kwa kuwa nguvu zote ni za Mwenyezi Mungu siku hiyo hakuna masanamu wa kuwashufaia wala mengineyo) na kuwa Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu".

Nia ya Imamu ilikuwa ni kutoa madai yanayotokana na imani yake kwamba watu humpenda sana shetani, akitarajia kwamba watabadilisha mienedo yao na kutambua kwamba Mwenyezi Mungu ndiye mweza juu ya kila kitu na ndiye apaswye kupendwa. Athari ya tamko ilikuwa kuchukizwa na madai ya Imamu kwamba wao humpenda sana shetani.

Tamko hilo limekiuka baadhi ya masharti ya ufelisiti. Kwanza, halikutolewa kikamilifu kama inavyotakiwa na sharti andalizi. Ni kweli kwamba watu wanampenda sana shetani? Kwa vile shetani anahusishwa na vitendo vibaya, hakuna apendaye kunasibishwa naye. Pengine kutotilia maanani mafundisho ya dini husababishwa na kutopata elimu ya kutosha kuhusu dini yenyewe. Halafu wanaohusika na kuwafunza watu maswala ya dini ni Mashekhe na Maimamu. Sharti lingine lililokiukwa ni la uaminifu. Si kitendo cha haki kuwatarajia Maamuma kubadilika katika siku moja. Kubadilika kiimani ni kama kubadilika kiwiliwili au ni sawasawa na ukuwaji wa mtoto. Jinsi mtoto anavyopitia katika hatua mbalimbali kama vile hatua za kukaa, kutambaa, kusimama dede, kutembea halafu kujitegemea katika kila jambo afanyalo ndivyo muumini anavyokuwa. Kama matendo yao ya kufuata mila na desturi yamekita mizizi, kuyang'oa ni kazi. Kwa hiyo sharti la umuhimu lingalitiliwa maanani, waumini wangalionyeshwa tu umuhimu wa kutupilia mbali vitendo vya kijadi ambavyo hukinzana na mafundisho ya dini yao.

2. *Mshirikina akichinja mnyama hatumli… [[umepewa kibuyu, umepewa majini, una "sumbati","kumwendo"…. Ukienda kwa Shekhe wa tarafa ukitaka kuozeshwa hatukupi]]. Ukiwa ulishaoa, ndoa hubatilishwa….mwanamke akiamua kwenda kuhudhuria sherehe wewe ukiwa unamwamini Mungu, ndoa hiyo ni batili. Wewe ukishiriki katika "mwendo", "sumbati"….Hatukuoshi mkimkafini katika nguo hizo mtakuwa mmemfunga katika sumu. Mshirikina hatumziki katika makaburi ya Waislamu.*

*Mushirik* ama mushirikina ni mtu anayetenda kitendo cha *shirki* ambacho ni kujiwekea miungu wengine mbali na Mwenyezi Mungu ukawa mwenye kuwaabudu na kutii amri zao jinsi ambavyo ungemwabudu Mwenyezi Mungu au badala ya kumwabudu na kumtii Mwenyezi Mungu. Katika tamko hilo Imamu alirejelea matendo wanayotenda katika sherehe ya tohara. Kuvaa *isumbaati* ambalo ni vazi rasmi linalovaliwa katika sherehe hiyo, kubeba pombe au kuinywa na kuhudhuria *imbalu*, yote hayo ni mambo yanayokinzana na mafundisho ya Uislamu.

Kwa mujibu wa Imamu huyo, Mwislamu yeyote anayekubali kubebeshwa kibuyu cha pombe atakuwa amekubali majini kwa sababu hayo ni matambiko ya ushirikina. Na yeyote anayevaa nguo iliyotengenezwa kutokana na ngozi akapewa jukumu la kuwarushia vijana pombe kwa kuipuliza kwa mdomo wake basi atakuwa anatenda dhambi kubwa na kwa hiyo hastahili

kuozeshwa, kuoshwa wala kuzikwa katika makaburi ya Waislamu. Aidha mwanamke anayeshiriki katika sherehe hiyo anapaswa kupewa talaka mara moja.

Nia ya Imamu ni kushikilia madai yake kwamba anayeshiriki katika miviga ni kafiri. Hata hivyo maamuma walikasirika wakidai kwamba Imamu anawachukulia kuwa makafiri na hali wanaswali na kutekeleza nguzo zote za Uislamu.

Matamko hayo yametolewa katika muktadha usomwafaka. Hii ni kwa sababu wakati wa miviga ya tohara unapowadia, yote yanayozungumzwa dhidi ya mambo hayo hayazingatiwi na washiriki wake. Laiti kama yangetolewa wakati mwengine kama vile katika miaka isiyokuwa ya tohara. Katika wakati kama huo, Uislamu na imani na nguzo zake vyapaswa kusisitizwa na yaliyo halali na haramu yafundishwe ili kupalilia masomo yanayohusiana na shirki. Masharti ya urejeleo wa yaliyomo na uaminifu yalikiukwa na tamko hilo pia kwa sababu bila kumwandaa msikilizaji huwezi kutarajia kuwa atabadilika.

3. *Kuna waliorukaruka usiku, wakachinja kuku eti kwa sababu wamemaliza mwaka… [[ni Waislamu]]?*

Tarehe mosi Januari, husheherekewa dunia nzima ambapo mwaka mpya hukaribishwa kwa vifijo na vigelegele. Kuna wanaochinja kuku na mbuzi na hata kuandaa maakuli na mashurubati ya kila namna. Kuna wanaopiga makelele na kucheza ifikapo saa sita, usiku wa kuamkia tarehe mosi Januari. Almuradi kila mtu ana namna yake ya kuukaribisha mwaka mpya. Wanafanya hivyo mwaka unapomalizika na huukaribisha mwaka mpya wakiwa na matumaini kwamba watafanikisha mengi katika siku zijazo, ambayo hawakujaliwa kuyafanikisha katika siku za nyuma. Imamu huyachukulia hayo yote kwamba hayafungamani kwa vyovyote na Uislamu.

Nia ya kutoa tamko kama hilo ni kushikilia kwamba wanaotenda hayo si Waislamu. Athari ya kitendo neni hicho ni kushangazwa. Hivyo ni kwa sababu hawaoni shida na kufurahika, kula na kunywa maadamu walivyovila ni halali.

Tamko hilo limekiuka baadhi ya masharti ya ufelisiti kwa vile kama onyo lingerejelea kitendo cha wakati ujao, lakini badala yake linahusu kitendo kilichopita. Kwa kufanya hivyo limekiuka

sharti la urejeleo wa yaliyomo. Sharti la umuhimu pia limekiukwa kwa sababu wasikilizaji hawaoni kuwa kuna ubaya katika kusherehekea mwaka mpya.

**Kuwahakikishia:**

4. *[[Tukiangalia makanisa yanayoozesha mbwa na wanadamu, yote ni ya huko magharibi]]. Hizo ni tabia zao. Makanisa yanayoruhusu mwana mume kumwoa mwana mume mwenzake ni ya huko magharibi.*

Tamko hilo lilijitokeza katika khutuba iliyozungumzia zama za mwisho wa dunia na dalili zake ambazo hudhihirika katika vitendo vya maasi vilivyozidi kiasi. Nia yake ilikuwa kuwahakikishia wasikilizaji kwamba swala analozungumzia ni la kweli na wala haropokwi tu na maneno. Alitaja mahali katika ulimwengu halisi ambapo tabia ya kutenda mambo kinyume na maumbile ya mwanadamu kama vile ushoga na kuwaozesha mbwa wanadamu imekita mizizi ili kuwathibitishia wasikilizaji madai yake. Imamu aliwatarajia waumini kulaani kitendo hicho na kusaili maadili ya kimagharibi kuhusu asasi ya ndoa. Athari ya tamko hilo ilikuwa chanya kwa sababu wasikilizaji waliitikia wito wa Imamu wao na kutenda kile alichowatarajia kutenda. Waumini walilaani kitendo hicho na kusema kuwa kamwe hawatokubali kufanya mambo yanayoenda kinyume na maadili ya jamii zao.

Kitendo neni hicho kimetimiza masharti ya ufelisiti kwa sababu waumini waliambiwa kutenda kilicho katika uwezo wao na ambacho huenda kikachangia kuondoa madhara wanayoweza kuyapata.

**Kutaja:**

5. *Tazama enzi hizi za akhiru zamani. Zama za mwisho wa dunia. [[Tangu uanze kusoma magazeti, ni mbwa wangapi walioozeshwa na watu na ndoa hiyo ikaitwa "Ndoa tukufu]]?"… Ni jambo la kushangaza. Hawa tuliowapa kura wakaenda bungeni. Wabunge wa Uganda . Mungu awarehemu. Kwa sababu hapa nchini, hata viongozi husema jambo moja: "Hairuhusiwi hapa Uganda, mwana mume kuolewa na mwana mume. Hatuwezi kukubali kitendo hicho hapa Uganda." Eti kwa nini? Kwa sababu huo si utamaduni wao.*

Tamko hilo limerejelea baadhi ya mambo ambayo bunge la Uganda liliyajadili na kufikia uamzi juu yake na mengine ambayo yametanda katika vyombo vya habari. Kutajwa kwa ndoa zinazofungishwa wanadamu na mnyama kama mbwa huko Ulaya kulikusudiwa kuthibitisha

kuwa dunia imepiga hatua katika kuibuka na ndoa mbadala kiasi kwamba Waafrika wanaweza kuthubutu kuangalia uwezekano wa kuwaruhusu wananchi kuiga mwenendo huo. Athari ilikuwa kuungama kwani waumini waliona kuwa ni kweli kuna vituko kama hivyo na hawawezi kukubali kupotoshwa.

Katika khutuba za Ijumaa vitendo neni viwakilishi vilijitokeza kwa aslimia ndogo ikilinganishwa na vielekezi, kama inavyobainika katika jedwali 4. Hii ni kwa sababu uamilifu wake hujikita tu katika kuwambia watu mambo yalivyo na kwa hiyo upeo wa matumizi yake katika muktadha wa khutuba si mpana sana.

### 4.2.3 Vitendo Neni Vitathminishi (VT)

Aina hii ya vitendo neni ilijitokeza kama kudharau, kusimanga, kupinga, kutukana na kulaumu. Uamilifu wake ni kuonyesha kuonyesha mwelekeo wa mzungumzaji juu ya kitendo kilichotokea na ambacho ndicho hurejelewa na matamko yaliyokitwa katika muktadha wa khutuba. Mifano ya vitathminishi ni kama ifuatavyo:

**Kudhrau:**1.

1. *Hivi sasa kuna watu wanaopeleka watu Hija. [[Yeye mwenyewe si halali na pesa yake si halali]].*

Kuna watu wa aina tatu ambao wanawasaidia wenzao kutimiza faradhi ya kwenda Makka kuhiji. Aina ya kwanza ni matajiri wa kutoka Uarabuni ambao wanatoa pesa zao kupitia mashirika yasiyo ya kiserikali kwa ajili ya kugaramia mipango ya hija kwa wasiojiweza. Aina ya pili ni matajiri wa kutoka nchini Uganda ambao huwanunulia watu tiketi za kwenda na kurudi kutoka Makka na kuwapa pesa kidogo za matumizi. Matajiri hawa hufaidika kutokana na fursa inayopewa mahujaji ya kubeba mizigo yenye uzito kama vile kilo mia moja bila ya kuilipia ushuru. Aina ya tatu ni wanasiasa ambao hujitafutia umaarufu utakaowawezesha kuibuka washindi katika uchaguzi. Hija ni nguzo ya tano kati ya nguzo za Uislamu. Mwislamu analazimika kuhiji pindi anapopata uwezo wa kulipia safari na mahitaji yake. Ulazima huo ni wa angalau mara moja katika umri wa muumini. Ni sharti pesa anazotumia katika hija ziwe

alizochuma kwa njia ya halali la sivyo hija yake haitosihi. Ikiwa kutajitokeza mdhamini, basi uhalali huo lazima uzingatiwe pia.

Imamu anawarejelea wafadhili wa aina ya pili na  tatu. Nia yake ilikuwa kuwatweza wafadhili hao na kuwaonya wasikilizaji wake juu ya hasara watakayoipata endapo watahiji kutokana na misaada hiyo. Kwa maoni yake, watu hao hawafai kuwa wadhamini wao kwa sababu pesa zao zinachumwa kutokana na njia ambazo si halali hasa ikizingatiwa kuwa ufisadi wa mali ya umma umetanda miongoni mwa wanasiasa. Tamko hilo liliwaathiri wasikilizaji kwa namna mbili. Huku waumini wengi ambao waliona kwamba wafadhili hao hutoa fursa ya kuwawezesha Waislamu kuhiji wakiudhika,  kulikuwa na wachache waliomuunga mkono.

Tamko hilo limekiuka baadhi ya masharti ya ufelisiti kama ilivyokuwa katika mifano iliyotangulia. Kwanza mzungumzaji hana mamlaka ya kutoa fatuwa kuhusu ni hija ipi inayosihi na ipi isiyosihi. Ingawa hadhira ni mwafaka kwa kauli kama hiyo, lakini Mufti ndiye aliye na mamlaka ya kutoa fatua kuhusu suala kama hilo na Imamu jukumu lake ni kuufikisha tu ujumbe wa Mufti. Halafu muktadha ambamo tamko hilo lilitolewa si mwafaka kwa sababu maswala nyeti kama hilo la hija yanahitaji muda wa kutosha kuyaelezea kwa kina. Khutuba huchukuwa dakika kati ya 20 na 40 muda ambao ni kidogo sana. Zaidi ya hayo waumini wana wasiwasi kuhusu kukatazwa kutafuta msaada kwani hawaoni ubaya wowote katika hija iliyotekelezwa kwa njia hiyo. Kwa hiyo, sharti la umuhimu pia halikuzingatiwa.

2. *[[Inabidi uwe na ushahidi katika Kur'ani na Hadithi za Mtume za sawa]].*

Kur'ani ni chimbuko la kwanza la sheria za Uislamu ikifuatiwa na hadithi za mtume Muhammad (SAW). Kauli yoyote inayotolewa kuhusu dini lazima iambatanishwe na ushahidi kutoka katika vitabu hivyo. Isitoshe, ushahidi kutokana na hadithi yapaswa uwe sahihi. Hivyo ni kwa sababu kuna hadithi zisizosahihi na Waisilamu wametahadharishwa nazo kwa kuwa zilibuniwa tu na watu waliokuwa na nia ya kuleta vurugu wakazinasabisha kwa mtume (SAW).

Nia ya Imamu ni kuwadharau Maimamu wenzake ambao kwa maoni yake hutoa mawaidha ya kidini bila kuyaambatanisha na ushahidi kutoka katika Kur'ani au hadithi za mtume (SAW). Imamu huona kwamba pale ambapo wenzake hujigamba kuwa wana ushahidi, hauwi wa kweli.

Athari iliyojitokeza kulingana na nguvu za tamko hilo ilikuwa kupuuzwa kwa Mashekhe na mafunzo yao kwa sababu waliona kwamba kumbe hayana mashiko. Hata hivyo, baadhi ya Maamuma walionyesha hisia za kuudhika.

Ikiwa wanaorejelewa na tamko nambari 11 ni Maimamu, basi masharti andalizi yamekiukwa. Mzungumzaji hana mamlaka juu ya Maimamu na mahali anapoongelea si mwafaka hata kidogo. Zaidi ya hayo masharti ya uaminifu yamekiukwa pia kwani tamko halikutolewa kikamilifu na kwa usahihi kama inavyotakiwa na ufelisiti. Hadhira inayomsikiliza ni ya Waislamu wa kawaida ambao si wasomi katika mambo yanayohusu dini. Kwa hiyo mambo ya ushahidi kutoka Kur'ani na Hadithi yako mbali nao kwa sababu si uwanja wao. Fauka ya hayo, hadithi za sawa ndiyo zipi? Swala hilo halikuwekwa wazi na Imamu kwa hiyo linaweza kuwakanganya wasikilizaji.

3. *Utakuta Shekhe hana kofia. Mtume alifanya hivyo?*

Mavazi kama vile kofia na kanzu ni vitambulisho kwa Waislamu. Kwa upande wa Imamu mavazi hayo huchukuliwa kama mavazi rasmi ambayo inatakikana ajipambe nayo kila aendapo msikitini kusalisha waumini au kuwasilisha khutuba ya Ijumaa. Mtume (SAW) ni kielelezo cha Waislamu katika kila kitu yakiwemo mavazi. Hata hivyo kwa vile Maimamu ndio maulama na wanachukuliwa kuwa warithi wa manabii wanatakikana wafuate sunna za mtume (SAW) hususani katika ucha Mungu, mavazi na kufuga ndevu ili wawe mfano bora kwa waumini.

Kauli hiyo ilitolewa mbele ya waumini ambao si Mashekhe ikirejelea Mashekhe. Kwa hiyo, nia yake ilikuwa kuwadharau waonekane kama wahuni mbele ya Waislamu. Wakishavuliwa heshima zao kwa kudunishwa hivyo, basi hata wakiwasilisha khutuba za namna gani, hazitofua dafu. Athari ya tamko hilo basi ni kupuuzwa kwa Mashekhe wasiovaa kofia, kitendo ambacho kimeonekana kama aibu. Hata hivyo, baadhi ya waumini waliudhika na kauli hiyo. Imamu huyu amekubali, kwa njia isiyo ya moja kwa moja, kuwa naye ana aibu fulani. Lakini hakubaliani na mtu yeyote anayechambua aibu za mwingine.

Tamko hilo limekiuka sharti andalizi kwa sababu ilikuwa lielekezwe kwa Maimamu wenzake na sio wasikilizaji. Kwa hiyo hadhira si mwafaka. Isitoshe mzungumzaji hana mamlaka ya kuwasema wale aliowarejelea na kauli yake.

4. *Watuulize wanazuoni. [[Watu wamekubaliwa kusoma visirasira]]?*

Kwa mujibu wa Kur'ani ikiwa kuna jambo usilolijua basi yafaa uwaulize wenye ujuzi (Al-Farsy, 1984). Ni sawa kuwauliza wanazuoni kwa sababu ndio waliomakinika katika elimu. Lakini hata katika taaluma ya dini kuna matawi Kadhaa wa Kadhaa. Haiwezekani kwa mtu mmoja kuwa hodari katika matawi hayo yote. Lakini kwa maoni ya Imamu huyu maswali yote yanayohusiana na dini yapaswa yaelekezwe kwake kwa sababu Mashekhe wana elimu duni. Isitoshe anaona wasikubaliwe kufundisha hivyo vihistoriahistoria ambavyo amevirejelea kama visirasira.

Nia ya Imamu katika kutoa tamko hilo ni kujikuza na kuwadharau wasomi wenzake. Athari ya tamko hilo, kwa hiyo, imekuwa kuudhika na kitendo neni hicho. Imamu, hakutaka kuwaacha maamuma wake bila kuwapa ushauri juu ya kujihami mbele ya mashekhe wenye madhaifu yaliojadiliwa tangu mwanzo wa khutuba.

Kitendo neni hicho si dhahiri kwa sababu huku kikionekana kama ni cha kusihi watu kuwauliza wenye taaluma ya dini na kushangaa jinsi watu wengine walivyokuwa na elimu duni, hamu ya Imamu ilikuwa kuwadharau wasomi na kutarajia kuwa wasikilizaji wake watafanya hivyo pia. Ingefaa kitendo neni hicho kuelekezwa kwa wasomi hao na sio kwa waumini ili kutimiza masharti ya ufelisiti. Aidha, wale wanaotakiwa kutekeleza kitendo ambacho kimekitwa katika matamko hayo hawana uwezo wa kufanya hivyo kwa sababu hawawatambui wasomi husika. Kwa hiyo tamko halikutolewa kikamilifu na kwa usahihi.

5. *Tusipokee tu…. [[Kwanza tuwaulizeni hao Mashekhe..*
*Hiyo elimu wanaitoa wapi]]?*

Ushauri ni kwamba ujumbe wautoao Mashekhe yatakikana uchujwe kabla ya kutiliwa maanani. Kisha Mashekhe hao wapewe kibarua cha kueleza chanzo cha elimu wanayoisambaza kwa waumini. Nia ya tamko hilo ni kuwadharau mashekhe kwa msingi kwamba yeye ndiye mwanazuoni anayepaswa kuulizwa juu ya maswala yanayohusiana na dini na kwamba mashekhe wengine wanaishia katika kufunza vihistoria vya dini na hawana elimu ya kutegemewa. Athari ya tamko hilo ni kuudhika kwa Maamuma kutokana na kitendo cha Imamu kuwadharau wenzake.

Kitendo neni hicho pia si cha moja kwa moja. Huonekana kama kinakusudia kuwakataza wasikilizaji wasipokee ovyo ujumbe wa kidini kutoka kwa Maimamu pasina kuuliza chanzo chake. Lakini kusudio la Imamu hasa lilikuwa kuchochea Maamuma ili wasitilie maanani mahubiri yanayotolewa na mashekhe wengine. Tamko hilo limekiuka masharti ya ufelisiti. Kwanza, Imamu hana haki kumwambia msikilizaji kuwahoji viongozi wao juu ya viwango vyao vya elimu. Maamuna nao hawana haki wala uwezo wa kufanya hivyo. Pili, tamko hilo halikuzingatia sharti la umwafaka kwa sababu ingefaa lielekezwe kwa Mashekhe. Pamoja na hayo, Maamuma walitambua kusudio la Imamu.

6. *Watu wanapokea vitabu kutoka Makka na wana hadithi mbili tatu…[[wanajifanya mashekhe]]?*

Vitabu vinavyokusudiwa hapa ni vitabu vya kufundusha dini ya Uislamu vinavyochapishwa huko Makka katika nchi ya Saudia, kwa lugha mbalimbali. Tamko "*Wana hadithi mbili tatu"* maana yake wana elimu kidogo isiyotegemewa. Tamko "*Wanajifanya Mashekhe"* maana yake si mashekhe kwa hakika bali wanajigamba tu.

Kwa mujibu wa kauli hiyo Imamu anashikilia kwamba kuna watu ambao wamejifunza hadithi chache kutoka katika vitabu walivyovipata kutoka Makka na kwa hiyo hawakubobea katika elimu. Kama ilivyodokezwa hapo awali, watu wanaorejelewa katika khutuba hii ni wale mashekhe waliosomea katika vyuo vikuu vya Saudia. Haiwezekani kwa mtu ambaye hakusomea katika chuo kikuu chochote kutoa madai kama hayo kama kweli amefuata sheria ya ushirikiano, isipokuwa kwa lengo na maana maalum.

Kwa hiyo nia ya Imamu ni kuwadunisha watu hao akitarajia kwamba maamuma hawatatilia maanani ujumbe unaotokana na mawaidha wanayoyatoa na badala yake wamfuate yeye. Athari ya tamko hili ilikuwa ni kuudhika kwa baadhi ya maamuma walioona kwamba aliye na kisomo kidogo ni Imamu huyo sio Mashekhe walio hitimu masomo yao katika vyuo vikuu. Yafaa ifahamike kwamba kabla ya kuanzishwa kwa mfumo wa shule na vyuo vikuu, watu walikuwa wakijifunza dini mabarazani kwa Mashekhe wao au misikitini kwenye halaka zilizokuwa zikiendeshwa na wasomi mbalimbali. Baadaye, mfumo wa madrasa ulianzishwa.

Tamko hilo ijapokuwa limetolewa na mtu aliye na mamlaka, lakini limejitokeza katika muktadha ambao si mwafaka  na limeelekezwa kwa hadhira isomwafaka. Ilipaswa lielekezwe kwa mashekhe wanaozungumziwa. Halafu kuwadharau wasomi ambao yeye hafikii kiwango chao cha kielimu sio tu kutowatendea haki bali pia ni kukiuka sharti la uaminifu. Maamuma nao wamenyimwa haki yao kwani badala ya kuwafundisha mambo yenye maana, wanapotezewa wakati kwa kufanywa wasikilize yasiyowahusu. Tamko la 4 ni kama hili katika ukiukaji wa masharti ya ufelisiti.

Matamko yaliyojitokeza katika nambari 3,  4, 10, 11, 12, 14, 15 na16 ni vitendo neni viso dhahiri. Katika 3, tamko limekaa kama kitendo neni cha kuuliza swali ilihali katika 4 likionekana kama kitendo neni cha kudai. Hata hivyo, Maamuma waliweza kutambua nia ya Imamu wao na kubaini kuwa Imamu alikusudia kuwadunisha Mashekhe na sio kuuliza wala kudai. Tamko la 10 limekaa kama kitendo neni cha kuonyesha mshangao wakati tamko la 11likidhihirisha kitendo cha kutilia shaka elimu walio nayo Maimamu wengineo. Hata hivyo, Maamuma waliweza kutambua nia ya mzungumzaji kutokana na muktadha ambamo matamko hayo yalijitokeza na kubaini kuwa alikusudia kuwabeza Mashekhe ili mawaidha na mahubiri yao yapuuzwe na Maamuma. Matamko kuanzia lile la 12 hadi la 16 yanaonekana kama vitendo neni vya kuuliza maswali lakini Maamuma hawakutilia maanani maana hiyo bali tafakuri zao ziliwawezesha kuibuka na maana iliyokusudiwa ambayo ilikuwa imejificha nyuma ya matamko hayo.

7. *[[Mtu anajifanya Shekhe na hajui kitu]]. Hana elimu.*

Kauli hiyo ilitolewa mbele ya maamuma huku ikielekezwa kwa wasomi ambao ni maimamu wa misikiti mingine. Maneno mazito yaliyotumika kama vile "*Anajifanya", "Hajui kitu" na "Hana elimu",* yametumika maksudi ili kutilia mkazo nia ya Imamu ambayo ni kuwabeza wasomi hao. Maamuma walitarajiwa kupuuza mashekhe hao na badala yake wazingatie tu mafundisho ya Imamu huyo kwa sababu ikiwa wengine hawana elimu basi yeye ndiye aliyenayo. Si alisema kwamba "*Watuulize wanazuoni"?*

Athari ya tamko hilo ilikuwa kuudhika kwa sababu ya kubezwa na kudunishwa kwa Mashekhe. Kwa nini wasiathirike kwa namna hiyo na hali kuna "mauaji ya mhusika" kwa lugha ya kifasihi. Kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu haifai kumwambia mtu "wewe ni kafiri" kwa sababu

asipokuwa kafiri mzungumzaji ndiye huwa. Ni kama kumwonyesha mwenzako kidole kwa kumzomea au kumwonya au kumtusi kwa sababu, huku kidole kimoja kikielekezwa kwake, vilivyo vingi vyamtazama mzungumzaji.

Tamko hilo limekiuka masharti ya ufelisiti kwa sababu Imamu hana mamlaka ya kuwasema Maimamu wenzake na hata kama angalikuwa nayo hadhira ambamo kitendo neni kilitolewa si mwafaka. Aidha kitendo neni hakikutendwa kikamilifu na kwa usahihi kama inavyotakikana. Hivyo ni kwa sababu Maamuma husika hawawaoni wale watu anaowalenga kwa matamko yake ili wapate kuwapuuza. Kwa hiyo ilivyo ni kama kumwamrisha mtu kuleta kitu ambacho hakipo.

8. *Mjinga mmoja alisema ni vizuri kuongea na shetani umjuaye kuliko malaika usiyemjua. [[Mtu huyo ni shetani. Watu hao mnawajua…huandika hirizi]].*

Katika tamko moja, Imamu alitaja kwamba watu humpenda sana shetani kuliko Mwenyezi Mungu. Katika tamko hili Imamu amemtambulisha shetani aliyemkusudia ambaye ni mganga. Ukioanisha matamko hayo mawili, maana itakayoibuliwa ni kwamba watu humpenda sana mganga wanayemjua kuliko Mungu wasiyemjua. Halafu sifa za mganga huyo ni mjinga, shetani, huandika hirizi na hupendwa sana na watu.

Nia ya Imamu ni kuwadunisha waganga na kuwataka waumini wawapuuze na badala yake wafuate amri za Mungu. Athari za kitendo neni hicho kwa waumini ilikuwa kuudhika na walichoona kwamba ni matusi kutoka kwa Imamu. Hivyo ni kwa sababu kitendo kibaya huondolewa na kizuri. Kama upigaji ramli ni kitendo kibaya, mpiga ramli hawezi kukiacha kwa kumwita mjinga au shetani. Vivyohivyo, anayewaendea waganga hawezi kuacha kufanya hivyo eti kwa sababu wamedunishwa. Matumizi ya mbinu yenye busara ndiyo yanayofaa kama inavyohimizwa na Kur'ani.

Tamko hilo limetimiza masharti ya ufelisiti kwa sababu mzungumzaji anaamini kuwa kitendo cha kuwapuuza waganga lazima kitendeke na ana haki ya kuwambia wafanye hivyo. Kwa upande mwengine, wasikilizaji wana uwezo wa kutenda kitendo hicho na wanawajibika kufanya hivyo.

9. [[*Mko hapa mmevaa kofia lakini mtoto mtampeleka kwa mjomba ili wamzawadie…Ni nini kinachotufanya hivyo? Shetani]]*.

Kuvaa kofia ni mojawapo ya vitambulisho wanavyotambulishwa navyo waumini wa Kiislamu. "*Mko hapa mmeva kofia*.." maana yake ni mnajifanya Waislamu lakini vitendo vyenu vinaonyesha sura zenu halisi. Waislamu wa kweli hawajihusishi na sherehe za jando ambazo zaongozwa na shetani.

Nia ya Imamu ni kuwakejeli waumini wanaoshiriki katika sherehe ya tohara inayofanyika kulingana na utamaduni wa Kigisu. Athari ya kitendo neni hicho ilikuwa kukasirika kwa waumini kutokana na walichoona kwamba Imamu wao amewatoa katika Uislamu.

Kitendo neni hicho kimezingatia masharti ya ufelisiti kutokana na ukweli kwamba kimewasilishwa na mtu aliye na mamlaka, aliyetumia mamlaka hayo katika mahali panapofaa na zaidi ya hayo kimetendwa kikamilifu na kwa njia sahihi.

10. [[*Wasema bwanako hajakupa ruhusa… na wewe una bwana]]? Hatukujua kwamba leo ni siku ya Ijumaa*? *Eh… kwa nini hatutii amri? Ni saa saba na dakika Kadhaa… khutuba ya kwanza ingekuwa sasa imekaribia kumalizika.*

Kauli hiyo ikifungamanishwa na ile iliyotangulia inaashiria kwamba kuna waliochelewa halafu wakadai kwamba mabwana zao walikuwa hawajawaachilia. Kinachomkera ni kuona kwamba ingawa Waislamu wanajua kwamba siku ya Ijumaa wanatakiwa kuwahi msiktini wanachelewa maksudi. Madai waliyoyatoa hayakumhusu ndewe wala sikio. Hivyo ni kwa sababu anaona kwamba hawastahiki kuwa na bwana anayewazuia kufanya ibada.

Kwa hiyo, nia ya Imamu ilikuwa kuonyesha kejeli kwa wasikilizaji wake. Kutokana na nia hiyo, maamuma waliathirika kwa kumchukia Imamu wao kwa sababu hawapi heshima wanayostahili.

11. *Kusema kwamba wewe[[ umesoma hadithi 15, 20 unataka kuwa mhubiri]]?*

Tamko hilo lililotolewa kurejelea mashekhe ambao kwa mtazamo wa Imamu hawakubobea kiusomi ijapokuwa wamesomea katika vyuo vikuu. Nia yake ilikuwa kuwabeza mashekhe hao. Kwa maoni yake haitoshi kusoma hadithi 15 hadi 20 bali kuna haja ya ujuzi na maarifa ambayo hupatikana kupitia uzoefu wa siku nyingi. Athari ya tamko hilo ni kudharauliwa kwa mafunzo ya wasomi hao. Msomi yeyote anayetaka kuwa mhubiri, haimtoshelezei kuwa na elimu na ujuzi tu wa mambo ya dini bali kwa maoni ya Imamu huyo anatakikana awe hodari katika Kurani, na taaluma ya hadithi hivi kwamba ushahidi unapohitajika autoe. Baadhi ya wasikilizaji waliudhika na tamko hilo kwa sababu lilikusudia kuwabeza wasomi.

Masharti ya ufelisiti yamekiukwa katika tamko hilo. Kwanza Imamu hana mamlaka ya kuwachambua Maimamu wenzake na hadhira anamofanyia uchambuzi wake si mwafaka. Aidha misingi ya kuwaongoza wasikilizaji wake ili wajue ni nani anayefaa kuwa mhubiri hakuiweka wazi. Ikiwa hadithi 15-20 hazimtoshelezei mtu ni ngapi zinazohitajika? Fauka ya hayo, wako wapi hao wanaojifanya kuwa wahubiri ili wasikilizaji wapate kupuuza mahubiri yao? Ikiwa hawapo basi tamko halisadifu uhalisia.

**Kusimanga:**

12. [[*Maimamu, kwa vile hatuna uwezo mnatuita kuwaombea dua…]] Allah mghufirie…*

Hapa, Imamu huyu anaeleza sababu ya kuhudhuria kwake na wenzake mazishi ya Waislamu ambao walikuwa wakishiriki katika sherehe ya tohara, ambayo ni kuonewa. Hii ina maana kwamba kama wangalikuwa na uwezo wa kukataa wasingethubutu kwenda kuwazika watu wa namna hiyo. Zaidi ya hayo, wasingethubutu kuwaombea msamaha na kughufiriwa madhambi kwa sababu hawafai kufanyiwa hayo.

Nia ya Imamu ilikuwa kuonyesha uchungu juu ya kuitwa na maamuma ili kuongoza shughuli za mazishi ya wanaowachukulia kuwa waasi. Athari ya tamko hilo ilikuwa kuudhika kwa baadhi ya waumini ambao wametenda matendo kama hayo.

Tamko hilo pia limetimiza masharti ya ufelisiti kwa sababu limeelezea hisia za Imamu kikamilifu na kwa usahihi na isitoshe mtamkaji na hadhira ni mwafaka.

**Kupinga:**

13. *Hadithi inayosema bismillahi ilipokelewa na nani?Yule aliyepokea hadithi zama za mtume na yule aliyepokea hadithi wakati wa khulafaa Rashidun [[ tufuate la nani]]?*

Tamko hilo lilitolewa kutokana na kutofautiana kuliopo kati ya wasomi kuhusu “Bismillahi”. Huku baadhi ya wasomi wakitoa fatuwa kwamba Bismillahi husomwa moyoni katika sala, wengine waliona kuwa lazima isomwe waziwazi. Nia ya tamko ni kupinga maoni ya wanazuoni na mafundisho ya mashekhe. Hivyo ni kwa sababu hadithi zote mbili zinazozungumzia usomaji wa bismillahi zilipokelewa kutoka kwa mtume Muhammad (SAW). Matumizi ya kila mojawapo ya hadithi hizo ndiyo tofauti. Athari ya tamko hilo ni kuudhika kwa Maamuma kutokana na kile wanachoona kwamba ni hujuma kwa mashekhe na kupinga hadithi isemayo kwamba bismillahi isomwe kimoyomoyo. Usomaji wa Bismillahi silo jambo pekee lililozua utata, bali pia kuna swala la dua.

Kama ilivyoelezewa hapo awali Kur’ani na Sunna ama hadithi ni vyanzo viwili kati ya vyanzo vya sheria za Kiislamu. Hadithi za mtume (SAW) hutoa mwongozo juu ya jinsi Mwislamu anavyotakikana kuendesha mambo yake katika maisha yake ya kila siku. Sahaba za mtume (SAW) walitunza hadithi nyingi kuhusu jinsi mambo fulani yanavyofanyika. Waislamu wanashauriwa kurejelea Kur’ani au hadithi katika kila jambo.

Ingawa mzungumzaji ana mamlaka ya kuwahutubia waumini, kauli hiyo haikutolewa katika muktadha mwafaka. Hivyo ni kwa sababu mas’ala ya hadithi na upokezi wake huwahusu wataalam na sio Waislamu wa kawaida. Inafaa waambiwe tu yale wanayopaswa kuyafanya na sio kuwahoji juu ya kufuata la nani na kuacha la nani ili wasikanganyike. Kwa hiyo kitendo neni hicho hakikutolewa kikamilifu na kwa usahihi.

**Kutukana:**

14. *Unajua anayepinga Kur’ani inafaa aitwe nani? Kafiri.[[Mwenye kupinga maneno ya Mwenyezi Mungu aitwe nani ? Kafiri]].*

Katika Uisilamu dua ni kitendo cha ibada, ni lazima kwa kila muumini kumlingania mola wake ili apate kumkidhia haja zake. Katika Kur'ani Mwenyezi Mungu amesema:"Niombeni nitakujibuni. Kwa hakika wale wajivunao kufanya ibada yangu, bila shaka wataingia Jahannamu, wadhalilike".(Al-Farsy, 1984; 40:60).

Katika aya nyengine ya Kur'ani, Mwenyezi Mungu anasema:
"Na waja wangu watakapokuuliza hakika yangu,(waambie kwamba) Mimi niko karibu nao. Naitikia mwombaji pindi anaponiomba. Basi na waitikie na waniamini, ili wapate kuongoka." Al-Farsy, 1984; 2: 186).

Aya hizo ni dalili toshelezi kwamba kuomba dua ni jambo la kidini linalomlazimu kila muumini kulitekeleza na wanazuoni wanakubaliana juu yake. Mushikili hujitokeza katika jinsi ya kuomba dua. Baadhi ya mashekhe wanaona kwamba lazima Imamu asome dua na waumini wake waitikie kwa amina. Lakini baadhi yao huona kwamba kila mtu ana shida zake ambazo zinaweza kutofautiana na walizonazo watu wengine, basi kuna haja ya kila mtu kuomba dua yake baada ya kumalizika kwa sala za faradha. Kwa hivyo, tamko la Imamu hurejelea mashekhe ambao wana msimamo wa pili. Anawachukulia kuwa wapinga Kur'ani.

Nia ya tamko ni kuwatukana na kuwadunisha Mashekhe ili waumini waone kwamba wakiwafuata watawapoteza njia. Wakati huo huo Imamu huyo anaonyesha kwamba yeye ndiye mwenye ujuzi juu ya mambo ya dini na kuwa ndiye anayepaswa kusikilizwa. Athari za tamko hilo ni kudharauliwa kwa wasomi wasiowaombea watu dua. Athari nyingine ni kuudhika kwa waumini ambao wanaona kwamba Imamu anawatukana waumini wakiwemo mashekhe wenzake.

Ikiwa wanaorejelewa na kitendo neni hicho ni Maimamu, basi ni dhahiri kuwa masharti ya ufelisiti yamekiukwa. Kwanza, Imamu huyo hana mamlaka na hata kama angalikuwa nayo mahali pa kuyatekelezea si mwafaka. Vivyo hivyo, tamko halikutolewa kikamilifu kwa sababu Imamu anawasawiri wenzake kama wanaopoteza watu kwa matamko yao na hali anawakanganya wasikilizaji wake kwa kujadilia mas'ala ambayo ni juu ya kiwango chao cha kielimu.

**Kulaumu:**

15. *Ndio maana unawaona viongozi wangali na fikra ya kupenda uongozi. [[Wewe mwanamume, mtu mzima, Mwenyezi Mungu amekupa majukumu, akakurahisishia dunia lakini bado una ile damu [kimya]].*

Ufikapo wakati wa uchaguzi wanasiasa hutafuta kura kwa udi na uvumba. Kwa hiyo kuna miko wanayovunja. Wakristo wataenda misikitini, washiriki katika sala na baadaye wauhutubie umati wa watu kwa madhumuni ya kuwaomba kura. Waislamu nao wataenda kanisani na hata katika vilabu vya pombe kusudi wapate fursa ya kuomba kura.

Fursa kama hiyo ilijitokeza siku moja katika kijiji kimoja kwenye mpaka wa Uganda na Kenya, ambapo Waislamu walitangamana na Wakristo katika ibada ya kumwombea maiti ya Bwana mmoja ndani ya Kanisa. Waislamu hao, inasemekana kuwa walishiriki katika uimbaji wa nyimbo zinazohusiana na sherehe hiyo ya mazishi na kwamba hawakubanduka kwenda kusali sala za dhuhri na Aswir.

Kauli ya Imamu inawerejelea watu hao kwa nia ya kuwalaumu maamuma kwa kutowahi sala kabla ya kwenda kuhudhuria mazishi na pia kujitia katika uimbaji wa nyimbo zisizowahusu ndewe wala sikio.Tamko hilo liliwaathiri wasikilizaji wa khutuba kwa kuudhika wakidai kwamba Imamu aliwaaibisha kwa kuwasema mbele ya hadhira kubwa kama hiyo badala ya kuwaita kando ili kuwakosoa.

16. *Akina mama! Mcheni sana Mwenyezi Mungu(SW). Wanaume wakitaka kuwanyoosha watoto wao, nyinyi huwawekea mbele vizingiti na kusema: "Sitaki umseme mwanangu". Taarifa tulizopata ni kwamba [[watoto wengi wamekuwa watovu wa nidhamu kutokana na akina mama]]. Msichana anaweza kushika mimba, mamaake akakataa kumwarifu mumewe. Maskini mwana mume hakai nyumbani. Hana habari. Ni baada ya miezi sita ndiyo apate kugundua ukweli wa mambo. Lakini sukari mama huwa ameinywa kitambo. Baba akifoka husema: "Mwache mwanangu"...*

Kauli hiyo huwarejelea wanawake ambao husemekana kuwa wanawatetea sana mabinti zao hata kama vitendo wavitendavyo hukiuka maadili ya dini ya Kiislamu. Nia ya kutoa kauli kama hiyo ilikuwa kuonyesha uchungu kutokana na ripoti zilizomfikia Imamu kwamba wazazi wa kiume wanapowakaripia mabinti zao kutokana na mienendo isiyoridhisha, wake zao huwafokea wakidai kuwa wana wao wanakoseshwa raha na starehe. Kwa kutoa kauli hiyo, Imamu aliwatarajia wazazi hao kusaidiana na waume zao ili kuwanyoosha watoto wao badala ya kuwaacha waaibishe jamii kutokana na vitendo kama vile zina, mavazi yasiyositiri sehemu za siri na kadhalika.

Pamoja na hayo, baadhi ya akina mama waliathirika kwa kuudhika wakiona kwamba ni jukumu lao kuhakikisha kuwa mabinti yao hufanya mambo yanayoambatana na usasa na hakuna aliye na haki ya kuwazuia kufanya hivyo.

Ijapokuwa Imamu alitaja moja kwa moja kitendo cha akina mama, lakini kwa njia isodhahiri alikusudia kuonyesha kero aliyokuwa nayo kuhusiana nacho. Wasikilizaji waliweza kugundua nia yake na kuathirika kwa namna hiyo. Kwa hiyo kitendo neni hicho si dhahiri.

Imamu alizingatia masharti ya ufelisiti kwa sababu ndiye aliye na mamlaka ya kuwaongoza maamuma katika mambo ya kidini, muktadha ambamo matamko yalitolewa ni faafu na hadhira ni mwafaka. Vivyo hivyo, aling'amua yale yaliyokuwa moyoni mwake akijua kwamba walengwa wake wana uwezo wa kujirekebisha na kwa kufanya hivyo ametimiza masharti ya uaminifu na umuhimu.

Vitathminishi viliwakilishwa na aslimia 33% ambacho ni kiwango kikubwa na ndicho kilichukuwa nafasi ya pili. Hii ni kwa vile ni aina pekee ambayo humpa mzungumzaji fursa ya kutoa tathmini yake binafsi juu ya kitendo kilichopita (Taz. Searle, 1968 na Fraser, 1996). Kwa hiyo, katika shughuli nzima ya uwasilishaji wa khutuba ambayo huchukuwa sana sana dakika 45, Imamu huwa na wasaa wa kuelezea hisia zake kuhusu vitendo anavyovirejelea na matako yake.

### 4.2.4. Vitendo Neni Vilazimishi (VL)

Vitendo neni viazimishi ni aina ya vitendo neni ambavyo huonyesha azma ya mzungumzaji juu ya kutenda jambo. Aina hii haikosekani katika khutuba na hujitokeza kama kutoa ushuhuda na

kumhimidi Mwenyezi Mungu. VL vina uamilifu wa kumwezesha mzungumzaji kuelezea nia ya kujitolea ambayo huambatana na kitendo mahsusi ndani ya urejeleo. Azma ya Imamu huweza pia kujitokeza kupitia katika kuahidi, kuapa, kuhakikisha, na kadhalika. Katika khutuba za Ijumaa mifano ifuatayo ilijitokeza :

**Kuhimidi:**

1. *[[Himdi zote ni za Mwenyezi Mungu]]. Tunamhimidi, tunamwomba msaada na kughufiriwa madhambi yetu. Tunajikinga na Mwenyezi Mungu kutokana na shari zetu na ubaya wa amali zetu.*

Tamko hilo huonyesha kujitolea kwa mzungumzaji kutenda jambo ambalo anaona kwamba ni lazima alitekeleze. Nia yake ni kuwataka wasikilizaji wadhihirishe ungamo lao kuwa kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi na viumbe wote. Wakisha ungama hivyo, ibada yao waielekeze kwake kwani yeye ndiye anayeweza kuwakidhia haja zao zote kama vile riziki, kughufiriwa madhambi na kukingwa kutokana na shari. Athari ya kitendo neni hicho ilikuwa kuungama kama ilivyotarajiwa. Hivyo ni kwa sababu maamuma walitambua maana ya mzungumzaji na tamko lilikuwa mwafaka kwa muktadha na hadhira. Aidha toni aliyoitumia ilichangia katika kuwathibitishia kuwa masharti ya uaminifu na umuhimu yamezingatiwa.

2. *[[sifa njema ni za Mwenyezi Mungu]]. Ni mmoja katika dhati yake hana mshirika. Ni mmoja katika majina yake hana hasimu. Ni mmoja katika uungu wake hana mithili yake. Tunamhimidi himdi zinazoendana na uadhama wake na utukufu wake.*

Kauli hiyo kama zile zilizotangulia za aina hiyo, huonyesha hali ya kujitolea na kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu. Nia yake ni kuwafanya wasikilizaji wafuate mfano wake wa kumweka Mwenyezi Mungu mbele ya kila jambo ili wafanye yale anayowaamrisha na waache anayowakataza. Hisia za wasikilizaji zilidhihirisha hali ya kuungama ambayo ni athari chanya.

**Kutoa ushuhud:**

[[*Natoa ushuhuda kwamba hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na Muhammad ni mja wake na mtume wake*]].

Tamko hilo ni msingi wa imani ya dini ya Kiislamu. Ndilo humwingiza mtu au kumtoa katika Uislamu kwani ni nguzo ya kwanza ya dini hiyo. Ingawa linaonekana kana kwamba kwalo Imamu anairejelea nafsi yake na kuilazimisha ishikilie jambo hilo, lakini kwa kulitaja mbele ya waumuini waliokuwa wakimsikiliza nia yake ilikuwa kuwafanya wakubaliane naye katika kitendo hicho. Athari ya kitendo neni hicho ilkuwa chanya kwani waumini walikubali na kukiri kuwa Mwenyezi Mungu ndiye anayestahili kuabudiwa na ndiye aliyemtuma Muhammad SAW) kuwafundisha watu dini yake. Kauli hiyo imetimiza masharti ya ufelisiti kama matamko mengine ya aina hiyo.

Ingawa VL havikosekani katika kila khutuba, lakini havijitokezi kwa wingi kama VE, VT na VW. Jedwali 4 limetudhihirishia kuwa vilikuwa aslimia 6% tu ya jumla ya vitendo neni vyote vilivyojitokeza .

Mifano yote ya vitendo neni kwa aina zake nne zilizochanganuliwa, imeakisi ruwaza maalumu ya uneni. Ruwaza hiyo ni ya matamko ambayo yanabeba maana ya sentensi na maana anayokusudia mzungumzaji kuiwasilisha. Hivyo ni kusema vitendo neni vilivyotumika si vya moja kwa moja kwa sababu ingawa mzumgumzaji anamaanisha kile anaochokisema, lakini zaidi ya hayo anamaanisha kitu kingine (Searle 1975).

### 4.2.5. Maana ya Matamko ya Khutuba Kulingana na Nadharia ya Udokezi (NU)

Kama ilivyoelezewa katika sura ya pili, nguvu na nia ya tamko hupatikana na kutambulikana endapo maana ya tamko hilo itajulikana. Kwa mujibu wa Grice (1975) na Leech(1983), Nadharia ya Udokezi inatekeleza jukumu la kutambua maana ya tamko kupitia kanuni zake za ushirikiano na unyenyekevu.

#### 4.2.5.1 Maana ya Vitendo Neni vya Khutuba kwa Mujibu wa Kanuni Shirikishi

Grice (1975) alieleza kuwa kuna kaida ya ushirikiano ambayo inatulazimisha kuhakikisha kwamba tunayoyasema katika uzungumzi wetu yawe yenye kuendeleza malengo yetu. Hivyo ni kusema kwamba mzungumzaji analazimika kutii kaida za uzungumzi ambazo ni kiasi , ubora, umwafaka na jinsi. Matumizi ya lugha hutawaliwa na kaida hizo ambazo zimewekwa na jamii tumizi lugha ili kuhakikisha kuwa kuna uaminifu na staha katika mawasiliano.

Kanuni ya kiasi inamtaka mzungumzaji atoe taarifa yake kwa kuzingatia mambo mawili:

- Jambo la kwanza ni kwamba mchango unaotolewa katika uzungumzi wapaswa uwe na taarifa kamili inayotakikana katika uzungumzi.
- Jambo la pili ni kwamba mchango huo usiwe na taarifa zaidi ya ile inayotakikana.

Kanuni ya ubora inamtaka mzungumzaji ajaribu kutoa taarifa ambayo ni sahihi anapochangia mazungumzo. Kanuni hii inamtaka azingatie mambo mawili:

- Asiseme yale ambayo anaamini kuwa si sahihi.
- Asiseme yale ambayo hana ushahidi juu yake.

Kanuni ya umwafaka inamtaka mzungumzaji atoe matamko ambayo ni mwafaka kwa mazungumzo yanayoendelea au muktadha yanamojikita.

Kanuni ya jinsi humshurutisha mzungumzaji kuwa mwazi kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

- Aepukane na matumizi ya istilahi zisizoeleweka na wasikilizaji.
- Aepukane na matumizi ya istilahi zenye utata (maana nyingi).
- Matamko yake yasiwe marefu.
- Matamko yake yapangiliwe sawa sawa. Yafuate nidhamu.

Akmajan na Wenzie (1995) walitoa mfano ufuatao kuelezea iwapo mzungumzaji anatii kanuni ya ushirikiano au la:-

a) Swali: Mume wako yuko wapi?
b) Jibu: Yuko sebuleni au jikoni.
c) Udokezi: Mzungumzaji hajui mume wake yuko katika chumba gani.

Walieleza kwamba mzungumzaji anapotoa jibu (b) anamaanisha kwamba (c) ni sahihi, ingawa yeye mwenyewe hakusema hivyo. Walifafanua kwamba maana hiyo ilitambulika kwa sababu mzungumzaji hakuonyesha dalili ya kutoshirikiana na kwa hiyo inachukuliwa kuwa ametoa taarifa kamili inayofaa na ambayo alitakikana aitoe. Lakini ikiwa mzungumzaji anajuwa mahala alipo mume wake, basi atakuwa anampotosha msikilizaji kwa sababu anajifanya tu kwamba anashirikiana wakati hafanyi hivyo.

Maimamu mbalimbala walitoa matamko kadhaa katika khutuba zao na kwa kutumia mkabala wa Grice tunaweza kupata maana iliyokusudiwa kama katika mifano ifuatayo:-

1. a) *Lakini Uganda "baganda bange". Ikiwa mashekhe tutawapa nafasi waseme wanalotaka, basi huku ni kuwapoteza. Inafaa kila wanalozungumza tuwaulize. Usikubali kuzungushwa. [[Mwambie nifundishe. Ikiwa hunifundishi basi wewe huna kitu]].*

b) Udokezi: Mhubiri hana imani na mafunzo wanayoyatoa mashekhe wengine na kwa hiyo anawataka maamuma wadharau mafunzo hayo ikiwa hawakutoa dalili juu ya ukweli wake. Ikiwa matamko ya mhubiri Katika (1a) yametii kaida za ushirikiano, basi (1b) ni sahihi, ingawa yeye mwenyewe hakusema hivyo.

2.a) *Mhubiri: Dua hii "Rabbana 'ghfir lana wal ikhwaninal ladhina sabakuna bil iyman" iko wapi. Katika Kurani. Ya kuwaombea watu gani? Waliokufa. Na wewe mbona wasema dua ya waliokufa haifai*?

b) Udokezi: Mhubiri anajaribu kuwathibitishia maamuna wake kwamba dua ya wafu inasihi kwa kunukuu aya ya Kurani.

Ikiwa dalili aliyoitoa ni mwafaka kwa maudhui basi (2b) itakuwa sahihi kwa sababu atakuwa ametii kaida ya ushirikiano. Kwa upande mwingine dalili hiyo isipoafikiana na muktadha wa mahubiri yake, mhubiri atakuwa akijifanya kwamba anashirikiana na wasikilizaji wake ilhali anatoa ujumbe potofu.

Katika mifano ifuatayo kanuni shirikishi imekiukwa na Maimamu:

KN13. *Mashekhe wengi hatuwaoni kwenye dua ya watu waliokufa kwa ajili wanasema ni bidia. [[Sasa itakuwa hatari kupinga Kur'an]].*

KN14. [[*Unajua anayepinga Kur'ani inafaa aitwe nani? [Kimya] Kafiri]].*

KN15. *Leo unasema hakuna arobaini. Lakini ikifika mwisho wa mwezi unagonga mlango. Unasema unataka mshahara.*

KN16. *Dua zetu sasa ni za upuuzi. Kila mmoja anainua mikono kuangalia madirisha. Anaangalia milango anasema Shekhe hamalizi. Sasa Mungu atajibu nini kwenye dua? Wewe huko kwenye dua.*

KN17.*Unamuomba Mungu umenyoosha miguu au umekaa umeegemea hivi. Inataka tumuonyeshe heshima.*

KN18. *Bush alipanga vitu vyake, akaingia, akaua watu wa Iraqi, akapindua gavumenti ya Sadam, mwisho akamwua na nani? [kimya] Kuonyesha udhaifu wetu alimwua siku ya udhuhiya. "Waislamu wanachinja chinja… wacha nimchinje, nimnyonge mtu wao".*

Imamu ametoa vitendo neni Kadhaa ambavyo vyote vinazungumzia swala hilohilo la dua. Katika matamko yake hayo ametumia sifa mbalimbali za usemi, kama vile kuuliza maswali na kuyajibu mwenyewe, kutoa ushahidi juu ya madai yake na kusimlia visa kutoka katika maisha halisi. Lengo lake kulingana na majibu ya wasailiwa na Nadharia ya Udokezi ni kuwazindua wasikilizaji na kuwaelimisha juu ya umuhimu wa dua, kulaumu watu ambao hawaombi dua na kuwashinikiza wasikilizaji wapinge mafundisho ya Maimamu ambao wanaona kwamba dua ya wafu si lazima isomwe. Lakini tukiyaweka matamko yake kwenye mizani ya kanuni shirikishi, tutakuta kwamba kuna ukiukaji wa kanuni hizo.

Matamko ya baadhi ya khutuba zilizoshughulikiwa yamekiuka kanuni ya jinsi. Yamekuwa marefu, yenye utata na hayakupangwa sawasawa. Kwa kufanya hivyo Maimamu walikuwa wakikwepa kusema ukweli kwani hawakuwa na ushahidi juu ya wanayoyasema lakini waliwachanganya wasikilizaji ili waendelee kuwaunga mkono katika matendo yao. Aidha, kuwasilishwa matamko hayo jinsi yalivyowasilishwa, kulikuwa na maana ya kulaumu Waislamu kwa kutoshabikia dua na kutotoa sadaka.

Kanuni ya kiasi inamtaka mzungumzaji atoe taarifa inayohitajika tu. Lakini katika baadhi ya khutuba kanuni hiyo imekiukwa kwa sababu imekuwa zaidi ya ile inayohitajika. Mfano ni khutuba iliyolengwa kushughulikia maudhui ya "mtoto wa shetani" ambapo Imamu alitaka kumtambulisha ili wasikilizaji wake wamjue. Badala ya kuzungukia katika mipaka hiyo ambayo

alijiwekea, alitoka nje na kuanza kutoa hukumu juu ya watu ambao wanashiriki katika miviga ya tohara na kusema:

KN19. Mshirikina akimchinja *Mnyama hatumli …hazikwi katika makaburi ya Waislamu.*

Kukiukwa kwake kaida hiyo ni ishara kwamba alikuwa akiwasiliana kwa namna isiyokuwa ya moja kwa moja na kwamba alitilia maanani kanuni ya unyenyekevu. Kwa kutumia kanuni ya huruma, Imamu hakutaka kuzusha uhasama kwa kuwaita washangiliaji wa miviga ya tohara "watoto wa shetani" kwa sababu angeonekana kuwa mtovu wa nidhamu. Kwa hiyo alitii sheria ya unyenyekevu na kanuni zake za busara, ukarimu, ukubalifu, staha, makubaliano na huruma.

Kwa mujibu wa kanuni ya ubora, inatakikana, ithibati itolewe juu ya kila tamko la mzumgumzaji. Ithibati isipotolewa, maana ya tamko hukiuka ile ya kileksia ambayo ni ya kawaida. Mfano wa matamko juu ya dua, umebainisha kwamba ithibati aliyoitoa mhubiri ni ya kijumla na haihusiani na kuwaombea waliokufa dua maalum. Kukiukwa kwa kanuni hiyo ni ishara kwamba Imamu hana ushahidi toshelezi ingawa anajifanya kuwa anashirikiana na wasikilizaji wake katika kutii kanuni ya ubora kama anavyotarajiwa na jamii. Kwa hivyo umaanisho wa matamko yake ukawa kuwakanganya na kuwapotosha wasikilizaji.

Kulingana na kanuni ya umwafaka, matamko yanatakikana kuwa mwafaka na mazungumzo au mada inayojadiliwa. Hata hivyo, utafiti huu umebaini kwamba baadhi ya khutuba hukiuka kanuni ya umwafaka kimakusudi. Hivyo ni kwa sababu mhubiri alikuwa akizungumzia dua ya wafu lakini mifano na ushahidi alioutoa ulikiuka kanuni hii na kugusia dua nyinginezo. Kwa hiyo matamko yake yalilenga kushawishi wasikilizaji wakubali maoni anayoyashikilia juu ya dua ya wafu. Mifano ifuatayo ni vielelezo vya ziada juu ya ukiukaji wa kanuni za uzungumzi:

KN20. *Ndio maana leo viongozi[kimya] viongozi bado wana fikra za kupenda mambo ya siasa, hapo hujampenda mtume(SAW)[kimya]Ndio maana leo viongozi wangali wanafikiria juu ya mambo ya siasa. Unamkuta mtu mzima, Allah amekupa majukumu, akakulainishia dunia[kimya]Bado mna ile damu[kimya] Mtume wetu Muhammad(SAW) alitubainishia, alituongoza. Yote yale yaliyofaradhishwa, alituletea. Hata jinsi tunavyomwabudu Allah(SW)*

*mtume alitubainishia… Nakuusiyeni, nikiiusia nafsi yangu pia, kwa sababu mimi si mbora kuliko nyinyi… tuungane katika kumtii Allah*.

Katika sehemu hii, Imamu alitakiwa kumhimidi Mwenyezi Mungu na kumsalia mtume Muhammad (SAW). Lakini badala kuendeleza himdi hizo na sala, alitoa matamko yaliyozidi kiasi cha haja. Kwa hiyo, alikiuka kanuni ya kiasi na lazima kuwe na sababu ya kufanya hivyo. Nadharia ya Udokezi ndiyo inayotuongoza kufikia ufasiri kwamba Imamu huyo huwachukulia Maamuma wake kama watu ambao bado hawajatambua Mwenyezi Mungu kama muumba wao ambaye kila sifa njema ni zake na ndiye ambaye anapaswa kuabudiwa kwa haki. Vivyo hivyo, anawachukulia Maamuma hao kuwa hawamtambui pia mtume Muhammad kwani wangalimtambua, wangalimwabudu Mwenyezi Mungu kulingana na mwongozo alioutoa mtume huyo. Kwa hivyo, nia yake ilikuwa kuwakaripia wale walioshirki katika shughuli ya mazishi kwa kushiriki kwao kikamilifu katika ibada ya mazishi badala ya kushuhudia tu na kuwaachia wenyewe kuimba kulingana na imani ya dini yao.

KN21. *Kwa hiyo waja wa Allah tutajifunza jinsi ambavyo mtu anapaswa kumfuata Allah(SW)… waja wa Allah, Allah(SW) amesema katika kitabu chake kitukufu Kur'ani kwamba: "Nimeandaa moto wa Jahannam kwa viumbe wengi" Lakini katika viumbe hao, alipofafanua alisema: " Wana nyoyo lakini hawatambui kwazo". Kutambua kile kinachotuongoza leo. Bali kila uchao. Mwislamu kila asubuhi Mwislamu ana jambo. Butiru, mahindi. Nakhupa, mahindi. Wenye magari, usukani. Walioko mashambani, nao hivyo hivyo. Kila mtu katika kazi inayokughuri ukawa humwabudu Allah. Ndio maana Allah akasema: "Wana nyoyo lakini hawatambui kwazo". Kwa mfano, jana tulikuja hapa. Tulikuwa na misiba mingi… wengine walienda kuhudhuria mazishi huko Sironko, wengine tulihudhuria mazishi ya kansala…[[Lakini kwa vile Allah ameuandaa moto wa jahannam kwa ajili ya nyoyo zisizofikiria juu ya miili yao, Waislamu wote walienda pale kanisani na tuliokuja kusali hapa, tulikuwa hapa na mweka hazina na kijana Yasin…hilo mlilichukulia kama jambo kubwa sana na hakuna aliyejali ibada…]] Mlichukulia maiti kama ibada kuu...*

Baada ya kuitambulisha mada yake ambayo ni jinsi ya kumfuata ama kumtii Allah, Imamu alisoma aya ya Kur'ani inayoelezea kuwa Mwenyezi Mungu ameuandaa moto wa Jahannam kwa

watu wenye nyoyo, masikio na macho, viungo vya mwiili ambavyo hawatambui wala kusikia na kuona kwavyo, na kwamba wao ni kama wanyama au wamepotea zaidi kuliko wanyama. Kisha akataja kitendo cha Waislamu kwenda kanisani na kukaa huko kutwa nzima na kwamba ni wachache waliotoka huko wakaenda msikitini kusali. Hapa kanuni ya kiasi ilikiukwa kwa sababu ya upungufu wa taarifa aliyoitoa baada ya kuitambulisha mada. Kanuni za umwafaka na jinsi zilikiukwa pia. Hivyo ni kwa sababu mada ni jinsi ya kumtii Mwenyezi Mungu na ushahidi ulitakikana uafikiane na mada hiyo. Aidha kulingana na kanuni ya jinsi, Imamu alitakikana kutoa matamko ambayo yanahusiana na jinsi ya kumtii Mwenyezi Mungu. Hata hivyo, ukiukaji wa kaida hizo uliashiria kwamba mtu anaweza kuonyesha utiifu wake kwa Mwenyezi Mungu kupitia matumizi ya viungo alivyojaliwa na Mungu. Kwa kutumia viungo hivyo, Waislamu walitakiwa watambue kuwa wakati wa sala umewadia na kwamba msiba kama huo wa kufiwa na jamaa au rafiki huonyesha kuwa walio hai hawana budi kuonyesha utiifu kwa Mungu kwa kuitikia adhana na kwenda msikitini kusali kisha warudi mazikoni. Nia ya Imamu ni kuwalaumu walioacha sala na kuwaonya Waislamu kwa ujumla dhidi ya kughafilika katika ibada.

KN22. *Hakuna funzo mlilopata kutoka kwake wala kujiuliza Allah amemtoa hapa, amempeleka wapi? Ameenda na nini? Tukienda kwenye kaburi, kwanza pateni funzo huko. Mwenzetu tuliye mpeleka kaburini amenda na nini? "Yaa ayyuhal insaan…". Mwenyezi Mungu amewaiteni, enyi watu. Mara hii hakuwarejeleeni kama waumini. Amemwiita mtu popote ulipokaa. Hata kama wewe ni nani , hata kama wewe ni nani katika heshima zako. "Innaka kaadihun ilaa rabbika kadhan famulaaqiih". Mwakazana sana… ndiyo maana mwenye maduka hawezi kuyafunga sasa. Anahofia nikitoka huko, nikienda kusali, nitakuta riziki imeshaenda. Mwengine kwamba nisipoenda kununua mahindi, kuzunguka huko leo nitaambulia patupu. Mwengine kwamba nisipotafuta ngo'mbe , mwengine nisipoendesha ghari, mwengine nisipojenga ghorofa, wengine mnasema nisipojenga nyumba ya kudumu…lakini mnakazania sana dunia…wanakubembeleza ulete mfuko mmoja wa simenti…*

Ilikuwa baada ya kuitambulisha mada, azame katika uelezaji wa jinsi Mwenyezi Mungu anavyoweza kutiiwa na ataje kinagaubaga mambo yanayoelezea mada hiyo. Lakini kinyume na hayo, tunamwona khatibu akitoa taarifa ambayo inaelekea kuwa zaidi ya inayohitajika, isiyoafikiana na mada, na akitumia matamko yasiyokuwa ya moja kwa moja. Kwa kufanya

hivyo, tunaona kuwa amekiuka kanuni za kiasi, ubora, umwafaka na jinsi. Kwa hiyo umaanishaji unatuongoza kuhitimisha kwamba Imamu alikusudia kuelezea kuwa Mwenyezi Mungu anaweza kutiiwa kwa kudumisha sala nyakati zote, za raha na za shida, kuiweka safi misikiti ambayo ni mahali pa kufanyia ibada, kuepukana au kusitisha shughuli ambazo zinaweza kutatiza shughuli ya ibada, kuacha kutafuta utukufu kwa wanadamu wenzetu na badala yake utafutwe kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa kutoa matamko hayo jinsi alivyofanya, Imamu alikuwa na nia ya kuwalaumu Waislamu wanaotenda vitendo alivyovitaja na kuwaonya wasikilizaji wake dhidi ya maasi.

Ijapokuwa baadhi ya khutuba za Ijumaa zilikiuka kanuni za ushirikiano, Maamuma waliweza kutambua maana ya vitendo neni vya khutuba hizo kulingana na majibu waliyoyatoa. Katika tamko lifuatalo kuna ukiukaji wa kanuni vilevile:

KN23. *Waislamu wa Raudha tuwe kitu kimoja. Fitna hazituhusu. Tunatumiwa ma spy. Miaka minne mwanamke ananikoroga. Muulize. Utapata habari. Kapigwa na nuclear. Si headmistress tena bali ni mwalimu tu.*

Katika tamko hilo, Imamu alitumia istilahi *nuclear* yenye utata mwingi kwani inaweza kuwa kama ile iliyorushiwa watu wa Hiroshima na Nagasaki huko Japan. Lakini tukizingatia ukweli kwamba yeye ni Imamu wa kawaida na hana ufungamano wowote na mambo ya silaha kwani si mwanajeshi, inatubainikia kwamba hawezi kupata zana za *nuclear* ya kawaida ili azitumie kuwadhuru watu. Kwa hiyo hapa Imamu kakiuka kanuni ya jinsi na ugunduzi huo unatuongoza kufikia ufasiri kwamba Imamu haelekei kuuwasilisha ujumbe wake moja kwa moja. Muktadha ambamo istilahi hiyo imejitokeza hudhihirisha kuwa alichokusudia ni kwamba alimpiga mlengwa wake kisomo ambacho kilimkosesha cheo. Kwa hiyo nia yake ilikuwa kutoa tishio kwa wasikilizaji wasithubutu kumkoroga ili wasipate kilichompata mtema kuni.

Ifahamike kwamba mifano iliyotolewa huthibitisha kuwa Maimamu huwasilisha ujumbe wa khutuba za Ijumaa wakitumia mbinu mbalimbali. Wanaweza kutumia mbinu ya uwasilishaji ujumbe moja kwa moja au kinyume chake na wanaweza kuchanganya mbinu hizo zote. Nadharia ya Udokezi imeonyesha kuwa kulikuwa na hali ya kuwasilisha khutuba kwa kutumia matamko

yasokuwa ya aina ya moja kwa moja. Hata hivyo, nia zao ziligundulika kutokana na muktadha ambamo matamko yalijitokeza.

### 4.3 Athari za Vitendo neni vya Khutuba Kulingana na Wasailiwa

Vitendo neni hutumika kama nyenzo ya kupata vitendo athari. Tamko la mzungumzaji, kwa hivyo, huwa na athari juu ya mawazo ama hisia za msikilizaji iwapo msikilizaji huyo atatambua nia ya mzungumzaji (Brown na Yule, 1993; na Akmajan na Wenzake, 1995).

Kama ilivyoelezewa katika sura ya kwanza, mwanzoni khutuba hazikuwa zikitafsiriwa katika lugha za kienyeji kutokana na shinikizo liliokuwepo kwamba Kiarabu ndiyo lugha ambayo ilifaa kutumika na Maimamu kuwasilishia matamko ya namna hiyo. Kwa hivyo, kutokana na ukweli kwamba Waislamu walikuwa hawakijui Kiarabu, ujumbe uliokitwa katika khutuba hawakuupata. Athari walizozipata katika matamko ya khutuba zilitokana na matamko kama vile "*shahaadah*", *"swalaat"*, *"zakat"*, *"swaum Ramadhan"*, *"hijju baitillahil haraam"* ambayo hupatikana katika nguzo za Uislamu na mengine kama *"Allah"*, *"malaika"*, *"kutubihi"*, *"rusulihi"*, *"yaumil aakhir"* na *"kadar"* ambayo huyapata katika nguzo za imani. Nguzo hizo hutambulikana kwa Waislamu wengi kiasi kwamba hata kama hawajui Kiarabu, kutajwa kwa mojawapo ya maneno hayo humwezesha msikilizaji kupata fununu kuhusu kile kinachozungumziwa. Hivyo basi wasikilizaji wa khutuba zama hizo walipata kuathirika kwa namna ambayo iliwawezesha kushikamana na mafundisho ya dini yao.

Hata hivyo, hawakuathirika kiasi cha kuwafanya wachukie khutuba na waamue kuikimbia misikiti kama Maimamu wanavyobainisha. Athari hasi zilianza kuzungumziwa baada ya khutuba kupiga hatua fulani. Kwanza kwa kutafsiriwa kwa zile zilizokuwa zikiwasilishwa kutoka vitabuni halafu kuwasilishwa na wasomi katika lugha za kienyeji.

Kufuatia maendeleo hayo ya khutuba, kulizuka mgogoro baina ya wazee na vijana. Huku wazee wakiona kwamba vijana wameingiza katika dini fikra mpya, vijana waliwaona wazee kama wanaoficha ukweli ili kuendeleza ujinga, ushirikina na uzushi, mambo ambayo yamepingwa vikali katika mafunzo ya Uislamu wanayopata kutoka kwa Maimamu na Mashekhe chipukizi. Maendeleo hayo ya khutuba pia yalidhihirisha kwamba kumbe matamko hayo yatolewayo

kwenye mimbari, hulaani vitendo vya maasi, huelimisha, huhimiza na hutoa vitisho ili waumini wapate kusalimika katika dunia hii iliyojaa masaibu. Kutokana na maana kama hizo, athari hasi zilianza kupatikana kwa sababu Maimamu walionekana na wanaendelea kuonekana kama wanaowatungia watu khutuba kwa minajili ya kuwakashifu mbele ya wenzao.

**4.3.1 Maoni ya Maimamu (MI) kuhusu athari za vitendo neni.**

Maoni yafuatayo, ambayo yalitokana na mahojiano na Maimamu huthibitisha madai kwamba Maimamu huwakashifu Maamuma katika khutuba.Wakijibu swali iwapo kuna wanaolalamika dhidi ya khutuba, Maimamu walisema:

MI1.*"Nga wasomele ikhutuba imukuunyakho waakhalala wakhukanikhakho ari Imamu niye uuli khuukhuoona mu muzigiti."*

*'Ukisoma khutuba inayomgusa hukasirika na kulalamika dhidi yako eti Imamu* ndiye *anayetufukuza msikitini'.*

MI2*. "Iwase baliyo banji babiilukha mumuzigiti bari lwekhuba nabakanikhilekho."*

*'Kwangu kuna wengi wanaoutoroka msikiti eti kwa sababu nimewataja'.*

Matamko yatolewayo na Maimamu katika khutuba yanawarejelea wasikilizaji ili wapate kuyatilia maanani. Mara nyingi Maamuma hukumbushwa juu ya umuhimu wa kutekeleza nguzo tano za Uislamu ambazo ni kuhakikisha kwamba hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, kusali sala tano kila siku, kutoa zaka, kufunga mwezi mzima wa Ramadhani na kwenda Makka kutekeleza ibada ya Hija. Vilevile katika mahubiri ya kawaida Maimamu hugusia maswala yanayoambatana na nguzo sita za imani ambazo ni kumwamini Mwenyezi Mungu, malaika zake, vitabu vyake, mitume zake , siku ya akhera na kadar ama maamuzi ya Mwenyezi Mungu mazuri na mabaya hutoka kwake. Iwapo Mwislamu atakuwa na upungufu katika kutekeleza matendo yanayoshikamana na mafundisho hayo, Imamu atalazimika kutaja hayo katika khutuba zake. Lakini kulingana na maoni ya Maimamu wote waliohojiwa, Maamuma wengi hawapendelei kutajwa kasoro kama hizo kwa namna ambayo watawekwa lawamani au kuonekana kuwa ndio wanaotenda maasi. Matendo yaliyoshutumiwa ni kama vile kuacha sala, kukataa kutoa zaka, kuonyesha unyenyekevu katika mwezi wa Ramadhani na siyo

katika miezi yote, kuacha hija kwa wale ambao ni matajiri, kuzini, vitendo vya ushirikina na kadhalika. Wanaoyatenda huwa miongoni mwa hadhira inayosikiliza khutuba. Kwa hiyo haishangazi kuona kwamba wanapata kero na kuamua kuikimbia misikiti yao.

MI3.*"Nga wasomesele khu shindu shesi bakhola baambasa bari wakanikhile khu nibo. Nga naalomele ndi uukhasaala imbiitsi imufuura aloma ari waakhufumile. Umundu ukundi nga witsile wasomesele khusheeneesho baloma bari uyo baamukulile "*

*'Unapofundisha juu ya jambo wanalotenda wao, hufikiria kwamba umewataja. Nikisema kwamba asiyesali nguruwe ni bora kuliko yeye, husema kwamba nimewatukana. Mtu mwengine akija akazungumzia hayo hayo husema kwamba amenunuliwa'.*

MI4.*"Uri uloma uri iswala ndwela nga wakilekhele shikhumalila khuuba umukaafiili, baloma bari wabakafuasile. Baloma bari bali khureela idini injaakha."*

*'Unaposema kwamba ukiiacha sala moja, inakutoshelezea kuwa kafiri, husema kuwa umewaita makafiri. Husema kwamba wameleta dini mpya'.*

Ili kuwafanya waepukane na matendo na tabia isiyorandana na mafundisho ya dini yao, Maimamu wanawatisha waumini wao kwa kuwamithilisha watendao mabaya na wanyama. Hivyo ni kwa sababu wanyama waliumbwa kama wanyama na kwa hiyo hawana akili inayowawezesha kutambua na kuzingatia yanenwayo. Mifano kama hiyo huzidisha kero kwani wanaona kuwa wametukanwa.

Pamoja na hayo, si waumini wote wenye mtazamo kama huo. Maoni ya Maimamu huonyesha kuwa katika baadhi ya misikiti kuna wanaopinga na wanaotilia maanani matamko ya Maimamu :

MI5. *"Nga wasomesele, mulimo tsigrupu tsibili. Baafubukha bafukilisa. Baazeeyi uri ukuunya khu shiriki baaloma bari warelele idini injaakha."*

*'Unapofundisha, kuna makundi mawili. Vijana huamini. Wazee ukitaja ushirikina wao husema umeleta dini mpya'.*

MI6. *"Baalala biila tsindulo baloma bari ilala Imaamu byaakanikhaabyo bituufu namwe bibye?Biitimisa boonyene mu muzigiti".*

*'Wengine wanarudi pembeni na kusema hayo ayasemayo Imamu ni ya kweli? Wao hujifukuza wenyewe msikitini'.*

Mifano hiyo ni ithibati toshelezi kwamba baadhi ya matamko yanayojitokeza katika khutuba huwaathiri wasikilizaji taathira hasi. Pamoja na hayo, Maimamu walipoulizwa iwapo wanajali hisia za Maamuma wao walisema:

MI7. "*Ise iifayo ta nga ndi khusoma ikhutuba khubanga isoma aya iya Kur'ani ni hadithi*. *Nga naamanyile ndi shamuambilekho, imulanga naamwokesa aya ni hadithi".*

*'Mimi sijali nikiwa nawasilisha khutuba kwa sababu nasoma aya za Kur'ani na hadithi. Nikitambua kuwa ameguswa namwita na kumwonyesha aya na hadithi'.*

Maoni ya Maimamu yaliyojitokeza hapo juu huthibitisha kuwa Maamuma huathirika na matamko yao kama yanavyojitokeza katika khutuba na kwamba baadhi ya athari hizo ni hasi. Kwa upande mwengine, maoni ya maamuma hudhihirisha kuwa kuna athari hasi na chanya katika vitendo neni vya khutuba.

### 4.3.2 Maoni ya Maamuma (MM) kuhusu Athari za Vitendo Neni.

Maoni hayo yalikuwa ya aina mbili, yaani maoni ya kijumla juu ya uwasilishaji wa khutuba na maoni maalum ambayo yalihusu matamko yaliyoainishwa kama vitendo neni. Maoni hayo ndiyo yaliyochukuliwa kama athari na yaliainishwa katika viwango mbalimbali kama inavyobainika katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali la 5: Viwango vya Athari ya Vitendo Neni vya Khutuba kwa Waumini**

| | | | | Athari | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Khutuba | KZK | KLK | KZT | KGM | KHK | KBK | KDK | KPZ | KKN | **Jumla** |
| 01 | 08 | 03 | 03 | 01 | - | 01 | 03 | - | - | **19** |
| 02 | 02 | 03 | 08 | 01 | - | 02 | 10 | 01 | - | **27** |
| 03 | - | - | - | 01 | - | - | 21 | - | - | **22** |
| 04 | 01 | - | 02 | 01 | - | - | 11 | - | - | **15** |
| 05 | - | - | - | 01 | - | 01 | 17 | - | 02 | **21** |
| 06 | 02 | - | - | 01 | - | 05 | - | - | - | **08** |
| 07 | 01 | 01 | 10 | 05 | - | 03 | 3 | - | - | **23** |
| 08 | 03 | - | 03 | 01 | - | - | 02 | 01 | - | **10** |
| 09 | 07 | 02 | 05 | 02 | 04 | - | 02 | - | - | **22** |
| 010 | 03 | - | 05 | 03 | - | - | - | - | - | **11** |
| 011 | - | - | 09 | 02 | - | - | 09 | 03 | - | **23** |
| 012 | 11 | 03 | 02 | 01 | - | - | - | - | - | **17** |
| 013 | 01 | 01 | 05 | 01 | - | - | 02 | 01 | - | **11** |
| 014 | - | - | 02 | 01 | - | - | 09 | 02 | - | **14** |
| 015 | 01 | - | - | 03 | - | - | 03 | 05 | - | **12** |
| 016 | 01 | - | 04 | 01 | - | - | 10 | - | - | **16** |
| 017 | 01 | - | 06 | 01 | - | - | 02 | 02 | - | **12** |
| 018 | 03 | - | 02 | 01 | - | - | 03 | - | - | **09** |
| 019 | - | 01 | 08 | 01 | - | - | 05 | - | - | **15** |
| 020 | - | - | 03 | 01 | - | - | 11 | 01 | 02 | **18** |
| Jumla | 45 | 14 | 77 | 30 | 04 | 12 | 123 | 16 | 04 | **325** |
| **Aslimia** | **14%** | **4%** | **24%** | **9%** | **1%** | **4%** | **38%** | **5%** | **1%** | **100%** |

Jedwali 5 limetoa muhtasari wa athari za vitendo neni vilivyojitokeza katika khutuba kwa waumini. Wasikilizaji walionyesha hisia mbalimbali kutokana na vitendo neni 325 vilivyohusishwa katika uchunguzi huu. Hisia hizo zilijitokeza kama kuzinduka (KZK), kuelimika (KLK), kuzingatia (KZT), kuungama (KGM), kuhuzunika (KHK), kuaibika (KBK), kuudhika (KDK), kupuuza (KPZ) na kukanganyika (KKN). Jinsi waumini hao walivyoathirika imedhihirika kutokana na hisia hizo. Kuzinduka, kuelimika, kuzingatia na kuungama huchukuliwa kama hisia chanya. Kuhuzunika kulikojitokeza katika matamko ya khutuba pia kumeegemezwa upande wa athari chanya. Hivyo ni kwa sababu kulingana na matamko hayo,

wasikilizaji walitakiwa kuwaonea huruma waathirika wa mmomonyoko wa udongo jambo ambalo walifanya bila ya kuyachukulia kuwa yamewakashifu kwa namna yote ile kama ambavyo matamko mengine yalivyochukuliwa. Kwa hiyo maratokezi ya hisia hizo ilikuwa 45 ambayo ni aslimia 14% kwa upande wa kuzinduka, 14 ambayo ni aslimia 4% ya hisia zinazoonyesha kuelimika, 77 ambayo ni aslimia 24% ya hisia zinazoonyesha kuzingatia, 30 ambayo ni aslimia 9% ya hisia za kuungama na 4 inayowakilishwa na aslimia 1% ya hisia za kuhuzunika. Jumla ya umara tokezi wa hisia hizo ni 170 na huwakilisha aslimia 52% ya athari chanya.

Kwa upande mwingine, kuaibika, kuudhika, kupuuza na kukanganyika ni athari hasi zilizojitokeza katika khutuba kwa mujibu wa uchunguzi uliofanyika. Umaratokezi wa hisia za kuaibika ilikuwa 12 ambayo ni aslimia 4%, kuudhika 123 ambayo ni aslimia 38%, kupuuza 16 ambayo ni aslimia 5% na kukanganyika mara 4 ambayo huwakilisha aslimia 1% tu ya vitendo neni vilivyoangaziwa. Kwa hiyo, jedwali hilo hutubainishia kwamba kulikuwa na athari chanya na hasi katika khutuba za Juma zilizochunguzwa na jumla ya umaratokezi wa hisia zenye mwelekeo hasi ni 155 ambayo huwakilisha aslimia 48%.

#### 4.3.2.1 Maoni ya Kijumla Kuhusu Vitendo Neni vya Khutuba Zinazowasilishwa:

MM1. *Imamu alitaja dhambi anayofanya mtu fulani kinagaubaga nikakasirika.. kilichonikarisha ni kumuaibisha mbele ya wenzake.*

Maoni hayo yanaonyesha kuwa Imamu alitaja jina la mtu aliyefanya dhambi jambo ambalo lilimgusa maamuma huyo. Kitendo hicho ni cha uchochezi kwa sababu kila mwanadamu anastahiki heshima hata kama ni mhalifu. Kusitiri aibu za mtu ni kitendo cha imani na waumini wanajua hilo. Kwa hiyo ingemtoshelezea Imamu kutaja ubaya wa kujitosa katika madhambi na adhabu inayomsubiri mwenye kufanya hivyo badala ya kumnyooshea mtu kidole. Ikiwa mtu huyo habadili mwenendo wake basi Imamu ana haki ya kumwiita na kumsihi ajitahadhari na maovu. Lakini kumuaibisha kunaweza kumfanya aendelee na ufedhuli.

MM2. *Nilikasirishwa na khutuba moja ambayo ilikuwa juu ya miraa. Nilikuwa nikiitumia miraa wakati huo nikafikiri kwamba Imamu amenihujumu*.

Maoni hayo huonyesha kuwa Maamuma huathirika na matamko ya Maimamu wao hasa pale ambapo mabaya wanayoyafanya hutajwa. Maamuma huyo alikasirika si kwa sababu hajui kosa lake bali kwa vile anaona hana uso mbele ya wenzake. Kama Imamu angemweka faragani akamnasihi pengine asingechukulia kitendo hicho vibaya kama alivyochukulia kile cha kutajwa hadharani na pengine angebadilisha tabia na kuacha kutumia miraa.

MM3. *Ijapokuwa zinagusia mambo tunayoyafanya yasiyofaa, lakini ni nzuri kwa sababu zinatuelimisha.*

Maoni hayo huonyesha kuwa kuna waumini ambao hutambua kuwa Imamu anatekeleza majukumu yake kwenye mimbari. Hata kama kuna mabaya wanayoyafanya, wanaelewa kuwa Imamu huyataja ili wapate kuyaacha na sio kwa lengo la kuwaaibisha.

MM4. *Baadhi ya Maimamu huwashambulia matajiri mara kwa mara katika khutuba zao. Imamu alitumia lugha inayowakasirisha watu. Badala ya kusema: Jamani toeni katika mali yenu fungu fulani ili kuwasaidia wasiojiweza, anawashambulia moja kwa moja na kuongeza maarifa yake badala ya kusoma kitabu kitukufu*.

Maoni hayo huonyesha kwamba matajiri hawakatai kutoa zaka au sadaka bali huchukizwa na lugha waitumiayo Maimamu wao. Lugha inayotumika ni ya kutoa vitisho kwamba wakati wowote wanaweza kukumbwa na ajali ya barabarani wakafa na kuiacha mali wanaojigamba nayo au kuwambia kwamba hawawezi kumfikia Qaaruun ambaye aliangamizwa na mali yake. Lugha kama hiyo hutumika katika khutuba zinazohusu uchangaji pesa misikitini ili kuwasaidia wasiojiweza na kugharamia shughuli mbalimbali zinazohitaji ufadhili. Maarifa yanayoongezewa ni vitisho hivyo na matamko mengine yatolewayo ambayo hayaelekei kuwafurahisha wasikilizaji. Ndiyo maana msailiwa huyo anawashauri Maimamu wajitosheleze na kuwahimiza matajiri kutoa sehemu ya mali yao ili kuwasaidia maskini kama hatua inayoweza kuondoa athari hasi.

MM5. *Imamu huuleta msikitini ugomvi ulioko nyumbani kwa watu. Khutuba za aina hiyo huwasilishwa katika miezi ya Mei na Juni ambapo kuna ufukara mwingi.*

Hisia hizo hudhihirisha kuwa katika majira aliyoyaelezea, maisha huwa magumu na njaa hushtadi. Katika nyakati hizo, mwanamume asiporudi na kitu nyumbani, watu wake watashinda

na njaa. Kutokana na hali hiyo, ugomvi unaweza kujitokeza na Imamu anaweza kutunga khutuba yake kuelezea ugumu wa maisha na kuwasihi wanaume kujali familia zao. Matamko kama hayo yakitolewa hufasiriwa na waumini wengine kama kuyaongea mambo ya nyumbani.

Hayo ni maoni ya kijumla. Umuhimu wake ni kwamba yanaonyesha jinsi Maamuma wanavyozichukulia khutuba kwa ujumla wake na kuathirika na matamko yanayotokana na khutuba za Ijumaa zinazowasilishwa katika misikiti mbalimbali nchini Uganda. Kuhusu khutuba zilizoshughulikiwa katika utafiti huu. Maoni yafuatayo yalitolewa:

#### 4.3.2.2 Maoni Yaliyotokana na Usaili Kuhusu kila Tamko Miongoni mwa Matamko ya Khutuba:

MM6. *Iyo iili imbulila indayi ta. Andibeeye nga naye iiramo khubanga naye umundu anyala waakhola insobi. Khukhwiirusamo aba waaluumbile buteleevu baashikhola.*

*Hiyo si njia bora ya kutoa mawaidha. Ingekuwa vyema kama angejiweka miongoni mwa wanaohusika kwa sababu naye ni mwanadamu na anaweza kukosea. Kujitoa huonyesha kuwa amewahujumu wale wanaotenda kitendo hicho moja kwa moja.*

MM7. *Naapilisiwile khuurya Weele khu byeengola khushibala shino. Naariisiwile khu makambila ka Allah ni buulamu bweesi khuli khuutsyamo….*

*Nimehimizwa kumcha Mungu katika mambo niyatendayo hapa duniani. Nimetishwa kutokana na maamrisho ya Allah na maisha tunayoyaendea.*

MM8. *Naakha khuulondelela bya Allah niyo mbe bulayi. Inaakha khukhwiikhalilawo nga'se ta.*

*Lazima nifuate maamrisho ya Allah ndiyo niishi vyema. Sipaswi kujiamulia.*

MM9. *Ikhutuba yandekheeye liikobi lye khuusasula. Ndi niikhuuba umwiirengefurengefu khuukhola bya Allah.*

*Khutuba imeniachia deni la kulipa. Lazima nijiandae kufanya yale ayaamrishao Allah.*

MM10. *Khuruliilisa shiibi. Andibaaprochingile bonyene abareeula khu lomo'yo mushifo she khuukireela mu bandu baakali waabaswaaza isaambo'yo.*

*Khuuruliilisa ni jambo baya. Ingekuwa vyema kama angewaendea faraghani peke yao akawaonya kuhusiana na jambo hilo badala ya kulileta hadharani na kuwaaibisha kwa namna hiyo.*

MM11. *The khutuba was relevant. It is one of the few khutubas that have kept me awake. It was a positive criticism to the institution over things which are true.*

*Khutuba ilikuwa faafu. Ni mojawapo ya khutuba chache ambazo zimenizindua. Ulikuwa uhakiki chanya ulioelekezwa kwa taasisi kuhusu mambo ambayo kweli yapo.*

Majibu ya wasailiwa yalidhihirisha kwamba waliathirika kwa namna kadhaa. Mifano hiyo ni baadhi ya matamko ya Maamuma ambayo yaliainishwa kama vitendo athari. Hivyo ni kwa sababu kwavyo, athari za vitendo neni hupambanuka.

Athari zilizojitokeza ni pamoja na kuzinduka, kuelimika, kuaibika, kuzingatia, kuungama, kupuuza, kuudhika, kuhuzunika na kukanganyika.

Hata hivyo, majibu ya Maimamu na Maamuma yalidhihirisha kwamba kulikuwa na ugumu katika kutambua nia ya Imamu. Kwa mfano, huku baadhi ya Maimamu wakisema kwamba matamko yao yalikusudia kuelimisha au kuzindua, baadhi ya wasailiwa walisema kuwa hayakukusudia isipokuwa kudharau au kutoa vitisho.

Hata hivyo, mtafti alichukulia hisia za Maamuma na maoni yao juu ya matamko ya khutuba za Ijumaa kama athari. Mifano mingine ni kama ifuatayo:

MM12. *Khutuba ya jana haikunifurahisha kwa sababu ilikuwa na mashambulizi dhidi ya watu wa madhehebu mengine ya Kiislamu. Anapofafanua jambo anajaribu kulipinda ili liafikiane na matakwa yake na msimamo wa baadhi ya wasikilizaji wake.*

Maoni hayo yalitolewa kutokana na tamko la Imamu kwamba “Kuna hadithi zilizoingizwa humu ndani hazina maana yoyote” na kwamba “Unaona radio inanguruma na watu wanazungumza vinavyotambulikana na visivyotambulikana”. Katika kitabu cha Imamu Annawawi wa madhehebu ya Kiislamu ya Asshaafi-iyyah, kuna hadithi kuhusu kusoma bismillahi kabla ya kusoma Suratul Fatiha. Swala lililojadiliwa ni je bismillahi inasomwa

waziwazi au kimoyomoyo? Kulingana na hadithi hiyo, mtume Muhammud (SAW) na sahaba hawakusoma bismillahi waziwazi bali waliisoma kimoyomoyo. Kwa vile mtume (SAW) ndiye anayepaswa kuigwa katika vitendo vya ibada, ndiyo maana maoni ya wanazuoni wengi yakawa kwamba bismillahi isomwe kimoyomoyo. Hao ndio walioshambuliwa na Imamu kwa tamko lake kwamba "Hazina maana yoyote" na "...wanazungumza yanayotambulikana na yasiyotambulikana. Maamuma huyo anaona kwamba Imamu alitoa ufafanuzi kuhusu hadithi hiyo kwa maana isiyokuwa sahihi muradi apate kuwashawishi wasikilizaji wake kuwapuuza Mashekhe wenzake. Ufafanuzi huo ni kauli *za* Imamu zisemazo kwamba "*Hadithi inayosema bismillahi ilipokelewa na nani..... tufuate la nani? Yule aliyepokea hadithi zama za khulafaa Rashiduna na Yule aliyepokea hadithi zama za mtume (SAW) tufuate la nani? Watu wa da'wa tuliopo si wasomi".*

Maoni hayo huonyesha kuwa katika safu za waumini kuna wale ambao wanayaelewa maswala ya dini na kwa hiyo huwezi kuwapotosha. Kama wangepewa fursa wangeweza kuwakosoa viongozi wao.

MM13. *Sikufurahishwa na kila tamko kutokana na jinsi alivyowasilisha hoja zake. Lugha ilikuwa inakera ... haikuwa ya kirafiki.*

Hisia za maamuma huyo huonyesha kwamba hutuba ya Imamu wake ilikuwa na matamko yenye athari chanya na hasi. Kusema kwamba hakufurahishwa na kila tamko kuna maana kwamba alifurahishwa na baadhi ya matamko na kuna mengine ambayo hayakumfurahisha. Kilichozua utata kulingana na maoni yake ni matamko yenye sifa zinazowakera wasikilizaji kwa sababu zimesheheni bezo na matusi. Mifano ya matamko hayo ni kauli ya Imamu kwamba "*Na hufuati njia za Muhammadi (SAW), wewe ni da'wa gani wewe.... Hizo zinaitwa da'wa za shetani*". Hisia hizo zinaashiria kwamba Imamu alitakiwa atumie busara na mantiki kupangilia hoja zake. Vile vile alitarajiwa kutumia lugha inayoteka fikra za wasikilizaji ili wakubali yale anayowambia.

MM14. *Nilikasirika kwa sababu Imamu alianza khutuba kwa kuwashambulia watu hasa kaimu Imamu. Asipoondolewa tutaukimbia msikiti. Aidha anawasilisha khutuba huku akipokea simu.*

Maamuma huyu alichukizwa na kauli za Imamu alizotoa mwanzoni mwa khutuba kama vile "*Lakini nyinyi.... nyinyi shingo zenu mmezifanya ngumu kama Wayahudi .... na nyinyi mnataka kuwa wakorofi kama Wayahudi? Mmechangia kushindwa kwangu kwa ajili ya viburi vyenu"*.
Maamuma huyu anamtarajia Imamu kuwa mfano bora wa kuigwa lakini kitendo cha kupokea simu ijapokuwa ni kiziada cha lugha huonyesha kwamba hajali hisia za wasikilizaji wake. Isitoshe jinsi khutuba inavyoanza huashiria jinsi itakavyomalizika. Wahenga walisema kitakachokuwa kibuyu hutambuliwa kutokana na mkonowe. Maoni ya maamuma ni kwamba si vyema kuwashambulia watu na ikiwa tabia hiyo itaendelea basi itakuwa bora kuukimbia msikiti huo.

MM15. *Khutuba hiyo ni ya kuwadharau watu wa aina mbalimbali. Imamu anawadharau wasomi na hadithi za mtume (SAW). Pia anajifaharisha mbele ya watu na kuonyesha kuwa yeye ndiye msomi.*

Maoni hayo yalitokana na kauli ya Imamu isemayo kwamba *watuulize wanazuoni.... watu wamebakia kusoma visirasira.*

Katika hadithi sahaba mmoja kwa jina la *Abihurairah* alisema kwamba "Nilisalia nyuma ya mtume (SAW), Abubakar (RA) na Umar (RA) lakini sikuwasikia wakisoma bismillahi waziwazi".

Hadithi hiyo ndiyo inayotolewa na wanazuoni wa Kiislamu kama ushahidi kwamba bismillahi inatakikana isomwe kimoyomoyo. Lakini katika khutuba Imamu aliirejelea kama *visirasira*. Neno siira hutumika kurejelea taaluma inayohusiana na historia ama maisha ya mtume Muhammad (SAW). Kuirejelea kama visirasira ni kuwadharau wasomi kwa maoni ya maamuma huyu. Zaidi ya hayo, kusema kwamba watuulize wanazuoni ni kuonyesha kwamba Imamu anajichukulia kuwa miongoni mwa maulama maarufu ambao ndio wanaopaswa kusikilizwa na kurejelewa katika kila jambo linalohusu maswala ya dini na kwa hiyo anajifaharisha huku akiwadunisha Mashekhe wengine. Khutuba inatakikana iwajenge waumini kiimani na ionyeshe kuwa watu wote ni sawa mbele ya sheria za Mwenyezi Mungu. Kudharau mafundisho ya mtume (SAW) ni sawa na kumdharau mtume mwenyewe jambo ambalo halifai. Kuawadharau wasomi ni sawa na kudharau mafundisho yao pia. Ni kutokana na maoni hayo ndiyo waumini wakalalamika juu ya matamko hayo ya Imamu wao.

MM16. *Mwisho wa khutuba haukuwa mzuri. Khatibu alidhihirisha ugomvi na matusi kwa baadhi ya Waislamu... Hayo husikitisha na hayafai kuwa katika khutuba kwa sababu huzusha fitina na mgongano kati ya Waislamu.*

Maoni hayo yalitolewa kutokana na matamko kama vile *hutaki watu waitikie amina....Shetani we! Na miaka minne mwanamke ... ananikoroga...muulize mtapata habari...kapigwa na nuclear sasa si headmistress tena ni mwalimu tu...*

Kuomba dua si jambo baya na kuombewa na Imamu huku ukiitikia kwa kusema amina pia si jambo baya. Hata hivyo, msimamo wa Imamu huyu ni kwamba Waislamu waombewe dua na afundishaye watu kujiombea dua huwa shetani aliyelaaniwa. Maamuma anaona kwamba kumwiita mwenzake shetani ni kumtusi na kutaja ugomvi ulioko kati ya wafuasi wake hadharani ni tendo linaloweza kuongeza ugomvi na kuwafarakanisha watu jambo ambalo halifai kabisa. Fauka ya hayo, Imamu ni mchungaji anatakiwa kuwa na moyo wa subira. Tabia ya mifugo ni kumsumbua mchungaji ijapokuwa anaipeleka malishoni kwa manufaa yao. Hafai kuchukua fimbo na kuwapiga ovyo kwa sababu akiwadhuru atakuja kujibu mashtaka na ikiwa ni yake basi yeye ndiye atakayepata hasara. Imamu ni mzazi anayetakikana kuwalea waumini kulingana na maadili ya Kiislamu. Watoto wanasumbua sana kiasi kwamba wakisha lishwa na kushiba huwachafulia wazazi nguo zao. Lakini mzazi hakati ile sehemu ya nguo iliyo chafuliwa na kuitupa wala hampigi mtoto ngumi na kumrushia mateke bali huwa na subira akijua kwamba huyo mtoto ataerevuka na kutenda mambo ya kiutuuzima. Kumlaani mfuasi wake na kuonyesha hadharani kuwa kuna madhara aliyomtendea ni kitendo kilichowachukiza wasikilizaji.

Hiyo ni mifano ya hisia za baadhi ya waumini wa Kiislamu kuhusu khutuba za Ijumaa. Kama ilivyobainika katika mifano hiyo, hisia hizo zimedhihirisha mwelekeo wa kutoridhika na baadhi ya matamko yaliyojitokeza katika khutuba. Katika mifano ifuatayo, hisia za Maamuma zilionyesha mwelekeo tofauti ambao ni kuridhika na matamko ya khutuba. Maoni ya Maamuma yanaonyesha kwamba waliathirika na matamko ya khutuba kwa taathira chanya. Pamoja na kwamba wanakubali kuwa matamko ya Maimamu wakati mwingine yalizungumzia mambo mabaya wanayoyatenda baadhi ya waumini, walidhihirisha hisia za kuridhika nayo. Hali hiyo inaashiria kwamba maamuma hawakatazi Maimamu wao kutaja mabaya wanayoyatenda, bali

mbinu ya kuwasilisha ujumbe ndiyo inayohitaji kubadilishwa ili kuzua athari chanya. Aidha, maoni hayo yanaonyesha kuwa mara nyingi Maimamu hutumia vitendo neni vya moja kwa moja. Vitendo neni vya namna hiyo, ndivyo vinavyozua kero miongoni mwa baadhi ya wasikilizaji wa khutuba kwa sababu wanaona kwamba wanalengwa na Maimamu na kuaibishwa mbele ya wenzao.

MM17. *Khutuba ilikuwa nzuri sana kilichonifurahisha ni kwa sababu iliwasilishwa kwa namna nzuri. Imamu alikuwa mwazi katika matamko yake na alitumia ushahidi kutoka katika Kur'an na mifano katika maisha halisi.*

Maoni hayo yanathibitisha hoja ya baadhi ya waumini kwamba uhasi wa matamko unaweza kuondolewa iwapo Imamu atatumia ushahidi kutoka kwa Kur'ani na hadithi kwa kila tamko analotoa. Khutuba ya Imamu huyu imependwa kwa sababu ya mambo manne: Uwasilishwaji mzuri, uwazi, matumizi ya ushahidi kutoka katika Kur'ani na utoaji wa mifano kutoka katika maisha halisi. Ikumbukwe kwamba NU pia inahitaji mzungumzaji kuwa mwazi na kuwa na ushahidi juu ya lile analozungumzia.

MM18. *Khutuba ilikuwa nzuri. Ilinizindua nikatambua kuwa kuna haja ya kurudi mbele ya Allah. Hata hivyo, watenda maovu hawajisikii vizuri. Wanalalamika na kuona kwamba Imamu anawaingilia.*

Maoni hayo yalitolewa kuhusu khutuba iliyowasilishwa juu ya tabia za vijana. Imamu alizungumzia swala la unywaji pombe miongoni mwa baadhi ya vijana wa Kiislamu na kueleza kwamba wanaonekana wakiyumbayumba barabarani na hata kwenye vilabu vya pombe hawakosekani. Kurudi mbele ya Mwenyezi Mungu ni kuacha matendo kama hayo yaliyokatazwa. Wito kama huo, kulingana na maoni hayo, umepokelewa vyema isipokuwa kwa wale ambao wanashiriki katika ulevi. Wao huuchukulia kama hujuma dhidi ya mwenendo wao ambao hawana shida nao.

Kwa hivyo utafiti huu ulionyesha kwamba waumini waliathirika kwa namna mbalimbali. Athari hizo zimedhihirika kulingana na jinsi walivyoyapokea matamko ya Imamu na kuyapa maana kadhaa. Mifano mingine ya taathira hizo ni kama ifuatavyo:-

**Kuzinduka**

Hii ni mojawapo ya athari zilizopatikana kutokana na matamko ya khutuba mbalimbali zilizowasilishwa. Kwa mfano, msailiwa mmoja alipoulizwa aliathirika vipi na tamko la Imamu lisemalo *"Kama tungekuwa wazingatifu msikiti huu ungejaa Ijumaa hii. Kwa sababu wenzetu walikufa kwa namna ambayo haikueleweka na Mwenyezi Mungu hakushauriana na mtu yeyote… hawakuwa na habari kwamba wangefariki siku hiyo",* alisema kwamba:

MM19. *Matamko hayo yamechangia sana katika kutuongezea imani na kutuzindua ili tujirekebishe.*

Imamu alikuwa akirejerelea maafa yaliyotokea Wilayani Bududa ambapo mmomonyoko wa udongo uliua zaidi ya watu mia tatu na kuwajeruhi wengine Kadhaa na wengine wengi wakaachwa bila makazi. Waathirika hawa walilazimika kuishi kambini kwa kutegemea msaada wa serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na watu binafsi hadi pale walipopatiwa maeneo mapya huko magharibi mwa Uganda.

**Kuelimika**

Athari nyingine iliyodhihirika ni kuelimika. Waumini walipoulizwa walipokeaje matamko ya Imamu kuhusu kuacha kuomba omba na badala yake wawe wakifanya kazi kwa bidii ili wale kutokana na jasho lao walisema:

MM21. *Tulielimika kuhusiana na kujifanyia kazi na kujitegemea*

Maoni hayo yalitokana na matamko ya Imamu yaliyojitokeza katika khutuba yakielezea kisa cha sahaba mmoja aliyemwendea Mtume (SAW) na kumwomba msaada ili apate kununua chakula. Mtume hakumpatia msaada huo. Badala yake, alimwamrisha kwenda nyumbani akamletee kisahani na shuka ambavyo vilikuwa milki yake pekee maishani mwake. Alipovileta Mtume akaviuza kwa njia ya mnada akapata dirhamu mbili (sarafu ya Uarabuni) na kumwamrisha aende akanunue shoka amletee. Yule bwana alipomletea shoka, Mtume (SAW) alimsaidia kumwekea mpini kisha akamwamuru kwenda msituni akapasue kuni na kuziuza kisha arejee kwake baada ya siku kumi na tano. Sahaba huyo alidiriki kurudi kwa Mtume akiwa amepata dirhamu kumi na tano. Akamshukuru kwa ushauri wake uliomwezesha kupata kazi itakayomwezesha kujikimu maishani. Mtume akatumia nafasi hiyo kuwahimiza sahaba zake na Waislamu kwa ujumla

kujitegemea kwa kufanya kazi japo ya kuchanja kuni badala ya kuombaomba jambo ambalo linaweza kumwondolea mtu heshima yake.

Kutoa mifano kutoka katika maisha halisi huchangia sana katika kufikisha ujumbe kwa namna ipasayo. Maoni yaliyotolewa na waumini waliokuwa wakisikiliza khutuba huthibitisha hoja hiyo. Hivyo ni kwa sababu mifano kama hiyo husawiri maisha ya mwanadamu na kumwekea mbele yake picha ya kiumbe anayeishi kwa raha mstarehe akachuma mali, akawekeza katika miradi mbalimbali, akajenga nyumba na kununua magari ya kifahari, akaendeleza ukoo wake kwa kuoa, kuzaa watoto na kuwapatia elimu nzuri. Halafu, ghafla, akiwa katika mghafala kwamba mambo yataendelea vivyo hivyo, akakumbwa na mkasa ambao unamharibia maisha yake na kuondoa raha na starehe. Mkasa huo huchukua sura mbalimbali, kama vile mmomonyoko wa udongo uliotajwa katika khutuba, magonjwa hatari, umaskini na mambo mengineyo.

**Kuudhika**

Baadhi ya waumini walionyesha hisia za kuudhika, ikawa ni mojawapo ya athari zilizotokana na vitendo neni vya khutuba. Kwa mfano, msailiwa mmoja alinukuliwa akisema:

MM22. *Naudhika kwa sababu yeye ni mpiga ramli lakini hataki mawaidha yoyote ambayo yanaelekea kupinga kitendo chake hicho. Ndio maana anayarejelea kama vurugu.*

Waislamu wanashauriwa kuwa wasomi au wanafunzi au wasikilizaji wa mihadhara ama vipindi vya kielimu ili wapate kujifunza mengi kuhusu maisha yao. Kwa wale ambao wanaenda misikitini na kusikiliza mawaidha, au wale wanaopata mafunzo kupitia vipindi mbalimbali vya kidini vinavyorushwa kwenye redio na pia wale ambao wamebahatika kujifunza dini katika vyuo mbalimbali bila shaka watapata wasiwasi ikiwa matendo ya Imamu yataenda kinyume na mafundisho ya dini. Zamani watu waliosoma dini walikuwa waking’ang’ania sana upigaji ramli. Walikuwa na msemo kwamba Imamu hulia kwenye mkeka kwa maana kwamba hapati usumbufu wa kutafuta riziki bali hukaa tu nyumbani kwake na kuletewa riziki. Hata hivyo, kitendo hicho hukiuka mafundisho ya Uislamu kwa sababu wapiga ramli hudai kujua yaliyoko ugaibuni hali ya kuwa ajuaye yaliyofichamana ni Mwenyezi Mungu pekee. Kulingana na hadithi ya mtume (SAW) yeyote amwendeaye kahini au mpiga ramli akasadikisha anayomwambia sala zake za siku arobaini hazitakabaliwi na Mwenyezi Mungu. Waislamu hawafurahikii kuambiwa

kwamba wanaleta vurugu kwa sababu wanaona kwamba wana haki ya kuonyesha kutoridhika kwao kutokana na kuongozwa na mpiga ramli. Isitoshe wao wanaona kwamba Imamu anajua ukweli lakini kutokana na maslahi ya kibinafsi huuficha na kujificha nyuma ya ukali.

**Kuaibika**

Maoni ya baadhi ya waumini yalidhirisha athari za kuaibika Imamu alipong'amua kwamba kuna wanaokunywa pombe.

MM23. *Imamu ametuaibisha bwana. Ingefaa atuweke faraghani badala ya kutaja hayo mambo hadharani.*

**Kuzingatia**

Hisia nyingine zilidhihirisha hali ya kuzingatia matamko ya Maimamu kama inavyodhihirika katika kitendo athari kifuatacho:

MM24. *Tumezingatia onyo la Imamu kuhusu utiifu kwa Mwenyezi Mungu na kuacha njia ya shetani.*

**Kuungama**

Vitendo athari vingine vilidhihirisha hali ya kuungama miongoni mwa wasikilizaji kama inavyobainika katika mfano ufuatao:

MM25. *Bila shaka Mwenyezi Mungu ndiye anayepaswa kuabudiwa.*

**Kupuuza**

Hisia zinazoonyesha kupuuzwa kwa matamko ya Maimamu zilijitokeza pia katika utafiti huu. Mfano wa hisia hizo ni kama ifuatavyo:

MM26. *Na aseme ayasemayo. Sisi hatutoacha mila yetu. Watoto wetu tutaendelea kuwatahiri kama tulivyotahiriwa.*

### 4.3.3 Kiasi cha Athari kwa Mkabala wa Aina za Vitendo Neni

Kulingana na utafiti huu aina za vitendo neni vilivyojitokeza katika khutuba za Ijumaa ni nne. Aina hizo ni viwakilishi, vielekezi, vitathminishi na vilazimishi. Ingawa vitendo neni hivyo kwa aina hizo viliwaathiri wazungumzaji, vitathminishi ndivyo vilikuwa na athari hasi nyingi. Hii ni

kwa sababu aina hiyo huonyesha mwelekeo wa mzungumzaji juu ya kitendo kilichotokea. Kwa hiyo wasikilizaji waliudhika walipotambua kuwa Imamu ana mwelekeo wa kuwadharau na kuwakejeli watu. Aidha vitendo neni hivyo vinaweza kutumika pasina kuambatanishwa na ushahidi unaonyesha msimamo wa dini kuhusu jambo linalozungumziwa. Ushahidi ukikosekana, tamko hilo litanasabishwa moja kwa moja na mzungumzaji ambaye hana kinga kama ambavyo yangenasabishwa kwa Mwenyezi Mungu au Mtume wake au Maulama wanaotegemewa kama makhalifa wa Mtume na Maimamu wa madhehebu manne ya Kiislamu.

Vitendo neni vielekezi ni aina nyingine iliyochangia athari hasi. Hivyo ni kwa sababu kulingana na tabia yake vinamwezesha mzungunzaji kuelezea hamu yake kuhusu kitendo mahasusi kwa hiyo vitendo neni kama kukataza, kuamrisha, kuonya na kukanya ndivyo vinavyotumika kurejelea mambo ambayo yanafaa kutendwa au kuachwa. Tatizo hapa ni kwamba kuna vitendo ambavyo waumini wanakatazwa au kuamrishwa kuvifanya lakini kwa vile vimekita mizizi katika utamaduni wao au hawaoni umuhimu wa kuvitenda ama kuviacha wakaona kwamba kutajwa kwake ni njama ya kushambulia ada na itikadi zao. Mfano, ni kukatazwa kwa waumini wenye asili ya Kigisu kushiriki katika miviga ya tohara, kitendo ambacho baadhi yao wanaona kwamba ni cha kuupiga vita utamadumi wao na kupuuza maadili ya jamii yao. Vitendo neni pia vilizua athari hasi kwa sababu Maamuma waliona kwamba baadhi ya Maimamu wao si mfano bora wa kuigwa. Wao wenyewe au watu wa familia zao hawashikamani na mafunzo ya dini na hivyo basi waumini hukerwa na kukanganyika na matamko yao yanayowaelekeza juu ya wanayopaswa kufanya na kuacha. Zaidi ya hayo, ushahidi kutoka katika Kur’ani na Hadithi unaopaswa kuambatanishwa na matamko hayo hutolewa kwa nadra sana. Isitoshe viziada vya lugha ambavyo maimamu huvitumia kama vile toni, viungo vya mwili na matumizi ya vioneshi kama *wewe, na nyinyi* huyapa matamko hayo nguvu zinazozua taathira hasi kwa waumini. Hivyo ni kwa sababu wao hujichukulia kuwa hawawezi kukosea, wanaokosea ni Maamuma.

Vitendo neni viwakilishi vilikuwa na uhasi mdogo ikilinganishwa na aina mbili zilizotajwa hapo juu. Uhasi wake ulitokea kwa sababu ya kushikilia imani kwamba yaliyotajwa katika urejeleo wa yaliyomo katika khutuba ni sahihi wakati watu wameshachukizwa na baadhi yake.

### 4.4 Matumizi ya Vitendo Neni Vinavyopendelewa Zaidi

Nadharia tete ya mwisho ya utafiti huu ilikisia kuwepo kwa uwezekano kwamba vitendo neni vinavyopendelewa na Maamuma zaidi vinaweza kutumika na Maimamu ili kuleta athari chanya. Maoni yafuatayo yalienda sambamba na nadharia tete hiyo:

MM27. *"Luulimi lubeeye luulai lwe huimploaringa ela buli iisi akanikhiiye khu adhabu, asabile idua ikhushiingilisa ni iisi asomeeye khu shilayi asabile Weele ashikhuwe".*

*"Lugha ilikuwa nzuri, ya kuhimiza na kila alipozungumza juu ya adhabu, aliomba dua ya kutukinga na alipotaja mambo mazuri, alimwomba Mwenyezi Mungu atuwezeshe kuyapata".*

MM28. *"Baimaamu baalala ibamatiza bulayi ta. Ibaelaboretinga bulayi ta. Bauliilisi balakha khumutegeela ta".*

*"Maimamu wengine hawaridhishi. Hawafafanui vizuri. Kwa hiyo wasikilizaji hawawaelewi".*

MM29. *"Baimamu baraambise luulimi luuolu. Nga wamubooleeye shishindu umulekhele akhaleo. Shekhuubonelakho, khuusadaaka. Umusomele buulayi ni buubi buushilimo niye umweene abone sheekhuukhalao".*

*"Maimamu wanapaswa kutumia lugha ya upole. Iwapo amemwambia msikilizaji jambo lolote, ni vyema amwache aamue la kufanya. Kwa mfano: Anapofundisha juu ya kutoa sadaka, amwambie faida za kuitoa na hasara zinazotokana na kuiacha ili mwenyewe aone cha kufanya".*

MM30. *"Imamu umutendeke waaka kuusoma ikhutuba iisi umanya uti baatu iza kubahambako. Uli ni kuuleeta information iili related naabi ku mbeela… Imamu biiteeketeeke. Umanye message kyiina iisi uza kubawa".*

*"Imamu hodari unapaswa kuwasilisha khutuba ambayo unajua kwamba itawagusa watu. Unapaswa kutoa taarifa inayohusiana na hali … Maimamu wanatakikana kujiandaa. Ujue ni ujumbe gani unaowapa".*

MM31. *"Watenda maasi wasitajwe katika khutuba. Imamu atumie mbinu nzuri inayowafanya watambue lengo lake"*.

Maoni hayo hudhihirisha kuwa wasailiwa walionyesha mwelekeo wa kupendelea zaidi matumizi ya vitendo neni ambavyo kwa kawaida huibua athari chanya. Lugha yenye sifa za uwazi, upole, na ufaafu ndiyo inayopendekezwa kutumika katika khutuba kulingana na maoni hayo. Imamu anapaswa kuweka ujumbe wake wazi ili aeleweke vyema. Aidha, ujumbe unatakikana kuwasilishwa kwa upole ama unyenyekevu kiasi cha kuwafanya waumini wavutiwe nao. Halika dhalika, matamko ya khutuba lazima yapangwe sawa sawa na yajadilie mambo yanayofaa kwa kiasi kinachofaa. Maoni hayo yamerandana na Nadharia ya Udokezi ambayo inasisitiza kuwa mzungumzaji anapaswa kutilia maanani kaida za kiasi, ubora, jinsi na ufaafu.

Jedwali lifuatalo limetoa muhtasari wa vitendo neni vya khutuba na jinsi waumini walivyoathirika:

**Jedwali 6: Vitendo Neni vya Khutuba za Ijumaa na Athari zake kwa Waumini**

| No. | VWC | VWH | VEC | VEH | VTC | VTH | VLC | VLH | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 01 | 04 | 03 | 10 | 01 | - | - | 01 | - | **19** |
| 02 | 02 | 02 | 10 | 01 | 01 | 10 | 01 | - | **27** |
| 03 | - | - | - | 01 | - | 20 | 01 | - | **22** |
| 04 | - | - | 03 | 01 | - | 10 | 01 | - | **15** |
| 05 | - | 01 | - | 03 | - | 16 | 01 | - | **21** |
| 06 | - | - | 02 | 04 | - | 01 | 01 | - | **08** |
| 07 | 03 | - | 10 | 03 | 03 | 03 | 01 | - | **23** |
| 08 | - | - | 06 | - | - | 03 | 01 | - | **10** |
| 09 | - | - | 14 | 01 | 05 | 01 | 01 | - | **22** |
| 10 | 02 | - | 08 | - | - | - | 01 | - | **11** |
| 11 | 01 | - | 09 | 05 | - | 07 | 01 | - | **23** |
| 12 | - | - | 16 | - | - | - | 01 | - | **17** |
| 13 | - | 01 | 07 | 02 | - | - | 01 | - | **11** |
| 14 | - | 02 | 02 | 05 | - | 04 | 01 | - | **14** |
| 15 | 01 | - | 02 | 06 | - | 02 | 01 | - | **12** |
| 16 | - | - | 05 | 02 | - | 08 | 01 | - | **16** |
| 17 | - | 01 | 07 | 03 | - | - | 01 | - | **12** |
| 18 | - | - | 05 | 03 | - | - | 01 | - | **09** |
| 19 | - | 03 | 09 | 01 | - | 01 | 01 | - | **15** |
| 20 | - | - | 03 | 03 | - | 11 | 01 | - | **18** |
| **Jumla** | **13** | **13** | **128** | **45** | **09** | **97** | **20** | | **325** |
| **Aslimia** | **4%** | **4%** | **39%** | **14%** | **3%** | **30%** | **6%** | | **100%** |

Jedwali 6, tofauti na majedwali yaliyotangulia katika sura hii, limepiga hatua mbele zaidi kwa kudhihirisha vitendo neni vilivyojitokeza katika khutuba pamoja na viwango vyake vyote – hasi (H) na chanya (C). Limeonyesha matumizi ya lugha katika khutuba kwa ihtisari na ukamilifu, na sifa zinazoibua athari chanya au hasi zaidi. Ugunduzi huo ndio ulimwongoza mtafiti kwanza kudhihirisha vitendo neni vilivyokita katika khutuba na athari zake kwa waumini na pili, kupendekeza matumizi ya vitendo neni vyenye sifa zinazopendelewa zaidi na waumini. Aina za vitendo neni vilivyojitokeza katika khutuba kulingana na jedwali hilo ni viwakilishi, vielekezi, vitathminishi na vilazimishi. Aina hizo zote  isipokuwa moja yaani vilazimishi, ziliangukia pande mbili. Upande wa uhasi na ule wa uchanya.

Jumla ya vitendo neni viwakilishi ilikuwa 26 ambayo ni aslimia 8%. Viwakilishi viligawana idadi hiyo nusu kwa nusu ambapo vyenye athari chanya na hasi, kila mojawapo iliwakilishwa na aslimia 4%.  Vielekezi vilikuwa 173, yaani aslimia 53% ya jumla ya vitendo neni. Uchanya ulikuwa mwingi katika aina hii kwani uliongoza kwa mara 128 ambayo ni aslimia 39% huku uhasi ukiwakilishwa na 45 ambayo ni aslimia 14%.

Ukija kwa upande wa vitendo neni vitathminishi, ilidhihirika kuwa kati ya vitendo neni 106 vya aina hii, uchanya ulisalia nyuma kwa mara 9 ambayo ni aslimia 3% huku uhasi ukiongoza kwa mara 97 inayowakilisha aslimia 30%. Aidha , jedwali hilo limedhihirisha kuwa vitendo neni vilivyo mwisho kwa upande wa idadi ya maratokezi ni vilazimishi. Isitoshe, imedhihirika pia kuwa aina hii imeangukia upande mmoja tu ambao ni wa athari chanya pekee. Vitendo neni hivyo vilikuwa 20 ambayo ni aslimia 6% ya jumla ya vitendo neni vilivyojitokeza katika khutuba.

Jambo ambalo ni muhimu zaidi kulingana na jedwali hilo ni kwamba ukiangalia upande wa uchanya  vielekezi ndivyo viliongoza katika umaratokezi huku vitathminishi vikiongoza kwa upande wa uhasi katika umaratokezi. Lakini vitendo neni viwakilishi viliangukia kati katika kuzua athari chanya na hasi kwa kiwango sawa. Kwa hiyo ugunduzi huo ulimpelekea mtafiti kupendekeza ni vitendo neni vya aina gani vitumike zaidi  na ni vipi vipunguzwe kimatumizi ili kuboresha uwasilishaji wa khutuba.

**4.5 Matokeo ya Utafiti**

Utafiti huu umedhirisha kuwa kuna vitendo neni maalum katika khutuba za Ijumaa. Jumla ya vitendo neni vilivyojitokeza katika khutuba zilizochanganuliwa ilikuwa 325. Ulidhihirisha pia sifa za vitendo neni hivyo kwa kutumia nadharia ya vitendo neni, mkabala wa Searle. Sifa hizo ni matumizi ya vielekezi, viwakilishi, vitathminishi, vilazimishi na pia matumizi ya vitendo neni viso dhahiri.

Utafiti ulidhihirisha kuwa baadhi ya vitendo neni vilivyojitokeza havikukuwa dhahiri. Kwa hiyo Maimamu walipendelea kuwasilisha ujumbe kwa njia iso kuwa ya moja kwa moja. Hata hivyo, kwa vile Maamuma walikuwa na umilisi wa kimawasiliano, waliweza kutambua nia za Maimamu kulingana na miktadha mbalimbali ambamo matamko hayo yalijitokeza. Utambuzi wa nia hizo ndio uliowapelekea kuathirika kwa namna mbalimbali kama ilivyobainika katika mifano ya matamko yaliyojitokeza katika khutuba mbalimbali.

Aidha utafiti ulibainisha athari za vitendo neni hivyo kwa aina zake nne zilizojitokeza katika khutuba. Waumini wa Kiislamu waliokuwa wakisikiliza khutuba zilizochunguzwa waliathirika kwa kuzinduka, kuelimika, kuzingatia, kuungama, kuhuzunika, kuaibika, kupuuza, kuudhika na kukanganyika. Athari hizo zilikuwa chanya na hasi. Athari hasi ziliwakilishwa na asilimia 48%.

Mtafiti aligundua kwamba ingawa vitendo neni vielekezi na viwakilishi vilikuwa na athari hasi, vitathminishi ndivyo vilivyokuwa na uhasi mwingi. Kwa hiyo matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwamba khutuba za Ijumaa zimesheheni vitendo neni vyenye athari hasi na chanya. Vilazimishi havikuzua athari hasi hata kidogo.

Hali ya kufaa na kutofaa kwa tamko ama ufelisiti ilichunguzwa pia. Matamko yaliyojitokeza katika khutuba zilizochunguzwa yalidhihirisha kuwa baadhi yake yalitimiza masharti ya ufelisiti huku mengine yakikiuka masharti hayo. Hali hiyo ilichangia katika kuzua athari mbalimbali kama ilivyobainishwa katika uchambuzi.

Vivyo hivyo, vitendo neni vya khutuba vilionyesha hali ya kukiukwa kwa kanuni shirikishi zilizomo katika Nadharia ya Udokezi. Halikadhalika, kanuni za unyenyekevu zilikiukwa na

baadhi ya Maimamu. Ukiukaji wa sheria na kanuni hizo ulidhihirisha maana ambazo zilivishwa matamko yaliyokuwa yakiwasilishwa.

Vilevile, imebainika kwamba, utamaduni na mienendo ya baadhi ya waumini wa Kiislamu huchangia sana katika kuzua athari hasi. Hivyo ni kwa sababu baadhi ya athari hizo zilitokana na matamko yaliyogusia mila na matendo wanayotenda. Kwa hiyo utafiti huu umegundua kuwa mara nyingi athari hasi hutegemea mada zinazowasilishwa katika khutuba. Pale ambapo khatibu anazungumzia mada zisizompiku msikilizaji, athari huwa chanya. Kwa mfano tohara miongoni mwa Wagisu huenziwa sana jinsi ambavyo dini inavyoenziwa miongoni mwa wafuasi wake. Kwa hiyo washangiliaji wa ada hiyo, hawapendezwi na matamko yanayosaili jinsi inavyotekelezwa. Aidha, maswala mengine ya utamaduni kama vile ndoa, kifo na mazishi yakigusiwa kwa mtazamo wa Kiislamu, huzua malalamishi. Swala la mienendo kama vile unywaji pombe, matumizi ya madawa ya kulevya, uchezaji kamari, uzinifu na kadhalika, huzua ugomvi pia baina ya Maimamu na Maamuma wao.

Kwa upande mwingine, kiwango cha elimu walichofikia baadhi ya Maimamu huwapelekea kutoa matamko yanayochochea malalamishi dhidi yao. Elimu duni huwafanya wawasilishe khutuba kama wanavyotaka na wasijali hisia za wasikilizaji wao. Aidha elimu ndogo haimwezeshi Imamu kuyatafsiri mafundisho ya dini kwa namna nzuri na kutumia mbinu mwafaka katika mahubiri yake.

Utafiti huu umedhihirisha pia kuwa vitendo neni ambavyo kama vingetumika nje ya muktadha wa khutuba visingewapelekea wasikilizaji kukereka ndivyo vimezua uhasama. Hivyo ni kwa sababu khutuba huhudhuriwa na kusikilizwa na umati mkubwa wa watu ambao wanajua tabia za wenzao. Kwa hiyo, Imamu anapozungumza juu ya tabia au kitendo fulani, yule anayehusika atachukulia kuwa amekusudiwa kuaibishwa. Isitoshe, katika muktadha wa kawaida, mtu huenda asichukulie jambo kwa uzito wake linalostahili. Lakini katika muktadha wa khutuba, toni ya Imamu na viziada lugha vingine kama vile uradidi, mkazo na mkao wa uso huonyesha anamaanisha yale ayanenayo wala hamtanii mtu yeyote.

### 4.6. Hitimisho

Sura hii imeshughulikia data ya utafiti ambayo ni khutuba za Ijumaa na maoni ya waumini kuhusu khutuba hizo. Data hiyo imewasilishwa na kuchanganuliwa kwa mujibu wa Nadharia ya Vitendo neni na Nadharia ya Udokezi. Vitendo neni vilivyojitokeza katika khutuba hizo, athari zake kwa waumini wa Kiislamu na sifa zinazozua uhasi katika khutuba na zile ambazo hupendelewa zaidi na Waumini zimebainishwa. Vitendo neni viwakilishi vilijitokeza kwa aslimia 8%, vielekezi kwa aslimia 53%, vitathminishi kwa aslimia 33% na vilazimishi kwa aslimia 6%. Aidha, utafiti huu ulidhihirisha kuwa vitendo neni hivyo vilikuwa na athari hasi ambazo zilijitokeza kwa aslimia 48%. Utafiti ulidhihirisha pia kuwa Maamuma hupendelea matumizi ya vitendo neni vilazimishi kwa sababu havikuzua athari hasi hata kidogo na vitendo neni vielekezi kwa sababu uhasi wake ulijitokeza kwa kiwango kidogo sana. Vitendo neni vilivyopendelewa kwa kiwango kidogo ni viwakilishi lakini vitathminishi havikupendelewa kwani vilizua uhasi mwingi sana.

Katika sura ya tano muhtasari na hitimisho la Utafiti limetolewa kwa misingi ya madhumuni na maswali ya utafiti. Vivyo hivyo, mapendekezo kuhusu lugha inayopendelewa zaidi katika khutuba ambayo uzingatifu wake unaweza kuchangia katika kulipatia swala utafiti huu suluhisho la kudumu yametolewa. Halikadhalika, maeneo yanayotakikana kufanyiwa uchunguzi na watafiti wengine ili kuchangia zaidi taaluma ya Uchanganuzi Usemi yalipendekezwa na mtafiti.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii imetoa muhtasari wa matokeo ya utafiti huu, hitimisho lake kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti na matlaba yake na mapendekezo ya jinsi khutuba za Ijumaa zinavyoweza kuboreshwa. Hatimaye maeneo mengine yanayotakikana kushughulikiwa katika tafiti za baadaye, yamependekezwa.

## 5.2 Muhtasari

Mada ya utafiti huu ni kwamba ingawa khutuba za Ijumaa zina maadili ya kijamii ambayo yangewafaidi waumini wa Kiislamu, kumekuweko na madai miongoni mwa Waislamu kwamba maadili hayo hupitishwa kwa lugha yenye taathira hasi. Hata hivyo, sifa za lugha hiyo ambazo zilikuwa zikizua malalamishi na athari zake kwa waumini hazikuwa zikijulikana wala kubainishwa na tafiti za hapo awali.

Kutokana na tatizo hilo, madhumuni yaliyoangaziwa yalikuwa kubainisha vitendo neni katika lugha ya khutuba za Ijumaa, kudhihirisha athari za vitendo neni hivyo kwa Waislamu wanaosikiza khutuba hizo na kupendekeza matumizi ya lugha yanayodhihirika kupendelewa zaidi na waumini katika khutuba. Utafiti huu umebainisha vitendo neni vya khutuba za Ijumaa kulingana na madhumuni hayo na maswali ya utafiti. Aidha umebainisha athari za vitendo neni hivyo kwa wasikilizaji wa khutuba na kupendekeza namna ambavyo Maimamu wanavyoweza kutumia sifa zinazopendelewa zaidi na Maamuna ili kuboresha uwasilishaji wa maadili ya kijamii na kidini kupitia khutuba za Ijumaa.

Ili kufanikisha kazi hii, Nadharia ya Kitendo Neni ilitumika sambamba na Nadharia ya Udokezi kama mwongozo. Data iliyokusanywa ilikuwa vitendo neni vilivyojitokeza katika khutuba za Ijumaa na hisia za wasikilizaji kuhusu khutuba hizo. Vitendo neni na hisia za waumini zilipatikana kupitia unasaji wa khutuba kwa vinasa sauti na unukuzi wa maalumati na viziada vya lugha katika madaftari. Baadaye mtafiti aliwahoji wasailiwa wake kuhusu vitendo neni hivyo na athari zake, kisha akachanganua data ili kufikia utatuzi wa tatizo la utafiti wake.

Utafiti ulionyesha kuwa kuna mchakato wa kutafsiri matini ya Kiarabu kwa lugha za kienyeji miongoni mwa baadhi ya Maamuma. Aidha, kuna Maimamu ambao husoma matini ya Kiarabu yaliyoandikwa kwenye kitabu au daftari au kijikaratasi na kuitafsiri papo hapo kwa lugha za kienyeji au Kiswahili na Kiingereza.

Uchunguzi huu ulionyesha pia kuwa Maimamu wengi hawapati mafunzo juu ya khutuba na tafsiri jambo ambalo huchangia kuzua athari hasi miongoni mwa wasikilizaji. Vivyo hivyo, Maimamu wengi hawafanyi matayarisho ya awali ambayo yangewasaidia katika kuboresha khutuba zao. Ukosefu wa mafunzo juu ya uwasilishjaji wa khutuba na hali ya kutofanya matayarisho ya awali vimeleta shida nyingine ambayo ni kushindwa kuelezea aya za Kur'ani na Hadithi kulingana na muktadha faafu.

Aidha, ulionyesha kuwa katika khutuba, lugha ilitumika kuelezea hisia na mielekeo ya Maimamu ili kuathiri mielekeo na tabia za wasikilizaji. Kazi hii ilidhihirisha kuwa lugha ya khutuba za Ijumaa ina vitendo neni ambavyo vina athari hasi na chanya. Walioathirika na vitendo neni hivyo ni waumini wa Kiislamu wanaosikiliza khutuba hizo wanaume kwa wanawake.

Halikadhalika, ulidhihirisha kuwa khutuba moja inaweza kuzua mitazamo tofauti na kwamba maana ya matamko yatolewayo na Imamu hutambuliwa na wasikilizaji kwa namna mbalimbali. Ndiyo maana huku baadhi ya waumini wakisema kwamba khutuba fulani ilikuwa na athari chanya, wengine waliona kuwa khutuba hiyo hiyo ilizua athari hasi. Hivyo ni kwa sababu Maimamu mara nyingi walikiuka kanunu shirikishi na kuwasilisha ujumbe kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja.

Matokeo ya kazi hii yalionyesha pia kwamba baadhi ya khutuba hazina athari kubwa kwa wasikilizaji kwa sababu mbinu zinazotumika hazifai na mada zinazoteuliwa hazilingani na maswala yanayoikabili jamii katika maisha ya kila siku. Kutokana na kasoro hiyo, baadhi ya waumini husinzia tu khutuba zinapowasilishwa. Fauka ya hayo, ilibainika kuwa kulikuwa na Maimamu wenye msimamo mkali na wale ambao kimaumbile wanaongea kwa namna ambayo huzua kero kwa wasikilizaji.

Kazi hii pia iligundua kuwa hakuna mamlaka inayotoa mwongozo wala kufuatilia khutuba na uwasilishaji wake ili kuzuia athari hasi kwa waumini na kuwashauri Maimamu kuhusu jinsi wanavyoweza kuzifanya khutuba zao zipendeze. Maoni ya wasailiwa yalidhihirisha kuwa katika misikiti ya vijijini na hata baadhi ya misikiti ya mijini, Imamu hazungumzi juu ya mada moja katika khutuba yake bali hugusiagusia maswala mengi kiasi kwamba hapati muda wa kuyaelezea ipasavyo. Kurandaranda huku na urefushaji wa khutuba huwafanya wasikilizaji wasifuatilie ujumbe kwa makini na baadhi yao kusinzia. Kwa upande mwengine Maimamu wengi wa mijini hutunga khutuba zao juu ya mada moja jambo ambalo hupelekea khutuba zao kupendwa. Aidha wanafupisha khutuba hata kama athari hasi hazikosekani.

Zaidi ya hayo ilibainika kuwa Maimamu wengi hawatilii maanani sheria ya unyenyekevu. Mara nyingi wasikilizaji husawiriwa kama wapinga maadili ama watu wasiotaka kubadili mienendo yao. Maimamu wa namna hiyo hutoa matamko yao kwa lugha inayoonyesha kuwa ujumbe unaotolewa hauwahusu bali wanaohusika ni wasikilizaji tu. Hata kama Maamuma wamefanya bidii na kujaribu kutekeleza baadhi ya mafundisho, Maimamu hawaonyeshi dalili ya kuridhika ili kuwapa motisha wapate kutenda mazuri zaidi. Maimamu wengine walionyesha hali ya ukiukaji wa masharti ya ufelisiti na kaida za uzungumzi. Ukiukaji huo pia ulichangia sana kuathirika kwa Maamuma jinsi walivyoathirika.

Wa aidha, kazi hii imedhihirisha kwamba Kiarabu huchukuliwa na waumini wa Kiislamu kama lugha ya dini yao kwa sababu Kur'ani na Hadithi vimeandikwa katika lugha hiyo. Kwa hiyo, Waislamu hupendelea sana unukuzi wa maandiko hayo ufanywe kwa Kiarabu halafu tafsiri yake itolewe kwa lugha zinazoeleweka na wasikilizaji. Upendeleo huo huonyesha kuwa waumini wa Kiislamu wana hamu ya kuhakikisha kuwa ujumbe unaotolewa katika khutuba hautokani na utashi wa Maimamu wao bali ni mwongozo kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Katika miskiti ya mijini Maamuma hupendelea uchanganyi ndimi ambapo Kiarabu, Kiswahili, Luganda, na Kiingereza inatakikana zitumike. Hivyo ni kwa sababu, mnasaliwa watu kutoka katika makabila tofauti na hata katika nchi za kigeni. Kwa upande wa miskiti ya vijijini, Kiarabu na mojawapo ya lugha za kimkoa kama vile Luganda na Kigisu hupendelewa zaidi.

Iligundulika vilevile kwamba baadhi ya Maimamu wa vijijini hutumia vitabu vya khutuba ambavyo viliandikwa zamani na ambavyo baadhi ya mada zake si mwafaka kwa hadhira iliyopo, mahali au mazingira na wakati uliopo na kwa hiyo huzua athari hasi.

Hayo yote yamedhihirika kwa mwongozo wa NKN ambayo imemwezesha mtafiti kuchunguza utendakazi wa khutuba za Ijumaa. NKN imechangia sana utafiti huu kwa kudhihirisha vitendo neni vya khutuba za Ijumaa ambavyo vimejitokeza kama vielekezi, viwakilishi, vilazimishi na vitathminishi. Aidha imemwezesha kubainisha athari mbalimbali za vitendo neni. Kwa upande mwingine, NU ilimwezesha mtafiti kupata ufasiri wa matamko kadhaa ya khutuba kupitia kanuni zake shirikishi. Ufasiri huo ulimpelekea kutambua aina ya vitendo neni vilivyojitokeza katika khutuba zilizoshughulikiwa na jinsi wasikilizaji walivyoathirika navyo. Nadharia zote mbili zimedhihirisha uwezo mkubwa wa kuchambua usemi wa kidini uliokitwa katika matamshi ili kuweka bayana maswala ya kiisimu yanayojitokeza katika muktadha wa msikitini.

Kabla ya kufikia matokeo na mahitimisho ya uchunguzi, ilibidi data ya utafiti huu ichanganuliwe. Data hiyo ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo na wingi idadi ambapo maelezo kuhusu vitendo neni vya khutuba vilivyodhihirika kwa viwango vyake na athari zilizojitokeza yalitolewa. Zaidi ya hayo majedwali yalitumika kuonyesha idadi ya vitendo neni, sifa zake na kiasi cha matumizi ya kiwango kimoja cha vitendo neni ikilinganishwa na vingine.

## 5.3 Hitimisho

Utafiti huu ulikuwa na madhumuni matatu. Kwanza, kubainisha vitendo neni katika lugha ya khutuba za Ijumaa zinazotolewa misikitini. Pili, kudhihirisha athari za vitendo neni hivyo kwa Waislamu wanaosilikiza khutuba hizo. Tatu kupendekeza matumizi ya vitendo neni vitakavyodhihirika kupendelewa zaidi na waumini katika khutuba. Kutokana na madhumuni hayo, maswali ya utafiti yalikuwa: Je, khutuba za Ijumaa zimesheheni vitendo neni maalum? Je, khutuba za Ijumaa zina athari hasi kwa waumini wanaozisikiliza? Na Je, kuna uwezekano kwamba vitendo neni vinavyopendelewa zaidi na Maamuma vinaweza kutumika ili kuleta athari chanya kwa wasikilizaji?

### 5.3.1 Vitendo Neni vya Lugha ya Khutuba za Ijuma.

Ili kukidhi matlaba ya madhumuni ya kwanza, mtafiti alifanya uchunguzi shirikishi akanasa khutuba za Ijumaa, akanakili maalumati ya ziada kuhusiana na khutuba hizo, akafanya unukuzi wa khutuba hizo kwenye daftari, akazitafsri kwa Kiswahili kisha akawahoji wasikilizaji kuhusu lugha ya khutuba hizo. Kutokana na mahojiano hayo, mtafiti aliweza kupata jumla ya vitendo neni 325 katika khutuba za Ijumaa zilizochanganuliwa na kuainisha sifa za lugha ya khutuba hizo. Kutokana na uchanganuzi uliofanywa, ilidhihirika kwamba kama ilivyokisiwa, khutuba za Ijumaa zilisheheni vitendo neni maalum. Viwango vya vitendo neni hivyo vilikuwa vinne kati ya vitano vilivyoainishwa na Searle. Viwango hivyo ni viwakilishi, vielekezi, vitathminishi na vilazimishi. Utafiti ulidhihirisha kuwa ijapokuwa viwango hivyo vilitumika katika muktadha wa khutuba, vilipishana katika umaratokezi. Kwa hiyo ilibainika kuwa vitendo neni vielekezi ndivyo vilivyokuwa vikitumika zaidi katika khutuba za Ijumaa kwani vilikuwa aslimia 53% kulingana na muktadha wa msikitini ambao unahitaji kuelimisha, kuzindua, kuonya, kuhimiza na kadhalika. Vilifuatiwa na vitathminishi ambavyo viliwakilishwa na aslimia 33% huku viwakilishi vikichukuwa nafasi ya tatu kwani viliwakilishwa na aslimia 8%. Vitendo neni vilazimishi ndivyo vilikuwa vya mwisho katika umara tokezi kwa sababu vilikuwa aslimia 6% ya jumla ya vitendo neni. Ifahamike kwamba viarifu havikujitokeza katika khutuba kwa sababu vina mahali pake maalum na havihusishwi katika ibada ya sala.

### 5.3.2 Athari za Vitendo Neni Vilivyojitokeza katika Lugha ya Khutuba.

Madhumuni ya pili nayo yalifanyiwa kazi kupitia mahojiano na wasailiwa. Kwa vile waliweza kutambua nia ya Maimamu, waliguswa na matamko hayo. Mguso huo uliotokana na nguvu za matamko, uliwaathiri kwa namna mbalimbali. Athari za vitendo neni vya khutuba zilikuwa kuzinduka, kuelimika, kuudhika, kuaibika, kupuuza, kuhuzunika, kuungama, kuzingatia na kukanganyika.

Ingawa swali la pili la utafiti huu lilikuwa likiulizia iwapo vitendo neni vinavyojikita katika lugha ya khutuba za msikitini vina athari hasi, ilidhihirika kwamba vitendo neni vingi vilikuwa na athari chanya na vichache ndivyo vilikuwa na athari hasi. Kuzinduka kuliwakilishwa na aslimia 14%, kuelimika aslimia 4%, kuzingatia aslimia 24%, kuungama aslimia 9%, kuhuzunika aslimia 1% na takwimu hizo ni za athari chanya. Kwa upande mwingine athari hasi zilikuwa

kuudhika kukiwakilishwa na aslimia 38%, kuaibika aslimia 4%, kupuuza 5% na kukanganyika aslimia 1%.

Ifahamike kwamba matokeo hayo yametoa jibu kwa swali la pili lililoulizia iwapo khutuba za Ijumaa zina athari hasi. Takwimu za athari hasi zilizodhihirika ni kubwa kiasi na haziwezi kupuuzwa. Takwimu hizo zilionyesha kuwa jumla ya athari hasi ilikuwa aslimia 48%. Kwa hiyo, utafiti huu ulidhihirisha kwamba kuna athari hasi katika vitendo neni vinavyojikita katika lugha ya khutuba za Ijumaa.

## 5.4 Mapendekezo

Mapendekezo yaliyotolewa katika sehemu hii ni ya aina mbili. Kwanza ni yale yanayohusiana moja kwa moja na utafiti huu ambayo yanakidhi matlaba ya madhumuni ya tatu ya kazi hii. Pili mapendekezo ya maeneo ya tafiti zinazoweza kushughulikiwa na watafiti wa baadaye.

### 5.4.1 Matumizi ya Sifa za Lugha Zinazopendelewa Zaidi

Swali la tatu la utafiti huu lilikuwa likiulizia iwapo kuna uwezekano wa kupendekeza matumizi ya vitendo neni vinavyodhihirika kupendelewa zaidi na waumini katika khutuba.

Kulingana na mahojiano kati ya mtafiti na wasailiwa wake ilidhirika kuwa vitendo neni vielekezi vina athari chanya nyingi kuliko aina tatu zilizosalia. Vielekezi chanya vilikuwa aslimia 39% huku vilazimishi vikiwa aslimia 6% na viwakilishi aslimia 4%. Vitendo neni vitathminishi vyenye mwelekeo chanya vilikwa aslimia 3%. Kutokana na ugunduzi huo, mapendekezo yafuatayo yalifikiwa:

1. Imamu anatakikana ajifunze namna ya kutumia lugha kwa sababu swala la lugha lina nafasi kubwa katika kufanikisha kazi yake. Vitendo neni vielekezi vinaweza kutumika ili kuleta athari chanya iwapo Maimamu watatoa ushahidi juu ya matamko yao kama kinga ya kuwazuia wasikilizaji kufikiria kwamba yamekusudiwa kuwaudhi. Viwakilishi navyo vinaweza kutumika kwa mpwito huo huo. Ijapokuwa vilazimishi havikuzua athari hasi, haviwezi kutumika peke yake kwa sababu muktadha wa khutuba unamlazimisha Imamu kuamrisha, kushikilia, kuonya na kadhalika. Kwa hiyo, vinaweza kutumika sambamba na

viwakilishi na vielekezi. Fauka ya hayo, vitendo neni vilazimishi (*commissives*) kama vile kuapa, kuahidi, kushabikia na pia vitendo neni vitathminishi vyenye mwelekeo chanya kama vile kuomba radhi, kutoa shukrani, kuliwaza, kutoa changamoto, kupongeza na kusifu vinaweza kuleta mvuto katika khutuba na kuzuia athari hasi.

2. Anapaswa kujifunza kanuni shirikishi na zile za unyenyekevu ili kuimudu lugha kiasi cha kumfanya aepukane na kutoa matamko yanayoweza kuwa na athari zisizopendeza kwa wasikilizaji wake. Ni vyema awaombe radhi wasikilizaji wake kutokana na matamko ambayo huenda yamewabughudhi na kuwaomba watilie maanani faida za khutuba. Ni vyema pia awashukuru kwa usikilizaji wao. Hivyo ni kwa sababu matunda mazuri ambayo analenga kuyachuma yanaweza tu kupatikana kwa kutumia lugha ya unyenyekevu kama inavyopendekezwa na kaida za unyenyekevu zilizokitwa katika Nadharia ya Udokezi.

3. Aepukane na vitathminishi vinavyozua athari hasi kama vile kudharau, kutweza na kuaibisha. Aidha anatakikana atangulize somo lake kwa muhtasari ili maana na kusudio lake viwekwe wazi mapema. Aeleze mada yake, dhana muhimu na faida za mada anayoishughulikia.

4. Imamu ajiepushe na matamko yaliyosheheni mashambulizi kwa Maamuma au watu wengine ili asizue ugomvi na malalamishi. Anaweza kufanya hivyo kwa kujiweka miongoni mwa wale ambao ujumbe wa khutuba huwahusu. Matumizi ya maneno kama vile “sisi”, “tusiwe hivi”, “tusifanye hivi” na kadhalika yanaonyesha kwamba Imamu hawanyoshei waumini wake vidole vya lawama bali anazungumzia swala nyeti ambalo anatakikana waungane bega kwa bega ili kulipatia ufumbuzi.

5. Mhubiri anukuu vitabu vinavyotegemewa kama vile Kur’ani na hadithi za Mtume Muhammad (SAW) ili kuthibitisha hoja zake. Kufanya hivyo, kutachangia sana ukubalifu wa ujumbe unaotolewa na Maimamu na kuwadhihirishia wasikilizaji kuwa hautokani na utashi wa khatibu.

6. Mada za kushugulikiwa katika khutuba ziwe zikihusiana na maisha halisi ya waumini wa Kiislamu ili wapate kunufaika. Iwapo atalazimika kusoma zile zilizotungwa zamani basi afanye maandalizi ya awali kwa kuzipitia ili aingize mada ambazo ni mwafaka kwa wakati, hadhira na mazingira anamofanyia kazi yake. Khutuba isiwe juu ya mada moja kila Ijumaa bali ibadilikebadilike kulingana na matukio. Zaidi ya hayo, mhubiri anatakikana kutoa mifano ya yale anayoyajadili kutoka katika maisha ya kila siku ili kufafanua hoja zake na kuufanya ujumbe ueleweke ipasavyo na uwe katika muktadha mwafaka.

7. Khutuba isiwe ndefu sana kiasi cha kuwachosha wasikilizaji. Ni vyema iwe ya wastani. Inamtoshelezea Imamu kutumia dakika tano katika kutoa kitangulizi cha mada, dakika ishirini na tano kuielezea na kuifafanua na dakika tano kutoa muhtasari kwa kubainisha mafunzo yaliyokitwa katika khutuba. Vinginevyo wasikilizaji watasinzia jambo ambalo huenda likamchochea khatibu kutoa matamko makali yanayoweza kuwakasirisha wasikilizaji.

8. Ni vyema iwasilishwe katika lugha wanayoielewa vizuri watu wa mji. Kwa kufanya hivyo Maimamu watakuwa wameshughulikia manug'uniko ya Maamuma juu ya uwasilishaji wa khutuba. Endapo watalazimika kukhutubu kwa Kiarabu ili kutosheleza matlaba ya wanazuoni wanaoona kwamba lazima iwasilishwe kwa lugha hiyo, basi ni jambo zuri waitafsiri ili waumini wote wapate kuelewa ujumbe. Vinginevyo waumini wengi watakimbia na kuacha wanajadi peke yao ambao pia hawatofaidika kikamilifu na khutuba.

9. Ni jambo zuri pia kwa viongozi wa dini ya Kiislamu kuanzisha taasisi ama vyuo vya kuwapa mafunzo wahubiri ili khutuba zisomwe kufuata mbinu maalum. Maimamu waliofunzwa mbinu za usemi wanatarajia kuonyesha na kutumia weledi wao katika kuwashughulikia wasikilizaji wenye misingi tofauti kielimu, kiumri, na kihadhi. Fauka ya hayo, pawepo kozi za kunoa ubongo kila mara ili Maimamu wapate mbinu za kisasa za kuwasilisha khutuba.

10. Pawepo kamati ama timu fuatilizi inayosikiliza khutuba kisha ikosoe wahubiri na kuwashauri juu ya uwasilishaji bora wa khutuba. Ukosefu wa timu kama hiyo huwafanya Maamuma kuwasilisha khutuba zao kwa uhuru uliopindukia kiasi cha haja na kuzishindilia

athari hasi nyingi. Ni kamati kama hiyo ndiyo inayoweza kuwashauri Maimamu ambao wana udhaifu wao ya uzawa unaowafanya waongee kwa namna ya kumchukiza kila anayewasikiliza. Halikadhalika, UMSC ianzishe kamisheni ya kitaifa ambayo jukumu lake ni kuhakikisha kuwa khutuba zinazoweza kuchochea uhasama, chuki na vurugu haziwasilishwi misikitini. Ili kufuatilia kadhia hiyo ipasavyo, baraza hilo lifanye mpango wa kutoa mafunzo kwa timu zitakazoenda katika misikiti mbalimbali nchini.

11. Khatibu awe mvumilivu na asikate tamaa. Asitegemee kwamba waumini watabadilisha mienendo yao katika juma moja au mwezi mmoja. Uvumilivu wake ndio unaoweza kuchangia katika kuzua taathira chanya na kupunguza makali ya waumini wenye sifa za ukaidi. Maswala yanayohusu utamaduni na ambayo huzua athari hasi nyinyi yafaa yashughulikiwe kwa uangalifu mkubwa. Ni vyema Maimamu wajifunze jinsi wananavyopaswa kuyaendea maswala kama hayo kutokana na mapisi ya Uislamu na jinsi Mtume Muhammad (SAW) alivyoweza kubadilisha mwenendo wa jamii yake. Ikumbukwe kwamba hali ya kisaikolojia ya mzungumzaji ina nafasi kubwa katika kufanikisha malengo ambayo kwayo hutoa matamshi kadhaa.

12. Baraza kuu la Waislamu lifanye mpango wa kuwafunza Maimamu angalau lugha tatu, Kiarabu, Kiingereza na Kiswahili ili wapate umilisi katika kuwasiliana na waweze kufikisha ujumbe kwa waumini wenye asili mbalimbali. Halikadhalika, katika misikiti ya vijijini ambako Maimamu wanahitaji kusaidiwa ili kuiboresha kazi yao, Baraza hilo au wenye mamlaka katika ngazi ya mkoa au wilaya waandae miongozo ya khutuba kwa manufaa ya Maimamu na Maamuma wao. Ili kuleta ufanisi katika shughuli nzima ya khutuba, inafaa baraza hilo lifanye mpango kabambe wa kuingiza fani ya khutuba katika mtalaa wa vyuo vya Kiislamu. Hivyo ni kwa sababu baadhi ya makhatibu si Maimamu walioteuliwa rasmi bali hata wale waliosomea dini huruhusiwa au kulazimisha mazingira na kupanda mimbari.

13. Khatibu akubali kukosolewa ili khutuba zake zisiwe za kukashifu na kuzua malalamishi. Ilivyo ni kwamba Maamuma wamepewa ruhusa kumkosoa Imamu katika sala endapo atasoma aya ya Kur’ani kimakosa ili asiupotoshe ujumbe. Kukubali kukosolewa humpelekea Imamu kuwa hodari katika uwasilishaji wake wa khutuba.

14. Imam anatakikana awe mfano bora wa kuigwa.Yale anayoyafundisha yawe yakiambatana na tabia zake. Hivyo ni kwa sababu ni mwalimu na kwa hiyo anatarajiwa kujipamba na sifa nzuri zinazoafikiana na hadhi yake katika jamii. Kulinda ulimi ni kitendo ambacho bila shaka kitamlainishia mambo yake na njia pekee ya kufanya hivyo ni kutahadhari kutoa matamko wanayoweza kuwakera watu. Aidha, asionekane akijitosa katika yale anayowakataza waumini.

15. Ni vyema pia ajue hali za maamuma wake na mitazamo yao ndipo awasilishe ujumbe wake kwa ufanisi. Ujuzi huo, unaweza kumsaidia katika kutoa matamko yanayoweza kufasiriwa kulingana na nia yake na kwa hiyo kupelekea vitendo neni vyake kufaulu kiutendaji. Aidha, ni vyema pia afanye utafiti wa kina kuhusu mada atakayoiwasilisha ili imuwie rahisi kuiwasilisha na kuitolea mifano, la sivyo atajirudiarudia na kuwachosha wasikilizaji wake.

16. Vigezo vya umri na elimu lazima vizingatiwe kwa sababu khatibu anatakikana awe na umri usio pungua miaka 20 na kiwango chake cha elimu kiwe cha juu zaidi kuliko cha Maamuma wake. Inapendekezwa Imamu awe na shahada ya kidato cha sita au chuo kikuu na shahada ya *thaalitha thaanawi* kwa uchache.

17. Ni vyema mhubiri aonyeshe faida na hasara zilizomo katika utendaji wa jambo linalojadiliwa. Iwapo faida ndizo nyingi basi awahimize kushikamana nazo kwa manufaa yao binafsi na jamii kwa ujumla na endapo hasara ndizo nyingi, basi awausie kuondokana nazo ili wasije wakadhurika. Ni vyema pia kuziendea mada zenye utata kwa uangalifu wa hali ya juu na lugha iliyochovya asali ili kukwepa uzuaji wa athari hasi nyingi.

18. Imamu avae mavazi yanayomtunzia heshima yake kama vile kanzu, juba na kofia. Mavazi hayo yawe nadhifu ili kumpa haiba anayostahili.

19. Imamu atumie viziada vya lugha vinavyoweza kuchangia uwasilishaji ujumbe ipasavyo. Kwa mfano, sauti iwe ikisikika vyema na kuipaza na kuishusha kuwe kukitoa ujumbe maalum.

### 5.4.2 Mapendekezo Juu ya Tafiti za Baadaye.

Utafiti huu unapendekeza tafiti zingine zifanyike kuhusu :

Khutuba zinazowasilishwa katika miktadha mingine kama vile kanisani, katika kampeni za kisiasa, sherehe za ndoa na Idi kutumia mkabala wa vitendo neni. Hii ni kwa sababu maeneo hayo yana umuhimu mkubwa kwa watu binafsi na jamii kwa ujumla. Kutafitiwa kwa kina yumkini kutachangia elimu na maarifa ambayo kwayo maendeleo katika nyanja mbalimbali za maisha yanaweza kupatikana.

**MAREJELEO**

Abdul Fallah, M.M. (2004). *Simplified Islamic Jurisprudence* Vol. 1. El Mansoura: Dar Almanarah for Translation and Publication.

Abubakar, M. (2012). Mahojiano ya ana kwa ana yaliyofanyika Industrial Division Mbale tarehe 20 Mei.

Adelakun, T.O. (2001). *Lexical Cohesion in Muslim Sermons: A Discourse Analysis of some cohesive Devises in Friday Khutba.* In: *Islamic University Journal*, Volume 2 no 2. Mbale: Islamic University in Uganda.

Akmajan, A., Demers, R.A., Farmer, A.K. & Harnish, R.M. (1995). *Linguistics: An Introduction to Language and Communication.* Cambrige: MIT Press.

Al-Buhutiy, M.Y. (1993). *Ar-rawdh Al Murbi: Sherh Zaad- Al-Mustaqna.* Beirut: Darul Arqam Bin Abi AI Arqam.

Al-Farsy, A.S. (1984). *Quran Takatifu.* Nairobi: The Islamic Foundation.

Al-Fauzan, S.A (2009). Almulakhas Alfiqhii. Cairo: Dar Ibn Hazm.

Al-Gabid, H.(1993). *The Organisation of Islamic Conference (OIC) and the Development of Africa*. In: *Proceedings of the Islam in Africa Conference*. Ibadan: Spectrum Books Ltd.

Al-Haddad, H. (2008, May, 31). *Questions Pertaining to Friday Sermon*. http://www.sunnahonline.com.

Al-Jaziry, A. (2003). *Alfiqhu Alal Madhahibil Aruba*. Beirut: Darul Kutub Alilmiyyah.

Ali, A.Y. (1973). *The Glorious Holy Kur'an, Translation and Commentary.* Tripoli: Islamic Call Society.

Alkhairo, W. (1998). *Speaking for Change: A Guide to Making Effective Friday Sermons* (Khutbas). Beltsville, Maryland: Amana publications.

Al-Oadah, S. (2008, May 31). *A Fresh Look at the Friday Sermon*. http://www.islamtoday.com.

Anderson, L., & Trudgill, P. (1990). *Bad Language*. Oxford: Basil Blackwell Ltd.

An-nadwy, S. (1993). *AI-Mustafa*: *Mukhutasari wa Sira ya Mtume (S.A* W). Mombasa: Ansaar Muslims Youth Organization.

As-swabuniy, M.A. (1981). *Swafuat - Tafaasiir*. Beirut: Dar-ul Quran al- Karim.

Austin, J.L. (1962). *How to Do Things with Words.* Cambridge: M.A HarvardUniversity Press.

Ayot, H.O. (1975). *Topics in East Africa History*. Nairobi: East African Literature Bureau

Bach, K. (2008, May 31). Speech Acts. http://online.sfsu.edu/kbach/spchacts.html.

Bloommaert, J. (1990) *Mordern African Political Style: Strategies and genre in Swahili Political Discourse.* In: *Discourse in Society*. London: SAGE.

Bosworth, C.E., Donzel, E., Lewis, B. & Pellat, C. (1986). *The Encyclopedia of Islam.* Vol. V. Leiden: E.J Brill.

Brazil, D. (1995). *A Grammar of Speech*. Oxford: OUP

Briggs, R. (2001). *Words in Action: Speech Act Theory and Biblical Interpretation*. University of Heidelberg, Germany. http://ww.google.com.

Brown, G. & Yule, G. (1983). *Discourse Analysis.* Cambridge: Cambridge University Press.

Bryman, A. & Cramer, D. (1994). *Quantitative Data Analysis for Social Scientists*. London: Routledge.

Buyera, M. (2008). *The Tribe and Culture of Bamasaba* (Unpublished).

Chris, H. (2009) *Doing a Literature Review*. London: SAGE Publications Ltd.

Cook, G. (1989). *Discourse*. Oxford: Oxford University Press.

Coulthard, M. (1985). *An Introduction to Discourse Analysis*. London: Longman Group Ltd.

Crow, K.D. (2000). *Nurturing Islamic Peace Discourse.* In: *American Journal of Social Sciences*. Volume 17,number 3.Washington DC: International Institute of Islamic Thought.

Crow, K.D. (2000). *The use of peaceful IslamicaDiscourse*. In: *Islamic Horizons 27. No5* (September/ October).

Crystal, D. & Davy, D. (1973). *Investigating English Style*. London: Longman Group Ltd.

Crystal, D. (1992). *The Cambridge Encyclopedia of Langauge*. Cambridge: Cambridge University Press.

Denzin, N. and Lincoln, Y. (eds) (2000) *Handbook of Qualitative Research,* 2nd edn. Thousand Oaks, CA: Sage.

Elia, A. (1989). *Fannul Khatwabal Arabiyyah*. Lebanon: Darul Kutubil Arabiyyah.

Fraser, B. (1996). *The Domain of Pragmatics.* In: *Language and Communication.* Richards 1. C and Schmidt, R. W (Eds). New York: Longman Group Ltd.

Fromkin, V and Rodman, R (1988). *An Introduction to Language*, 4th Edition, New York: Holt, Rinehart and Winston Inc.

Geis, M.L. (1982). *The Language of Television Advertising*. New York: Academic Press Inc.

Golingay, J. (1985). *Models for Interpretation of Scripture.* Michgan: William B. Eerdmans Publishing Company.

Grice, H.P. (1990) *Logic and Conversation*. In: *The Philosophy of Language,* edited by A.P. Martinich. Oxford: OUP.

Group of Muftis. (2008, May 31). *Delivering the Friday Sermon in a Language other than Arabic*. http://www.islamonline.net

Halion, K. (2008, May 31). *Deconstruction and Speech Act Theory: A Defence of the Distinction between Normal and Parasitic speech Acts*. http://www.e-anglais.com/thesis.html.

Hamidullah, M. (1983). *Introduction to Islam*. Kwalalumpar: Polygraphic Press.

Hart, C. (2009). *Doing a Literature Review: Releasing the Social Science Research Imagination*. London: SAGE.

Hogan,P.C(2000). *Philosophical Approaches to the Study of Literature*. Florida: University Press of Florida.

Idowu, E.B (1973). *African Tranditional religion*. London: SCM Press Ltd.

Kasozi, A.B.K (1996).*The Life of Prince Badru Kakungulu Wasajja: The Development of a Forward Looking Muslim Community in Uganda 1907-1991*. Kampala: Progressive Publishing House.

Katherine, A.A (1997) *Perspectives on Contemporary Issues: Readings Across the Disciplines.* Newyork: Harcourt Brace College Publishers.

Kathleen, G, Bruce, E.G, Dauglas, E and Alan, H.M (2001).*Principles of Public Speaking.* New York: Longman.

Khamis, W. (2010). Mahojiano ya ana kwa ana yaliyofanyika Busoba, tarehe 2 February.

Kitakule, R(2011). Mahojiano ya ana kwa ana yaliyofanyika Manyonyi, tarehe 5 Januari.

Lee, D. (1996). *Language, Children and Society: An Introduction to Linguistics and Language Development*. Sussex: The Harvester Press Ltd.

Leech, G. & Svartvik, J. (2002). *A Communicative Grammar of English*. London: Pearson Education Ltd.

Leech, G.N. (1995). *Principles of Pragmatics.* New York: Longman Group Ltd.

Lukyamuzi, H.M. (2005). *Islamics Simplified: For Ordinary level in Uganda*. Kampala: Nest Printers.

Mahadi, A. (2001). *The main Sources of Malaise in the Muslim Ummah in Nigeria and Uganda*. Katika: Islamic University Journal, Mbale: Islamic University in Uganda.

Maher, H. (1998). *Islamic Intellectual Discourse in America: In Islamic Horizons* 27. No. 5 (September/October): 24 – 25.

Markman,R.H, Markman, P.T and Waddel, M.L. (1982). *10 Steps in Writing the Reseach Paper*. New York: Barrons Educvational Series, Inc.

Marshall, C and Rossman, G.B. (2006). *Designing Qualitative Research*. London: Sage Publications.

Masayi, Z (2012). Mahojiano ya ana kwa ana yaliyofanyika Bukonde, tarehe 23 Disemba.

Maududi, A.A (1985). *Fundamentals of Islam*. Delhi: Markazi Maktaba Islami.

Mbiti, J.S (1969). *African Religions and Philosophy*. London: Hienemann.

Mbogo, A (2012). Mahojiano ya ana kwa ana yaliyofanyika tarehe 11huko Katika msikiti wa Gadafi jijini Kampala Februari.

Mills, S. (1999). *Discourse*. London: Routledge.

Mubaje, S.R. (1995). *Traditional, Vis-à-vis Islamic Circumcision among the Bagisu Muslims of Uganda*. M.A Dissertation (unpublished), Makerere University.

Mugenda, O.M. & Mugenda, A.G. (1999). *Research Methods: Quantitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.

Muslim, A.(2008). *Sahih Muslim*. Cairo: Darul Kutubil Islamiyyah.

Namonye, K. (2012). Mahojiano ya ana kwa ana yaliyofanyika Bukonde, tarehe 23 Disemba.

Nsiimba, A. (2012). Mahojiano ya ana kwa ana yaliyofanyika Njoro, tarehe 12 Februari.

Ogilvy, D. (1963). *The Confessions of an Advertising Man*. New York: David Ogilvy Trustees.

Ogolla, A.R. (2007). *Uchanganuzi wa Jinsi lugha inavyotumika kuhamasisha wanawake kuhusu haki zao: Mfano kutoka wilayani Kisumu.* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Egerton.

Parker, F. (1986). *Linguistics for Non-Linguists*. San Diego: Littlewood, Brown and company.

Paxson, W.C. (1985). *Principles of Style for the Business writer*. Newyork: Dodd, Mead and Company.

Pearson, J.C, & Nelson, P.E. (1982). *Understanding and Sharing: An Introduction to Speech Communciation*. Iowa: Web publishers.

Penelope, B and S teven,C.L. (1987). *Politeness: Some Universals in Language Usage*. Cambridge: CUP.

Routledge. (1996). *Routledge Dictionary of Langauge and Linguistics*. London: Routledge.

Searle, J. (1975). "*Indirect Speech Acts". In: Syntax and Semantics*. ed. P. Cole and J.L. Morgan. New York: Academic Press.

Searle, R. & Kiefer. (1980). *Speech Act Theory and Pragmatics.* London: Reiche Publishing Company.

_______________ (1990) *What is a Speech Act?* In: *The Philosophy of Language*, second edition. Oxford: OUP.

Searle, J.R. (1979). *Expression and Meaning: Studies in the theory of Speech Acts.* New york: Cambridge University Press.

Seyler, D.U. (1993). *Doing Research.* Boston: MCGraw- Hill Companies.

Shauqi, D. (1963) *Tarekh Aladab Al- Arabiy: Alasr al-Islamiy*. Cairo: Darul Maarif.

Shiffrin, D. (1995). *Approaches to Discourse.* O.U.P: Blackwell Publishers Inc.

Silverman, D. (2005). *Doing Qualitative Research*. London: SAGE Publications.

Smith, B. (2008, May, 31). *Towards a History of Speech Acts Theory*. http://ontology.buffalo.edu.

Steven, T.M. (2009, February12) *Journal for the Study of the Old Testament*. http://www.Sage pub.com.uk.

Stewart, T.W. & Vaillette, N. (2001). *Language Files: Materials for an Introduction to Language and Linguistics.* Columbus: The OhioUniversity Press.

Tegle, J. (2008, May 31). *The Muslim Friday Sermon – A Message to the Islamic Nation*. http://www.infosphere.se.

Tibenderana, K.P. (2006). *Islamic Fundamentalism: The Quest for the Rights of Muslims in Uganda*. Kampala: Fountain Publishers.

TUC(1983) *Encyclopaedia Britanica*. Vol.5. Fifth Edition. Chicago: Helen Hemingway Benton Publishers.

UBOS (2005). *2002 Uganda Population and Housing Census*. Entebbe: Uganda Bureau of Statistics.

Walwenje, Y (2012). Mahojiano ya ana kwa ana yaliyofanyika Mbale tarehe 15 Oktoba.

Walya, E. (1995). *Discourse Strategies in Banking Discourse.* M.A. Thesis, Kenyatta University.

Wardhaugh, R. (1992). *An Introduction to Sociolinguistics*. Oxford: Blackwell. Publishers

Wikipedia. (2008, May, 31). *Speech Acts*. http:/en.wikipedia.org.

Wray, A, Trot, K. & Bloomer, A. (1998). *Projects in Linguistics*: *A Practical Guide to Researching Language*. London: Arnold.

Yule, G. (1985). *The Study of Language*. Cambridges: Cambridge University Press.

## KIAMBATISHO A: MWONGOZO WA MASWALI

**Sehemu A. Maswali kwa Maamuma**

1. a) Je, kuna khutuba yoyote ambayo haikukufurahisha?
   b) Iliwasilishwa lini?
   c) Iliwasilishwa na nani?
   d) Ni nini ambacho hakikukufurahisha?
2. Sikiliza kanda kisha ujibu maswali yafuatayo.
   i. Kutokana na tamko x umehisi nini?
   ii. Tamko y la Imamu lina maana gani?
   iii. Je, umefurahishwa na kila tamko katika khutuba? Kwa nini unaona hivyo?
   iv. Je, kiwango cha elimu alichonacho kinachangia kwa vyovyote katika uwasilishaji khutuba jinsi anavyofanya?
   v. Kwa maoni yako, kwa nini baadhi ya Maamuma hawatilii maanani ujumbe wa Imamu kama unavyojitokeza katika khutuba?
3. Je, una mapendekezo yoyote juu ya namna ya kuwasilisha khutuba?

**Sehemu B: Maswali kwa Imamu**

1. Ulikuwa ukimaanisha nini kwa matamko hayo uliyoyatoa?
2. Ni nini ulichotarajia kutoka kwa wasikilizaji kutokana matamko uliyoyatoa katika khutuba yako?
3. Kwa ujumla khutuba za Ijumaa huwaathiri vipi wasikilizaji?
4. Kwa maoni yako matamko yako yaliwaathiri vipi wasikilizaji? Kwa nini unasema hivyo?
5. Je unapowahutubia Maamuma unajali hisia zao?
6. Waumini wanasema nini kuhusu khutuba zako?
7. Je, unategemea uandishi katika kukhutubu au la? Kwa nini?
8. Ukigundua kwamba khutuba yako imekuwa na athari hasi au chanya unafanyaje?
9. a)Kwa maoni yako, ni mambo gani yanayoweza kuathiri uwasilishaji wako wa khutuba?
   b)Pendekeza jinsi khutuba inavyoweza kuboreshwa ili kuleta athari chanya kwa wasikilizaji.

## KIAMBATISHO B: VITENDO NENI KATIKA KHUTUBA ZA IJUMAA NA ATHARI ZAKE KWA WAUMINI

### Sehemu A) Vitendo neni Vilivyojitokeza katika Khutuba za Ijumaa

### Khutuba 1

1. Namhimidi Mwenyezi Mungu Muumba wa mbingu na ardhi…
2. Ingekuwa vyema matamko haya machache uyazingatie. Lakini ukikataa, Mwenyezi Mungu atakuweka katika kundi la waovu kisha aamrishe mjipambanue…mwanze kuzozana kwa ajili ya mali kwa sababu hamna subira, mzozane kwa ajili ya wanawake, mzozane kwa ajili ya magari, mzozane kwa ajili ya heshima…
3. Ukiomba elimu, Mungu anaweza kukupa…anaweza kukupa elimu asikupe fahamu…yote yakawa kichwani lakini ukashindwa kutofautisha kati ya halali na haramu.
4. Tuvumilie… mambo ya dunia hayeshi. Mwangalie mwenzako kwa jicho la huruma...ukiwahurumia wale unaowazidi katika cheo, Mwenyezi Mungu atakupandisha cheo...
5. Kijana asipokuwa na simu huhuzunika. Asipokuwa na nguo ya thamani , huhuzunika eti hiyo ni shida.
6. Kama wewe si muumini, basi humo miongoni mwa Waislamu… muumini huwa Mwislamu lakini Mwislamu hawi muumini.
7. Wewe ni nani? Waislamu . Wewe ni nani ambaye Mwenyezi Mungu hampi mtihani? Ikiwa aliwapa manabii mtihani, wewe ni nani? Wanakuroga wewe peke yako?
8. Tutambue kuwa mazuri na mabaya hutoka kwa Allah.
9. Waislamu twaogopa ufukara lakini tumafukara. Tumekuwa wasahaulifu juu ya sala zetu. Hakuna atakayekuwa fakiri siku ya kiyama kama aliyeghafilika katika sala zake…
10. Fakiri ni yule aliyetoa sadaka…akaegesha pale gari yake, akaamrisha msikiti upakwe rangi ili kila mmoja aone anayotenda.
11. Ikiwa unatenda jambo lolote tenda kwa ajili ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Sio kutoa sadaka na kuwaita watu waje washuhudie, watoe takbira…
12. Usimame pale ukionyesha kitambi … Waislamu hayo ni bure tu… utakuwa fakiri siku ya kiyama.

13. Unasema waogopa ufukara. Basi subiri siku ya kiyama . Tutaulizwa juu ya matendo yetu.
14. Kutakuwa na jua. Wewe na mimi tutakuwa chini ya hilo jua…mwavuli, kivuli au soda baridi utaitoa wapi?
15. Ulikuwa ukisali ili wakuone au kwa ajili ya kuwaogopa watu.
16. …wasema hutoadhini kwa sababu Waislamu hawakulipi. Ni nani aliyekwambia kwamba Waislamu ndio wanaokulipa.
17. Kutakuwa na jua, ubongo utachemka, hutakuwa na miavuli wala kofia.
18. Watu wengi hawajahiji ijapokuwa wana pesa. Ukimwambia ahiji, husema watoto wake hawajamaliza masomo ya chuo kikuu.
19. Wasema huyu Hamisi sitamsema ilhali ni tajiri…yule hasali lakini akifiwa na mtoto eti kwa sababu ana kanzu ya utukufu... kwa sabu ni RDC…Imamu ana kanzu yenye kiraka hapa na kingine pale… hammnunulii kanzu…Maimamu msiwaogope hao mabwana, msiwaheshimu, mheshimuni Allah.

**Khutuba 2**

1. Nashuhudia kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Allah.
2. Mtume alikuwa na habari kuhusu zama hizi, mstakbala wake na hali zetu… akasema itakuwaje vijana watakapokuwa na tabia zisizopendeza.
3. Ikiwa kilichomliza mtume ni tabia zetu, tufanye nini…pepo twaipenda sisi tuliomliza.
4. Tukifika katika mwaka kama huu, watu hufurahika eti ni mwaka mzuri, mwaka mpya, lakini huu hawaufurahikii kwa sababu ni mpya, bali kwa sababu una visa. Visa vilivyomo katika mwaka huu ni pamoja na sherehe ya tohara ambayo Wagisu huichukulia kuwa halali.
5. Mwenye mtoto sasa anatafuta mbuzi…na mbuzi huyo ni wa kuchinjia uani ili mtoto astahmili maumivu.
6. Leo watamchinja mbuzi ilhali katika Idi hawakufanya hivyo.
7. Mbuzi wako subiri umchinje siku ya Idul Adhuhaa ili upate thawabu.
8. Lakini huyo mbuzi tumchinjiaye uani, kitendo hicho ni cha shiriki.
9. Haifai Mwislamu kumchinja. Haifai kwa Mwislamu kumla. Nilikuelezeni kitambo kwamba mbuzi anayehusishwa na miungu na matambiko hafai…

10. Nilikwambieni kwamba miviga ya kishirikina si katika matendo ya Waislamu. Atendaye hayo si Mwislamu.
11. Ndio maana…Uislamu tuliupiga kisogo kitambo. Una mtoto, amekua, umekataa kumtahiri. Wasubiri kumtahiri ukipata mbuzi. Hivyo ni vitendo vya kishirikina. Waja wa Allah hivyo ni vitendo vya fedheha.
12. Jambo hili nalizungumzia kila mara. Huko Mutoto, watu walivuliwa nguo wakatembea wakiwa uchi…
13. Leo hii kuna mambo miongoni mwa vijana. Unamkuta mtoto wa miaka 10, 15 akiwa na mpenzi. Lakini wazazi wake wanafurahia kitendo hicho na kusema: “Wanitafutia binti yangu?”. Mama anamwambia binti: “Mwanangu wanitafutia mkwe wangu”? Ni vitendo vya fedheha.
14. Nenda kwenye televisheni. Watu huchukua pesa zao wakanunua televisheni. Vitendo vilioko kwenye televisheni hushuhudiwa na watoto. Wakafahamu mambo yote yanayotokea baina ya mama na baba.
15. Mama hajali. Baba ndiye anayewasha T.V. nakuwaita watoto wake kuja kutazama…
16. Jambo la pili ni unywaji pombe. Taarifa tuliyo nayo katika kitongoji hiki ni kwamba kuna akina mama ambao hunywa pombe...swala hilo tutalichunguza na mama huyo tutamwambia...
17. Kuna wengine wanaoenda kwa Nabugodi eti wanatafuta kuombewa…watu wanawashutumu Mashekhe… ambao wangewaombea dua.
18. Shekhe anayesema ukweli ndiye wanayemchukulia kuwa mbaya.
19. Kuna anayesema: “Uislamu umenishinda…Shekhe mzima anatenda jambo fulani”. Usimfuate yule ambaye ana walakini. Ikiwa unaweza kumkanya mwambie: “Unaharibu Uislamu”. Ushikamane na mwenendo wa mtume (SAW).
20. Usimuumbue, bali mwambie mtu anayemfahamu amkanye…kwa sababu Shekhe naye ni mwanadamu. Anaweza kukosea au wanaweza kumsingizia.
21. Watu ambao mtume wetu katwambia tuwafuate ndio watakaotufaa.
22. Yule anasema: Shekhe kasoma. Kwa nini hatupi hiki. Shekhe kazi yake ni kusoma na kufundisha watu…hawagawii watu pesa, huwagawia wino.

23. Twaomba Mwenyezi Mungu watoto watahiriwe ili tusimwone mtu anayefyeka mashamba ya watu eti kwa sababu ndizo njia zinazowapeleka uwanjani…wakaharibu vyakula vya watu… hiyo ni hatia mbele ya Mwenyezi Mungu.
24. Yeyote…mwenye kazi… ya mizimu aiache. Wallahi ikiwa wewe ni mkubwa anayetazama iwapo ndege…hayo yote yaache.
25. Na nyinyi wenye kuchinjia mbuzi uani na kuyaweka mapafu kwenye kijiti, hayo ni matendo ya ushirikina. Jisalimisheni.
26. Watakuleta ukiwa umejifunga majani, ukiwa huko Mutoto…unafikiri huo ni mchezo.
27. Kuna Shekhe mmoja alikana kwamba hakuenda Mutoto lakini Bwana mkubwa aliamrisha apigwe picha akapigwa kisha akaachishwa kazi.

**Khutuba 3**

1. Namhimidi Mwenyezi Mungu …ni mmoja tu. Hana mshirika.
2. Lakini nyinyi shingo zenu mmezifanya ngumu sana kama Mayahudi…na nyinyi mnataka kuwa wakorofi kama Mayahudi?
3. Na nyinyi watu wa kisiwa hiki…mnataka kuwa kama Waisraili?
4. Mmekuwa wakaidi juu ya aya za Mwenyezi Mungu na hadithi za mtume (SAW).
5. Na sasa nimeshagundua kwamba tumekuwa na roho ngumu kama Waisraili.
6. Wewe unakuja msikitini saa ngapi? Na wewe saa ngapi?
7. Wasema Bwanako hajakupa ruhusa. Na wewe una Bwana?
8. Mmechangia kushindwa kwangu kwa ajili ya viburi vyenu.
9. Hatukujua kwamba leo ni siku ya Ijumaa?
10. Kuna walioruka usiku wakachinja kuku eti kwa sababu wamemaliza mwaka. Ni Waislamu?
11. Ijumaa iliyopita tulikuwa katika mwezi wa Ashuuraa…ni nani aliyefunga?
12. Watoto wawekeni sawa. Mwazini ndiye angefanya hivyo lakini hajui kazi yake.
13. Waja wa Allah. Baada ya hayo mliyosikia na ambayo hamkuyaelewa…
14. Sisi waja wa Allah twafanya mambo yetu jinsi tunavyotaka. Twatembea tutakavyo na ibada twaifanya tutakavyo. Wenye ndevu mikono yao iko kwenye ndevu na walionyolewa mtindo wa kishaurini mikono yao iko kwenye vichwa vyao.
15. Baadhi yetu, jambo linalotufanya tuzubae ni kutaka utukufu.

16. Sasa wewe uliopo hapa, mheshimiwa jitazame. Sala 5 unazisali na sala ya Ijumaa unaiendea katika majira yake.
17. Lakini tuna safari ambayo kwayo unaandaliwa kwa kuoshwa, kuvishwa na kuzikwa alikozikwa babu yetu Adam (AS).
18. Kuna aliyesema: Fulani akiwa katika mji fulani hataenda huko. Alipofariki ndipo akaenda. Yeye hatakufa?
19. Adhabu za Mwenyezi Mungu ni kali jamani...kuna wanaocheka wakiwa kaburini.
20. Kuna waliofungua mwaka wa 2010 kwa kuwatahiri wavulana huko Mudodo na hicho kikawa kitendo cha ibada Ugisuni…Mcheni Allah.
21. Wewe uliyemaliza mwaka bila kuugua. Unafikiri wewe ni adhimu sana.
22. Mwilini mwako huna sala…kuna wale ambao tunawaosha kwa mara ya kwanza na mwisho… tukakuzika katika sanda tatu.

**Khutuba 4**

1. Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu (SW)...
2. Hata kama wewe ni mkubwa kiasi gani, unapendeza namna gani, umbabe kiasi gani, Mwenyezi Mungu anataka ufanye tu kitu kimoja –kumcha.
3. Na Uislamu ni ni? Wazurura tu ovyo katika Uislamu au unao katika sheria?
4. Wewe ambaye twasoma ukawa huongoki, unavunja sheria.
5. Akatuchagulia sisi umma wa Muhammad (SAW) dini ya Uislamu. Lakini nyinyi tunaosomea…mnalala tu.
6. Nimekwambieni kwamba zindukeni. Mauti yu karibu.
7. Kama tungekuwepo, mwenzako anapofariki, tungefahamu.
8. Ukiwa Haji na hali husali, tutasema wewe ni Haji magendo. Usiposali, jua kwamba una adhabu. Mwacha sala amelaaniwa.
9. Tumeambiwa tusimtolee salamu. Ikiwa yeye ndiye aliyeyutangulia, tusimjibu. Akiugua, hatembelewi. Haozeshwi.
10. Una msimamo gani ewe mwacha sala? Yumkini upo...una msimamo gani ? Hata humo katika mwenendo wa Uislamu. Tuwe watu wanaozungukia kwenye nguzo za Uislamu.
11. Kwa hiyo waja wa Mwenyezi Mungu, tusingependa kuishi katika hali ya kubabaisha. *Allahu Achibar*. *Allahu Achibar*. Unagonga tu kichwa na hujui kitu.

12. Tunahangaika kutafuta waganga kwa sababu hatujui kudura ya Mwenyezi Mungu. Inafaa umtegemee. Ni yeye ndiye anayeleta jambo na kuliondoa.
13. Mtume ametuamrisha kusali jinsi alivyokuwa akisali. Wewe unataka kusali ukiwa peke yako? Wewe unataka kufanya mambo yako peke yako?
14. Sisi hasa, wasomi…ni sababu ya kuuvuruga Uislamu. Msomi mmoja akiwa na Waislamu, huwafundisha wayasiyofaa. Fundisheni mafundisho ya Bwana wetu Muhammad (SAW) yanayounganisha watu.
15. Mcheni Mwenyezi Mungu nyinyi wenye akili. Jitazame. Una akili au huna? Ikiwa una akili umche Mwenyezi Mungu (SW).

**Khutuba 5**

1. Tunamhimidi Mwenyezi Mungu kwa kila hali na kumsalia mtume wake (SAW). Na aali zake na sahaba zake na waliomfuata kwa ihsani mpaka siku ya Kiyama.
2. Kuna hadithi zilizoingizwa humu ndani. Hazina maana yoyote.
3. Hadithi inayosema Bismillahi ilipokelewa na nani…tufuate la nani? Yule aliyepokea hadithi zama za Khulafaa Rashiduuna na yule aliyepokea hadithi zama za Mtume (SAW) tufuate la nani ? Sasa uyashike yale ya aliyekuwa nyuma ya Mtume na yale uyaache.
4. Hata wale wanaosema bismillahi lazima isomwe huisoma kwa siri. Why? Watu unawapeleka wapi? Ikiwa wewe hujakuwa msomi na huku unawaambia watu hiki hakuna, haifai…huna hakika. Tafuta hakika Bwana.
5. Wewe mwenye kuingia radio jiulize unaingia kama nani? Unaingia umetimia kuingia kwa radio sio unaingia tu kwa radio ukatoa fatuwa zako: "*Lailaaha illallah* haifai. Kumsalia mtume haifai. *Talkini* Haifa. Una hakika?
6. Huna hakika.. inafaa uwe na hakika. Inabidi uwe na ushahidi katika Kur'ani na hadithi za Mtume za sawa.
7. Kusema wewe umesoma hadithi 15-20 unataka kuwa mhubiri?
8. Unasikia tu makelele vitu fulani vinafaa vitu fulani havifai. Utakuta wahubiri wengine wako wrong side.
9. Sisi wahubiri tunafanya makosa kuwambia watu: "Haya yanafaa. Haya hayafai''. Imekuwa sasa ni kuwachanganya Waislamu. Ukija kwa huyu anasema dua inafaa. Ukija

kwa Shekhe mwengine anasema dua haifai. Sasa Waislamu wanaelekea magrupu magrupu. Kila mtu anasema ya Shekhe wangu ni bora…sasa tunawagawanya Waislamu.

10. Utakuta Shekhe hana kofia. Mtume alifanya hivyo? Wamepambwa na bidia kweli kweli.
11. Kama ukikuta wewe una aibu kama zile za mwenzako usizichambue…Funga mdomo. Ukizichambua na yule mwenye kusikia atachambua zako.
12. Msiseme sala ndiyo ibada. Na dua ni nini? Mtume anasema: “Dua ni kiini cha ibada”. Ilijibiwa dua ya Nabi Musa na wewe ukimaliza kusali unatupa watu wanagongana na milango kwa nini ? Wacha kufanya da’wa na kuwapoteza watu.
13. Wanasema mtume alipokuwa akisali akamwona shetani, Mungu akatuma Jibril aende amwambie mtume apige kidole amvunjevunje shetani. Wacha nikupe aya ya kuvunja hiyo kwanza. Kisha nikupe hadithi nikuvunjevunje kabisa. Kwa ajili hujafika. Huzijui hizi. Sasa kazi gani Mungu kutuma Jibril Mtume anapoona shetani? Ikiwa amemwona shetani inafaa Nabii mwenyewe ajikontrol.
14. Kwa hiyo, hiyo hadithi urongo kabisa. Imepingwa na Kur’ani. Wewe mhubiri nakwambia imepingwa na Kur’ani.
16. Unaona watu wa da’wa walivyo na problem? Wanazungumza kitu bila kupima. Bila kuangalia. Huzungumzi tu: “Hadithi waali. Hadithi waali”. Nenda kwa Kur’ani na tafuta hadithi ambayo ni sahihi. Wacha kupoteza watu kwa kuwagawanya magrupu magrupu.
17. Nyinyi Maamuma mna nini? Mnafaa mchambue khutuba yangu halafu muende mwaulize: “Shekhe ametoa wino. *Ogamba ki*”? Ili mtusaidie sisi tukuwe kitu kimoja. “Leo Shekhe ametuthibitishia kwa Kur’ani. Una *sababu nuzuli* yako nyingine utatupa” ?
18. Dua hii: “*Rabbana’ghfir lana wal ikhwaanina alladhiina sabaquuna bil iymani*”, iko wapi? Katika Kur’ani. Ya kuwaombea watu gani? Waliokufa. Na wewe mbona wasema dua ya waliokufa haifai?
19. Unajua anayepinga Kur’ani inafaa aitwe nani? Kafiri. Mwenye kupinga maneno ya Mungu aitwe nani? Kafiri.
20. Dua zetu ni za upuuzi. Kila mmoja anainua mikono, kuangalia madirisha, anangalia milango anasema Shekhe hamalizi ? Sasa Mungu atajibu nini kwa dua ? Wewe huko kwenye dua. Unamwomba Mungu umenyoosha miguu au umekaa umeegemea hivi. Inataka tuonyeshe heshima.

21. Bush alipanga vita vyake, akaingia, akaua watu wa Iraq, akapindua gavumenti ya Sadamu, mwisho akamwua na nani ? Kuonyesha udhaifu wetu, alimwua siku ya udhuhiya. Waislamu wanachinja chinja, wacha nimchinje, nimnyonge mtu wao.
22. Naomba Mashekhe, watu wa ahl da'wa wakuwe wenye kufikiria zitu za maana.

**Khutuba 6**

1. Namhimidi Mwenyezi Mungu aliyetupa mwongozo.Tusingekuwa wenye kuongoka kama hakutuongoza.
2. Waislamu wana mfano mzuri wa kuigwa kutokana na maisha ya mtume Muhammad (SAW) ambaye ijapokuwa aliteswa, akatukanwa, akadhalilishwa, akapigwa, akahamishwa aliendelea kushikilia na kushikamana na tamko kuwa : " Hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu".
3. Ukiangalia hali zetu na aya aliyoiteremsha Mwenyezi Mungu iliyoharamisha unywaji pombe, kucheza kamari…ingetutoshelezea…Mwislamu asingekunywa pombe, Mwislamu asingekuwa mwenye kupiga ramli…aya hiyo ilipoteremshwa, pombe iliyokuwa kwenye mitungi, vyungu na mapipa waliimwaga ikatiririka mitaani kama maji.
4. Lakini leo shetani ametenda kazi . Ukipita kwetu hapa Bugema utashangaa. Waislamu ndio waliozidi katika unywaji pombe. Kila baa hapa Bugema waliomo wengi ni Waislamu.
5. Wako hapo wakidhani kwamba ni Waislamu lakini si Waislamu……
6. Ukipita huko Munkaga watoto wa Waislamu hunywa pombe …usiku utawakuta barabarani wanayumbayumba wamelewa.
7. Wameng'ang'ania mambo ambayo Mwenyezi Mungu ameharamisha. Mwenyezi Mungu ameharamisha kamari.
8. Ni wachache mno wasemao: *Lailaaha ill'Allah* "Hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Allah", ikawa kwamba kauli hiyo imechimbuka kwenye nyoyo zao.

**Khutuba 7**

1. Hakika himdi ni za Mwenyezi Mungu…natoa ushuhuda kuwa hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu.
2. Nausia nafsi yangu na nafsi zenu kumcha Mwenyezi Mungu mwemye nguvu na utukufu.

3. Lakini baadhi ya Waislamu, yule akiwa peke yake husali jinsi anavyotaka, hufanya mambo yake jinsi anavyotaka.
4. Ndugu zangu. Tusipomcha Muumba wetu, hatuwezi kufaulu. Tutakuta kwamba tumeongeza matatizo.
5. Ndugu yangu unayenisikiliza. Kwa nini Mwenyezi Mungu aliapa kwa zama akasema: "Walaswir"? Kuhusu sura hii wafasiri wamesema MwenyeziMungu aliapa kwa zama za mwisho wa dunia" akhiru zamani". Ndugu zangu ukiangalia zama za mwisho ambazo zimekaribia akhera, utakuta kwamba ni hizi zama zetu ndizo zinazokusudiwa.
6. Ukiangalia mambo yaliyosababisha kuangamia kwa watu wa Luut (AS) utakuta kwamba yapo zama hizi pia. Ukajiuliza, tuko wapi? …ikiwa Mwenyezi Mungu aliangamiza watu kutokana na madhambi… nasi tukawa wenye kutenda madhambi hayo na zaidi ya waliyotenda.
7. Tazama watu walivyokuwa waovu katika dunia hii. Tazama wanawafuata. Tazama wanabisha kwenye mlango wa Nabii Luut (AS) wanasema watoe nje hao wageni. Luut akasema siwezi kuwapeni hawa. Chukueni wasichana wangu kwani wao ni wanawake. Wakasema ni nani aliyekwambia kwamba sisi tunawataka wanawake? Sisi tunawataka wale vijana waliokuja.
8. Ripoti tulizopata husema kwamba watoto wengi kuharibika chanzo chake ni akina mama. Msichana akafikia hatua ya kupata mimba akiwa bado nyumbani. Mama akaficha ushahidi. Babaake kugundua ukweli wa mambo baada ya miezi sita…baba akifika, husema mwache mwanangu…
9. Angalia. Mke wake Luut alivyokuwa akitembea akasikia mripuko akauliza ni nini hicho? Alibaki hapo. Mwenyezi Mungu akamwangamiza. Alikuwa mwanamke mwovu akiwaunga mkono wale watu.
10. Yaliyotendeka zama za Luut yapo duniani au hayapo? Nashangaa! Unasoma gazeti kwamba yule alikuwa Patrick na mwengine David. Sherehe ilifanyika kanisani. Pasta akatoa maombi eti. Eti akamwozesha mwanamume na mwanamume ili wawe katika ndoa tukufu. Hiyo dunia imefika wapi? Twavidanganya kuwa twaviombea dua. Watu wameenda mbali.
11. Ni jambo la kushangaza. Hao tuliowapa kura wakaenda bungeni. Wabunge wa Uganda Mwenyezi Mungu awasamehe. Kwa sababu hata viongozi…walisema jambo moja. Kwamba hatuwezi kutoa ruhusa mwanamume kumwoa mwanamume mwenzake…Eti kwa

nini? Eti kwa sababu huo si utamaduni wao…Hoja yenu ni sawa. Lakini tunawajibu tukisema kwamba kitendo cha mwanamume kutoolewa ni kutokana na Mwenyezi Mungu…kitendo cha ushoga kimewekewa adhabu.

12. Ni kwa vile jambo hili tukitoa hukumu wanasema kwamba tumechukulia sheria mikononi. Lakini walahi huyo mwanamume asingetoka hapo. Hicho kitendo kukitendea hapa Mbale, huyo Bwana asingetoka hapo...ilikuwa auawe moja kwa moja. Mwenyezi Mungu baada ya kumuumba Adam hakumuumba mwanamume ...kutokana na ubavu wake. Kwa nini alimuumba mwanamke ?
13. Mada yetu ni Naapa kwa zama ambapo mwanadamu atakuwa katika hasara. Ndio maana tukaleta hayo mambo kwamba sisi wanaume tumepata hasara kutokana na kufanya vitendo vilivyompelekea Mwenyezi Mungu kuzihilikisha enzi zilizopita na hata tukapindukia....tukaifikia hatua ya kuwasilisha hoja kama hizo eti tuzijadili.
14. Ee Mola! Tuonyeshe ukweli na uturuzuku kuufuata. Na utuonyeshe batili kisha uturuzuku kuiepuka. Kwa rehema yako ewe aliye mbora kuliko wanaorehemu.
15. Wenzetu tunaowarejelea kama Wazungu wana fikra zao zinazojulikana kama Western Culture. Utamaduni wa Kimagharibi. Sehemu kubwa ya Utamaduni wa Kimagharibi ni ya kishetani. ..kwa sababu kile ambacho Kur’ani huzuia, wao hukiendeleza. Tukiangalia makanisa ambayo huwaozesha mbwa na mwanadamu, yote ni ya huko magharibi...
16. Kwa nini wanajitokeza na kusema kwamba huyu ni raisi wa taifa fulani na huyu ni First Lady ? Kama wangesema Second Man tungekubaliana nao. Tungeona mwana mume mvaa siruali ndiye anayemtayarishia matoke...hicho kitendo sisi kama wanadini tunakipinga....hayo ni maovu. Tunasema kwamba mwanamume hamwoi mwanamume mwenzake. Humwoa nani ? Mwanamke.
17. Wanasema: “Lakini tutatambulika vipi ? Sisi washoga tutatambulika vipi”? Wakaibua mwenendo. Unajua wao wanapopiga vita jambo hufanya hivyo kupitia mafunzo ya kiutendaji. Kutahamaki yule changu doa anayejiuza usiku na yule anayejiuza mchana wote wana alama inayowatambulisha. Ukitaka kumnunua huulizi. Wanaume wa Uingereza, wa ulimwengu wa kimagharibi wote wakazindua sera yao na kusema kuwa yeyote anayeiunga mkono tutamtambua kwa mtindo wa kushusha siruali (pull down)...kutahamaki vijana... wa shule za msingi...upili...vyuo vikuu wote siruli zao zikashuka chini.

18. Mtoto anakuja nyubani hali ya kuwa amefura. Lakini mzazi husema tu kwamba: "Wenzangu... leo hii, wenzangu hatuna la kufanya. Ah ! Huyu mhuni wangu leo amepiga kamtindo kengine". *Innaa lillahi wa innaa ilaihi raajiuuna*.
19. Angalieni nyinyi vijana mliopo hapa. Msichukue tu Utamaduni wa Kimagharibi...vijana siruali zirejesheni. Zifungieni mahali pake.
20. Waislamu mmezidi sana. Watoto wenu akina Madina huvaa siruali. Mkawaangalia tu pamoja na kuwa nyinyi ni wazazi. Wewe mzazi unamnunulia siruali eti mko katika *outing*…mnawangalia wasichana wakiharibika hamwakanyi.
21. Akina mama tumesema nyinyi ndio mnaoendeleza watu wale…tafadhalini ongeeni nao. Wafunzeni dini hao binti zetu. Hizo *jeans* wanazovaa ni mavazi yanayowaaibisha na kuendeleza maovu.
22. Hiyo ndiyo hali pekee inayofaa. Hali ya kufuata sheria ya Mwenyezi Mungu (SW). La sivyo tutakuwa tukiendeleza sehemu ya Utamaduni wa Kimagharibi…itatuangamiza.
23. Hatutasahau kumsalia mwenye heshima Muhammad (SAW)… Ee Allah msalie Muhammad na aali za Muhammad…

**Khutuba 8**

1. Himdi zote ni za Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu wote. Sala na salamu zimshukie Mtume Muhammad (SAW) na aali zake na sahaba zake. Natoa ushuhuda kwamba hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu.
2. Waja wa Mwenyezi Mungu. Naiusia nafsi yangu na nafsi zenu kumcha Mwenyezi Mungu… "Enyi mlioamini. Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha wala msife isipokuwa mmekwisha kuwa Waislamu kamili"(Al-Farsy, 3:102).
3. Ndugu yangu. Akili yako isikudanganye uanze kutakabari mbele ya Mwenyezi Mungu. Usidhani kwamba una hadhi kubwa sana Mwenyezi Mungu anapokutaka utoe 2.5% kama zaka katika mali yako. Ndugu zangu. Tumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetujalia kuwa Waislamu. Uislamu umekamilika hauhitaji kuongezea mambo kadhaa wa kadhaa.
4. Mwanadamu anapaswa kuutambua huo mfumo na yeyote anayeuacha hupotea. Mwacha mpangilio wa Mwenyezi Mungu huwa kaandama njia ya shetani. Ndugu zangu. Ningependa kukujulisheni kwamba Uislamu umekamilka. Yeyote anayeutaka mfumo huu wa maisha

hushikamana na Kur'ani na sunna za Mtume (SAW). Mtume alisema: "Nimekuachieni vitu viwili. Mkishikamana navyo, hamtapotea. Kitabu cha Mwenyezi Mungu na sunna zangu".

5. Kwa nini mnawaoa wanawake na hali shetani ndiye aliyewapeni ruhusa. Unamkuta msichana njiani anaenda shuleni ukamwoa, anaenda ngomani ukamwoa. Mwenyezi Mungu anasema: "Basi waoeni kwa idhini ya mabwana wao na wapeni mahari yao kwa sharia.(Waoeni na hali ya kuwa) ni wanawake wema wasiokuwa wenye kuzini na wanaume makhsusi wa kinyumba)"(Al-Farsy, 4:25).
6. Wapeni mahari yao. Nakutahadharisheni na wanaosema eti ningependa unifundishe Kura'ni ili iwe kama mahari yangu. Mimi nimejifunza Kur'ani kwa miaka 20 na siijui yote…mwanamume aliyesoma Kur'ani ikawa kama mahari kwa mkewe, Mtume kwanza alimtaka atafute kitu cha thamani. Aliposhindwa akaambiwa atoe pete hata kama ni ya chuma. Aliposhindwa kupata kitu chochote, ndiyo akamruhusu kuoa kutokana na Kur'ani anayoijua.
7. Uislamu una sheria. Hakuna jambo ambalo Mwenyezi Mungu hakulitaja katika Kur'ani. Ulizeni wanazuoni ikiwa hamjui. Hivyo ndivyo mnavyopaswa kufanya. Mwenyezi Mungu anataka uwe mwaminifu katika kuuza na kununua na uwe na huruma. Ukiutupilia mbali huo mwenendo, watu watakukimbia.
8. Waislamu huipeleka kodi ya VAT wenyewe lakini zaka hawaitoi.
9. Nawashukuru Waislamu waliozunguka wakazifanyia kazi mizani ili kuhakikisha kuwa ni nzuri. Kuna aliyesema: "Shekhe mnatuingiza katika hasara". Nikamwambia hasara ni zile gramu ulizozipunguza na utakuja kuzilipia.
10. Nakutahadharisheni na sheria ambayo wanaenda kuipitisha bungeni yaani 'Domestic Relations Bill". Tuliwambieni kwamba oeni mke wa pili kabla ya kupitishwa kwa sheria inayohusu ndoa mkatushtaki kwa wake zenu. Nakwambieni: "Oeni kabla haijapitishwa. Lakini zingatia kigezo cha uwezo. Ukiwa hujiwezi, acha".

**Khutuba 9**

1. Namhimidi Mwenyezi Mungu (SW).
2. Tukitaka kunusurika kwanza tumuamini Mwenyezi Mungu (SW). Tusipofanya hivyo hatima yetu itakuwa kuangamia.
3. Mwenyezi Mungu kaanda moto wa jahannama, nao uko hapo ukitusubiri.

4. Mweyezi Mungu ametupa nyoyo lakini watu wengi hawazitumii kutafakari na kujiuliza ilikuwaje nikawepo?
5. Wengi wetu tumemwasi Mwenyezi Mungu, hatumwabudu, hatumtii ukakuta kwamba hali zetu si za Uislamu.
6. Waweza kumwona Mwislamu na hali yake wallahi si ya Uislamu.
7. Lakini Mwenyezi Mungu alitujalia nyoyo hizo kusudi kila mmoja wetu atafakari, atambue ni wapi alikotoka na kuwa alivyo alipitia katika njia gani ili akawa jinsi alivyo?
8. Kama mwanadamu angezingatia jinsi alivyo na wapi alitoka wallahi kusingekuwa na mtu yeyote anayemwasi Mwenyezi Mungu.
9. Wallahi. Mchakato alimopitia mwanadamu na alimotoka ni kutokana na maji. Mwanadamu alitokana na maji yasiyokuwa na thamani. Maji ambayo yangawekwa kenye chombo ukatakiwa kuyanywa usingethubutu kwa sababu yanaonekana vibaya.
10. Mwenyezi Mungu ametenda mengi lakini hatujali kupata funzo.
11. Kuna wenzetu mliosikia kwamba wamefariki lakini hakuna kati yao aliyekuwa na habari kwamba kifo hicho kingetokea. Ungaliona jinsi walivyofishwa na Mwenyezi Mungu wallahi ingalikutoshelezea kupata funzo.
12. Waja wa Allah. Tumcheni Mungu… aliwafunika na udongo wote wakaangamia.
13. Kama tungekuwa wazingatifu, msikti huu ungejaa Ijumaa hii. Kwa sababu wenzetu walikufa kwa namna ambayo haikueleweka na Mwenyezi Mungu hakumshauri mtu yeyote.
14. Kaka zetu na dada zetu wamepotea…Mwenyezi Mungu walimpiga kisogo kitambo. Nguvu za Mwenyezi Mungu hawazitambui.
15. Utakuta vijana wengi wa zama hizi hawatilii maanani swala la kumwabudu Mwenyezi Mungu. Hakika Waislamu walioko katika eneo hili kulingana na idadi yao msikiti huu ungejaa.
16. Vijana wengi hawajatambua jukumu lao na kwa nini Mwenyezi Mungu aliwaumba. Nina hakika katika eneo ambamo Mwenyezi Mungu alifikisha balaa, kuna Waislamu ambao hawakwenda kusali ijapokuwa wameshuhudia matukio ya kutisha.
17. Mwenyezi Mungu amekujaalia macho mawili ili uweze kuona kizuri na kibaya …halali na haramu.
18. Ni vipofu wangapi ambao wamenyimwa neema hiyo lakini wewe Mwenyezi Mungu akakujaalia kuona.

19. Masikio, Mwenyezi Mungu ameyajaalia kuwa yenye manufaa kwetu… ili usikie maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake. Unasikia kwamba Mwenyezi Mungu kakataza jambo fulani kama vile zina lakini wewe unaendelea tu. Wewe na yule ambaye hakusikia ni sawa.
20. Wengi wetu wa zama hizi tunaepukana na halali na kufanya haramu. Mwenyezi Mungu atatuadhibu.
21. Wewe kama mtu aliyepewa akili ndiye unatakikana kuwa na udhibiti juu ya mnyama lakini sisi twatenda madhambi kuliko wanyama.
22. Mwenyezi Mungu atatutoa katika ardhi hii na atakuja kutulipa kulingana na matendo yetu

**Khutuba 10**

1. Sifa timilifu ni za Mwenyezi Mungu mwenye uwezo.
2. Enyi wanafunzi mnaohitimu kesho, baadhi yenu, mkiwa hapa mlikuwa mkiona kwamba uhuru wenu umekaliwa. Uhuru wa kutotaka mtu yeyote kuwaamsheni kwa ajili ya kusali sala ya Subhi. Tena mliona kwamba vipaza sauti huwapigieni kelele. Mlikuwa hapa mkichukia mtu yeyote anayekuamsheni kutoka usingizini, mkitaka mlale hadi pale jua linapochomoza mwende kwenye mihadhara. Mlikuwa hapa mkitwambia kwamba tumekuchelewesheni. Mwataka kutoka mwende mkafanye kazi. Hebu twambieni! Uwanja mmeukutaje? Hamkukuta mambo yakiwa yamebadilika? Mlikuwa mkifikiri kuwa watawapeni kazi kutokana na stahili zenu. Kutahamaki mkapata habari tofauti. Ni "Mtoto wa nani" siku hizi ndiye hufanya kazi. Dhuluma imekithiri huko nyanjani mliko. Mmerudi leo ili kesho tukukabidhini shahada zenu mwende mwone namna ya kumudu maisha katika dunia hii.
3. Enyi wasichana mnaohitimu kesho! Twambieni ni nini mlichokuta huko nyanjani? Kuna nini huko? Mlipokuwa hapa tulikuwa tukikufunzeni sheria ili mvae ipasavyo. Baadhi yenu mliona sheria hizo kama ukaliaji wa uhuru wenu. Tena mkaomba mhitimu mapema mwende mkavae jinsi mtakavyo. Wakati mlikuwa huko, mlikuwa mkivaa namna gani? Twambieni uhuru wenu mlioutumia, mkatembea jinsi mlivyotaka mmeuonaje? Mkienda kule kutafuta kazi mlizokuwa mkitafuta, mmezipataje? Hamkuona kwamba baadhi ya watu, mabwana zao hupenda kuwapa kazi baada ya kutekeleza mambo fulani?
4. Dunia imeharibika. Wanadamu hawapendi kujua mambo ya dini yakoje? Lakini sisi kesho tukikuageni twakwambieni: "Nendeni mkabadilishe. Kuweni ngangari ili kudhihrisha

kwamba kijana Mwislamu anaweza kusimama imara akawa na mchango katika kuleta mabadiliko. Sisi tumekukabidhini kwa Mwenyezi Mungu. Mkiamua kutoka katika mikono ya Mwenyezi Mungu, tokeni kwa hiari yenu. Lakini sisi yale tuliyokuwa tukikuelimisheni hapa, yale tuliokuwa tukikufunzeni hapa, tulikuwa tukimiminia elementi ya *tawhidi*. Mcheni Allah katika yale myatendayo. Tulipokuwa tukikupeni mafunzo, tulikwambieni: “Jikimuni wenyewe bila kuogopa lolote”.

5. Enyi wanafunzi mnaohitimu, tunapokuageni tunakuusieni kumcha Mwenyezi Mungu. Kesho tutakukabidhini shahada zenu. Ziangalieni vizuri kwa sababu baadhi yenu hamzisomi ili kuona yaliomo. Shahada zenu zina jina la Allah (SW). Kuna tamko la Bismillahir Rahmanir Rahim. Naye Chansela wa Chuo hiki anapokukabidhini hizo shahada, husema Bismillahir Rahmanir Rahim.
6. Wanafunzi wa ndaki ya sheria, kesho tukikuageni twasema Bismillahi nendeni mkabadilishe mambo. Kuwa mwanasheria haina maana kwamba uwaibie watu. Kuwa hakimu haina maana kwamba uuombe mlungula. Nendeni mkabadilishe ili maskini naye apate kushinda kesi. Tunapokukabidhini shahada kesho twasema nendeni mwathibitishie watu kuwa kuna tofauti kati ya mwanafunzi aliyesomea sheria katika chuo hiki na aliyesomea katika chuo kingine.
7. Wanafunzi wa sayansi tunakukabidhini shahada ambazo zina Bismillahi tukikwambieni kuwa miitikio ya kemikali haitoshi.Wengi wenu mnafikiri kwamba ukijumlisha hiki na kile unapata matokeo.
8. Wanafunzi wa kompyuta tunakukabidhini shahada ambayo ina Bismillahi tukikuarifuni kwamba kompyuta si kitu cha mwisho. Kuna aliye juu ya kompyuta . Naye ni Allah. Lakini mkifikiri kwamba ukijumlisha hili na lile utakuwa umemaliza, ndugu yangu hakutakuwa na tofauti kati yako na yule aliyetoka katika taasisi nyingine.
9. Wanafunzi wa ndaki ya elimu za kijamii, mnayosoma huwahusu watu, hali ya maisha ya kila siku. Tunakukabidhini shahada iliyo na Bismillahi tukikwambieni nendeni mkahakikishe kwamba kuna amani, maendeleo na utengamano duniani.
10. Wanafunzi wa ndaki ya Uongozi, mnasomea biashara, mkasomea uchumi ambao leo umekuwa tatizo sugu. Wakaguzi wa vitabu, kwa nini wanafikiri kwamba wao ni werevu sana? Lakini sisi tunapokukabidhini shahada twasema: “Nendeni mkawambie watu kwamba kuleta tu stakabadhi haitoshi. Kwamba accountability huifanyii bosi wako. Unaifanyia Mwenyezi Mungu ambaye hukuona ingawa wewe humwoni.

11. Wanafunzi wa ndaki ya masomo ya Kiislamu, nikwambieni nini? Hamjui kwamba jukumu ambalo ni kubwa kabisa ni juu yenu? Hamjui kwamba nyinyi ndio mnastahili kuwa mfano bora kwa watu wengine? Mnapotoka twakwambieni jambo moja kwamba: "Kuweni mfano bora.". leo hii watu wana namna wanavyowachukulia waliosomea dini. Baadhi yao hufikiri kwamba mmesoma lakini hamtopata kazi ya ajira. Wahakikishie kwamba Mwenyezi Mungu ndiye anayewapa watu kazi.
12. Nikikuageni enyi wanafunzi wanaohitimu kesho, nasema nendeni mbadilishe mambo. Mkathibitishe kuwa Uislamu hutawala. Mkifanya hivyo, Mwenyezi Mungu atakurahisieni hali. Mkikataa, Mwenyezi Mungu atakuondoeni kisha awalete watu ambao watayaweka mafundisho ya Uislamu vitendoni. "Na kama mkirudi nyuma mkaupa mgongo Uislamu, Mwenyezi Mungu ataleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi"(Al-Farsy, 47:38).

**Khutuba 11**

1. Himdi zote ni za Mwenyezi Mungu aliyeandika kwa viumbe wote kuondoka na kupotea kabisa. Watu miti na majabali vyote vitakufa.
2. Nakuusiyeni na nafsi yangu kumwogopa Mwenyezi Mungu.
3. Ramadhani yakaribia kuondoka . Itashuhudia mbele ya Mola . Itatoa ushahidi juu yako. Ikiwa nia yako ilikuwa Ramadhani iondoke nirejelee vitendo vyangu, itatoa ushuhuda.
4. Tusighafilike na dunia. Tufanye yale yanayomridhisha Mola. Si kuabudu Mungu katika Ramadhani tu.
5. Ikiwa ni kusengenya basi hakuna saumu.
6. Furaha kubwa ni kwa yule aliyezuia nafsi yake kufanya mambo ya maasia.
7. Ramadhani imeenda. Huwezi kupata tena fadhila. Unakunja tu mikono hutaki kutoa kusaidia masikini, vilema wako hapa.
8. Mtume amesema: Yuko mbali yule ambaye Ramadhani humjia na asighufiriwe madhambi yake.
9. Yu mbali mwenye kutia nia ya kurejelea maasia. Utakuta wanacheza kamari, wanakunywa matembo.
10. Adhabu kali ni juu ya yule aliyetupa sheria na haki za Mwenyezi Mungu katika mwezi wa Ramadhani. Wewe walala fofo. Katika misikiti hakuna watu wenye kufanya ibada.

11. Ikiwa yule aliyeua watu 100 alisamehewa akapata tauba, basi itakuwaje wewe ?
12. Siku ya idi unakwenda resort kunakouziwa tembo kutolea Idi kule na Ramadhani ulikuwa ukiabudu Mungu. Unaabudu Mola wangapi ?
13. Uganda yetu hakuna kutembeleana. Kila mtu anamenya vitu vyake na watu wake.
14. Toeni zakatul fitri. Saumu haiendi kwa Mwenyezi Mungu mpaka uitolee zakatulfitri. Huning'inia mbinguni. Ikiwa una *vijanjaro* uza upate pesa umpe thamani ya kilo mbili na nusu ili mtu asinung'unike na saumu yako ikaning'inia. Mtume alifaradhisha zakatul fitri. Wanazuoni walisisitiza kuwa ikiwa una nguo, uza utoe zakatul fitri.
15. Tukiomba dua, watu wengine hawainui mikono. Wanakaa kwa kiburi tu. Wameambiwa msiinui. Hamtaki kuitikia amina. Ikiwa Jibril alitaja kuwa mtume aseme amina, wewe ni nani?
16. Huisha usiku wa Idi ujitayarishe kuwatembelea Waislamu. Mchunge mayatima. Mwepukane na mambo ya bidia na maasia.
17. Mfunge siku sita baada ya Ramadhani. Hapa pana matatizo kwa mashekhe wa kisasa. Wanasema unaweza kufunga leo kesho ukaacha. Hesabu itakuwaje sita?
18. Tena mmesoma Kiarabu. Hamna elimu. Hamjui Kiarabu . Mtume anakufunzeni Kiarabu. Soma vizuri Kiarabu. Kama ulisoma Makka au Madina shauri yako.
19. Msipoteze watu. Tulienda radio kuwafundisha watu dua katika swala. Hutaki watu waitike amina. Unasema swala *eweddewo*. Shetani we! Kila kitu ni bidia!
20. Miaka miwili mbona unakwenda Madina…unataka kuwapoteza watu… miaka miwili ni ya lugha tu. *Fiqhi*, *tawhidi* na kadhalika inataka miaka 14.
21. Waislamu wa Raudha tuwe kitu kimoja. Fitna hazituhusu. Tunatumiwa maspy.
22. Msitutie kwenye fitna. Acha tuwaombee islahi. Ukitutia kwenye fitna utapigwa na *nuclear*. Miaka 4 mwanamke ananikoroga…muulize. Mtapata habari…kapigwa na nuclear sasa si Headmistresss tena bali ni mwalimu tu. Subiri, msituletee fitna…mtapata cha mtema kuni. Mtasema Shekhe niombee, niombe yaongezeke.
23. Ikiwa hakuna dua, miskiti imebomoka.

**Khutuba 12**

1. Sifa njema ni za Allah ambaye ni mmoja, hana mshirika.
2. Ukiona mtu haoni haya katika matendo yake, ujue kuwa ni ni dalili ya kutokuwa na imani.

3. Hata wewe mwenyewe una mizani yako inayoonyesha iwapo umiongoni mwa watu wa motoni au peponi.
4. Wewe unapenda mtume atoke kaburini ndiyo uamini?
5. Unafikiri mmomonyoko wa udongo uliotokea Bududa hauwezi kutokea hapa?
6. Mwenyezi Mungu kufanya hivyo...amekuwacha wewe ili upate kuamini.
   vijiji vitatu vikateketea... unafikiri walijitakia?
7. Muda wa ibada ukifika, unasema huna wakati. Na hao waliokufa hawakuwa na wakati.
8. Wengine walifariki na ng'ombe wao, mali yao iliyokuwa ikiwashughulisha.
9. Yapasa tumwamini Mwenyezi Mungu imani ya kweli sio imani ya ujanja.
10. Watu wamekufa kwa ajili ya ukafiri.
11. Maskini kidogo ulicho nacho, mpiga ramli anakudaganya na kukichukua kwa kutomwamini Muumba wake. Hajui kuwa mbadilishaji wa hali ni Mwenyezi Mungu.
12. Ukiona mtu anatenda amali yake kutokana na hali, ujue kwamba hajamwamini Mwenyezi Mungu. Moyo ni kama sponji, ukiwekacho ndanimwe ndicho ukikamuacho.
13. Tofauti kati watu wa zama hizi na wa zama za kabla ya mtume ni kuwa wao walikuwa wakiabudu masanamu na siku hizi watu huabudu teknolojia.
14. Yapasa mtu atambue kuwa Mwenyezi Mungu ndiye huwafaa na sio pesa na shamba.
15. Mwanadamu hutamani kuwa na pesa ili astarehe, lakini akizipata shida huongezeka…waona wanaoanguka kutoka katika ghorofa na kujiua.
16. Muumini hutayarisha kaburi yake na kujiandaa kabla hajawekwa ndani yake.
17. Huyo ndiye aliyepumzika. Lakini wewe huamini. Wakasema umepumzika! Uongo.

**Khutuba 13**

1. Tunamsifu Allah na sifa zake kamili ambaye ni ana uhai wa daima dawama.
2. Mcheni Allah na siku ambayo tutakuja kukutana naye.
3. Wapaswa kupata mafunzo juu ya maisha hayo ewe anayenisikiliza. Kabla hujaingizwa kaburini.
4. Kaburi ni nyumba ya kipekee ambayo hupenda amali nzuri usiyoijali katika maisha yako ya dunia.
5. Kifo ni chombo cha kunywea maji. Kila mtu atakunya kwacho.

6. Wewe unakwepa kifo. Ukajiona shupavu lakini mtume (SAW) amesema kwamba utaonja kifo.
7. Asubuhi kucha, mchana kutwa, kila wiki hakuna siku ipitayo pasina kumzika mwenzetu ambaye kaitwa na Mwenyezi Mungu.
8. Wallahi twashinda katika dini ya Uislamu kwa majina tu. Mtu anashinda na hali hataki kusali, hataki kufunga, hataki kutoa zaka, hataki kuhiji ingawa ana pesa…akawa Mwislamu kwa jina lakini matendo yake hayarandani na dini.
9. Umbeya umeharibu sana jamii ya Kiislamu. Mtu hutoa huku udaku na kuupeleka kule kuwagombanisha watu.
10. Utajibu nini wewe asiyemtambua Mwenyezi Mungu na ukipata shida unawaendea washirikina au ukipata masaibu wakimbilia kwa Muswezi eti watafuta nguvu zinazozidi nguvu za Allah ?
11. Kuna wale watakaofufuliwa wakiwa wamevishwa picha za kima kama wale walioko Busitema. Hao ndio walikuwa hawang'atuki panapokuwa mambo ya zina.

**Khutuba 14**

1. Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu(SW)… sala na salamu zimshukie mtume wake Muhammad (SAW).
2. Enyi mlioamini mcheni Mwenyezi Mungu ipasavyo wala msife isipokuwa mkiwa Wenye kujisalimisha (mbele ya Mwenyezi Mungu)…mcheni Mwenyezi Mungu mkiwa peke yenu au kati ya mkusanyiko wa watu.
3. Watu humpenda sana shetani Ibilis kuliko Allah aliyewaumba.
4. Mjinga mmoja alisema ni vizuri kuongea na shetani umjuaye kuliko malaika usiyemjua. Mtu huyo ni shetani. Watu hao mnawajuwa. Huandika hirizi.
5. Unaenda kwa mganga akakwambia akukinge. Akakupa majini, akakupandia majini njiani, akakukata chale ili kukukinga. Mwenyezi Mungu anasema: Nyinyi mlimfuata shetani, mkaenda kuabudu *basambwa*, jitengeni.
6. Basi wewe mwenyewe amua. Umemfahamu *khannas*. Nimeitafsiri sura hiyo katika Kigisu cha Manjia. Kama hutoondokana na shetani… motoni.

7. Tumembaini shetani aliyelaaniwa, Ibilis. Lakini waumini wameshindwa kutofautisha kati ya Allah na shetani.Unamkuta mtu anachanganya. Na yeyote anaye changanya, ameacha Uislamu.
8. Wanamanjia mmekataa kuwatahiri watoto wenu! Mnasubiri wakue mfuate shetani? Mko hapa. Mwavaa kofia lakini mtoto mtampeleka kwa wajomba ili wawazawadie, ucheze. Ni nini kinachotufanya hivyo? Shetani.
9. Mko hapa. Mwavaa kofia lakini mtoto mtampeleka kwa wajomba ili wawazawadie, ucheze. Ni nini kinachotufanya hivyo? Shetani.
10. Isipokuwa tukitubia … tukikataa tutaonekana kama Waislamu lakini Uislamu hakuna. Twafuata Ibilis.
11. Kuna walioenda Mutoto wakiwa wamevaa kofia. Shetani kutoka Kenya akajitambulisha na kuwatambua wafuasi wake. Ni kama Yule aliyekuwa katika kikao cha Makureishi. Mutoto hamkuenda kuona kitu isipokuwa Ibilis na watoto wake wengine.
12. Mwajua *kumwanda*? Mliwarushia vijana pombe?Acheni hayo. Ukisema hutocheza lakini utaenda tu kwa wajomba wakurejeshee ng’ombe angalau mmoja. Hiyo ni shiriki.
13. Mshirikina akimchinja mnyama hatumli.Umepewa chungu.Umepewa majini. Una *sumbati, kumwendo,* ukienda kwa shekhe wa Tarafa ukitaka kuozeshwa, hatukupi. Ukifanya nikahi kama hiyo, itabatilishwa. Mwanamke akiamua kwenda kuhudhuria sherehe, wewe ukiwa na imani, nikahi hiyo ni batili. Wewe ukishiriki katika kumwendo...sumbati, hatukuoshi. Mkimkafini katika nguo hizo mtakuwa mmemkafini katika sumu. Mshirikina hatumziki kwenye makaburi ya Waislamu.
14. Maimamu, kwa vile twaonewa, mnatuita tuwaombee dua: “Eh Mola mghufirie”.
15. Waislamu! Tuko katika mwezi wa Ramadhan. Tubuni. Ukikataa, utaingia katika moto wa jahannama

**Khutuba 15**

1. Namhimidi Allah aliyemtuma mtume wake na uongofu na dini ya haki.
2. Mwenyezi Mungu ndiye mlezi wetu. Hutulea kwa neema zake…
3. Muumini akitoka katika nyumba yake husema: “ Kwa jina la Mwenyezi Mungu. Namtegemea  Mwenyezi Mungu. Hakuna mwenye uwezo wala nguvu isipokuwa Mwenyezi Mungu”.

4. Leo tutajifunza kuhusu shiriki ambayo mababu zetu walikuwa wakifanya. Na sisi watoto, wajukuu, na vitikuu tunaifanya. Ukilinganisha kipengee cha utamaduni wa Wagisu cha imbalu utakuta kwamba kwa namna fulani kinafanana na kile cha Uislamu. Wamasaba hutahiriwa na Uislamu huamrisha kufanya tohara watoto wakiwa wadogo.
5. Waislamu wengi tumeuweka kando mwenendo huo. Sisi tumewakomaza watoto na kukataa kuwatahiri wakiwa wadogo.
6. Kwa nini Waislamu hawafuati mwenendo wa Uislamu? Wanasema: "Siwezi kuruhusu mtoto wangu atahiriwe kwenye mgomba. Siwezi kumtahiri akiwa mchanga. Akitahiriwa huenda asibarikiwe…tangu jadi sisi tunacheza ngoma". Mmeamua kuwafuata babu zenu na baba zenu na hali hawakuwa wakifahamu chochote.
7. Si vyema kusilimu mwaka mmoja ukakufuru mwaka mwingine. Tulikuwa katika mwaka ujulikanao kama mwaka wa wanawake. Sijui nani aliuita hivyo? Katika Uislamu tunaambiwa kwamba miaka ni 12 na hakuna mwaka ambao unarejelewa kama wa wanawake.
8. Wakati huu Waislamu wanatazamia. Wapoangalia utumbo wa mbuzi hutoa utabiri iwapo kijana atastahmili maumivu ya kisu cha ngariba. Kitendo hicho ni cha kumshirikisha Mwenyezi Mungu.
9. Ndugu zangu. Hivyo vitendo si vya Kiislamu. Haifai kufika sasa kama hatujatubia kutokana na madhambi.
10. Wazee wetu sasa hawapo. Lakini sisi watoto wao ni nini tunachopaswa kufanya? Lazima tufanye tauba kisha tumwombe Mwenyezi Mungu awaghufirie wazazi wetu madhambi yao na siyo kusema kwamba tutafanya kama baba zetu walivyokuwa wakifanya.
11. Tukikataa basi ngojeni. Mwenyezi Mungu atakushika kwa nguvu...nguvu zako zote ambazo zilikudanganya ukaasi zitakwisha malaika atakapokutoa roho...
12. Watakuweka katika kaburi yako ulazwe kwa upande mmoja, wakufukie udongo kisha wakuache. Mwenyezi Mungu aseme: "Mmetujia na hali kila mmoja wenu yu peke yake kama tulivyokuumbeni mara ya awali".

**Khutuba 16**

1. Nimemhimidi Allah (SW) katika khutuba yetu ya pili katika mwezi wa showwaal mwaka wa 1433H. Kama mlivyosikia, kila sifa njema ni za Allah (SW) ambaye alimwumba mwanadamu akamfunza yale anayoyajua na asiyoyajua.

2. Waja wa Allah. Nakuusiyeni, nikiiusia nafsi yangu vilevile, kwani mimi si mbora kuliko nyinyi. Tuungane katika kumtii Allah (SW), kumcha Allah (SW). Kwa sababu tumo katika wakati mgumu.
3. Mwislamu, kila asubuhi, Mwislamu ana jambo. Butiru, mahindi. Nakhupa, mahindi. Wenye maghari, usukani. Walioko mashambani nao hivyo hivyo. Walioko madukani nao hivyo. Kila mtu katika kazi inayomghuri ukawa humwabudu Allah. Ndiyo maana Allah akasema: " Wana nyoyo laklini hawatambui kwazo".
4. Lakini kwa vile Allah ameuandaa moto kwa ajili ya nyoyo zisizofikiria juu ya miili, Waislamu wote walienda pale kanisani. Na tulipokuja kusali hapa, tulikuwa hapa na mweka hazina na kijana Yasin. Tukasubiri, tukisema tutasali saa nane. Kwa nini hawana nyoyo zinazofikiria juu ya miili yao? Kwa sababu waliona kwamba mtu amefariki. Hilo mlikuwa mkilichukulia kuwa jambo kubwa sana na hakuna aliyeijali ibada. Mlichukulia maiti kama ibada kuu.
5. Lakini watu hawawezi kuangalia ni wapi tunapomweka mwenzetu na zama hizi, mtume (SAW) amezizungumzia na kusema kwamba: "Akhiru zamani itakapofika, watu watawasahau wafu wao". Watawatupa tu huko wafu wao wawasahau. Sasa Yule jana tulimzika na ukimwuliza Mwislamu: "Domiano je?" Hamkumbuki tena. Hakuna funzo mlilopata kutoka kwake wala kujiuliza, Allah amemtoa hapa, amampeleka wapi? Ameenda na nini? Tukienda kwenye kaburi, kwanza pateni funzo huko. Mwenzetu tuliyempeleka kaburini ameenda na nini?
6. Lakini mnakazania sana dunia, lakini wallahi wanakubembeleza ulete mfuko mmoja tu wa simenti msikitini, maneno yakaanza kupishana hivi. Ndiyo maana Allah anasema: "Mnakazania sana dunia". Nguo zimejaa masandukuni, vyakula mnakula na kutupa huku majirani zenu wakilala na njaa. Mnajenga majumba yanayong'ara. Waislamu mnastahiki kukaa kwenye vumbi. Mna macho. Mwaona msikiti wenu. Lakini hamwezi kununua mazulia. Mwasubiri: " Haji wa Kampala atatununulia". Lakini mwakazania nyumbazenu. Kila mtu aliopo hapa, analala kwenye godoro la six by six. Mablanketi maridadi. Si afadhali kama mngenunua hayo mkayapeleka msikitini tukasalia juu yake. Mwakazania sana dunia lakini kwa Allah mtapeleka nini?[kimya] Wewe na mimi aliopo hapa ni nini utakachoonyesha kwamba nami nilikazana.

7. Unakuwa na fikra mbaya juu ya wenzako, ukajiona kuwa adhimu sana ukawa sharia za Kiislamu, tena moyo huo ndio unaokufanya utembee katika ardhi kama, hata ndege ni bora kuliko wewe. Kwa sababu hutambua kwamba nikienda malishoni, nitarudi nilale kwenye mti wangu fulani.
8. Waislamu wengi mna fikra mbaya kwa sababu mtu akienda kwenye maiti, kama yule aliyefariki jana, ukakaa huko bila kusali sala ya dhuhuri, hizo ni fikra mbaya za ukafiri na ukitaka kufanya jambo lolote ili wakusifu, ukifikiria kwamba uchifu utaupata kwa kusema Bwana asifiwe, Allah atakupa. Ukiona kuwa usipotaja jina la Patiri hawatakupenda, basi Allah atakujaalia wakupende. Lakini siku ya kiyama utakuja kueleza hilo jina la Patiri ulilitaja kwa nini?
9. Unataka waje wakuhimize tu, wakwambie leo njoo usali Aswir? Ni juu yako. Unataka wakukumbushe, waja wa Allah kwamba leo Sali dhuhuri? Unatenga moyo wako na Allah na hali hujui unaenda wapi? Katika dunia hii hatujui tulilokujia? Waja wa Allah. Acheni mchezo mlioucheza zamani.
10. Akauntabiliti imetufikia naona kila mtu ana faili lake mkononi. Lakini kila mtu yu mchezoni. Tukisikia kwamba fulani amefariki, tunajifanya wanaolia sana, lakini hatujui kwa nini Allah amemchukua. Bali twaomboleza “amekufa akiwa mdogo sana”. Wewe ulitaka afe akiwa mzima?
11. Husema wanaosali ni watu wa chini wasio na chochote. Ah! Mwenye ng’ombe hasali. Ng’ombe watapelekwa malishoni saa ngapi? Mwenye gari hapaswi kusali. Biashara itasimama. Mwenye duka hapaswi kusali. Kwani wanaosali ni wasiokuwa na kazi!
12. Nami nitaulizwa juu ya uchungaji wangu. Lakini kusimama kama mlivyofanya jana, mnafanya nini katika Uislamu? Haifai kuimba nyimbo halafu wakaja msikitini tukasali nao. Haifai Mwislamu asiyesali kutangamana na Mwislamu anayesali kwa sababu si muumini.
13. Tuache mchezo Waislamu… Tulikuwa hapa katika mwezi wa Ramadhani tukisema: “*Allahumma innaka afuwwun tuhibbul afwan fa’f annaa*”. “ ewe mola. Wewe ni mwingi wa kusamehe. Wapenda sana kusamehe. Basi twaomba utusamehe.”Sasa safu haifikishi watu kumi.
14. Utashangaa kufika mbele ya Allah ukiwa huna tendo zuri hata kidogo. Ndio hao watakaokuja wakiwa wameinamisha shingo zao Allah anaelezea juu yao anaposema: “Msinilaumu zilaumu nafsi zenu”. Ndio maana baada ya viungo kutoa ushahidi juu ya mwanadamu, utupu

utakapotoa ushahidi juu ya jinsi mwanadamu alivyozini, mikono itoe ushahidi juu ya jinsi alivyokuwa akiiba na kuua, mdomo utoe ushahidi juu ya jinsi ulivyowatukana watu na kudhulumu na kutoa ushahidi wa uwongo, miguu itoe ushahidi, ndipo Allah atakapouachilia mdomo useme: “Enyi viungo vyangu! Kwa nini mmetoa ushahidi juu ya maisha yetu?” Viungo vitasema: “Mwenyezi Mungu aliyejaalia kila kitu kutamka ndiye ametutamkisha”…

15. Kwa hiyo Waislamu wa Lwakhakha, tujitahidi kusali. Tukisha Sali kuweni na nyoyo zinazotoa sadaka. Kile unachotoa ni chako utakikuta katika kaburi yako. Angalia jinsi tunavyokaa waja wa Allah! Mwislamu mmoja aliniambia: “Kwa nini huji mapema ukaupiga deki msikiti. Nimekaa kwenye vumbi. Kanzu yangu!” Nikamwambia: “Hivyo ndivyo Allah alivyopanga. Wewe nyumbani kwako unatandika mablanketi ya thamani, hujali kununua mkeka wa shilingi elfu tano ukautandike pale! Vumilia shida hiyo”.

16. Kwa hiyo nakuhimizeni tuchukue ibada tuitangulize kama jambo kuu. Mwislamu, usingekula chakula kama hujasali sala tano. Kuwa mwenye kuidai nafsi yako kwa sababu dunia ni ngumu. Kiama imekaribia kufika. Shurutisha maisha yako, ujiulize: “Je, nimesali dhuhuri”? Ifikapo saa tisa ukakumbuka kwamba hujasali, fanya hima usali.

**Khutuba 17**

1. Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye tunamwomba msaada na kughufuriwa madhambi. Twamuamini na kumtegemea. Twajikinga na Allah kutokana na shari ya nafsi zetu na ubaya wa amali zetu.
2. Waislamu wengi mara nyingi huipiga chenga sala ya Juma wakakataa kutekeleza ibada. Hali kama hiyo si nzuri. Mtu anajifanya mashghuli wiki nzima hata wakati wa Juma akaikosa sala. Hiyo ndiyo Mwenyezi Mungu alisema ni hasara kubwa. Mtu anaweza kupiga chenga wiki nzima hata siku ya Juma. Ikawa kwamba sala zimempita. Akamaliza mwezi hata mwaka anasubiri Ramadhani ikaribie ndio asali.
3. Naiusia nafsi yangu na nafsi zenu kumcha Allah (SW) Muumba aliyetuumba. Kwa nini niiusie nafsi yangu na zenu? Ndugu zangu tunajikuza, tukawa wabishi, tukavunja sheria za Mwenyezi Mungu.

4. Wewe ambaye hujui mipango ya Mwenyezi Mungu. Hujui jinsi alivyokuleta hapa duniani na lini atakapokuchukua. Wallahi ukawa tu hapa wazubaa katika maisha ya dunia mpaka ukarudi bwerere, ukahasirika duniani na ahera!

5. Tulifanya uchunguzi tukagundua kwamba kila mtu analalamika kivyake kulingana na mtihani ambao Mwenyezi Mungu amempa. Uchunguzi unonyesha kuwa kuna wanaosema : ‘‘ Bw. Imam. Mimi nilikuwa nikifanya biashara ile ulionikuta nikiiendeleza. Si imeanguka. Hali yangu si nzuri hivyo. Tena nateseka. Nina shida ya hali ya juu’’.

6. Ndugu zangu. Sikiliza aya hiyo. Baada ya Mwenyezi Mungu kutuumba tukawa hapa duniani, atatupa mtihani katika kila hali. Atatupa mtihani ambao utachukuwa sura ya hofu. Waweza kujiuliza kwamba tena hofu itatokana na nini? Ndugu zetu wa huko Libya wameishi katika hali ya hofu. Hurushiwa mabomu na mtu huwa katika nyumba yake pasina kujua iwapo atakuwa hai au la. Vita vilianzia Misri mpaka saa hii ukitega radio utaambiwa Syria kuna vita vya ndani kwa ndani. Kubadilisha kituo waambiwa kwamba Yemen watu fulani walikuwa mahali fulani na wote wamekufa. Hiyo ni hofu ya hali ya juu. Ukitazama nchi zetu nyingi za Kiislamu huishi katika hali ya hofu. Wanaojua hutambua kwamba Mwenyezi Mungu anasema atatupa mtihani.

7. Tumefundisha hapa tukasema kwamba twajua kwamba Waislamu ambao ni matajiri mpo. Watu wengi wanaomiliki mashine ni Waislamu. Wale wanaofanya biashara ya mpunga ni Waislamu. Fulani anakwambia nina milioni tatu, … mimi nina milioni kumi, Haji fulani ana milioni kumi na tano. Tukafundisha kwamba toeni zaka. Kwa sababu Mwenyezi Mungu amesema kwamba kitendo hicho ndicho kinachoweza kuilinda mali yenu kutokana na huo mtihani. Ni mtu kupiga mahesabu atoe ushuru wa shilingi elfu ishirini na tano kutokana na milioni aliyonayo. Hayo yote tumefundisha lakini Waislamu mwanyamaza tu. Kutahamaki Waislamu waliokuwa na biashara wakawa wameishiwa. Wakaenda kwenye riba wakachukuwa pesa za benki, wakaziweka katika biashara.

8. Nilienda Hamdan Girls nilipopigiwa simu na binti yangu aliyeniambia kwamba wamefiwa na mwanafunzi mwenzao. Nikaenda kumliwaza Shekhe Musa Senyonga kwa kufiwa na mwanafunzi. Nilipofika huko, Shekhe Musa akanisimulia kisa. Mtoto aliugua wakajaribu kumpatia matibabu. Daktari Balyejusa alihangaika kadiri ya uwezo wake lakini hali

ikaendelea kuwa mbaya… Wazazi wa mtoto huyo walipewa taarifa siku ya Juma tatu, akaaga dunia… yule akamwambia mama mtoto: ‘‘Nani alikushauri kumpeleka mwanao katika shule iloko karibu na makaburi?” Inasemekana kuwa yule mama alimwambia mwenye kuleta fitna kwamba: “Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuhuisha na mwenye kufisha”.

9. Sio wale wanaolalamika na kusema: “Ndugu yangu umeniachia nani? Ndugu yangu kwa nini ulikufa? Ni nani atakayenisadia? Huko kwetu huo ndio umekuwa wimbo. Mtu anapofiwa, atawahesabu watu na msipokuwa wavumilivu, fitna itangia. Mtafikiri kuwa anaomboleza kumbe anasema fulani ndiye aliyemwua, lele lele le katika hali kama hiyo. Ina maana kwamba tukiomboleza hivyo tutakuwa hatuujui Uislamu.
10. Watu wengi mnaacha sala eti kwa sababu mmepata mali. Ni bure tu! Ndugu yangu kuna waja wa Allah walioishi katika dunia hii wakiwa na mali lakini mwishowe wakawa maskini. Ndugu zangu hizo ndizo hali tunamoishi. Turejee kwa Mwenyezi Mungu na tutii amri zake.

11. Ndugu zangu Wagisu mnaonisikiliza na nyinyi ambao si Wagisu. Acheni kumchezea Mwenyezi Mungu kwa maandalizi mnayofanya. Wagisu mliopo hapa, nikisimama na kusema aliyewatahiri watoto wake wakiwa wadogo anyooshe mkono unaweza kutompata. Kwa nini ? Wanasubiri. Wanasema lazima nifuate mila ya mababu. Siwezi kumtahiri akiwa mdogo ; anaweza kufa.
12. Kuna wakati tulisali Juma katika siku kama ya leo na kesho yake ni mwezi wa Ramadhani. Bwana mmoja alisema: Shekhe tumefanya ushirikina mwingi sana. Shekhe tulikuwa tumeangamia. Kwa sababu uchawi tulioufanya tulipokuwa tukitoka *mwigoya*, haukuwa wa kuchezea. Tazama hali kama hiyo ndugu yangu. Tusipokuonyeni, nani mwengine atafanya hivyo? Ukitaka kunifukuza kutoka katika kabila la Wagisu nimekubali kufukuzwa ; bora niseme ukweli.

**Khutuba 18**

1. Himdi zote ni za Mwenyezi Mungu…
2. Waja wa Allah.Nakuusiyeni kumcha Allah. Msighafilike mkaacha kumcha Allah kwa ajili ya tamaduni zenu.
3. Hakuna hata siku moja ambapo Mwenyezi Mungu ametuusia kushikamana na *kadodi*. Isipokuwa kumwabudu

4. Inakuwaje wewe kila uchao unakaa njiani ukicheza kamari. Mwenyezi Mungu ana kuahirisheni mpaka siku mtakuja kukutana naye.
5. Jiulize una watoto wangapi? Wangapi wanaosali? Umekuja na wangapi? Mtume (SAW) amesema: “Nyote ni wachungaji na nyote mtaulizwa juu ya uchungaji wenu”.
6. Je, unawahimiza watoto wako kusali au unawaacha wachukue ng’ombe malishoni?
7. Mwenyezi Mungu amesema: “Wambie waja wangu wadumishe sala…”.
8. Jambo la kwanza kuhesabiwa juu yake siku ya kiyama ni sala ambayo unaichezea. Sala unayosubiri wakusalie haitokufaa. Baadhi ya watu huichukulia sala kama adhabu. Tumia uvumilivu, mambo mengine uyaache uende ukasali.
9. Yule anayesali kwa ajili ya Allah huwezi kumkuta akiweka sigara mdomoni mwake. Huwezi kumwona akila miraa. Mwenyezi Mungu amesema: “Hao ni kama wanyama bali wao wamepotea zaidi”. Mwenyezi Mungu akimwambia Sali. Husema: “Siwezi kusali”. Akiambiwa funga husema: “Nina vidonda vya tumbo”. Yule ambaye hasali hatokuwa na dalili ionyeshayo kwamba duniani alikuwa akimcha Mwenyezi Mungu. Kumbuka siku hiyo Mwenyezi Mungu atakwambia: “Waite mashahidi wako”. Uwaite lakini hutomwona mtu yeyote, utaropokwa tu.
10. Waja wa Allah. Tujue kwamba tutakuja kuulizwa… tushikamane na mafundisho ya Allah.
11. Akauntabiliti utaifanya mwenyewe. Hata kama watakuja kwenye kaburi wakufunze mara mia…mnasema shida zitakuwa nyingi siku ya kiyama, lakini wanaosali watanusurika.

**Khutuba 19**

1. Hatuna budi kumsifu Allah (SW) na kumsalia mtume wake Muhammad (SAW).
2. Azumzaye huku khutuba ikiwasilishwa, huwa amechezea katika sala na ataambulia patupu.
3. Sala ya Juma ndiyo itakayokuwa sababu ya kufutwa kwa madhambi ambayo ameyatenda mtu bila kutambua maadamu hakumwendea mpiga ramli.
4. Mtu ambaye hukosa kuhudhuria Juma huchukuliwa kuwa mnafiki mbele ya Mwenyezi Mungu.
5. Mtu akikiri kuwa hakuna aabudiwaye isipokuwa Allah…lakini akaacha sala basi naye ajue kwamba kaingia katika unafiki.

6. Mtu anaweza kujifaharisha eti Allah kamjalia wanawake kumbe wamelaaniwa hawasali… na kwamba kajaaliwa watoto kutokana na ndoa yake lakini watoto hao wanashinda katika unywaji pombe, uchezaji kamari na kuvaa mavazi yanayoonyesha sehemu zao za siri…
7. Mtume katumwa kuonya na kubashiria mazuri. Kama si hivyo hizo nyumba maridadi zinazong'ara tungezibomoa.
8. Mtu asiposali huwa ametia doa katika dini yake.
9. Yapasa tuwe wahitaji sana katika kutekeleza ibada na tuache yale yote ambayo yanaweza kutufanya tughafilike.
10. watu huleta video ambazo huwapotosha watoto…wakati wa sala unafika na wao wako kwenye video.
11. Lakini nakukumbusheni siku ya kiyama na yatakayotokea siku hiyo. Tutahesabiwa kisha tupatikane na hatia.
12. Basi ni juu yako wewe mwenye akili kurejea kwa mola wako na utubie juu ya madhambi yako.
13. Mwezi mtukufu ukimalizika unajitosa katika madhambi. Lakini nakukumbusha rejea kwa mola wako kabla mauti hajakutembelea.
14. Hata kama umezama sana katika unywaji pombe, ukitubia na kuiacha Mwenyezi Mungu hukutakasa.
15. Watu wengi hutembea na hirizi, watu wengi hutumia dawa eti kudumisha mapenzi…unamwangalia mtu…wakati wa kupendana hapakuwa na dawa ya kumpa mtu. Badala ya mume kurekebisha tabia yako, unamwendea mpiga ramli eti akufungie mke asikukimbie. Nawe mwanamke badala ya kurekebisha tabia…ukajizuia na kuacha kugombana , unasema yule Bwana dawa yake ilinisaidia.

**Khutuba 20**

1. Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu (SW).
2. Dhulqaada ni mwezi wa furaha. Ni mwezi wa kutoa sadaka na mtu akitoa asidhani kuwa ametolea Sami.
3. Kwa sababu imekuwa ni kawaida watu kufichamana...hawataki kuonekana. Wanajificha huko nyuma.
4. Kuwa *open*. Hutaki kujitokeza mbele kwa kuhofia kutajwa.

5. Huu ndi mwezi pekee wa kuomba toba. Msighafilike katika mwezi huu.
6. Sisi tumebakia kupiga vidole wakati swala ina muda maalum. Wewe muda unaupata wapi wa kumpiga shetani?
7. Watu wamepokea vitabu kutoka Makka na wana hadithi mbili, tatu…wanajifanya mashekhe? Kilicho katika kitabu hicho si sahihi.
8. Inaudhi sana. Watuulize wanazuoni. Watu wamebakia kusoma visirasira?
9. Tusipokee tu. Tuwe na elimu hata ya majini pia. Tuwe na elimu sahihi katika yale ambayo Allah aliteremsha.
10. Kwanza tuwaulizeni hao mashekhe. Hiyo elimu wanaitoa wapi? Ee toba! Tutafuzu kupata radhi za Allah kweli?
11. Tufumbe macho. Tusiudhiane kwa macho, mikono na miguu.
12. Sasa hivi hata pesa zetu si halali. Tunakwenda kuhiji ili tuitwe Haji, lakini una pesa ya halali ya kukupeleka hija? Pesa zetu ni za riba tu. Sijui tunafuzu katika hija. Kupatikana kwa pesa halali katika mazingira yetu ni kazi kubwa.
13. Na hivi sasa kuna watu wanaopeleka watu hija. Yeye mwenyewe si halali na pesa yake si halali.
14. Mbona watu wanakwenda kutembelea makaburi ya Abubakar, Ali na kadhalika halafu wanajiita mahaji. Ikiwa zako si halali basi za kukupeleka zitakuwa halali ?
15. Watu wanaogopa katika mambo ya haki. Kuna mmoja ambaye alikuwa akipita na gari lake. Akiambiwa aje asali, hataki. Anasema kuwa huo ni msikiti wa wazee. Msikiti wa kuomba dua. Lakini alipokufa, hilo benzi ndilo lililomleta hapa na mimi mwenyewe ndiyo nilimsalia na kumweka kwenye mwanadani wake.
16. Mtu anajifanya Shekhe na hajui kitu…hana elimu.
17. Na tuwafanyie wema wazazi wawili, mayatima…msijifiche pembeni. Tuwalishe vyakula na tuamkeni usiku wakati watu wamelala…
18. Tengenezeni vipimo…mizani wallahi tutaangamia. Watu wa mizani Mwenyezi Mungu kashusha aya nzima kuelezea suala la mizani. Ndio sababu tunaendelea kuwa maskini.

## KIAMBATISHO C: MAONI YA MAAMUMA KUHUSU VITENDO NENI VILIVYOJITOKEZA KATIKA KHUTUBA

1. Khutuba si mbaya isipokuwa wakati mwengine hatupati zile zinazowasilishwa kulingana na maendeleo ya Uislamu. Kwa mfano, katika mwezi wa Hija ingekuwa vyema kama wangetusomea khutuba zinazohusu Hija na katika mwezi wa kufunga wafundishe kuhusu saumu ili mtu ajue anachotakiwa kufanya.

2. Sisi kama Waislamu tuna madhaifu. Mtu anasomewa khutuba lakini haitilii maanani. Asipokuja msikitini kwa majuma kadhaa, ikitokea kwamba amehudhuria sala ya Juma na Imamu amegusia kitendo cha kutodumisha sala, hukasirika.

3. Khutuba imenihimiza kumcha Mungu katika matendo yangu.

4. Khutuba ilinifurahisha kwa sababu ilinihimiza kufuata maamrisho ya Mwenyezi Mungu. Tena ilizungumzia mambo ambayo Waislamu huyafanya.

5. Kama khutuba zingezungumzia mambo yanayotokea katika maisha halisi zingependeza.

6. Kulingana na khutuba hiyo, sina budi kufuata mafundiso ya Mwenyezi Mungu ili hali yangu itengenee.

7. Nchini Uganda khutuba imeachiwa Maimamu waamue watafundisha nini. Ijapokuwa kuna Kur'ani, hakuna kitabu kinachoweza kuwaongoza katika utungaji wa khutuba.

8. Wakati mwengine Maimamu hutunga khutuba za kisiasa ambapo wanawakashifu watu. Imamu alisoma khutuba kama hiyo ikabidi Mwislamu mmoja asimame baada ya sala na kumwonya asiwaharibie watu ibada yao.

9. Khutuba hiyo ilinifurahissha kwa sababu ilizungumzia amri za Mwenyezi Mungu na kunihimiza kwenda msikitini kumwabudu Mungu.

10. Mazingira tunamoishi ndiyo huwafanya watu wasitilie maanani mafundisho ya Imamu.

11. Napendekeza kwamba viongozi wa idara husika waandae mwongozo wa khutuba ili Maimamu waweze kutunga khutuba juu ya maudhui maalum kama ilivyokuwa zama za mtume (SAW).

12. Khutuba hiyo imeniachia deni la kulipa. Lazima nijiweke tayari kufanya yale ambayo Mwenyezi Mungu ameamrisha.

13. Mwanzoni khutuba zlikuwa zikinifurahisha sana. Zilikuwa zikisomwa kwa Kiarabu na kutafsiriwa katika lugha zetu. Lakini baadaye Maimamu wakajitungia khutuba zenye maudhui zisizoendana na maisha halisi. Kuna wakati ambapo wanaleta migogoro yao na wenzao hapa msikitini jambo ambalo halifai.

14. Kuna khutuba iliyonikasirisha. Nilisalia Biina Imamu akawakashifu viongozi katika khutuba yake ikabidi nitoke nje na kuacha sala ya Juma.

15. Baadhi ya khutuba zina athari mbaya kwa sababu Maimamu wamepewa uhuru katika swala zima la kuziwasilisha. Ingekuwa vyema kama jopo la wanazuoni wangewapangia maudhui za kuwasilishwa.

16. Napendekeza kwamba anayeteuliwa kama Imamu awe na elimu ya kidato cha sita au chuo kikuu katika mambo ya Uislamu, awe na umri usiopunguwa miaka 18 na pawepo mamlaka inayopitia khutuba. Napendekeza pia kwamba Kiarabu kiwe msingi wa khutuba ingawa tafsiri inaweza kufanyika katika lugha tatu ambazo ni Luganda, Kiswahili na mojawapo ya lugha za sehemu ambapo khutuba inawasilishwa. Anaweza kuchanganya ndimi hizo ili watu wafahamu ujumbe.

17. Khutuba kama hii huwaongezea Waislamu imani na maarifa. Matamko mengi yalikusudiwa kurekebisha maisha ya mwanadamu.

18. Kwa ujumla, ukilinganisha khutuba za miaka hii na za miaka ya 70 na 80, utakuta kwamba Maimamu walikuwa wakiwasilisha khutuba zilizoandikwa. Waumini walizipa heshima ya hali ya juu kiasi kwamba walikuwa wakienda msikitini mapema kabla ya Imamu ingawa wengi wao walikuwa hawajui Kiarabu. Siku hizi hata vijana wasiobaleghe huwasilisha khutuba muradi wawe na elimu jambo ambalo limepunguza haiba ya khutuba. Kwa vile khutuba huwasilishwa tu kwa lugha zetu pasina kusoma maandiko maalum watu hawazipi umuhimu unaostahili.

19. Kwa vile Maimamu huzungumza juu ya mambo yaliopo katika jamii, baadhi ya watu hufikiria kwamba amewalenga katika khutuba jambo ambalo huwakasirisha.

20. Khutuba za zamani hazikuzua athari hasi kwa sababu zilikuwa zikisomwa tu kwa Kiarabu na Maimamu hawakuongeza maneno yao.

21. Imamu akiwa na elimu ya kutosha, hujua namna ya kuwasilisha ujumbe wake kwa sababu anatumia mbinu nzuri. Khutuba hiyo ilikuwa nzuri. Kwa wale wanaomcha Mwenyezi Mungu, khutuba hii imewafaa. Lakini wale wenye kufuata mila hizo wameichukia kwa sababu wanaona kwamba Imamu amewashambulia.

22. Imamu ametuaibisha sana. Hatutorudi katika msikiti wake.

23. Hayo ni matusi. Kwa sababu babu zetu hawakuwa wajinga kama anavyodai. Nao walikuwa na hamu ya kujua ukweli.

24. Tumekasirika sana kwa sababu Imamu hakuchukulia swala la mazishi kama muhimu.

25. Imamu ametudharau. Haifai kuwambia wenzako kwamba hawana mipango inayowafaa.

26. Nimezinduka kutokana na tamko hilo. Kuna haja ya kutilia maanani ujumbe huo ili ninufaike duniani na akhera.

27. Imamu alituudhi sana kwa sababu alionyesha kuwa alifurahikia kuuawa kwa Sadam Husein. Sasa huyo ni kiongozi gani?

28. Lugha yake ni chafu. Hafai kuwa Imamu.

29. Khutuba imedhihirisha kuwa Imamu huyo hana elimu ya kutosha na hataki kuwaonyesha Maamuma kwamba hajui. Ndiyo maana anajificha nyuma ya mashambulizi.

30. Khutuba haikunifurahisha kwa sababu Imamu hakumpa mtume heshima anayostahiki na aliwatukana waumini.

31. Ni dhahiri kuwa Imamu alitapatapa muda wote wa khutuba. Matamko yake yamekuwa tenge.

32. Sikufurahishwa na kila tamko kwa ajili ya mashambulizi yaliyokuwemo dhidi ya watu wa madhehebu mengine ya Kiislamu.

33. Yeye ni msomi lakini hana ujuzi. Anapofafanua jambo hujaribu kulipinda ili liafikiane na matakwa yake na matamanio ya baadhi ya wasikilizaji wake.

34. Khutuba zingine hazina ujumbe na kama zinao hauko bayana. Zingine ni za mashambulizi na hazielekezi.

35. Khutuba hiyo ni ya kuwadharau watu wa aina mbalimbali. Anawadharau wasomi na hadithi za mtume na amejifaharisha mbele ya watu. Ameonyesha kuwa yeye ndiye msomi.

36. Nimefurahishwa na kila tamko katika khutuba kwa sababu nimeelimishwa na kuhimizwa kutenda mema. Imelenga kubadilisha nyoyo za wasikilizaji wenye kuutilia ujumbe maanani kiasi kwamba wanaweza kurudi majumbani kwao wakiwa wamejifunza mengi.

37. Sikufurahishwa na kila tamko kutokana  na jinsi alivyowasilisha hoja zake na lugha inayokera isiyo ya kirafiki. Mtu akiwa amekosea, humtukani kwa sababu atachukia matamko yako. Hawi na hamu katika kile unachotaka kumpasha.

38. Sikufurahishwa na kila tamko. Baadhi ya matamko hayakuwa sawa. Yalifuata matamanio ya nafsi yake na hayakuegemezwa kwenye Kur’ani na hadithi.

39. Tulihimizwa kujifanyia kazi na kujitegemea. Nilifurahishwa sana na kuhimizwa kwa vijana kufanya kazi.

40. Khutuba ilikuwa nzuri kwa sababu ilituhimiza kuchapa kazi ili tuweze kujisaidia na kutunza familia zetu.

41. Ilituhimiza kufanya kazi na kuwekeza.

42. Ilikuwa nzuri kwa sababu iltuhimiza kufanya kazi hata kama ni ya kipato kidogo ili tuweze kutoa sadaka na kumudu maisha..

43. Khutuba ilikuwa nzuri kwa vile ilituhimiza kutenda matendo mazuri yatakayokuwa sababu ya kuingia peponi.

44. Tulielimishwa jinsi Mwislamu anavyotakikana kuendeleza maisha yake.

45. Sisi akina mama khutuba hutusaidia sana kwa sababu kwengineko hatupati wanaotufundisha.

46. Tumepata mafunzo yatakayotusaidia kujirekebishe kitabia.

47. Imamu amesoma khutuba nzuri kwa sababu imetufunza jinsi ya kujiandaa kwa maisha ya milele. Lugha imekuwa ya uwazi na nzuri.

48. Matamko ya khutuba yamechangia sana katika kutuongezea imani na kutuzindua ili tujirekebishe.

49. Khutuba imetusaidia sana. Wengine tumezinduka.

50. Khutuba ilikuwa nzuri. Iliniwezesha kuzinduka na kutambua haja ya kurudi kwa Mwenyezi Mungu.

51. Tumezinduka na kupata matumaini mazuri juu ya maisha ya akhera.

52. Iliwakanya Waislamu kuombaomba na kuwahimiza wajiendeleze.

53. Khutuba ya leo ilikuwa nzuri isipokuwa Imamu hakumudu wakati vizuri. Hivyo ni kwa sababu ilikuwa ndefu na watu wengine walikerwa kwa ajili ya jambo hilo.

54. Wale wanaotenda mabaya walikerwa kwa sababu khutuba iligusia mambo hayo.

55. Khutuba huwa ndefu na Imamu hanifurahishi wakati mwingine kwa sababu analeta mambo yaliyotokea nje hapa msikitini kitendo ambacho huwafukuza watu.

56. Imamu alianza na kuwashambulia watu. Asipotolewa msikitini tutaukimbia.

57. Naudhikakwa sababu yeye ni mpiga ramli lakini hataki mawaidha yoyote ambayo yanaelekea kupinga kitendo hicho. Ndiyo maana anayarejelea kama vurugu.

58. Naudhika kwa sababu lugha aliyoitumia ni ya matusi.

59. Nimeudhika kutokana na tamko hilo kwa sababu yeye mwenyewe hana elimu ya kutosha lakini anawakejeli Mashekhe wanaomzidi.

60. Tumekerwa na khutuba zinazozungumzia kitu kimoja; mara kupiga kidole; mara kukuza ndevu, badala ya kusoma khutuba zinazowajenga watu kiimani.

61. Sikupendezwa na kila tamko kwa sababu katika matamko yake kuna yanayoleta mfarakano kati ya wasikilizaji.

62. Imamu alitutukana sisi wazee na kutwambia tutoke katika msikiti wake.

63. Sikufurahishwa na kila tamko kwa ajili ya mashambulizi yaliyokuwemo, dhidi ya watu wa madhehebu mengine ya Kiislamu.

64. Imamu anatuudhi kwa kutaja ila zetu hadharani.

65. Nilijisikia vibaya kusikia kwamba watoto wetu wanajihusisha na mabo ya ulevi. Najisikia vibaya mimi kama mzazi.

66. Hatutaki kusalia nyuma yake kwa sababu yeye ni mshirikina.

67. Hatibu wetu huwasilisha khutuba zake vizuri. Tunajifunza mengi na kuyatia matendoni.

68. Nilikuwa nikitumia madawa ya kulevya lakini sasa nimeacha.

69. Tuliupata ujumbe na wengi wetu tumebadilisha mienendo yetu.

70. Khutuba hiyo ni ya kuwadharau wasomi na hadithi za mtume. Anaonyesha kuwa yeye ndiye msomi na wengine wana elimu duni.

71. Ile khutuba ni nzuri kwa upande mmoja kwa sababu ina mawaidha na kwa upande mwengine imewashambulia watu wasiofuata mwelekeo wake na kuwaaibisha. Hilo linaudhi sana.

72. Tumeaibishwa sana na matendo ya watoto wetu. Niliona aibu niliposikia kwamba wanalewa na kuyumbayumba barabarani.

73. Khutuba ilinitia hofu nikazinduka.

74. Imamu alitoa vizuri kitangulizi cha khutuba lakini alipotoa mawaidha akonyesha kiburi, akakosa diplomasia na akawahubiria Waislamu peke yao pasina kujiweka miongoni mwao.

75. Imamu alitufundisha kuhusu maisha ya baada ya kufa na uwezo wa Mungu wa kufanya atakalo.

76. Tulihimizwa kujiandaa kwa maisha ya kaburini na kujua kwamba baada ya kufa kuna maisha mengine. Tulielimishwa kwamba maisha ya kuzimuni na akhera yanahitaji tujiandae kwayo kwa kutenda amali nzuri tukiwa hapa duniani.

77. Matamko hayo yalikusudiwa kutoa wosia kwetu juu ya kumcha Mwenyezi Mungu na kufanya mambo ya kheri.

78. Hilo ni onyo lililokusudia kuwaathiri waumini katika fikra na tabia zao. Tumelizangatia kwa sababu hali aliyoelezea, ambayo watenda maasi watakuwemo ni ya kutisha.

79. Khutuba hiyo iligusa mitima ya waumini wengi kwa sababu alitumia lugha ya kusihi na kila alipotaja adhabu aliomba dua ya kinga…

80. Kuna mengi tuliyojifunza ambayo kama si khutuba hiyo, tusingeyapata. Khutuba kama hizo lazima ziwasilishwe ili zisambaze imani miongoni mwa wanadamu..

81. Khutuba zimetengeza mambo mengi hususani sala kwa sababu watu wengi siku hizi wanadumisha sala.

82. Khutuba imepuuzwa na waumini wengi kwa sababu yeye mwenyewe si mfano bora.

83. Wakati mwengine wanaopinga ujmbe wa Imamu na kulalamika huwa wanaotenda maovu kama vile zina na shirki. Watu kama hao hawataki vitendo hivyo vitajwe.

84. Maimamu wengine hawafafanui vizuri mambo wanayozungumzia katika khutuba. Hilo huwapelekea maamuma kuwaelewa vibaya, kukanganyika au kupuuza matamko yao.

85. Maimamu wengine huwatukana waumini badala ya kuwarai kuacha mabaya na kutenda mema. Kuna aliyesema: "Wanawake hamtaki kuvalia hijabu vichwa vimefura, mnamwonyesha nani"?

86. Imamu asipofafanua khutuba yake vizuri watu husinzia tu hata kama maudhui ni nzuri. Khutuba za vijijini ndizo huwasilishwa kwa namna hiyo. Kinachosababisha hali hiyo ni elimu duni.

87. Khutuba zina faida kubwa kwa sababu zinatuelimisha na kutuzindua juu ya maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu.

88. Khutuba zisizopangiliwa vizuri hazifurahishi kwa sababu wasikilizaji hawaelewi maana zinazokusudiwa bali wanapotezewa tu wakati.

89. Maimamu wanapaswa kutumia lugha ya upole na wasiwalazimishe watu. Kwa mfano, wasiwalazimishe watu kutoa sadaka. Ni vyema kuwambia tu faida za kutoa sadaka na kasoro za kutoitoa.

90. Baadhi ya maimamu, wakisikia kwamba kuna aliyegombana na jirani, huja msikitini na kuyazungumza mambo hayo kwenye khutuba. Hilo halipendezwi kwa sababu huwaaibisha wahusika.

91. Khutuba hiyo ni mwafaka kwa hali. Shida iliopo ni kwamba mtu anaweza kufariki na hakuna anayeijali familia; anaweza kuugua na hakuna anayejali.

92. Khutuba hiyo imetuzindua na kututaka tujiandae kila wakati kwa sababu mtu anaweza kufariki dunia wakati wowote.

93. Tamko hilo ni la kuchochea katika ngazi ya mtu binafsi ni vyema kuwa na cha kufanya siyo kusubiri wengine kukufanyia jambo lolote.

94. Sehemu ya khutuba iliyozua hisia zaidi ni ile iliyowasilishwa kwa Luganda. Ujumbe uliwasilishwa kwa nguvu katika lugha hiyo.

95. Nimechunguza hali na kuona kuwa vijijini khutuba hazizungumzii jambo moja. Hakuna jambo maalum. Khatibu anazungumza kwa ujumla sana. Huzungumzia kila kitu.

96. Imamu hakujiweka miongoni mwa watu. Anawahujumu moja kwa moja. Anawaona kama watenda maasi na yeye ndiye mtenda mema.

97. Khutuba za IUIU huwa na maudhui maalum. Huzungumzia jambo moja. Lakini zile za vijijini ni pana na huzungumzia mambo mengi.

98. Khutuba za vijijini huchukua muda mrefu. Inapokuwa ndefu sana uzuri hupungua na khatibu hujirudiarudia sana.

99. Maimamu wanapaswa kujifunza jinsi ya kutumia lugha kwa sababu huchangia pakubwa.

100. Ni muhimu sana kwa Imamu kubadilisha tabia . Kwa bahati mbaya wengine hawajui shida yao. Pengine kuna haja ya kutembelewa na baadhi ya Mashekhe wawape nasaha juu ya yale yanayotakikana kubadilishwa.

101. Nikisikiliza khutuba kwa mara ya kwanza, inanivutia sana. Lakini maudhui yakirudiwarudiwa sana na ikatokea kwamba nimewahi kuyasikiza kwa mhubiri hodari halafu mtu mwingine akaja nayo na hali imeiva nusu, sivutiwi.

102. Wanapaswa kutumia lugha inayoeleweka na watu. Mandela alisema kwamba: "Ukizungumza na mtu katika lugha ya kigeni, mazungumzo hayo yanaenda kichwani na ukizungumza naye katika lugha yake, yanaenda kwenye mtima wake".

103. Baadhi ya Maimamu huwashambulia matajiri mara kwa mara katika khutuba zao. Imamu alitumia lugha inayowakasirisha watu. Badala ya kusema: Jamani toeni katika mali yenu fungu fulani ili kuwasaidia wasiojiweza, anawashambulia moja kwa moja na kuongeza maarifa yake badala ya kusoma kitabu kitukufu.

104. Imamu huuleta ugomvi ulioko nyumbani kwa watu msikitini. Khutuba za aina hiyo huwasilishwa katika miezi ya Mei na Juni ambapo kuna ufukara mwingi.

## KIAMBATISHO D: MAONI YA MAIMAMU JUU YA KHUTUBA ZA IJUMAA

1. Niliwatarajia kubadilisha tabia zao washikamane na maamrisho ya Allah.
2. Wengi wao walipata hofu kutokana na toni niliyotumia kusoma aya za Kur'ani na kuzitafsiri.
3. Nawambia ukweli kutoka kwa Allah pasina kujali hisia zao.
4. Siandiki. Nategemea Kur'ani. Nina uzoefu wa siku nyingi katika kukhutubu.
5. Sitaki kutumia lugha inayowakera watu. Nasitiri na kutoa mifano kutoka katika historia.
6. Wanachukia kutaja maovu wanayotenda na ukiwasomea aya ya Kur'ani au hadithi ya mtume inayokataza tendo fulani, huchukulia kuwa umewashambulia.
7. Niliwatarajia kusikiliza kwa makini watilie maanani ninayowambia na wasali ikiwa hawafanyi hivyo.
8. Nilikusudia kuzijenga nyoyo zao kiimani waweze kutenda niliyowafunza.
9. Ningependa waache maovu kama vile kuvaa vibaya, kula riba na zina.
10. Sisi Maimamu tunawatarajia Maamuma kubadilika kitabia wafanye wanayoambiwa katika khutuba.
11. Athari ni ndogo sana inaweza kuwa 5%. Kwa mfano Imamu anaweza kuwaelimisha waumini kuhusu umhuhimu wa kusali lakini ni wale ambao walikuwa wakisali mwaka jana ndio wanaoendea na sala.
12. Baada ya kuwaonya jana, wameweza kubadilisha tabia zao japo kidogo.
13. Nikifundisha kuhusu kitendo wanachofanya, huchukulia kuwa ninawashambulia. Nikisema kwamba asiyesali, nguruwe huwa bora kuliko yeye husema kuwa nimewatukana. Na Imamu mwengine akija na kufundisha kuhusu jambo hilo hilo, husema kwamba amepewa pesa ili aje afanye kampeni.
14. Wengine hurudi kando na kusema mambo anayozungumzia ni ya kweli au ni uwongo? Wakajifukuza wenyewe kutoka katika misikiti.

15. Hawapendi khutuba nzuri.

16. Ukiwambia kuwa ukiacha sala moja, inakutoshelezea kuwa kafiri, husema umewaita makafiri.

17. Wale wanaotambua ujumbe wa khutuba hubadilika lakini wengine hawabadiliki.

18. Sisi kazi yetu ni kufikisha ujumbe. Wanaokasirika ni shauri yao.

19. Watu wengi huchelewa kuja msikitini. Kwa hiyo, nilikuwa nikiwahimiza kuja mapema.

20. Khutuba ilikuwa na athari chanya. Kuna waliokuja na kuniambia kuwa kuna tatizo la kutumia miraa katika eneo hili.

21. Ili kuiboresha khutuba, natumia maneno ya Allah na hadithi za mtume(SAW) pamoja na kauli za sahaba zake na maulama.

22. Maimamu wanapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

    - Wateue mada kulingana na yale yanayojiri katika eneo husika.
    - Wasitaje majina ya watu.
    - Wasitukane wala kuwadharau maamuma. Kama kuna jambo lililotokea, ni vyema wasubiri ili waje walizungumzie baada ya kupitikiwa na wakati fulani.
    - Wasitumie matamko ya ukali.
    - Watumie ushahidi kutokana na mafundisho ya mtume (SAW).
    - Mambo ya siasa yasiyofungamana kwa vyovyote na Uislamu yasiingizwe katika khutuba. Hapa nchini, Maimamu ndio wanaochochea mfarakano wakitumia khutuba.

23. Vijana hawapendi Maimamu wao kutaja mambo wanayofanya. Niliwasilisha ktutuba mwaka jana na baada ya sala nikaambiwa kwamba vijana wamenikasirikia. Vijana hao hao waliwahi kumwekea Imamu wao bangi katika kahawa siku ya maulud eti kwa sababu wamesinywa na khutuba zinazoshutumu matumizi ya madawa ya kulevya.

24. Si vizuri kuwasilisha khutuba kama umekasirika. Ripoti niliyopata katika ofisi yangu ni kwamba Imamu mmoja aliwatukana tu watu kisha akawambia wakimu sala.

**KIAMBATISHO E: BARUA YA RUHUSA WA KUFANYA UTAFITI**

UGANDA MUSLIM SUPREME COUNCIL
HEADQUARTERS

*Department of Religious Affairs*

المجلس الأعلى الإسلامي الأوغندي
المقر الرئيسي
قسم الشئون الدينية

Ref: *UMSC/MJS/08/2011* ..................................................الرقم :

Date: *10th June, 2011* ..................................................التاريخ:

**Matasi Badru Haroon**
**Egerton University**
**P.O. BOX 536,**
**Egerton, Njoro, Kenya.**

Dear Mr. Matasi,
***Assalarn Alaikurn.***

**RE: <u>PERMISSION TO CARRY OUT RESEARCH IN MOSQUES OF BUGISU SUB - REGION.</u>**

Reference is made to your letter dated 15th February, 2011, regarding the above subject.
I am glad to inform you that you have been granted permission to carry out research on Speech Acts in Friday Sermons in Bugisu Sub-Region.

I wish you success in your research.
***Wassalam Alaikum.***

Yours sincerely,

UGANDA MUSLIM SUPREME COUNCIL
SEC RELIGIOUS AFFAIRS
P.O. Box - 1146
KAMPALA - UGANDA

**Sheikh Muhammad Mursheed Luwemba**
**Secretary for Religious Affairs (UMSC).**

*c.c:* ***His Eminence the Mufti of Uganda.***
*c.c* ***The Secretary General UMSC.***
*c.c* ***The District Kadhi Bugisu District Muslim Council.***

Plot No. 23-25 Old Kampala Road
P.O.Box 1146 Kampala - Uganda
Tel. 256 312108115/041 4344499 Fax. 256 41 256500

Email: umscmajilis@yahoo.com